*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

__________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

___________

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 6 Februari, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JORAM I. HONGOLI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, sasa aulize swali lake

Na. 85

### Waendesha Bodaboda Nchini

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Kuendesha bodaboda ni ajira kama zilivyo ajira nyingine nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo vijana hao ili kuifanya kazi hiyo iwe rasmi na yenye kutambulika kama kazi nyingine zozote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kutambua bodaboda kama mojawapo ya usafiri wa kubeba abiria nchini kisheria, mwaka 2017 ilifanya marekebisho ya Kanuni za Usafirishaji za Mwaka 2010 ambapo waendesha bodaboda walirasimishwa kwa kupatiwa leseni za usafirishaji. Leseni hizo zinatolewa na Mamlaka za Miji, Wilaya na Majiji kwa niaba ya *SUMATRA* ili kuhalalisha shughuli za uendeshaji bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwajengea uwezo waendesha bodaboda, Serikali inatekeleza mipango ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kutoa mafunzo ya udereva kupitia Jeshi la Polisi kwa waendesha bodaboda na hatimaye kupatiwa leseni za udereva. Aidha, kama ilivyo katika vyombo vingine vinavyotoa huduma za usafirishaji, usalama wa waendesha bodaboda na abiria umeendelea kusimamiwa na kulindwa wanapotekeleza majukumu yao barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya waendesha bodaboda ili hatimaye viweze kuwezeshwa kwa mitaji na mafunzo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuwapatia maeneo ya kuegesha bodaboda na kuyatambua pamoja na kuwapatia vitambulisho na nne ni kuwapatia waendesha bodaboda mafunzo ya ujasiriamali na hatimaye kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu na kuwaunganisha na taasisi nyingine za fedha zinazotoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni kuwapatia elimu juu ya faida ya kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuwaunganisha na mifuko husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaaban Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni ukweli usiopingika kuwa bodaboda zimetoa ajira nyingi sana hapa nchini. Je, Serikali haioni sasa kuwa kuna haja kubwa ya kuwawezesha vijana hawa mikopo kwa wakati kuliko ilivyokuwa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa vijana wengi wamejiunga na vikundi na hawajawahi kupata mikopo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kuona vikundi vile vya vijana na kuwapatia mikopo ambayo hawajawahi kuiona wala kuisikia, hasa kwa vijana wa Wilaya ya Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali la kwanza la uwezeshaji kwa wakati kwa vikundi hivi vya bodaboda. Kama nilivyojibu katika jibu la msingi ni kwamba Serikali inachokifanya hivi sasa ni kushirikiana na Mamlaka za Halmashauri, Manispaa, Wilaya na Majiji ili kuona namna bora ya kusaidia uundwaji wa vikundi hivi kwa sababu ni ngumu sana kumwezesha bodaboda mmoja mmoja pasipo kukaa katika vikundi. Ndiyo maana sasa hivi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani tumeendelea kufanya maandalizi kuhakikisha kwamba vyama hivi vya bodaboda katika mikoa na katika ngazi ya Taifa vinasajiliwa ili tupate namna bora ya kuweza kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo linategemea utayari wa wahusika kwa maana ya kuunda vikundi na kuunda katiba ili wawe tayari kwa ajili ya kukopeshwa. Nitoe rai kwa vikundi vyote vya bodaboda nchini ambavyo viko rasmi watumie fursa ya mikopo inayotolewa na Serikali na taasisi mbalimbali za fedha, hasa ukiwemo Mfuko wa Uwezeshaji Vijana Kiuchumi ambao umelenga katika kuwapatia maendeleo vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhusu vijana wa Kilindi. Nitoe tu rai kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge wote, wale ambao wana vikundi vya vijana na wangependa

kunufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, sharti moja kubwa ambalo lipo ni uanzishwaji wa *SACCOS* ya vijana katika halmashauri husika. Hivyo, nipo tayari kwenda Kilindi pamoja na Mheshimiwa Omari Shekilindi kwenda kuangalia vikundi vya vijana. Vilevile kama watakuwa wamekidhi mahitaji ya uwezeshaji wa Mfuko wa Vijana basi tupo tayari kuwawezesha vijana wa Kilindi ili nao waweze kunufaika na fursa zilizopo katika nchi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba *SUMATRA* imefanya maboresho na inatoa leseni kwa waendesha bodaboda, nataka kujua ni kwa nini kumekuwa na *restriction* kwa bodaboda kuingiza bodaboda zao katikati ya Jiji la Dar es Salaam, lakini vilevile ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hairuhusiwi? Naomba majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Mkoa wa Dar es Salaam uongozi wa mkoa uliweka utaratibu wa namna vyombo hivi vya usafiri vitakavyoingia katikati ya mji kutokana na changamoto ambazo zilijitokeza awali likiwemo suala la msongamano pamoja na usalama. Tayari kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wameanza kuratibu zoezi hili katika umakini mkubwa ili kuona namna bora ambavyo wafanyabiashara hawa pia watafanya biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika maeneo mengine zipo sababu za kimsingi za kwa nini yametokea

masuala hayo lakini kubwa limekuwa ni suala la kiusalama. Ndiyo maana Serikali hivi sasa imeanza kuyatambua maeneo rasmi ya maegesho na kuwapatia vitambulisho ili likitokea jambo lolote la kiusalama tuweze kujua ni wapi limetokea na tuweze ku-*trace* ili kuondokana na dhana hii kwamba boaboda ni wahalifu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Kuboresha Posho za Madiwani Nchini**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Waheshimiwa Madiwani wana majukumu mengi ya kufanya katika kata zao; na posho wanayolipwa kwa mwezi hailingani kabisa na majukumu yao na ni ndogo sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza posho ya Waheshimiwa Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza posho na maslahi ya Madiwani nchini kwa awamu kulingana na uwezo wa halmashauri kukusanya mapato ya ndani. Serikali ilipandisha posho za mwezi za Madiwani kutosha Sh.120,000 kwa mwaka 2012/2013 hadi shilingi 250,000 kupitia Waraka wa tarehe 16, Agosti, 2012 na posho za madaraka kwa Wenyeviti wa Halmashauri na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri. Aidha, katika Mwaka wa Fedha

2014/2015 kupitia Waraka wa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa wa Tarehe 23, Desemba, 2014, Serikali ilipandisha posho za Madiwani kutoka Sh.250,000 hadi Sh.350,000 kwa mwezi kwa Madiwani na Sh.350,000 hadi Sh.400,000 kwa mwezi kwa Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya pamoja na posho nyingine kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa tarehe 26, Novemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la posho na maslahi ya Madiwani inatokana na halmashauri kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani. Hivyo, natoa wito kwa halmashauri kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri ili kujenga uwezo wa ndani na kulipa posho hizo kwa Madiwani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kwamba halmashauri waongeze makusanyo ya mapato ya ndani *(own source)* na kwa kuwa Serikali ilichukua vyanzo vingi vya mapato ambavyo vilikuwa vinaipatia halmashauri mapato, sasa Serikali inasema halmashauri ziongeze makusanyo ya mapato ya ndani, hayo makusanyo ya ndani yatatoka wapi na kwa nini Serikali isiongeze ruzuku ili Madiwani waongozwe posho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Madiwani ni viongozi kama sisi Wabunge; na kwa kuwa viongozi wa kisiasa wengi wamewekwa kwenye Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa, kwa nini hawa Madiwani nao wasiwekwe kwenye sheria hii ili waweze kutambulika kisheria kwa sababu ni viongozi muhimu? Katika Uchaguzi Mkuu ni mafiga matatu, baada ya uchaguzi figa la tatu linameguka wanakuwa viongozi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Mbunge anauliza kwamba kwa sababu kuna vyanzo vimechukuliwa na Serikali Kuu na kwa hiyo mapato ya halmashauri yamepungua ni kwa nini tusitoe ruzuku. Kwanza naomba ieleweke kwamba vyanzo vilivyochukuliwa ikiwemo kodi ya majengo inakusanywa na *TRA* kwa niaba ya Serikali nzima lakini fedha hizi zinarudishwa kwenye halmashauri kwa ujumla wake kwenda kufanyia kazi shughuli za maendeleo katika halmashauri zetu hizo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa sasa hili jambo la ruzuku halijafanyiwa kazi, naomba tulipokee tulifanyie kazi, kadri uwezo utakavyoruhusu basi tutaona kama kuna uwezekano wa kupeleka ruzuku. Kwa sasa kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba posho za Madiwani na malipo mbalimbali zinatokana na vyanzo vya ndani na sasa tupo kwenye mchakato wa kuandaa bajeti ya 2019/2020, naomba halmashauri zetu ziangalie uwezekano wa kuongeza posho na mapato ili waweze kujilipa wenyewe kwa sababu ndipo msingi wa malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili anazungumza habari ya sheria kuweza kuwatambua; hili ni jambo jema, lakini kwa sheria iliyopo huu ndiyo utaratibu wa kawaida, sasa kama kuna maoni mengine kama alivyopendekeza tupo tayari kuyapokea, tuyafanyie kazi na hatimaye kuyaingiza kwenye sheria ili waweze kulipwa kama watumishi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa

Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Kukarabati Kuta za Mito – Mikindani**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati mifereji ya maji ya mvua na kuta za mito inayoingiza maji ya bahari katika Mji wa Mikindani ili kuirejesha katika hali yake ya awali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kifungu cha 129(1) kinaeleza wajibu wa kila mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenye eneo lake itajenga au kuandaa mifereji ya maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kumekuwepo na changamoto ya kujaa kwa maji katika maeneo mengi nchini yanayopakana na bahari kunakosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi na hivyo kufanya baadhi ya mifereji kushindwa kumudu athari zake. Kufuatia hali hii, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imeanza kuchukua hatua zinazolenga kuzuia na kupunguza madhara yaliyojitokeza katika maeneo yaliyoathirika nchini ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya jumla ya maeneo haya ikiwemo Mikindani ili kuwezesha kuandaa Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ipo katika hatua za kuandaa Mpango Endelevu wa Kitaifa Kuhimili

Mabadiliko ya Tabianchi *(National Adaptation Plans)* wenye malengo ya muda wa kati na muda mrefu ili kuboresha usimamizi wa mabadiliko nchini kwa kushirikiana na halmashauri zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi, tunashauri halmashauri za maeneo husika kuingiza gharama za ukarabati wa mifereji kwenye bajeti zao ili kupunguza athari zilizozidi kuongezeka kwa kuiga mfano wa Jiji la Dar es Salaam.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri; hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Mji wa Mikindani ni miongoni mwa miji ambayo iko chini ya usawa wa bahari; kwa hiyo hii mifereji ninayoizungumzia ni ile ambayo maji ya bahari yakijaa inapitisha maji kuingia katikati ya mji na iko mingi na tangu zamani hii mifereji ilikuwa imejengewa lakini kutokana na uwezo mdogo wa halmashauri imeshindwa kuifanyia ukarabati mara kwa mara. Swali, je, Serikali iko tayari kuisaidia Manispaa ya Mtwara – Mikindani katika kukarabati mifereji hii ya Mji wa Mikindani kwa sababu kuiachia manispaa peke yake ni kuiongezea mzigo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kwenda Mikindani kuona hicho ninachokizungumzia ili aweze kunielewa zaidi na hatua za haraka ziweze kuchukuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

nichukue fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijajibu swali na mimi nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi zake na ushirikiano mkubwa ambao anatupa sisi Wizara ya Mazingira katika kukabiliana na hali hii ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na swali lake la kwanza; kwanza nipo tayari na tupo tayari pia kusaidia maeneo yote kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la swali la msingi, kuhakikisha kwamba maeneo yote haya tunajitahidi ili tunakabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia mifuko ambayo tunapata fedha kutoka kwa wenzetu, kwa maana ya *Global Climatic Change.*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu kwenda Mtwara. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ninayo ziara ya kuanzia tarehe 18 Iringa, lakini pia kwenda Mtwara, Njombe, Ruvuma, Lindi na baadaye nitakwenda Mtwara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba najionea mazingira halisi ya hiyo mifereji ambayo ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Salim, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF S. HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba niulize swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Hii mito ambayo inatoka baharini na kuingia nchi kavu inakuwa na kasi sana wakati yale maji yapoingia ama yanapotoka, kwa sababu tabia ya bahari, maji yanapojaa yanakuwa yana nguvu sana na yanapotoka vilevile yanakuwa na nguvu. Maana yake ni kwamba ongezeko la *soil erosion* linakuwa kubwa kuliko linavyotarajiwa. Ni upi sasa mkakati wa Kitaifa wa Serikali kwa sababu ardhi yetu inapungua kwa kasi? Msimbati itakuwa ni moja kati mfano mzuri wa kasi wa maji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mkakati hasa wa Kitaifa wa Serikali kudhibiti suala hili la *erosion* katika kingo za bahari zetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ulishaanza na nitoe mifano, ukiangalia kingo za bahari pale *Ocean Road* tumejenga. Pia ukienda Pangani tumejenga na maeneo mengine tutaendelea kadri ambavyo tutakapokuwa tunapata fedha za kuhakikisha tunakabiliana na haya mabadiliko ya tabia nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 88

**Uwanja wa Ndege Njombe Wawa Kero kwa Wananchi**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Njombe umekuwa kero kwa wananchi, kwani upo katikati ya Mji na haujakarabatiwa kwa muda mrefu matokeo yake uwanja huo umejaa barabara hizo. Aidha, watu wanaopita katika barabara hizo zisizo rasmi hukamatwa na kutozwa faini:-

Je, ni lini mkakati wa Serikali juu ya uwanja huo ili kupunguza kero kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha ndege cha Njombe kilijengwa na Wakoloni, yaani kabla ya uhuru miaka ya 1940 na kuanza kutumika rasmi 1945. Miaka hiyo Mji wa Njombe ulikuwa mdogo sana na hivyo kiwanja kilikuwa mbali na makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria za Kitamaifa za Usalama wa Anga hairuhusiwi watu, wanyama, magari na kadhalika kukatiza kwenye viwanja vyovyote vya ndege. Kwa mantiki hiyo, vitendo vya baadhi ya wananchi wa maeneo hayo kukatiza katika kiwanja hicho ni vya uvunjivu wa sheria na ndiyo maana wananchi hao hukamatwa na kutozwa faini au kuadhibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kukarabati kiwanja cha ndege cha Njombe, Serikali imepanga kufanya upembuzi yanikifu na usanifu wa kina kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia uliohusisha pia viwanja vya ndege vya Iringa, Songea, Lindi, Kilwa Masoko, Tanga, Moshi, *Lake* Manyara, Singida, Musoma na kiwanja kipya cha Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika kwa viwanja hivyo ambapo taarifa ya mwisho iliwasilishwa tarehe 28 Machi, 2017. Hatua iliyopo kwa sasa ni utafutaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hicho. Upanuzi huo utahusisha ujenzi wa uzio kuzunguka eneo lote la kiwanja ili kudhibiti wananchi wanaokatisha kiwanja hicho kinyume cha taratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucia Maichael Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba

kiwanja hicho kilijengwa kabla ya uhuru; na kwa kuwa kiwanja hicho kilijengwa kabla ya makazi ya watu hayajasogea maeneo yale na sasa hivi maeneo yale yamejaa makazi ya watu; na kwa kuwa Liganga na Mchuchuma ndiyo mradi ambao unakaribia sasa kuingia katika Mji wetu wa Njombe. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kukihamisha kiwanja hicho na kupeleka sehemu za Tanwati au Mgodeti, ama Ilembula? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlowe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tunatambua umuhimu wa kujenga kiwanja hiki. Pia nafahamu Njombe ina fursa nyingi za kiuchumi, mojawapo Mheshimiwa Mbunge ametaja, tunafahamu pia uhitaji wa huduma hii ya usafiri, hususan wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, suala la ujenzi wa uwanja huu pia mimi mwenyewe nimetembea Njombe, nimefanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa, lakini mara nyingi nimefanya mazungumzo na Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Mwalongo. Kwa hiyo, tulijaribu kuona namna bora ya kuweza kuendeleza uwanja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mahitaji ya kuendeleza uwanja huu bado yapo, kwa sababu kwenye taarifa ile ya usanifu kama ingeonesha kutokuwa na mahitaji ya kuendeleza kiwanja hiki katika eneo hili, basi ningeshauri namna tofauti. Hata hivyo, jambo hili kama wana Njombe mtaona kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa mnaweza, mkalizungumze mlilete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutahadharisha tu kwamba kwa sababu kulikuwa kuna hatua ambayo imefikiwa na kuna gharama ambazo kama Serikali tumetumia kwamba kuhamisha uwanja huu kupeleka maeneo mengine kunaweza kupoteza fursa ambayo ilikuwa iko tayari imeshapatika kwa sababu inaweza ikatahitaji muda mrefu kufanya usanifu mpya na wananchi hawa wanahitaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tu kwamba uwanja huu tuujenge na kama mtahitaji kuwa uwanja mkubwa, mzungumze katika *level* ya Mkoa halafu ushauri wenu muulete, sisi kama Serikali tutauzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi nami niulize swali moja dogo la nyongeza. Dodoma sasa ni Makao Makuu ya nchi, kiwanja cha ndege kilichopo hakikidhi haja ya kutua kwa ndege kubwa. Je, ule mkakati wa Serikali kukamilisha uwanja wa ndege wa Msalato umefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nkamia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba ni kweli Serikali imefanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na niseme tu kwamba uhimu wa kuwa na kiwanja kikubwa cha Kimataifa upo. Hatua ambazo zimefikia Mheshimiwa Nkamia anafahamu, liko eneo la kutosha kabisa kuweza kujenga huo uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, anafahamu na kwa kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwamba ule ufadhili kwa ajili ya kujenga uwanja huu kulikuwa kuna hatua nzuri kwamba tutapata fedha za kutosha kujenga uwanja huu. Ili huduma iweze kuanza, Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwamba badala ya kuanza na kujenga majengo makubwa ili huduma ianze, tutaanza kutengeneza *runway* ili ndege zianze kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Nkamia juhudi za kuujenga uwanja huo ziko katika kasi ambayo siyo ya kawaida. Kwa hiyo, nimtoe hofu yeye na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ambao wanakuja kupata huduma katika Makao Makuu kwamba tumejipanga vizuri kuweza kujenga huu uwanja. Kwa hiyo asiwe na wasiwasi. Avute subira, muda siyo mrefu ataona mambo yanavyoendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto iliyopo Njombe inafanana kabisa na changamoto iliyopo uwanja wa ndege wa Bukoba kwamba ni mfupi na kupelekea ndege kutua kwa shida au kuruka kwa shida mfano kama *Bombadier*. Je, ni lini Serikali itaongeza urefu wa uwanja huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, niliona hapa Mbunge wa Geita amesimama, Mbunge wa Kigoma kasimama. Kwa hiyo, ungejibu kuhusu viwanja vyote hivyo ili Waheshimiwa Wabunge wapate picha ya mipango ya Serikali, kwa sababu hata mimi hapa nataka kusimama.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie uwanja wa ndege wa Bukoba, yako maboresho muhimu yamefanyika na huduma inaendelea vizuri na ndege zinashuka vizuri na miruko imeongezeka. Pia ule mpango wa kuuboresha uwanja huu tunaendelea na hatua ya kutathmini

maeneo ambayo tutahamisha wananchi, Mheshimiwa Mbunge anafahamu ili sasa ule urefu wa sehemu ya kurukia na kutoa ndege iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba zile hatua za kufanya maboresho ya viwanja mbalimbali nchini ziko kwenye mpango na Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, mara kadhaa tumezungumza namna ya viwanja, hata leo nimerejea kuzungumza viwanja vingi ambavyo tunaendelea kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha ili kuhakikisha kwamba tuna viwanja wa ndege ambavyo vitamudu kutoa huduma katika maeneo ya Mikoa yote. Tutaendelea kutoa maeneo mengine ambayo ni maalumu kama ilivyoonekana kwamba uwanja wa ndege wa Mafia, kama nilivyozungumza jana, tunaupeleka katika hatua uwe na hadhi ya kimkoa ili huduma ziongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko viwanja vingine ambavyo tunaendelea kuvipanua. Kwa mfano, tunaendela kupanua uwanja wa ndege wa Kigoma, Tabora, Shinyanga na Bariadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge waamini tumejipanga kuhakikisha kwamba pamoja na Serikali kuendelea kuliboresha shirika letu kwa kununua ndege, italeta maana pale ambapo Serikali inanunua ndege na ndege zinaenda kuwahudumia Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi umetaja wa Musoma? Maana nilimwona Mheshimiwa Makilagi naye kasimama pale. Nadhani majibu hayo pia yanaenda na Musoma.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Nassor Suleiman Omar, Mbunge wa Ziwani, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Kuboresha Posho za Madiwani Nchini**

**MHE. NASSOR SULEIMAN OMAR** aliuliza:-

Kilimo cha mazao ya viungo vya chakula ni biashara yenye tija kubwa duniani kwa sasa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha kilimo hicho hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassor Suleiman Omar, Mbunge wa Jimbo la Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mazao ya viungo kutokana na mchango wake katika kipato cha mkulima mmoja mmoja na pia katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Kutokana na umuhimu huo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeandaa mkakati wa kuendeleza mazao ya viungo (*Spice Sub Sector Strategy twenty fourteen)* ambao unalenga kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mahususi katika mkakati huo ni utoaj mafunzo ya kuongeza ujuzi katika uzalishaji kwa wataalam na wakulima, uanzishwaji wa vituo vya kukusanyia mazao na kupanga madaraja na kuunda masoko ya pamoja ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine mahsusi yanayofanyiwa kazi ni kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji wa vitalu vya kuzalisha miche na mashamba ya miti mama kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya aina za mazao hayo. Mkakati huo unatekelezwa kwa pamoja na wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi zisizo za Kiserikali na Vyama vya Wakulima ambazo ni pamoja na *Sustainable Agriculture*

*Tanzania*, Chama cha Wakulima wa Viungo, Amani *(CHAWAVIA)* na Jumuiya ya Wakulima wa Viungo Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeandaa mwongozo wa uzalishaji wa mazao ambao umeainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo mazao ya viungo. Mwongozo huo unalenga kuonesha fursa za uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo mazao ya viungo. Wizara ndani ya miezi sita ijayo itakamilisha zoezi la usajili wa wakulima wa mazao mbalimbali nchini ikiwemo mazao ya viungo kwa kubaini idadi yao, ukubwa wa mashamba na mahali alipo ili kuwahudumia kwa ufanisi zaidi na kuongeza tija.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassor, swali la nyongeza.

**MHE. NASSOR SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa wakulima wa zao hilo hapa nchini kwetu wamekuwa wengi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia soko la uhakika wa bidhaa hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa kuna ongezeko la uzalishaji wa *spices* hapa nchini na sisi kama Serikali, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi, tunayo mikakati ya kusaidia wakulima wetu wa *spices* kuongeza uzalishaji; sanjari na hilo kuwasaidia kupata masoko ya uhakika. Azma ya Serikali ni kuhakikisha mazao yote ambayo yanatuingia fedha za kigeni tunawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kuwasaidia masoko ili waweze kusaidia kwenye pato la Taifa na kuingizia Taifa fedha za kigeni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. NAJMA M. GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa vile *spices* yaani viungo vya vyakula mbalimbali ni vinaonesha kwamba vina afya zaidi katika miili ya binadamu. Sasa kwa nini Serikali haitumi wataalam wake wakaja Zanzibar kujifunza faida za viungo hizo ili Watanzania wengine walioko Bara ambao hawajui kama vile Wasukuma, Wamasai na makabila mengine waweze kujua na kutumia na kupata afya njema? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa maswali haya. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake tumeupokea, ni kweli hizi *spices* zina faida nyingi ikiwemo faida kwa upande afya kwa akinababa na akinamama. Ni ushauri mzuri kwa sababu tunatafuta masoko ya nje, lakini pia masoko ya ndani lazima nayo tuyatumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa wanaume wenzangu, ukiangalia *spices* kuna faida nyingi sana kwa upande wa wanaume na ni namna mzuri ya kukuza soko la ndani. Kwa hiyo, ushauri wa Mheshimiwa Najma tumeuchukua.

**NAIBU SPIKA:** Naona Mheshimiwa Selasini anakubaliana nawe na naona Mheshimiwa Waziri wa Afya pia alikuwa anatingisha kichwa kidogo hapo. Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wilaya ya Mkinga, Muheza, Korogwe na Lushoto ni maeneo ambayo yanalima kwa wingi mazao ya *spices,* lakini kwa muda mrefu maeneo haya yamekabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma za Ugani, masoko duni ya bidhaa hizi na vilevile mazao haya kuuzwa kwa bei ya chini sana. Je, Waziri yuko tayari na wataalam wake kuja kwenye maeneo haya kujionea hali halisi ili kuweza kuondoa changamoto zinazowakabili wakulima wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dunstan Kitandula kwa namna anavyofuatilia masuala ya *spices* kwa niaba ya wakulima hapa nchini ikiwemo Jimboni kwake. Nimeshamhakikishia kwamba Serikali kwa kutambua kwamba *spices* hizi zina *potential* kubwa ya kutuingia fedha za kigeni, niko tayari kwenda Mkoa wa Tanga na kufika maeneo ambayo ameyataja kuhakikisha wakulima hawa tunawasaidia kwenye upande wa kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunawasaidia kwenye mambo ya *branding* na mikakati ya kimasoko ili kilimo chao kiweze kuwasaidia kuwakwamua kutoka kwenye umaskini, lakini uzalishaji wao usaidie kuchangia kwenye fedha za kigeni za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijiji.

Na. 90

**Utafiti Juu ya Gharama za Uzalishaji Kahawa - Mbinga**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya utafiti wa gharama za uzalishaji wa kahawa Wilayani Mbinga kwa mara ya mwisho?

(b) Je, utafiti huo ulibaini kilo moja ya kahawa kavu inazalishwa kwa gharama gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015/ 2016, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania *(TACRI)* imefanya utafiti wa gharama za uzalishaji wa kahawa katika Wilaya saba za Mbinga, Mbozi, Tarime, Rombo, Muleba, Karagwe na Buhigwe ambazo ni miongoni mwa Wilaya zinazozalisha zao la kahawa hapa Nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti cha *TACRI* kwa wakulima wa kahawa aina ya *arabica* umeonesha kuwa gharama za uzalishaji wa aina bora ya kahawa zenye ukinzani wa magonjwa ni shilingi Sh.2,192,000 kwa hekta sawa na wastani wa Sh.825.44 kwa kilo zenye tija ya wastani wa kilo 2,662 kwa hekta. Aidha, gharama za uzalishaji wa kahawa zisizo na ukinzani wa magonjwa ni Sh.2,571,200 kwa hekta sawa na wastani wa kilo 1,931.78 kwa kilo zenye tija za wastani wa kilo 1.331 kwa hekta. Aidha, gharama za uzalishaji wa kahawa wa aina hiyo zimeongezeka kutokana na matumizi makubwa ya viuatilifu vya kuzuia kutu ya majani *(Coffee Leaf Rust)* na Chulebuni ambayo *Coffee berry disease* yaani *CBD.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti pia umeonesha, wakulima wanaolima kilimo cha mseto yaani *intercropping* kwa kuchanganya zao la kahawa na migomba, gharama za uzalishaji ni wastani wa Sh.1,557,683 kwa hekta kwa kahawa bora na Sh.2,157,967 kwa kahawa isiyo na ukinzani kwa magonjwa. Aidha, kupitia tafiti hizo, Serikali imekuwa ikishauri wakulima kutumia aina bora za kahawa ili kuwa na kilimo chenye tija, faida na endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martin Msuha, swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni kwa kiasi gani Serikali imesambaza tafiti hizo za gharama za uzalishaji kwa wakulima wa kahawa ili kuwawezesha kufahamu msimu hadi msimu kama wanauza kwa faida ama hasara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakulima wengi wamekuwa wakilalamika juu ya bei duni ya mazao yao mwaka hadi mwaka; je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya tafiti za gharama za uzalishaji kwenye mazao mengine ya kipaumbele kama pamba, tumbaku, chai, korosho yakiwemo mahindi ili kuwawezesha wakulima hao kufahamu gharama zao za uzalishaji na hivyo kufahamu kama wanauza kwa hasara au kwa faida mwaka hadi mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Msuha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua matokeo ya tafiti hizi zimewafikia namna gani wakulima wa Tanzania; nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge, matokeo yote ya tafiti hizi tumeyifikisha kwa wakulima kwa njia mbalimbali; kwa njia ya mawasiliano ya *television*, *radio* na magazeti na vipeperushi vingine, lakini pia kwa kushiriki Taasisi zetu za *TACRI* na zingine zinazofanya utafiti wa kahawa na mazao mengine kwenye Maonyesho kama Nane Nane na maonyesho mengine ili wakulima na watu wengine wapate elimu ile pale. Pia zaidi, tuna mpango ambao ni endelevu ulioanza tangu *SDP I* wa kujenga kila kata vituo vya elimu kwa wakulima ili kutoa elimu kwa wakulima muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, anataka kujua kwamba, je, tafiti hizi za kujua gharama ya mazao mengine hasa mazao yale ya kimkakati na mazao ya mahindi ikoje. Kwanza nataka nimpe uelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya. Zao la mahindi ni moja ya zao la kimkakati. Labda Waheshimiwa wengi hapa wanashindwa kutambua kwamba kipaumbele cha kwanza cha Taifa ni mazao yale zamani tulikuwa tunaita mazao ya chakula. Kwa sasa hivi hatujaweka hiyo *demarcation* kwamba kuna mazao ya chakula na mazao yote ya biashara. Sasa hivi mazao yote ni ya biashara ila kipaumbele tumeyapa haya mazao nane ya mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujua tumefanya tafiti ngapi; tumefanya kila zao na kila mwaka kupitia ikutano yetu yote ya wadau. Kwa mfano, nimpe kwenye zao la korosho, kilo moja ya kuzalisha korosho ni Sh.1,350 na kwenye kilo moja ya kuzalisha mahindi, heka moja inatumia Sh.740,000. Kwa hiyo, kila mwaka tunafanya na kupeleka elimu hii kwa wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tunakubaliana kwamba masuala ya utafiti kwa ujumla nchini yamedorora sana. Hii ni kwa sababu vituo vya utafiti kikiwemo Kituo cha Utafiti Uyole - Mbeya viko hoi. Uyole iko hoi kimiundombinu na hata kibajeti. Sasa ni lini Serikali itatambua umuhimu wa vituo hivi kama zamani ili kuvipelekea bajeti stahiki tupate kuboresha kilimo nchini na hasa kituo cha Uyole Jijini Mbeya . Miundombinu iko hovyo, hata hali za wafanyakazi ziko hovyo. *Before* wakati tuko…

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza swali Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbilinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa ajili ya kuviona vituo hivyo, lakini nataka nimhakikishie kwamba, kama Serikali hatujawahi kuviacha nyuma vituo hivi kama anavyodai na ndiyo maana mwaka juzi 2017, tulileta Muswada wa Sheria na Bunge hili likaridhia. Kwa ajili ya kuviboresha vituo vile, tuliweza kuunda Sheria maalum ile Sheria hatari na kuunda vituo vyetu nane vikuu na nane vidogo, jumla vituo 16 na kuvipangia majukumu mahususi kwa kila kituo mazao mawili mawili ili kuyapunguzia mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya ni katika kuweka juhudi za msingi ili vituo hivi viwe na mazao machache ya ku-*focus* badala ya kubeba mazao yote na sasa hivi tuko kwenye mchakato wa bajeti na miongoni mwa vipaumbele tulivyovipa na katika hivi vituo vya utafiti kwenda kuviongezea uwezo pia kuviboresha miundombinu yake ili viweze kukidhi matarajio ya wakulima wa nchi hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 91

**Kuinua Bei ya Zao la Kahawa**

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Kahawa ni zao la biashara na la kimkakati ingawa kwa miaka kadhaa bei ya zao hilo imeendelea kuwa chini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua zao hilo Mkoani Kagera ikiwemo kupandisha bei ili kumnufaisha mkulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la kahawa ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambalo Serikali imeamua kuboresha mazingira ya uzalishaji pamoja na masoko ili kumnufaisha mkulima. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imeimarisha usimamizi katika uzalishaji na kuboresha mifumo ya masoko. Bei ya mazao ya kilimo ikiwemo kahawa inategemea nguvu ya soko kwa kuzingatia mahitaji na ugavi wa uzalishaji duniani. Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Kahawa imeruhusu na kuratibu uuzwaji wa kahawa moja kwa moja yaani *direct export* kwenye masoko ya Kimataifa yenye bei nzuri kuliko mnadani kwa kufuata Sheria na Kanuni zilizopo kwa kahawa maalum yaani Kahawa ya Haki yaani *fair and organic coffee* na kahawa zingine zenye mahitaji na masoko maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya biashara ya zao la kahawa, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pomoja na kuamua kuanzisha minada ya kahawa kwenye maeneo ya uzalishaji kuanzia msimu wa mwaka 2019/2020. Lengo la utaratibu huo ni kuharakisha malipo na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa minada na kuwashirikisha wakulima wengi zaidi katika mikoa inayozalisha zao la kahawa ukiwemo Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa naibu Spika, Serikali pia imedhibiti makato yasiyo na tija kwa wakulima na yanayokatwa kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika na Vyama vya Msingi ili kubaki na makato yanayolenga kuendeleza zao la kahawa. Aidha, kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB),* Serikali imewezesha Vyama vya Ushirika vya Kahawa vikiwemo Vyama vya Mkoa wa Kagera kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kufanikisha shughuli za ukusanyaji na uuzaji wa kahawa ya wakulima, hivyo kumpunguzia mkulima mzigo wa riba uliokuwa unatozwa na mabenki ya kibiashara kwani *TADB* inatoza riba ya kiwango cha asilimia nane ukilinganisha na benki za kibiashara zilizokuwa zinatoza na zinazotoza riba ya asilimia 18 hadi 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mikakati hiyo, Serikali imefuta tozo na kupunguza viwango vya makato mbalimbali vilivyokuwa vinatozwa kwa wakulima ikiwemo pamoja na kupunguza tozo zinazotozwa katika biashara ya kahawa pamoja na kupunguza viwango vya makato mbalimbali vilivyokuwa vinakusanywa kwa mkulima. Aidha, Serikali pia imepunguza kiwango cha ushguru wa mazao unaotozwa na mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu ya bei ya kahawa ya shambani. Kwa kufanya hivyo, wakulima wa kahawa Mkoani Kagera na mikoa mingine watapata bei nzuri na hivyo kuongeza mapato yao na kuinua uchumi wa Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benardetha Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na mikakati mizuri na mingi ya Serikali, lakini bei ya kahawa ya mkulima Mkoani Kagera bado ni Sh.1,000 kitu ambacho kinamuumiza mkulima. Kwa kuwa soko la kahawa linategemea soko la dunia, linategemea mauzo nje ya nchi, mahali ambapo mkulima wa kawaida au Vyama vyetu vya Ushirika hivi vya Msingi hawana uwezo wa kuyafikia hayo masoko. Pia kwa kuwa msimu unaofuata wa kahawa unaanza hivi keshokutwa mwezi wa Tano, ili makosa yasijirudie mkulima akaendelea kulipwa 1,000, je, Taasisi za Serikali ambazo zinahusika na utafutaji wa masoko wana mipango gani ya kwenda kule nje ya nchi wakawatafutia Watanzania masoko ikiwezekana wakaingia na mikataba na nchi hizo ili Watanzania wauze kahawa zao na waweze kupata bei nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwenye baadhi ya *super market* huko China imeonekana kahawa ambayo inaonekana imetoka Uganda imekaangwa tu haijasindikwa zaidi ya hapo na ikawekwa kwenye kifungashio kizuri, robo kilo inauzwa kwa dola 40 ambayo ni zaidi ya *Tanzanian Shillings 88,000* wakati sisi mkulima anapata 1,000 kwa kilo.

Je, Wizara zinazohusika kama Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, wanawaandaaje Watanzania kwa maana ya wakulima na wafanya biashara wasindike kahawa badala tu ya wakulima kuuza zile zilizo ghafi kusudi Mtanzania aweze kupata bei nzuri na hasa hasa mkulima kutoka Mkoa wa Kagera?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mushashu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua mikakati iliyopo kwa ajili ya kuongeza bei ya mkulima kutoka Sh.1,000 wanayolipwa sasa mpaka ile ambayo itaridhisha na kukidhi gharama za uzalishaji. Kwanza kwa niaba ya Serikali, Wizara ya Kilimo, baada ya kuona changamoto hiyo ya zao la kahawa, bei yake na mazao mengine, tumeanzisha Kitengo cha Utafiti wa Biashara na Masoko ambacho kimeanza kazi tangu tarehe Mosi Julai, 2018. Lengo la kitengo hiki ni kuratibu na kufuatilia mwenendo wa masoko duniani na kutoa taarifa sahihi kwa wakulima wetu wakishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili tunashirikiana kwa karibu sana na Balozi zetu zilizokuwa nje. Hapa nichukue nafasi kumpongeza sana Balozi wetu wa China, Ndugu Kairuki kwa kazi kubwa anayoifanya na ameweza kutupatia soko jipya la kahawa nchini China lakini pia na Mabalozi wa nchi nyingine kama za Japan, Ujerumani, wote hawa wamekuja na mikakati mizuri na kupanua soko la kahawa yetu inayotoka hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anataka kujua kwamba mikakati ya kuongeza thamani ya mazao

yetu ikiwemo kahawa ili kahawa hii badala ya kuuzwa ghafi tuweze kuiuza wakati imechakatwa. Kwanza niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa muono huu, lakini nataka nimwambie kwamba Serikali tulishaanza muda mrefu mipango hii na ndiyo maana siyo kwa zao tu la kahawa, hata korosho umeona mwaka huu tumeanza kubangua na mwakani *Insha Allah* tutabangua zaidi ya asilimia 50 kwenda juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la msingi la kahawa; pia tulishaanza kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vyetu na kiwanda kimojawapo cha Amir Hamza kimeshaanza kuchakata kahawa ya Mkoani Kagera kwa ajili ya kuiuza kahawa iliyokuwa imeshachakatwa badala ya kuuza kahawa ghafi. Pia kwa wakulima hawa tunaendelea kuwasisitiza wajiunge kwenye vikundi vyao vya ushirika ili Serikali tuweze kuwasaidia kwa ukaribu kwenye umoja wao kuongeza mitaji na kununua mashine ndogo ndogo za kuchakata mazao yao, kuuza mazao ya kahawa iliyosagwa badala ya kuuza kahawa ghafi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mwaka jana kwenye msimu wa kahawa, Serikali ilitangaza bei elekezi Sh.1,400 lakini wakulima wamelipwa Sh.1,106. Ni kwa nini wamelipwa hiyo badala ya bei elekezi iliyoelekezwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafsi hii. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bilakwate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kupitia Bodi ya Kahawa, mwezi Julai mwaka jana ilitangaza bei elekezi ya Sh.1,400 ya kahawa. Bei elekezi ni bei ya chini anayotakiwa kulipa mkulima maana yake kama tungeruhusu wafanyabiashara binafsi kununua, lakini kahawa hii haikununuliwa na wafanyabiashara binafsi, ni wakulima wenyewe kupitia Vyama vyao vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika waliamua kwenda kuuza kahawa yao kule mnadani Moshi. Kwa hiyo kama wakulima wenyewe kupitia vyama vyao ndiyo waliamua kwenda kuuza kule baada ya kukusanya kahawa yao, kwa hiyo wanakwenda kulipwa kutokana na bei waliyouza kwenye mnada, siyo bei iliyotangazwa ile elekezi kwa sababu hakuna mfanyabiashara binafsi aliyenunua kwa wakulima kule Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hivi Vyama vya Ushirika siyo wafanyabiashara bali wanakusanya kwa niaba ya wanachama wenzao, kwa niaba ya wakulima wenzao baadaye wanakwenda kuuza kwa pamoja kule Moshi na ndiyo maana kwamba sasa hivi kutokana na myumbo wa bei mwaka jana, bei ilishuka kwenye soko la dunia na ikaathiri mnadani pale Moshi na ndiyo maana sasa bei hiyo wanakwenda kulipwa kwa kuzingatia bei iliyouzwa hiyo kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Bulembo swali la nyongeza.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri anayejibu maswali kule Kagera walifika na wakafanya mambo lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa bei elekezi kama alivyouliza Mheshimiwa Bilakwate kahawa ikauzwa kwa Sh.1,000, huku Karagwe hamna shida lakini ukija Muleba, Bukoba Vijijini, Misenyi bei ya Sh.1,000 watu hawajalipwa

mpaka leo, mnasubiri nini? Si muende kama milivyoenda kwenye korosho watu wapate haki zao? Kahawa ipo kwenye maghala lakini mpaka leo watu hawajalipwa na ninyi Wizara ya Kilimo mmenyamaza. Nataka nipate majibu, ukienda Muleba, Chama cha Msingi Magata, Misenyi, Katoro, Kaibanja, Kazinga watu wana shida na kahawa mmeshachukua na hela hawajalipwa, ni lini watalipwa hela zao?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Alhaj Abdallah Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, sisi Serikali hatujanunua kahawa ya wakulima wa Tanzania popote pale. Wakulima hawa kwa kupitia vyama vyao vya msingi na vyama vikuu waliamua kwa hiari yao kwenda kuuza kahawa wenyewe kule mnadani Moshi. Kilichotokea kwenye Wilaya hizi alizozitaja Muleba, Bukoba na Bukoba Vijijini na sehemu nyingine ni kwamba kahawa yao wameshakoboa, wamefika pale Kilimanjaro Moshi kama nilivyosema kutokana na kuyumba kwa bei kwenye soko la dunia na uzalishaji mkubwa uliotokea kwa nchi ya Brazil kuingiza sokoni zaidi ya magunia milioni saba mwaka jana ikaathiri bei nzima ya kahawa na kusababisha bei kushuka chini mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu walienda kuuza wenyewe maana yake ile bei imewakuta wao moja kwa moja. Kilicholewesha mpaka sasa kutolipwa fedha zao ni hiki Chama cha *KCU* hakijauza kahawa yote. Kwa hiyo, sehemu nyingine hawajalipwa kwa sababu wenyewe hawajauza kahawa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na

Watoto, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 92

**Makundi yenye Msamaha wa Gharama za Matibabu**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Sera ya Afya imebainisha makundi yenye msamaha wa matibabu ambayo ni wazee kuanzia miaka 60 na kuendelea, watoto chini ya miaka 5, watoto wanaoishi na TB na UKIMWI:-

Je, ni lini Serikali itaweka Watu wenye Ulemavu kuwa miongoni mwa watu wanaohitaji msamaha wa gharama za matibabu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mhesimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 na kuandaa mapendekezo ya Sera mpya ya Afya. Katika mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 changamoto mbalimbali za matibabu kwa makundi ya msamaha ziliibuliwa na watoa huduma pamoja na watumiaji huduma hizo. Moja ya changamoto iliyojitokeza ni hospitali zetu kuwa na wagonjwa wengi wa msamaha na hivyo kushindwa kuboresha huduma za afya. Kutokana na changamoto hiyo ya kuwa na makundi mengi ya msamaha, Wizara iliona ni vyema ikaboresha utaratibu wa msamaha kwa kuhakikisha kuwa watu wasio na uwezo tu ndiyo wanaopatiwa msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo ya Sera mpya na Afya kila mwananchi mwenye uwezo atapaswa kugharamia huduma za afya. Sera pendekezwa inaainisha njia mahsusi zitakazowezesha Serikali kubaini wananchi wote wenye uwezo ili waweze kuchangia gharama kabla ya kupokea huduma, kwani ni wazi kuwa si kila mlemavu ana kipato duni. Hivyo, wananchi watakaothibitika katika maeneo yao kuwa hawana uwezo wa kuchangia wakiwemo walemavu wataendelea kupatiwa matibabu bila kuchangia gharama za matibabu. Aidha, Serikali inatambua changamoto ya uchangiaji wa huduma za afya na inaandaa utaratibu wa bima ya afya kwa Watanzania wote ikiwa ni pamoja na kundi la walemavu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda Serikali isikwepe wajibu wake wa kuhudumia watu wasiojiweza. Natambua kabisa kuwa kuna walemavu wenye uwezo lakini watu wengi wenye ulemavu wana matatizo mengi; kuna wale ambao ni yatima, kuna wengine ambao wametelekezwa na kuna wengine ambao kaya zao ni maskini sana. Ni kwa nini Serikali isiwajibike kuwahudumia watu hawa wenye ulemavu hasa kwa kuwatambua na pili kuwapatia bima ya afya bure? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema wagonjwa kuna wagonjwa wengi sana wa msamaha ambao wako katika hospitali zetu. Sawa wako wagonjwa wengi lakini ni lini Serikali sasa itatekeleza wajibu wake wa kutoa ruzuku katika hospitali zetu za mikoa au hospitali zetu za rufaa kwa sababu hawa wagonjwa ambapo wengine ni watu wenye ulemavu,

watoto umri chini ya miaka mitano na wazee wanakwenda katika hospitali hizi kutibiwa na hizi hospitali zinakuwa na watu wengi ambao wanatakiwa kupata vifaatiba na vitendanishi? Ni lini Serikali itatoa ruzuku katika hospitali zetu ili ziweze kujikimu na kutoa huduma bora? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Serikali inaendelea kutoa huduma za afya na haijawahi kusitisha kutoa huduma ya afya kutokana na sababu eti kwamba mtu anashindwa kugharamia matibabu. Hilo lipo vizuri ndani ya Sera yetu ya Afya na kuna makundi ambayo tumeyaainisha katika sera ambapo watu wanapata matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la walemavu kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, si kila mlemavu hana uwezo wa kupata matibabu, nataka niweke msisitizo. Ndiyo maana nimesema katika Sera hii Mpya tutaweka utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya sasa kati ya asilimia 60 - 70 ya wagonjwa ambao wanafika katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya wanapata matibabu bure. Sasa hivi tunataka tuweke mfumo mzuri na kuhuisha na mifumo mingine kama ile ya *TASAF* kuhakikisha kwamba tunawatambua tu wale ambao kweli hawana uwezo na wanahitaji kupata matibabu. Tutakapokuja na huu utaratibu wa bima ya afya kwa wananchi wote tutakuwa na kundi dogo sana ambalo limebaki ambalo litakuwa linagharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza kwa nini Serikali haipeleki ruzuku. Nimthibitishie Mheshimiwa

Mbunge na bahati nzuri naye ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na analijua na hivi karibuni tumetoa taarifa ya utekelezaji ya nusu mwaka, Serikali inapelekea mishahara hatujashindwa kupeleka mishahara, dawa na hela ya uendeshaji. Hakuna hospitali ya rufaa ya mkoa ambayo haijapata huduma zote hizo ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuna vyanzo vingi vya mapato ndani ya hospitali. Pamoja na ruzuku ya Serikali tuna fedha za papo kwa papo, fedha za bima na nyingine zinapata *basket fund*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Kuwawezesha Wachimbaji wa Madini Kata ya Mandamera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Wakazi wa Kitongoji cha Mafulungu kilichopo katika Kijiji cha Ilangali, Kata ya Manda wanajishuhgulisha na uchimbaji wa madini.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wakazi hao ili shughuli zao za uchimbaji ziwe za ufanisi na zenye tija?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Manda, Kijiji cha Ilangali, Kitongoji cha Mafulungu, Wizara ilishatoa

leseni 16 za wachimbaji wadogo wa madini ya jasi (*gypsum)* zilizotolewa kuanzia mwaka 2014 hadi 2016. Hadi sasa Tume ya Madini imepokea maombi 32 ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini ya jasi kutoka katika eneo hilo. Maombi 16 yapo katika hatua za mwisho za kutolewa leseni na maombi 16 bado hayajakamilisha vigezo vya kupatiwa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwahamasisha wakazi wa Mafulungu kujishughulisha na uchimbaji wa madini sambamba na kutunza kumbukumbu za uzalishaji na mauzo ili waweze kuaminika na kukopeshwa na taasisi za fedha. Aidha, nawashauri wachangamkie fursa ya uwepo wa madini hayo katika kitongoji chao kwani mahitaji yake ni makubwa hasa katika viwanda vya saruji nchini na nchi za nje baada ya Serikali kuzuia uingizaji wa madini hayo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini inaendelea kutoa elimu kwa wamiliki wa leseni kuhusu uchimbaji bora wa madini ya jasi na kuwataka kuchangia miradi ya maendeleo katika jamii kwenye maeneo yanayowazunguka katika migodi yaani kwa maana ya *Corporate Social Responsibility* kwani ni takwa la kisheria kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 105 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Waziri wake kwa namna ambavyo wanafanya kazi kwenye Wizara hii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa eneo lile na Tarafa nzima ya Mkwayungu limegundulika kuwa na madini mengi sana ya *gypsum* na dhahabu kwa upande

wa Mafulungu na ninyi Serikali mlikuwa mmeona kabisa watu wanachimba na wanapata fedha na nyie mnapata kodi lakini baadaye mlisimamisha uchimbaji wa madini ya *gypsum*. Je, ni lini Serikali itawafungulia wale wachimbaji wengine ili waendelee kuchimba na nyie muendelee kupata mapato na wananchi waendelee kufanya kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami ili twende tukajionee hali halisi ya watu wanaochimba dhahabu Mafulungu na wale wanaopata tabu ya kuchimba madini ya *gypsum* pale Manda ili tukaone na tukatatue matatizo yao kwa macho huku akishuhudia? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu nimpongeza Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa kuweza kufuatilia mambo ya wapiga kura wake na hasa wachimbaji wa maeneo ya pale Manda. Kwa kweli Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wachimbaji wa *gypsum* eneo la Manda na Mafulungu ni kweli walikuwa wamesimamishwa kwa sababu hawakufuata taratibu ambazo zilikuwa zimewekwa na Tume ya Madini katika uchimbaji huo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda na watafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwataarifu wachimbaji wote wa *gypsum* na wachimbaji wengine wote Tanzania, madini ya *gypsum* tuliyazuia kwa maana ya madini ghafi kuyapeleka nje ya nchi, naomba wapitie *GN* Na.60 ambayo tumeitoa siku ya tarehe 25 Januari, waangalie ile *GN* ambayo imetoa mwongozo wa madini yote,

wanachenjua katika kiwango gani na kiwango kipi ambacho kinaruhusiwa kutoa nje ya nchi. Wakishapitia mwongozo huo wachimbaji watakuwa hawapati shida tena katika kufanya biashara hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Mbunge ameomba niongozane naye kwenda katika eneo la Manda kuangalia changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo. Nimhakikishie baada ya Bunge hili niko tayari kuongozana naye twende tukaangalie changamoto zinazowakabili wachimbaji wa Manda tuangalie namna ya kutatua changamoto hizo vilevile tuwawezeshe wachimbaji hawa waweze kuchimba wapate faida na waweze kufanya biashara hiyo ya madini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Kijiji cha Kwahemu, Kata ya Haneti, kuna vikundi 16 ambavyo vina wachimbaji zaidi ya 200 lakini havina maeneo ya kuchimba madini licha ya kupeleka maombi Tume ya Madini. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuwapa maeneo wachimbaji hawa wadogo ili waweze kujikimu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maeneo ya Kwahemu (Haneti), kuna uchimbaji mdogo mdogo wa madini ya vito. Katika eneo lile kuna leseni moja inamilikiwa na Bwana Dimitri, raia mmoja wa kigeni lakini kuna maeneo mengine ambayo yako katika utafiti kwa maana ya *PL.* Kama nilivyosema siku zilizopita ni kwamba tunafuatilia zile *PL* zote

ambazo hazifanyiwi kazi tutazichukua na tutazifuta na tutawapa wachimbaji wadogo wadogo waweze kuchimba na waweze kujipatia riziki kama tulivyojipangia katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge watu wa Kwahemu maeneo ya Haneti tuna mpango kabambe wa kuwapa maeneo ya kuchimba. Wale wachimbaji walioko pale nilishafika na wakatoa kero zao na mimi kwa kweli naendelea kuzifuatilia kwa maana ya kuzitatua na tunahakikisha kwamba hawa watu wa Kwahemu watapata leseni na wataweza kupata nafasi ya kuchimba.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 94

**TANESCO Kupewa Hadhi ya Kiwilaya – Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Mji wa Itigi unakua kwa kasi na umeme umeenda vijiji vya Lulanga, Itagata, Ukimbu, Chabutwa, Mtakuja, Makale na Mitundu ambapo ni kilomita 71; kwenda Itigi hadi Mwamagembe ni zaidi ya kilomita 130:-

(a) Je, Serikali haioni ni vema sasa kuipa *TANESCO* hadhi ya Kiwilaya katika Wilaya ya Itigi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi wa Shirika la Umeme katika Jimbo la Manyoni Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary

Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta ufanisi katika kuwahudumia wananchi wa Mji wa Itigi katika Jimbo la Manyoni Magharibi mwaka 2003 *TANESCO* ilianzisha Ofisi ndogo ya Itigi kwa lengo la kuongeza huduma za umeme kwa wananchi. Aidha, *TANESCO* imekuwa ikifungua ofisi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wake katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile Ofisi hizo zimekuwa zikipandishwa hadhi kutoka ofisi ndogo hadi kuwa Ofisi za Wilaya na Mkoa za *TANESCO* kwa kuzingatia mahitaji ikiwa pamoja na kukua kwa shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa *TANESCO* imefungua ofisi katika Mji wa Itigi kwa ajili ya kuwahudumia wateja katika hadhi ya ofisi ndogo. Hata hivyo, *TANESCO* imeanza taratibu za kupandisha ofisi hiyo hadhi ili kuwa ofisi ya *TANESCO* ya Kiwilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya *TANESCO* Itigi inasimamiwa na *Techinician* na watumishi wengine 11. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, *TANESCO* inatarajia kuongeza watumishi wengine watano pamoja na Mwandisi ili kuwahudumia wateja wa maeneo yote ya Itigi ikiwa ni pamoja na wateja kutoka Vijiji vya Lukanga, Itagata, Ukimbu, Chabutwa, Mtakigi, Makle, Mitundu na Mwamagembe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya wananchi lakini dhamira ya Serikali ya kupeleka umeme vijijini kwa maana

ya *REA* utekelezaji wake umekuwa mdogo na unasuasua sana. Katika Jimbo langu kuna vijiji vya Kashangu, Jeje, Idodyandole, Ipangamasasi, Mbugani, Agondi, Mabondeni, Kitopeni, Ipande, Muhanga, Damwelu, Kitalaka, *Kaskazi Station*, Kintanula na Rungwa havina umeme. Je, nini kauli ya Serikali kwa wananchi wa vijiji hivi wategemee lini kupelekewa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa umeme wa Mkoa wa Singida unakwenda hadi katika Wilaya ya Manyoni pamoja na Itigi lakini hatuna *substation* ipo *station* moja tu kubwa kule Singida. Je, Serikali iko tayari sasa kuweka *substation* Itigi kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii ya umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi. Kwanza, nimpe pole kwa ajili ambayo aliipata na namwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema. Pamoja na changamoto hiyo ya afya Mheshimiwa Massare ameendelea kulitumikia Jimbo lake hususani katika sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yake mawili ya nyongeza, la kwanza lilijielekeza katika utekelezaji wa mradi huu wa *REA III.* Katika Wilaya ya Manyoni *REA III,* mzunguko wa kwanza kuna vijiji 30 na Jimbo lake lina vijiji 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge mkandarasi yupo anaendele na kazi katika maeneo ya Manyoni Mashariki katika Vijiji vya Majengo, Selia, lakini kwa kuwa, yeye Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake la Manyoni Magharibi ameuliza utekelezaji, nataka nimtaarifu hata asubuhi hii nimeongea na mkandarasi, ameshaanza kupeleka vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kutokana na utatuzi wa changamoto ambazo zilikuwa zinaukabili mradi. Mradi vizuri, sasa hivi unaendelea vizuri kwa sababu, mpaka sasa tunavyozungumza mpaka Januari vijiji takribani 5766 vimeshapata umeme kutokana na utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameulizia juu ya ujenzi wa *substation* katika eneo la Itigi Manyoni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Singida tuna *substation.* Kutokana na mipango ya Serikali na ujenzi ulioanza wa *line* ya Kv 400 kutoka Singida mpaka Namanga, Serikali ina mpango wa ku-*upgrade* Kituo cha Singida. Kwa hiyo, nataka nimtaarifu kwamba, kutokana na matengenezo yatakayoendelea tutakipandisha hadhi Kituo cha Singida, ili kuhimili umeme mkubwa utakaosafirishwa mpaka Namanga, hivyo ni wazi kwamba, Mkoa mzima wa Singida kuhusu changamoto ya labda pengine usafirishaji wa umeme haitakuwpo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge aendelee tu kuiunga mkono Serikali, mipango ya kupandisha hadhi *substation* ya Singida inaendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maftah, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kujua mara nyingi nimekuwa naongea Vijiji vya Manispaa ya Mtwara Mjini nimekuwa nikivitaja vijiji hivi katika Bunge hili miaka yote mitatu na Serikali ikiwa inaahidi kwamba, inatekeleza suala la kupeleka umeme. Vijiji hivi ni Mkangara ambako Naibu Waziri alishaenda kule na akaona hali halisi, Naulongo, Mkunjanguo, Namayanga na maeneo...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Maftah, uliza swali.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujua kwa nini Serikali haitaki kutenga bajeti ili kupeleka umeme katika vijiji hivi au mitaa hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maftaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo yeye mwenyewe amekiri kwenye swali lake la nyongeza kwamba, mimi hata pamoja na Waziri wa Nishati tumeshafanya ziara zaidi ya mara mbili katika Mkoa wa Mtwara. Maeneo ambayo ameyataja ikiwemo Mkangara, Chipuputa na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi hata *TANESCO* Mkoa wa Mtwara imekuwa ikijitahidi kufanya miradi. Nilipofanya ziara mwaka jana zaidi ya mitaa saba *TANESCO* imefanya miradi, lakini kwa eneo maalum ambalo ni maeneo aliyoyataja yameshaingia kwenye mpango wa utekelezaji wa mradi wa ujazilizi unaoanza Machi, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, hata alipofanya ziara Mheshimiwa Waziri wa Nishati pia ametoa maelekezo yale ambayo tuliyaelekeza siku za nyuma na kwa kuwa Mtwara imepitiwa na bomba la gesi na Serikali ilitoa punguzo kwa ajili ya kuwasambazia umeme wananchi wa maeneo ya gesi na mitaa mingi ipo katika Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge ambaye amekuwa akifuatilia mara kwa mara kwamba, vijiji, mitaa aliyoitaja na vijiji katika Manispaa ya Mtwara Mikindani na maeneo ya Mtwara vitapatiwa umeme na kazi zinaendelea na mradi wa ujazilizi utaanza mwezi Machi, 2019. Ahsante sana.

Na. 95

**Hitaji la Umeme wa Gridi ya Taifa – Tarafa ya Nguruka**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

Tarafa ya Nguruka ina wakazi zaidi ya 100,000 na ndio kitovu cha biashara:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka umeme wa *Grid* ya Taifa kutoka Usinge, Wilaya ya Kaliuwa?

(b) Wakazi wa Kata za Mwambao, Sunuka, Kaliya, Buhigu, Igalula, Haramba na Sigunga hawana umeme na Jiografia ya kuwaunganishia umeme kutoka Uvinza ni ngumu. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka umeme kutoka Mpanda, Mwese kwenda Kata ya Kaliye, ili iwe rahisi kuzipitia kata zingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye Sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 katika Mikoa ya Kusini Magharibi, ikiwemo Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma kwa lengo la kuwaunganisha wananchi wa maeneo hayo na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za awali Serikali kupitia *TANESCO* kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika imeanza kutekeleza mradi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 *North West Grid Kv* 400, Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi wenye urefu wa kilometa 1,372. Kwa sasa Benki ya Dunia imeshatoa dola za Kimarekani milioni 455 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji wa mradi huu Serikali kupitia *TANESCO* mwezi Disemba, 2018 imeanza kutekeleza mradi wa kuunganisha Mkoa wa Kigoma na *Grid* ya Taifa kutoka Mkoa wa Tabora. Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora, Urambo, Usinge – Kaliua, Nguruka hadi Kidahwe Kigoma Mjini wenye urefu wa kilometa 370. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya 132/33 *Kv* katika Miji ya Urambo na Nguruka. Gharama ya kazi hiyo inakadiriwa kufikia dola za kimarekani milioni 81 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mradi huu na miradi mingine inayoendelea kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Kigoma ikiwa ni pamoja na kuwasambazia wananchi umeme katika Kata za Mwambao, Sunuka, Kaliya, Buhigu, Igalula, Haramba na Sigunga. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasna Mwilima, swali la nyongeza.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, natambua kazi nzuri wanayoifanya. Ni kweli kabisa kwamba, Nguruka pale tulitoa ekari 30 kwa ajili ya ujenzi wa hiyo *substation,* lakini Meneja wa *TANESCO* alienda, hadi leo utekelezaji haujaonekana. Sambamba na hilo mwaka jana mwezi wa Nane mkandarasi alifanya *survey* katika Kata ya Nguruka, Kata ya Mtego wa Noti, Kata ya Itebula, Kata ya Mganza, Kata ya Sunuka, sambamba na vijiji ambavyo vilisahaulika kwenye Mradi wa *REA* awamu ya pili. Swali langu. Je, Wizara hii mnawaambia nini wananchi wa kata hizi, ni lini mkandarasi atapeleka *materials* ili sasa utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu uweze kuanza rasmi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, natambua kwamba, kuna mazungumzo baina ya mwekezaji kutoka Marekani pamoja na Wizara ya Nishati

kufua umeme kwenye Mto Ruwegere uliopo kwenye Kijiji cha Mgambazi, Kata ya Igalula. Sasa wananchi wa Kata ya Buhingu, Kata ya Herembe, Kata ya Sigunga na Kata ya Igalula yenyewe wanataka kusikia Kauli ya Serikali. Ni lini sasa mkandarasi huyu ataanza rasmi kutekeleza uzalishaji wa kufua umeme kwenye Mto Ruwegere, megawati tano? Nataka majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi wa swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge kwa vile ambavyo amelieleza. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge jinsi ambavyo anafuatilia masuala ya nishati kwa wananchi wa Uvinza. Baada ya kusema hayo napenda sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mbunge wa Maeneo ya Uvinza, Jimbo la Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kabisa mkandarasi alipata kazi dakika za mwisho ukilinganisha na mikoa mingine. Hata hivyo, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na jinsi anavyofuatilia, hivi sasa mkandarasi ameshaanza ku-*order materials* na ataanza kupeleka *materials* kwenye eneo la Uvinza kuanzia tarehe 22 mwezi huu. Maeneo yatakayopelekewa ni pamoja na Kazuramimba, Ilagala, Kajeje kuelekea Sunuka, lakini pia maeneo ya Nguruka na katika maeneo mengine ya Uvinza ambayo hayajapelekewa nishati ya umeme. Maeneo yote 27 ya kwa Mheshimiwa Mbunge yatapelekewa umeme ndani ya miezi tisa ijayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nimpe tu uhakika kwa wananchi wa Uvinza kwamba, mkandarasi amesha-*mobilise material* na kuanzia tarehe 22 mwezi huu ujenzi utaanza rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la pili, ni kweli kulikuwa na mkandarasi aliyetarajia kufanya *survey* kwa ajili ya kuzalisha umeme megawati nane katika Mto

Rwegere, lakini taarifa za awali baada ya kupewa kazi na baada ya kufanya tathmini za awali inaonesha Mto Rwegere unaweza kutupatia megawati tano kutokana na maporomoko ya maji ya Mto Rwegere.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi inayofanyika mara baada ya kuleta taarifa mkandarasi amefanya mapitio na wataalam wetu, ni matumaini yetu kwamba, mwezi ujao atatuletea taarifa za mwisho, ili kuona kama mradi huo utakuwa na tija na kuzalisha megawati tano. Kwa hiyo, nimpe pongezi Mheshimiwa Mbunge kwamba, hiyo kazi inatushirikisha sana, inaendelea vizuri na tunaweza tukapata megawati tano mbali na megawati 45 za Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani kidogo niongeze kwenye mradi muhimu sana kwa Kigoma, ujenzi wa *transmission line* kutoka Tabora kupita Urambo kwenda mpaka Nguruka hadi Kidahwe umeshaanza. Tunatarajia mkandarasi atakamilisha kazi Februari mwakani ili wananchi wa Kigoma waweze kupata umeme wa gridi nao kutoka umeme wa gridi unaotoka Tabora wa kilovoti 120. Nimeona nilifafanue kwa sababu, sasa hivi *clearance* ya *major substation* inafanyika Urambo na wiki inayokuja itafanyika Nguruka na Kidahwe wanamalizia mwezi ujao. Hiyo ni taarifa kwa ajili ya umeme wa wananchi wa Kigoma. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 96

**Bajeti ya Upimaji Ardhi Nchini (2010 – 2015)**

**MHE. RUTH H. MOLLEL** aliuliza:-

Ardhi ni rasilimali ya msingi katika nchi yoyote duniani na tamaa ya kupora ardhi imesababisha migogoro na vita:-

(a) Je, Serikali ilitenga bajeti kiasi gani kuanzia mwaka 2010 – 2015 kwa ajili ya kupima matumizi ya ardhi?

(b) Je, kati ya kilometa za mrada 945,000 za Tanzania ni eneo kiasi gani limepimwa hadi Disemba 2015?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Ruth Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa nabu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Namba 6 ya Mwaka 2007, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ni jukumu la mamlaka za upangaji ambazo ni Tume ya Taifa ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi kwa ngazi ya Taifa, Halmashauri za Wilaya pamoja na Halmashauri za Vijiji. Serikali imekuwa ikitenga fedha za kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa Fedha 2010 na 2011 hadi 2014/2015, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitenga na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, wadau wa maendeleo wamekuwa wakiziwezesha mamlaka za uandaaji kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi imekuwa ikiboreshwa mwaka hadi mwaka. Kati ya mwaka 2015 hadi 2018 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitenga jumla ya shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kimetumika kati ya mwaka 2015/2016 na 2017/2018 na kiasi cha bilioni tano kimetengwa kwa bajeti ya Tume kwa Mwaka 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya Tanzania imegawanyika, katika aina tatu ambazo ni ardhi ya kawaida, ardhi ya hifadhi na ardhi ya vijiji. Hadi sasa kuna takribani vipande vya ardhi 2,000 vilivyopimwa ambavyo vinakadiriwa kuwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 141,750 sawa na asilimia 15 ya eneo la nchi. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaendelea na uboreshaji wa kumbukumbu za ardhi ikiwemo takwimu za upimaji ardhi kupitia mfumo unganishi wa kutunza kumbukumbu za ardhi, yaani *ILMIS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa eneo la ardhi ya nchi lililopimwa linaongezeka. Mojawapo ya mikakati hiyo ni mkakati wa kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini ulioanza kutekelezwa mwaka 2016 kupitia programu mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi, yaani *Land Tenure Support Progamme,* katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi Mkoani Morogoro. Ni matarajio ya Wizara kuwa, kupitia mkakati huu idadi ya vipande vya ardhi vilivyopimwa itaongezeka na hivyo kupunguza eneo la nchi ambalo halijapimwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ukiangalia bajeti ambayo imekuwa ikitengwa kila mara kwa ajili ya hii kazi ya kupima matumizi ya ardhi ni ndogo sana. Mpaka sasa miaka 57 ya uhuru tumepima asilimia 15 tu ya nchi ya Tanzania na migogoro bado ni mingi kila siku kukicha kuna migogoro. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba, kwa *style* hii migogoro haitaisha na kwamba, nchi itakuwa haina amani na utulivu kwa sababu ya migogoro ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni mikoa mingapi ambayo mpaka sasa hivi imeanzisha Benki za Ardhi

ili kurahisisha uwekezaji na pia kuwawezesha wakulima wakubwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Nyongeza ya Mheshimiwa Ruth Mollel kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anasema bajeti ni ndogo kiasi kwamba, migogoro bado inaongezeka kuwa mingi na huenda pengine ikasababisha kutokuwa na amani. Katika jibu langu la msingi nimeonesha takwimu ikionesha bajeti ilianza kiasi gani na sasa iko kiasi gani. Ilianza na bilioni 1.5 lakini sasa hivi tumefikia bilioni 6. 3. Kwa hiyo, ni vitu ambavyo vinaongezeka mara kwa mara, lakini kama hiyo haitoshi Wizara yangu inalo jukumu la kuwezesha halmashauri katika kuwapa uwezo wa kuweza kusimamia masuala ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuhakikisha kwamba, eneo lote linapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii imekuwa ikifanyika na mpaka sasa tunapoongea jumla ya vijiji 1,880 vimekwishafanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi na sasa hivi tunazo wilaya kama 40 ambazo mpango bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo ni kwamba, pale ambapo halmashauri zinawezeshwa tuna imani kwamba, zoezi la upimaji litaendelea na sio kusubiri Wizara kwa sababu, sheria yenyewe inatamka wazi kwamba, mamlaka za kupanga na kupima maeneo ni halmashauri zetu za wilaya na vijiji katika maeneo. Kwa hiyo, ni jukumu pia la halmashauri zetu na sisi pia tukiwa ni washiriki katika mabaraza yetu, basi tusimamie zoezi hilo ili kila halmashauri iweze kutekeleza wajibu wake ambao inapaswa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu kuainisha ni mikoa mingapi, naomba swali hili nisimjibu kwa sababu linahusu takwimu, pia niweze kuwa na uhakika ni kiasi gani, nisije nikampa jibu lisilo sahihi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kupanga na kupima kila kipande cha ardhi. Ndio maana mwaka huu tumeamua kuandaa mradi mkubwa ambao utatuwezesha katika miaka mitano hii tuwe tumekamilisha upimaji na upangaji, upangaji na upimaji kila kipande cha ardhi nchini. Kwa hiyo, pamoja na hiyo fedha ya bajeti ya Serikali ya kawaida tumeamua tukope kwa sababu, ina faida kubwa zaidi kwa kupanga na kupima nchi nzima kwa wakati mmoja kwa sababu, vilevile tunajua itatusaidia katika kupata mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwananchi akimiliki kwa hati, atalipa kodi kila mwaka, kwa maana hiyo kila mtu atafaidika na upangaji na upimaji. Kwa hiyo, pamoja na hiyo ya bajeti, lakini Serikali tumeamua kuanzisha huo mradi mkubwa wa kupanga na kupima kila kipande cha ardhi na mradi huo utaanza mwaka huu baada ya Bajeti ya Serikali ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza majaribio wilaya tatu, Kamati yetu ilikwenda juzi kuangalia namna tunavyoweza kufanya. Wameridhika na taarifa imetolewa jana kwamba, jambo lile linawezekana tukiwa na uwezo wa kutosha. Kwa hiyo, kutokana na ule mfano tulioufanya katika Wilaya tatu za Mkoa wa Morogoro tunataka kuusambaza nchi nzima mijini na vijijini. Kwa hiyo, jambo hilo Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge tunalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumefanya uwezeshaji mikoani kwa kununua vifaa, jambo moja linalowafanya Halmashauri washindwe kupima na kupanga ni vifaa. Serikali, kupitia Wizara yangu, tumeshanunua vifaa vya kutosha vya upimaji ambavyo kila halmashauri inayotaka kupanga na kupima maeneo waende kwenye kanda wakaazime bila kukodisha ili viwasaidie katika zoezi la upangaji na upimaji kwenye wilaya zao.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Amina Mollel.

Na. 97

**Miradi Mikubwa ya Maji – Kibaha**

**MHE. AMINA S. MOLLEL (K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA)** aliuliza:-

Kuna miradi mikubwa ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ambayo hadi sasa haijakamilika. Miradi hiyo ipo Kijiji cha Mperamumbi Kata ya Kwala, Kijiji cha Boki Mnemera Kata ya Bokomnemera, Kijiji cha Vukunti Kata ya Mlandizi na Kijiji cha Dutumi Kata ya Dutumi:-

Je, ni lini miradi hiyo itakamilika ili kuwaletea matumaini wananchi wa maeneo hayo, hususan akinamama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013, Serikali ilianza kutekeleza miradi ya maji mikubwa katika Vijiji vya Mperamumbi, Kata ya Kwala, Boko Mnemela, Kata ya Bokomnemela na Vukunti, Kata ya Mlandizi vilivyopo

Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha. Utekelezaji wa miradi hiyo imekamilika mwaka 2018 na tayari inatoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi. Miradi hii ina changamoto ya uendeshaji inayosababisha maji kukatwa mara kwa mara kutokana na bili ya maji kuwa kubwa. Kwa kuwa eneo la Kibaha linapatiwa maji na *DAWASA*, Wizara inaangalia uwezekano wa mradi huo kusimamiwa na *DAWASA* na si Jumuiya ya Watumiaji Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Dutumi umekamilika na unatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi na kwa sasa mradi huo unafanyiwa upanuzi kutoka vituo sita (6) hadi kufikia vituo tisa (9) vya kuchotea maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Kijiji cha Kipangege, Kata ya Soga mradi wa maji tayari umeshakamilika lakini hadi hivi sasa wananchi hawajaanza kutumia maji hayo. Je, lini sasa mradi huu utakamilika na kuanza kutoa maji ili wananchi wa Kata ya Soga waanze kufurahia huduma ya maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tatizo hili pia linafanana na tatizo la Wilaya ya Arumeru katika Jimbo la Arumeru Magharibi, Kata ya Bwawani ambapo mradi wa maji tangu enzi za aliyekuwa Mbunge Elisa Mollel na Ole-Medeye ulianza kujengwa mpaka leo hii bado haujakamilika na Serikali imekwishatoa fedha mkandarasi hayupo. Napenda tu kufahamu majibu kutoka kwa Serikali, nisikie kauli yao juu ya mradi huu ili wananchi wa Kata ya Bwawani nao waweze kupata maji na kuondokana na changamoto kubwa iliyopo hivi sasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma kwa kazi nzuri anayoifanya katika Mkoa wa Pwani. Kikubwa sisi kama Wizara ya maji jukumu letu ni kuhakikisha Wanapwani, kwa maana ya Soga, waweze kupata maji safi na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema katika Kijiji kile cha Kipagenge katika Kata ya Soga kuna mradi lakini wananchi hawapati maji. Nataka nimhakikishie baada ya Bunge nitafanya ziara katika eneo hilo la Soga, niangalie ili mwisho wa siku mradi ule uweze kukamilika na wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia dada yangu Amina Mollel amezungumza kwamba sasa mradi umekuwa wa muda mrefu sana, kwamba Serikali imekwishatoa fedha lakini mkandarasi hayupo *site*. Nimhakikishie katika maeneo nitakayotembelea basi na Arumeru Mashariki nitafika na kuhakikisha tunaongeza nguvu katika mradi ule ili wananchi waweze kupata maji safi na salama na yenye kutosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Tatizo la Pwani linafanana kabisa na tatizo lilipo Wilaya ya Magu katika miradi inayoendelea Sola, Kisamba, Bubinza, Matelamuda, pamoja na Kabila Ndagalu na Kitongo Sima, miradi hii imesimama sasa kwa sababu wakandarasi wamesha-*raise certificate* na Wizara tayari inazo taarifa hizo. Je, ni lini Wizara italipa fedha kwa wakandarasi ili miradi hiyo iweze kuendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Kiswaga kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika Jimbo lake la Magu. Tunatambua kwamba utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha. Sasa sisi kama viongozi wa Wizara hatutakuwa kikwazo katika kuwapatia wakandarasi wake fedha. Nimwombe baada ya Bunge tukutane ili tupate zile *certificate* tuangalie namna bora ya kuwapatia fedha ili wakandarasi waendelee na kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Waziri siku za karibuni alitembelea Rombo na walimtembeza kwenye miradi ya Leto, Ngareni na Shimbi Mashariki. Hii ni miradi ambayo ilikuwa katika ile miradi ya *World Bank* ya visima 10 na ni ya siku nyingi na imeshakamilika; na kila Waziri anapokuja Rombo hapelekwi kwenye miradi mingine ni hiyo mitatu tu. Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari kuiagiza halmashauri, maji ambayo yameshapatikana wagawiwe wananchi badala ya kufanya siasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kumjibu mzee wangu hapa; kwamba sisi kama viongozi wa Wizara tunapotoa huduma ya maji tunalinda uhai wa Watanzania na tunapeleka huduma hii kwa wana-CCM na hata Wana-UKAWA. Nataka nimuhakikishie kwa kutibitisha hilo, kwamba hata katika *certificate* tulizozilipa mwaka huu katika mwezi huu zaidi ya milioni 20 tumepeleka katika jimbo lake. Sasa nataka niwaambie wataalam wetu wa Wizara ya Maji, wahakikishe wanapeleka huduma hii muhimu kwa Wanarombo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Halmashauri ya Lindi Vijijini na hasa Jimbo la Mtama tulipanga mwaka huu wa fedha kuchimba visima virefu 25 na fedha zipo, tumeomba kibali toka kibali toka mwezi wa Nane mwaka jana, tukaandika barua kukumbusha mwezi wa Kumi na Mbili lakini mpaka sasa hatujibiwi chochote, tatizo la vibali hivi ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mbunge, Mheshimiwa Nape, nimefanya ziara katika Jimbo la Mtama, ni mmoja kati ya Waheshimiwa Wabunge wanaofanya kazi nzuri sana katika majimbo yao. Sisi kama Wizara ya Maji hatuko tayari kukwamisha jitihada anazozifanya. Nimwombe tu baada ya Bunge tuweze kukutana na Katibu Mkuu ili tuweze kupata vibali hivyo ili wananchi wake waweze kupata huduma ya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagim swali la nyongeza.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyonge. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri sana iliyofanya ya kujenga miundombinu katika Mji wa Musoma kiasi kwamba maji sasa hivi yanapasua mpaka mabomba na maji yanayozalishwa kwa saa ni takribani lita elfu 12, lakini maji yale yanaweza kupelekwa mpaka Wilaya ya Butiama, Kata za Bukaga, Mkanga, Makatende mpaka Bisuma. Vile vile maji haya yanaweza kufika mpaka Jimbo la Musoma Vijijini katika Kata za Etalo, Nyakatende, Nyigima pamoja na Nyamimange. Ningependa kujua, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo ambako chanzo cha maji yaliyoleta maji ya Musoma wanaweza kupata na wenyewe huduma ya maji safi na salama kutokana na chanzo hicho cha maji? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Makilagi kwa kazi nzuri ya kuwatetea Wanamara, lakini kikubwa Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuwekeza mradi zaidi ya bilioni 45 pale Musoma. Kwa hiyo changamoto kubwa ni suala zima la usambazaji, sisi hilo tumeliona na tutahakikisha tunawekeza fedha ili tusambaze maji ili maeneo hayo aliyoyataja yaweze kupata maji safi salama na yenye kutosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Hitaji la Kiwanda cha kusindika Nyanya**

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Seikali ina mkakati gani wa kujenga Kiwanda cha Kusindika Nyanya katika maeneo ya Mto Ngarenanyuki?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya marekebisho kidogo ya Kiswahili sanifu kwenye majibu yangu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa eneo la Mto Ngarenanyuki katika Wilaya za Arumeru na Longido ni miongoni mwa maeneo yanayolimwa nyanya kwa wingi nchini. Ndiyo maana kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tumeendelea kuweka mazingira wezeshi sambamba na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kusindika nyanya. Kwa kuwa ni

muhimu kwa kiwanda kuwa na uhakika wa malighafi za kutosha mwaka mzima namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhamasisha uzalishaji zaidi wa nyanya ikiwezekana zipatikane kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupita *SIDO* imekuwa ikitoa mafunzo ya aina mbalimbali kuhusu ujasiriamali na usindikaji wa mazao ya kilimo. Naomba wananchi wa eneo wa Mto Ngarenanyuki katika Wilaya hizo mbili na Wilaya nyingine nchini waitumie fursa hiyo kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ikiwemo nyanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza ni kuhusiana na uhalisia na Mto Ngarenanyuki. Mto huu ni moja ya mito michache ambayo imetokea katika maeneo yaliyohifadhiwa, unatokea katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha, chanzo chake ni salama na unapitisha maji mengi ya kutosha na kutiririsha katika nyanda za chini ambapo unapotoka ndani ya hifadhi, kijiji cha kwanza unafikia Kijiji cha Ngarenanyuki yanatiririka mpaka Kijiji cha Ngabobo na zamani za kale yalikuwa yanatiririka mpaka Kijiji cha Jimbo langu la Longido cha Ngereani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba; kwa kuwa maji haya yalipoingia Kijiji cha Ngarenanyuki wananchi wakagundua kwamba ni maji safi ya kuoteshea nyanya; wamekatakata mto mifereji mashine za kunyonya maji mtoni mpaka mto ukakaushwa na maji hayatiririki tena kwenda kwenye vile vijiji vya kusini zaidi. Serikali ina mpango gani wa kusanifu miundombinu ya umwangiliaji wa kisasa itakayowezesha matumizi bora ya maji haya ili yaendelee kutiririka kufikia jamii zilizo chini zaidi kwenye nyanda za chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa tunakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na uwezekano wa maji haya kutosha wakulima wa nyanya waliopo Ngarenanyuki, Ngabobo Mpaka Ngereani kuwafikia wote kwa mtiririko wa asili. Serikali haioni kwamba ni bora sasa wajenge tanki kubwa la kuvuta maji Ngereani ili nao waendeleze kilimo cha umwangiliaji wa nyanya; hasa ukizingatia kwamba ni kilomita 10 mpaka 20 tu katikati Ngereani kutoka mtoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stephen Lemomo Kiruswa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yake yote mawili yamegusa utaalam ambao upo ndani ya Serikali ingawa haupo ndani ya Wizara yangu. Ni jambo la msingi alilolizungumza, kwamba kila Mtanzania anawiwa na dhima ya kulinda rasilimali za maji na hasa hasa kwa sababu haya maji mazuri yametoka katika eneo limeifadhiwa yalikuwa yanatiririka vizuri kwenda kwenye vijiji. Sasa wananchi wameya-*tap* na kuyachota na kupeleka kwenye miradi ya umwagiliaji bila kuzingatia ushauri mzuri wa kitaalam wa kutumia maji kidogo na kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi natoa ushauri kwa Tume ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bonde washirikiane, kwa sababu hizi ni mamlaka za Serikali, waende katika eneo husika wakawaelimishe wananchi kuhusu kilimo bora cha umwangiliaji bila kuchukua maji mengi kutoka kwenye mto ule ili maji yale yaifadhiwe yaendelee kutumika vile vile kwa shughuli zingine na kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuhusu ujenzi wa tanki kubwa litatokana na ushauri ambao wataalam wataona kadri inayofaa katika kutumia maji ya Mto Ngarenanyuki. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwani kati ya vile vijiji 12 ambavyo havikuwahi kuona gari, jana wakati wakiadhiimisha sherehe ya kuzaliwa wa Chama cha Mapinduzi wameiona *excavator* kwa mara ya kwanza. Sasa wakawa wananiuliza *excavator* ile ni ya kike au ya kiume mimi nikasema Serikali itakuja kujibu kama ni ya kiume au ya kike. Sasa kwa niaba ya wananchi wa Ludewa naomba sasa swali lao namba 96 lipate majibu ya Serikali. *(Kicheko/ Makofi)*

Na. 99

**Hitaji la Kituo cha Forodha Bandari ya Manda – Ludewa**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Kituo cha Forodha katika Bandari ya Manda, Ludewa ili kurahisisha huduma kwa wananchi wanaoenda nchi jirani hasa kwa shughuli za biashara?

**NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogatias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kufungua Kituo kipya cha Forodha unatakiwa kuzingatia Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004 ambayo inaitaka nchi mwanachama kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki maombi ya idhini ya kuanzisha Kituo kipya cha Forodha na hatimaye kutangazwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kupata nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ndani wa kuwasilisha maombi ya kufungua kituo kipya cha forodha unaanza katika ngazi ya mkoa ambapo mkoa husika unatakiwa kuwasilisha maombi ya kufungua kituo kipya cha forodha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Baada ya Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kujiridhisha, itamfahamisha Kamishna Mkuu wa mamlaka ya Mapato Tanzania ili kufanyia kazi maombi husika kwa kuzingatia Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki na hatimaye kuwasilisha maombi hayo kwenye Sekretaieti ya Jumuiya ya Afika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia taratibu za kufungua kituo kipya cha forodha hapa nchini, tunamshauri Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na uongozi wa mkoa ili kuandaa andiko na kuwasilisha Serikalini kwa hatua stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, swali la nyongeza.

**MHE. DEORATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Eneo la Manda ni bandari nzuri ambayo ingeweza kutumika ku-*tap* soko la nchi ya Malawi. Eneo la Malawi au nchi ya Malawi ina tatizo kubwa sana la bidhaa au vyakula kama mahindi na kadhalika ambako Ludewa mahindi yanalimwa kwa wingi kiasi ambacho mengine yanaoza kwenye maghala. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga hicho Kituo cha Forodha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili. Utaratibu wa kupata forodha ni kama ulivyoelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. Je, baada ya kuandika *proposal* hiyo inachukua muda gani mpaka kukamilika kwake? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ngalawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza alivyoanza kuipongeza Serikali kwa kufungua miundombinu kuwafikia wananchi ambao walikuwa hawajafikiwa nami naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niwapongeze sana wananchi wa Manda kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya shughuli za kiuchumi zinazowaondoa katika mzunguko wa umaskini kama ambavyo wenzetu wanaendelea kutangaza sifa za Taifa hili ambazo si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambe Watanzania kwamba Taifa hili, alisema Mheshimiwa Waziri wa Fedha siku mbili zilizopita, kwamba kiwango cha umaskini kimepungua kwa kiwango kikubwa na sasa tunasubiri utafiti huu watakapotoa matokeo yao rasmi *(household based survey)* Watanzania wataona na wapuuze haya yote yanayoendelea kuenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalisema kwa sababu sisi kama Serikali tunaitambua Manda kama eneo la kimkakati na ndiyo maana Bunge lililopita nilipojibu swali la 73 la Mheshimiwa Mbene kuhusu ujenzi wa Kituo cha Forodha Ileje na swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngalawa nilimwambia tayari Serikali na namhakikishia tumeshaanza kufanya utafiti, tunachosubiri ni maombi hayo rasmi kutoka kwenye mkoa ili nasi tuifanyie kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimwa Naibu Spika, swali lake la pili, kwamba kwa muda gani unachukuliwa; kwa sababu tumeshaanza utafiti kama Serikali, namhakikishia, tutakapopata maombi hayo, tutayawasilisha rasmi Wizara ya Afrika Mashariki ili waweze kuwasilisha katika Sekretarieti ya Afrika Mashariki

na haitachukua muda kwa sababu Manda ni eneo la kimkakati kwa Taifa hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fester Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 100

**Kituo cha Polisi Chipanga**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuza:-

Kituo cha Polisi Chipanga kilijengwa kwa nguvu za wananchi takribani miaka 18 iliyopita:-

Je, ni lini kituo hicho kitafunguliwa na kutoa huduma kwa wananchi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Polisi Chipanga kilichopo Wilaya ya Bahi Mkoa wa Dodoma kilijengwa muda mrefu kwa nguvu za wananchi wa eneo hilo, lakini baadaye jengo hilo lilipangiwa matumizi mengine ya makazi ya Walimu hadi ilipofika mwezi Februari, 2017. Baada ya jengo hili kutumika kama makazi kwa muda mrefu, maeneo mengi yanahitaji marekebisho ili kuweza kukidhi mahitaji ya kutumika kama Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya maeneo yanayohitajika kufanyiwa ukarabati ni milango, madirisha kuvuja na nyufa katika paa, vyoo, vyumba viwili vya ofisi, chumba cha mahabusu na chumba cha kuweka silaha kwani kwa sasa kilivyo hakiwezi kutumika na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi maeneo mbalimbali nchini wana mwamko wa kujenga Vituo vya Polisi ambayo kwa namna moja au nyingine Serikali imekuwa ikivimalizia na kwa kuwa mahitaji ya kufanya ukarabati wa vituo nchini ni makubwa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali kupitia Jeshi la Polisi, itaendelea kufanya juhudi mbalimbali ili kuweza kukimalizia kituo hicho na kianze kutoa huduma kwa wananchi wa Chipanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo nyongeza. Tangu mwaka 2017 mwezi wa Pili, huu ni mwaka wa tatu jengo hili halijawahi kutumika baada ya kulikabidhi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wananchi wanatoka kilometa 30 kufuata huduma Dodoma Mjini badala ya kwenda Bahi ambayo ndiyo Wilaya iliyopo Tarafa ya Chipanga. Wananchi wanateseka kwa sababu hawana mahali pa kupeleka wahalifu wanapokamatwa. Je, Serikali iko tayari sasa kufanya ukarabati kwa mwaka huu wa fedha katika jengo hili ambalo tulikabidhi litumike kama Kituo cha Polisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa aandamane pamoja nami baada ya Bunge hili twende akaongee na wananchi ambao wamekaa kwa muda mrefu wakisubiri jengo lile litumike kama Kituo cha Polisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Bura kwa namna ambavyo anachapa kazi kwa umahiri na juhudi kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma. Ndiyo maana Mheshimiwa Bura namfananisha

na kumlinganisha na mama mmoja kwenye Biblia naitwa Ester. Mama huyu akiwa bikira alipata kibali machoni pa Mfalme Ahasuero wa kule Shushani Ngomeni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bura amepata kibali kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma katika kuwafanyia kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ni kweli kwamba Kituo hiki cha Polisi cha Chipanga kina matatizo ambayo tumeyafanyia tathmini. Namhakikishia Mheshimiwa Bura awe na amani, kwamba kituo hicho baada ya kufanya tathmini, tutatenga fedha kwa ajili ya kwenda kukikarabati ili kianze kutoa huduma kwa wananchi wa Chipanga katika Wilaya ya Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Felister Bura nikukuhakikishie kwamba huko unakotaka twende labda wewe ndio umechelewa, mimi niko tayari hata leo hii ukitaka tutakwenda wote kule Bahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe wito kwa Mabaraza ya Madiwani kote nchini kwamba katika Ilani hii ya CCM, Ibara ya 146 chama kimeelekeza Serikali zake mbili kwa maana ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Nawaomba Waheshimiwa Madiwani, kwenye makusanyo ya ndani watenge pia fedha kwa ajili ya kujenga Vituo vya Polisi pamoja na nyumba za askari ili tuweze kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora kwa wananchi hapa nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola, pamoja na utayari wako wa kwenda huko, miaka 18 ni mingi sana kwa wananchi kusubiri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa nitaleta kwenu matangazo niliyonayo hapa mezani. Tutaanza na matangazo ya wageni. Kwanza ni wageni 53 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga Waziri wa Kilimo, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma waliongozwa na Ndugu Vumilia Tulyanje. Karibuni sana Bungeni. *Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Juliana Shonza, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; huyu ni Ndugu Chid Designer Suit Bega. Nadhani ameshasimama pale. Jina lake la kazi ndio anaitwa *Chid Designer Suit* Bega. Kwa hiyo, Mheshimiwa Shonza leo hebu asimame kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri kule Wizarani kwake, anasaidia vijana wasanii kama hivi, kwa hiyo, mmeona amependeza? Kwa hiyo, anayetaka kupendeza kama Mheshimiwa Juliana Shonza, kijana yupo pale juu kwa ajili ya kazi hiyo. Tuwasaidie vijana wetu wa ndani, tusinunue suti nje ya nchi tu jamani, hata hapa zipo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambaye ni Katibu wa Chama cha Wananchi (*CUF)* Wilaya ya Lindi, Ndugu Shazil Mosha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Sixtus Mapunda, ambao ni Wananchama wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kutoka Mbinga wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Stanley Ngonyani. Karibuni Sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Geoge Malima Lubeleje ambao ni wapiga kura wake kutoka Mpwapwa; na hawa ni Ndugu Sehewa Mgale na Ndugu Yohana Mgale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nassor Suleiman Omar, ambao ni wajukuu zake kutoka Kusini Pemba; nao ni Ndugu Saida Salim na Ndugu Fatma Nassor. Karibu sana. *Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam; Ndugu Sadiki Rashid na Ndugu Omary Digulu. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye vile vile mgeni wa Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam; Dkt. Mohammed Khalifa. Karibu sana (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimwa Cecil Mwambe, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma; Ndugu Linda Rydee na Ndugu Gilbert Massawe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *(TWPG)* ambao ni Wataalam Waelekezi wa Mpango wa Malezi, tukianza na Dkt. Godfrey Chambua, Ndugu Irine Damian na Ndugu Martha Kikwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Deo Sanga kutoka Makambako. Karibu sana*. (Makofi)*

Tunao Wageni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 70 na Walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari Dendego ya Kilosa Mkani Morogoro wakiongozwa na Mwalimu Omary Zuberi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wahemimiwa Wabunge, ninalo pia tangazo kutoka wa Mwenyikiti wa Jumuiya ya Mt. Thomas Moore, Mheshimiwa Shally Raymond anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo siku ya Jumatano tarehe 6 Februari, 2019 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristo Wakatoriki kuanzia saa 7.00 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote, mnaalikwa kujumuika katika Misa hiyo itakayofanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili, mnakaribishwa nyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba yetu**.**

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Katika Bunge lako hili kulitokea mtafaruku mkubwa sana kutokana na sauti ambayo ilisikika ndani ya

Bunge. Pia siku za nyuma kuna mwenzetu mmoja alikuwa ana-*charge* simu mtafaruku kama huo ukatokea. Sasa tangu mtafaruku huo umetokea nimekuwa nikiwaza, sisi Wabunge hakuna mafunzo yoyote ambayo tumepewa namna ya kukabiliana na matukio kama hayo. Pamoja na hayo, hata watu wenyewe wa Zimamoto jana tuliwaona ni kama walikuwa wamezubaa tu, hawajui nini cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa hali hiyo na wengine hatuna mbio kama za Mheshimiwa Mwijange jana, naomba mwongozo wako, kwa nini Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikishirikiana na Bunge isiwape mafunzo maalum Waheshimiwa Wabunge, namna ya kukabiliana hali kama hiyo siku ikitokea tena? *(Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Selasini. Pamoja na kwamba ametumia kanuni yetu inayozungumzia mwongozo ambayo kwa masharti yake jambo hili lisingetakiwa kutolewa mwongozo, lakini kwa kuwa ni jambo linalohusu usalama wetu hapa ndani, nieleze machache tu.

Waheshimiwa Wabunge, moja ni kwamba, yale maeneo mnayoingilia, wengi tumezoea kuingia kwa kutumia mlango mkubwa, lakini iko milango iliyoandikwa "sehemu za kutokea" kwenye maeneo mbalimbali humu Bungeni. Kwa hiyo, likitokea jambo kama lile ambalo hatuombei litokee, tutokee milango mingine ya dharura, siyo lazima wote tuje huku mbele. Kwa sababu hata Mheshimiwa Mwijage alitoka huku. Kwa hiyo, mlango mwingine uko pale, lakini yeye akakumbuka mlango mmoja tu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawakumbusha kuangalia lile eneo unalokaa mlango upi uko karibu zaidi na wewe? Usiutafute mlango mkubwa wakati ule mkubwa upo karibu na watu wengine. Upitie milango mingine ambayo ipo.

Mheshimiwa Selasini pia amezungumza kuhusu jambo kutokea na pia kuonekana kama kuna sintofahamu hivi kwamba ni jambo gani lililotokea? Tunachoshukuru ni kwamba mitambo yetu inaonyesha kwamba iko vizuri, likitokea jambo inaweza kunusa hivi. Kwa hiyo, tuko vizuri. Kwa hiyo, lililotokea jana limeshawekwa vizuri, hakukuwa na tatizo kubwa na ndiyo maana leo tupo hapa. Kwa hiyo, tukae kwa amani, mitambo yetu inayolinda usalama hapa iko vizuri na vijana wetu pia wapo vizuri. Kwa hiyo, tuko salama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola, naomba ukae. Mheshimiwa Janeth Mbene.

**MHE. JANETH Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa maelekezo kuhusiana na milango ya kutokea. Milango ya kutokea, mwisho wa yote ina-*converge* kwenye huu mkubwa kwa sababu hapa pembeni kuna kufuli, upande huu wa kushoto kwangu. Ukitoka hivi, ule mlango hauna *access* ya kutoka, kuna kufuli, *unless* kuna mtu anakaa na ufunguo pale; na huku vilevile kumefungwa. Kwa hiyo, mwisho wa yote tutazunguka hivi, tutarudi kukutana hapa. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako chini ya kanuni ya 68(7). Maneno na maelezo ambayo yametolewa na Baba Paroko, Mheshimiwa Joseph Selasini kuhusiana na tukio lililotekea jana kwamba Askari wetu wa Zimamoto walikuwa maeneo haya wamezubaa tu wanazunguka; nimeona

tusipoweka kumbumbuku sawa, inaweza ikatafsiriwa kwamba Jeshi la Zimamoto Tanzania ambalo lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi lina Askari na Maofisa goigoi ambao hawatimizi wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio hili baada ya kutokea jana, mimi mwenyewe pamoja na kushuhudia Waheshimiwa Wabunge wakitoka, nilihusika pia kuwaelekeza maeneo ya kupita na nilikuwa mtu wa mwisho kutoka humu ndani, mpaka Waheshimiwa Wabunge wengine wakawa wananiuliza, siogopi tukio kama hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa hapo nje, Kamanda wetu wa Jeshi la Zimamoto wa Mkoa wa Dodoma akiwa na Askari hapo, akishirikiana na Maafisa wa Bunge, pamoja na Mpambe wa Bunge na Askari wake, walikuwa wakifuatilia kuona tukio hili ni tukio la namna gani ili waweze kujua hatua. Kwa hiyo, kulisema Jeshi hili hivyo, siyo lugha sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokubaliana naye ni kwamba lazima tutoe mafunzo. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Mkutano ujao kabla hatujaingia humu ndani, lazima tuhakikishe Waheshimiwa Wabunge wote mmepewa semina au mafunzo kwa ufupi ikiwa ni pamoja na kufanya hiyo *drill* kwa ajili ya kuona kwamba tatizo likitokea, ni milango gani na wapi pa kwenda kukusanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nianze na Mheshimwa Janeth Mbene, ameonesha kwamba milango tunayosema inaweza kutumika kutoka kwa sasa ina makufuli. Niseme kwamba kuna Maaskari wamekaa huko na milango iko wazi. Hata mimi jana nilitokea ule mlango pale na kulikuwa na Askari na mlango ulikuwa wazi. Kwa hiyo, hakuna tena milango inayofungwa. Kuna Maaskari na inakuwa wazi. Ukitokea huko, inabidi uendelee huko huko, usirudi tena huku. Wanaotokea huku, kuna mlango mkubwa uko kule; wanaotekea upande huu, kuna eneo la wazi kabisa unaendelea kutoka mpaka nje.

Kwa hiyo, tutumie hayo maeneo tunapotoka nje na wanaotumia mlango mkubwa pia, wanatakiwa wakishatoka, waende kabisa nje, kwa sababu inaonekana shida inakuwa kwenye jengo zima, kwa hiyo, utoke nje. Usianze kutoka hapo nje kidogo halafu unasubiria watu wengine.

Kwa lile alilozungumza Mheshimiwa Kangi Lugola kuhusu Maaskari kama wanalandalanda hivi, sikulitolea maelezo sana kwa sababu ya namna yeye alivyolileta. Tuwashukuru Jeshi la Zimamoto, walifka hapo kwa haraka sana na katika muda mfupi tuliona gari yakiwa yamefika katika hili eneo. Maana yake kama kungekuwa na changamoto, wangeweza kuchukua hatua za haraka. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa hatua walizochukua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyozungumza mwanzo, tuwe na utulivu, tuko salama, vyombo vyetu vipo vizuri.

Tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kauli za Mawaziri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe kauli ya Serikali kuhusu matukio ya utekaji na mauaji ya watoto yaliyofanyika Mkoani Njombe. Tarehe 4 Februari, 2019 ilitolewa hoja na Mheshimiwa Joram Hongoli, Mbunge wa Jimbo la Lupembe akiomba utenge angalau dakika 20 Bunge lijadili juu ya hali inayoendelea Mkoa wa Njombe ya utekaji na mauaji ya watoto wadogo. Hoja hii iliyoungwa mkono na Wabunge wengi ilisemwa pia na Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako na baadaye Mnadhimu Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni Mheshimiwa Jenista Mhagama aliomba Serikali kupatiwa muda wa kuandaa Kauli ya Serikali

ili Watanzania wafahamu hali halisi na hatua zilizokwishachukuliwa na Serikali mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa historia ya suala hili kwa ufupi. Hivi karibuni kumejitokeza matukio yasiyo ya kawaida ya utekaji na mauaji ya watoto yaliyokuwa yakihusishwa na imani potofu za kishirikina katika Mkoa wa Njombe. Kufuatia matukio hayo hadi sasa watoto saba wa umri chini ya miaka 16 wameripotiwa kuuawa; mmoja ameripotiwa kujeruhiwa; na wawili wameripotiwa kupotea na baadaye kuonekana. Matukio haya yametokea katika maeneo ya Ikando, Matembwe, Mji Mwema, Msitu wa Sekondari ya Njombe, Lukosa, *SIDO* na Mfereke. Aidha, uchunguzi unaonesha kwamba mauaji yamefanyika kwa unyongaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa za mauaji hayo, tarehe 28 Januari, 2019, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni Naibu Waziri wangu alifanya ziara ya siku mbili Mkoani Njombe ili kufuatilia juu ya hatua zilizochukuliwa na vyombo vya dola katika kutanzua na kuzuia matukio haya sanjari na kutoa maelekezo ya hatua zaidi za kupambana na uhalifu huu. Mpaka sasa hatua zilizochukuliwa na Serikali kama nilivyoainisha awali zimefanikishwa kukamatwa kwa watuhumiwa 29 kwa ajili ya uchunguzi na mahojiano zaidi na kazi bado inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo za Serikali, Jeshi la Polisi na Kamati ya Ulinzi wa Usalama ya Mkoa wa Njombe imechukua hatua mbalimbali za kuzuia na kutanzua aina hii ya kinyama ya uhalifu. Baadhi ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutuma timu ya wataalam wa upelelezi kuvisaidia vyombo vya dola Mkoani Njombe kuchunguza matukio haya;

(b) Kutumia falsafa ya ulinzi shirikishi, ushirikishwaji wa jamii kwa kutoa elimu mashuleni kwa Walimu ili waweze kuwaelimisha wanafunzi kuongeza umakini katika mienendo yao;

(c) Kutumia vyombo vya habari kutoa elimu kwa wazazi na wananchi kwa ujumla juu ya elimu ya ulinzi na usalama;

(d) Kukusanya taarifa fiche za intelijensia ili kuwabaini na kuwakamata wahalifu halisi waliohusika na matukio na pia kuzuia matukio mengine kutendeka;

(e) Kufanya vikao na Waganga wa Kienyeji, Viongozi wa Dini, Wazee wa Mila, Viongozi wa Kata, ili kuweka mikakati thabiti ya pamoja ya kukomesha mauaji hayo;

(f) Kufanya sensa ya kuwatambua Waganga wote wa Jadi wanaojihusisha na shughuli za uganga na kuainisha walio na leseni na wasio na leseni pia kuwabaini waganga matapeli na wapiga ramli chonganishi; na

(g) Kufanya doria na misako kwenye maeneo mbalimbali ya misitu na nyumba za kulala wageni zilizopo pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni kuwa pamoja na Serikali na Watanzania wengi kushtushwa na matukio haya, wapo baadhi ya Watanzania wenzetu wanaojaribu kutumia matukio haya kuzua taharuki miongoni mwa wanajamii. Kama ilivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kutoa hoja zao, kumekuwepo na matukio ya watu kuchukua picha za kwenye mitandao zinazoonesha miili ya watoto na kuwaaminisha wasomaji kuwa ni picha za hivi karibuni Mkoani Njombe. Aidha, wapo baadhi ya wananchi wengine, waliojaribu kuhusisha matukio haya na itikadi za kisiasa, imani za kidini, au shughuli za kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, si vyema kuhusisha mauaji haya na itikadi za aina yoyote au shughuli za uzalishaji mali au biashara, kwani kwa kufanya hivyo unaweza kuwaingiza katika mzunguko huo watu wasiohusika. Watu wote 29

waliokamatwa ni wananchi wa kawaida, usioweza kuwahusisha na udini, siasa au biashara. Nashauri tutulie wakati Serikali kupitia Wizara yangu tunaendelea kufuatilia na kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba kama ambavyo tumekomesha matendo maovu na ya kuchukiza yanayofanana na hili. Tutahakikisha wote waliohusika wanaendelea kusakwa, kuhojiwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria bila kujali nafasi zao katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kupitia Bunge lako Tukufu, nataka niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba kama ambavyo tumekomesha matendo maovu na ya kuchukiza yanayofanana na hili, tutahakikisha wote waliohusika wanaendelea kusakwa, kuhojiwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria bila kujali nafasi zao katika jamii. Hivi ninavyoongea Serikali imetuma timu kabambe yenye askari na makachero makini, hodari na mahiri ili kukabiliana na uhalifu huu mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mtandao, naomba kuchukua nafasi hii kuwaasa Watanzania kuacha, kuanzisha na kusambaza taarifa za uzushi kwa nia yoyote ile. Serikali itawachukulia hatua wale wote watakaothibitika kujihusisha na vitendo hivi vya kusambaza taarifa za uchochezi mitandaoni. Aidha, wote waliosambaza taarifa za kuzua taharuki tutawakamata na kuwafikisha mahakamani ili wakajifunze kutumia uhuru wa kujieleza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesikitishwa sana na matukio ya mauaji ya watoto wetu huko Njombe. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu wazazi na ndugu, jamaa na marafiki wote wa watoto waliopoteza maisha. Aidha, naomba niwahakikishie kuwa Serikali yao itahakikisha matukio haya yanaisha na wahusika wote wanatiwa mbaroni na kufikishwa katika vyombo vya sharia.

Hivyo basi, nawaomba wananchi watulie na waache kujichukulia sheria mkononi ila waendelee kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili kwa pamoja tukomeshe uhalifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kuwa mara zote haki hushinda uovu. Narudia nimalizie kwa kusema kuwa mara zote haki hushinda uovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018 na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2018**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Februari, 2018 mpaka Januari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani. Taarifa tuliyonayo hapa ni *summary*, taarifa kamili tumewagawia Wabunge ambazo wanazo kwenye nafasi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa hatua anazoendelea kuchukua katika kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za haraka za muafaka kutatua changamoto zinazovikabili vyombo hivyo, ikiwemo changamoto za makazi na stahiki zingine za watumishi wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Mawaziri wote Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Kange Lugola na Dkt. Mahiga, na Wakuu wa Vyombo hivyo kwa umakini na utayari wao wa kukabiliana na majukumu yao ya kiulinzi na usalama wa nchi nzima kwa weledi na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua hii napenda kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa jinsi vinavyoshirikiana na wananchi katika kukabiliana na majanga na matatizo mbalimbali kama vile ilivyokabiliana na maafa ya *MV* Nyerere, huko katika Visiwa vya Ukerewe Mkoani Mwanza. Hongereni sana vyombo vyote vya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa kwa mujibu wa kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali taarifa ya shughuli za mwaka za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ya mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza katika kipindi cha pili cha mwisho cha uhai wa Kamati ya kipindi cha miaka miwili na nusu ya iliyobaki ya uhai wa Bunge la Kumi na Moja kwa mujibu wa Kanuni ya 116(7). Kwa kuzingatia hilo, naomba niwashukuru Wajumbe 25 wa Kamati ambayo katika kipindi cha takriban miezi tisa tangu kuundwa upya kwa Kamati

wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majina yote ya Wajumbe wa Kamati hii ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa kwanza mpaka wa pili. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne, kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza; sehemu hii inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa; majukumu hayo yameainishwa katika ukurasa wa 3 - 5. Aidha, shughuli ambazo Kamati imezitekeleza kwa kipindi kinachotolewa taarifa ni pamoja na:-

(i) Semina;

(ii) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara inazozisimamia;

(iii) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo;

(iv) Kuchambua taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na makadirio na mapato ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2018/2019;

(v) Kuchambua mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia; na

(vi) Mapitio ya taarifa za wawakilishi Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge; Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati yanapatikana katika ukurasa wa tano hadi ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili; sehemu hii inahusu uchambuzi, na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ikiwa ni pamoja na masuala ya yaliyotolewa ushauri katika Bunge la Tisa na la Kumi, lakini hayajatekelezwa kwa ukamilifu. Changamoto nyingine ambazo Kamati imezibaini katika utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi kinachotolewa taarifa. Maelezo hayo yanapatikana katika ukurasa wa nane hadi ukurasa wa 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu; sehemu hii inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo sasa, naomba kuiwasilisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni; masuala ambayo yamekuwa yakitolewa ushauri mara kwa mara lakini utekelezaji wake si wa kuridhisha; Kutotekeleza kwa muda mrefu wa masuala 13 ambayo yamekuwa yakishauriwa mara kwa mara na Kamati hususan kuhusu Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki; Umiliki wa Chuo cha Diplomasia; Ubovu wa barabara za mipakani; Kukosekana kwa sera za ulinzi na *APRM* kutokuwa na hadhi ya taasisi, pamoja na masuala mengine yaliyoainishwa katika sehemu ya pili, kipengele cha 2.1.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kwa mara nyingine inaendelea kuishauri Serikali, kuona umuhimu wa kuyashughulikia masuala hayo kwa manufaa ya Taifa na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(i) Kutofuata taratibu za kisheria na kikanuni katika kutekeleza miradi ya maendeleo, hususan ya Uhamiaji katika Mkoa wa Mtwara kunasababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango na hivyo kupoteza fedha nyingi za walipa kodi ambazo zingiweza kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

(ii) Kuendelea kutumika kwa Sheria ya Magereza ya mwaka 1974 kunaathiri ufanisi wa utendaji wa Shirika la Magereza kwani halijiendeshi kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992;

(iii) Shirika la Magereza kujiendesha bila bodi kunasababisha shirika hilo kutokutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwani linakosa usimamizi ulioainishwa kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wake; Taasisi za Serikali hususan Jeshi la Magereza Fungu 29;

(iv) Kutokulipa madeni yanayodaiwa na Shirika la Magereza kunaathiri uzalishaji wa shirika hilo; Kutokulipwa kwa madeni ya wazabuni wa majeshi ya Wizara hiyo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya majeshi hayo kwa taasisi za Wizara hiyo;

(v) Kuchelewesha kutolewa kwa hukumu za kesi za mahabusu kunachangia msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani;

(vi) Jeshi la Magereza kutokuwa na mpango mkakati na madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula kunasababisha Serikali kuingia gharama kubwa katika kutoa huduma ya chakula kwa wafungwa na mahabusu;

(vii) Ukomo wa bajeti usiozingatia mahitaji halisi ya mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa unaathiri utendaji wa mamlaka hiyo hususan katika kufika malengo ya vitambulisho vinavyokusudiwa kutolewa; na

(viii) Kutotumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole* na matumizi hafifu ya sheria zinazohusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa:-

(i) Kukosekana kwa Sera ya Uinzi wa Taifa nchini *(Natioal Defence Policy)* kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;

(ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi, *beacons* kunachangia uvamizi wa raia wa kigeni katika baadhi ya maeneo ya mipaka jambo ambalo linaweza kuathiri ulinzi na usalama wa nchi;

(iii) Ubovu wa barabara za mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria kudhibiti mipaka ya nchi;

(iv) Madeni kwa mashirika yaliyochini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa Shirika hilo;

(v) Kukosekana kwa uzio katika baadhi ya kambi za jeshi kunasababisha migogoro ya ardhi kutokana na wananchi kuvamia maeneo hayo;

(vi) Wananchi kutokulipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya wananchi na vikosi vya jeshi hilo;

(vii) Uchakavu wa majengo ya Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi cha Monduli, kunashusha hadhi ya Chuo hicho kinachotoa mafunzo ya Kimataifa; na

(viii) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa Shirika la Nyumbu kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na za kibunifu za Shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

(i) *OPRM* kutokuwa na hadhi ya kisheria, kunasababisha Taasisi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;

(ii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kunaikosesha nchi fursa ya kuvutia mikutano na Maonesho ya Kimataifa mengi zaidi kufanyika hapa nchini;

(iii) *AICC* kutokuwa na majengo ya kutosha kwa ajili ya shughuli za mikutano unakiondolea kituo hicho ufanisi kwa kushindwa kushindana katika soko;

(iv) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunasababisha Balozi zetu kutumia magari na majengo yaliyochakaa jambo linaloathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

(v) Kukosekana kwa sera ya Taifa kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki ni changamoto katika mustakabali wa nchi. Serikali imekuwa ikitekeleza shughuli za mtangamano wa Afrika Mashariki bila kuwa na mwongozo bora wa kisera;

(vi) Mchakato wa kuifanyia marekebisho Sera ya Mambo ya Nje, 2001 unachukua muda mrefu jambo linaloifanya sera hiyo kutoendana na kasi ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo sasa;

(vii) Ucheleweshaji wa kuridhia mikataba ya Kimataifa na Itifaki zilizosainiwa kunachelewesha nchi yetu kunufaika na masuala muhimu yaliyopo kwenye mikataba na itifaki hizo; na

(viii) Serikali kutotoa fedha za kutosha za uendeshaji *(OC)* kunasababisha balozi zetu za nje kushindwa kutekeleza vyema majukumu yake hususani katika nyanja za diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Kibunge:-

(i) Ukosefu wa ajira kwa vijana katika bara la Afrika bado ni changamoto kubwa ambapo kila nchi

mwachami wa *PAP* inatakiwa kulishughulikia. Ni vyema Serikali ikaandaa mkakati mahususi wa kuhamasisha vijana kujihusisha na kilimo chenye tija ikiwa ni pamoja na kuanzisha mitaala ya kilimo na ufugaji kuanzia ngazi ya elimu ya msingi kama njia mojawapo ya kukubaliana na tatizo la ajira kwa vijana.

(ii) Serikali iwasilishe Bungeni Itifaki na Mikataba yote iliyopitishwa na Bunge la Umoja wa Afrika ambayo ina tija kwa Taifa letu ili iweze kuridhiwa kwa maslahi ya Taifa. Itifaki hizi zijumuishe Itifaki inayounda Bunge la Afrika ili kuwezesha Bunge hilo kuwa chombo cha kutunga sheria.

(iii) Upo umuhimu wa Serikali kuweka na kuendeleza mikakati ya kuwashirikisha wanaume na wavulana katika kutatua changamoto zinazowakabili wanawake na wasichana hususani zile zilizohusu ubaguzi na uonevu wa kijinsia. *(Makofi)*

(iv) Upo umuhimu wa nchi wanachama kuridhia Itifaki zinazohusu usalama na amani katika Bara la Afrika na kutekeleza Itifafi hizo.

(v) Upo umuhimu wa Serikali kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(vi) Kutokuwa na Ofisi kwa ajili ya wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Kibunge kwa wawakilishi hao wanapokuwa nchini nje ya vipindi vya mikutano ya Kibunge na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo. Baada ya kueleza maoni ya Kamati, sasa naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Shirika la Uzalishaji la Magereza.

KWA KUWA Sheria ya Shirika la Magereza ya mwaka 1974 (*The Corporation Sole Act, 1974)* ilianzishwa kabla ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992, hivyo kutoendana na matakwa ya Sheria ya Mashirika.

NA KWA KUWA kuendelea kutumika kwa Sheria ya Magereza ya mwaka 1974, kunaathiri ufanisi wa shirika katika kujiendesha kiushindani kwani linaendeshwa chini ya uongozi wa Jeshi la Magereza.

KWA HIYO BASI, Sheria ya Magereza ya mwaka 1974 ifanyiwe marekebisho ili shirika hili lijiendeshe kwa kujitegemea, jambo ambalo litaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

(ii) Mkakati wa Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula.

KWA KUWA kuwa Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Magereza halina mpango mkakati madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula.

NA KWA KUWA kutokuwa na mkakati huo madhubuti, kunasababisha Serikali kuingia gharama kubwa katika kutoa huduma ya chakula kwa wafungwa na mahabusu.

KWA HIVYO BASI, Jeshi la Magereza liandae mkakati madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula ikiwa ni pamoja na kutumia rasilimali za ardhi, nguvu kazi na dhana za kilimo walizonazo katika kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi ya magerezani na kwa ajili kuuza kwa lengo la kuliongezea Jeshi hilo kipato. Aidha, mkakati huo ukamilike ndani ya mwaka wa fedha wa 2018/2019.

(iii) Migogoro ya ardhi katika maeneo ya Jeshi.

KWA KUWA baadhi ya maeneo ya Kambi na Vyuo vya Jeshi havina uzio kuzunguka maeneo hayo. Hapa

nitaeleza kidogo, kumejitokeza tabia ya baadhi wananchi, viongozi kupenda kuingia katika maeneo ya Jeshi na kusingizia maeneo ya Jeshi kuwa ni mapori. Mapori haya ndiyo Ofisi za Majeshi. Tunaomba maeneo haya yaachwe kwa matumizi ya vyombo vya ulinzi. *(Makofi)*

NA KWA KUWA kukosekana kwa uzio katika maeneo hayo kunasababisha wananchi kuvamia maeneo hayo kwa ajili ya shughuli za kijamii zikiwemo za kilimo na ufugaji, jambo ambalo si tu husababisha migogoro pale wananchi wanapotakiwa kuhama bali pia linahatarisha ulinzi na usalama wa maeneo hayo.

KWA HIVYO BASI, Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Makambi na Vyuo vya Jeshi ili pamoja na kuondoa migogoro ya ardhi inayotokana na wananchi kuvamia maeneo hayo, kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo hayo.

(iv) Utekelezaji wa majukumu ya Balozi za Tanzania nje ya Nchi.

KWA KUWA baadhi ya Balozi za Tanzania nje ya nchi zina upungufu wa watumishi hususan wenye taaluma ya masuala ya uchumi.

NA KWA KUWA upungufu huo unaathiri shughuli za Balozi katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi hususan katika kutangaza vivutio vya utalii na kutafuta fursa za ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje.

KWA HIVYO BASI, Serikali ipeleke watumishi zaidi ambao wana taaluma ya masuala ya uchumi ili kuziwezesha Balozi zetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii itengeneze mkakati thabiti wa kuziwesha Balozi zetu kutangaza utalii. Mkakati huu ni pamoja na kutenga na kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza utalii nje ya

nchi pamoja na kutumia watu mashuhuri *(celebrities)* waliowahi kutembelea vivutio vya utalii nchini. *(Makofi)*

(v) Upungufu na uchakavu wa majengo ya Ubalozi.

KWA KUWA Mkakati wa Miaka Kumi na Tano (2001 - 2017) wa kuendeleza viwanja, kukarabati na kununua majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozini haukutekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha.

NA KWA KUWA kutokutekelezeka kwa Mkakati huo kumesababisha Serikali kuendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kukodi nyumba za makazi na Ofisi.

KWA HIYO BASI, Serikali ione umuhimu wa kutumia mikopo ya muda mrefu lakini yenye riba nafuu *(mortgage financing)* katika kuendeleza viwanja vya Balozi zote kumi na mbili, ambavyo baadhi yake vimetelekezwa kama London- Uingereza, Muscat- Oman, Nairobi- Kenya, pamoja na kuboresha majengo, ofisi na makazi ya watumishi. Hii itasaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za walipa kodi zinazotumika kwa ajii ya kodi za pango na fedha hizo kuelekezwa katika miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu umetolewa miaka mingi mpaka sasa hivi Serikali imeshatumia takribani bilioni 216 kulipia kodi kwa miaka 10. Kamati haiombi pesa za ziada, inaomba pesa hizi za kodi zitumike ku-*service* mikopo ambayo Serikali itaingia na kujenga majengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tu ni Msumbiji. Tumejenga jengo letu la ghorofa tisa na jengo hili sasa linakaliwa na Balozi na Ofisi za Balozi na sasa hivi linatumika kibiashara na Balozi na Serikali inapata kodi. Katika mgao wa fedha wa mwaka huu Ubalozi wa Msumbiji haukuwekewa fedha za pango kwa sababu wanajitegemea. *(Makofi)*

(vi) Uendeshaji wa Chuo cha Diplomasia.

KWA KUWA Serikali ya Msumbiji imeendelea kutokuchangia michango ya Chuo cha Diplomasia tangu mwaka 1982 ilhali bado inatambulika kisheria kuwa ni mmiliki halali wa chuo hicho pamoja na Tanzania.

NA KWA KUWA Serikali ya Msumbiji kutokuchangia michango hiyo kunasababisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuendelea kubeba jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za chuo hicho.

NA KWA KUWA Serikali imeendelea kuitumia Tume ya Pamoja ya Ushirikiano yaani *Joint Permanent Commission* katika kulipatia ufumbuzi suala la umiliki wa chuo hicho bila mafanikio.

KWA HIYO BASI, Serikali ifanye maamuzi ya kukichukua na kukimiliki chuo hicho bila ubia na Msumbiji. Kwa taarifa, sasa hivi Msumbuji wana Chuo chao cha Diplomasia hiki cha kwetu hawakihitaji tena. *(Makofi)*

(vii) Utalii wa mikutano.

KWA KUWA majengo ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha hayakujengwa rasmi kwa shughuli za mikutano.

NA KWA KUWA kutokuwa na majengo rasmi kwa ajili ya shughuli za mikutano unakiondolea kituo hicho uwezo wa kushindana katika soko na hivyo kuathiri utalii wa mikutano.

KWA HIYO BASI, Serikali itekeleze mpango wake mahsusi wa kujenga kituo kipya cha mikutano cha *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MKICC)* ambacho pamoja na mambo mengine kitakuwa na eneo la kutosha la maonesho na huduma nyingine muhimu kwa shughuli za utalii wa mikutano. Aidha, vituo mahsusi vya mikutano

vianzishwe katika mikoa ambayo ina fursa za kitalii kama vile Iringa, Zanzibar, Mwanza na vilevile katika Makao Makuu ya Nchi, Dodoma.

(viii) Ofisi za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki.

KWA KUWA Wabunge wanaoiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki hawana ofisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ikiwemo kukutana wawapo nchini.

NA KWA KUWA kutokuwepo kwa ofisi hiyo si tu kunaathiri utendaji kazi za Wabunge hao bali pia ni fedheha kwa Wabunge hao na kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ndilo linalowakilishwa na Wabunge hao.

HIVYO BASI, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iharakishe upatikanaji wa Ofisi kwa ajili ya Wawakilishi hao hususan katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi wanapokuwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inahusu shukrani. Naanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola na Naibu wake Mheshimiwa Mhandisi Alhaj Hamad Masauni; Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi; Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Damas Ndumbaro; na Watendaji

wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walioonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani za dhati sana kwa *Commander in Chief* wa vyombo vyote vya ulinzi nchini, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake uliotukuka katika kuviboresha vyombo vyote vya ulinzi kwenye maeneo ya ulinzi, maslahi na kutatua changamoto zinazowakabili katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilisha taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati. Baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, lijadili na hatimaye kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2018- JANUARI, 2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEZO YA JUMLA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Kamati Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa hatua anazoendelea kuchukua katika kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za haraka na mwafaka kutatua changamoto zinazovikabili vyombo hivyo ikiwemo changamoto za makazi na stahili nyingine nyingi za watumishi wa vyombo hivyo. Aidha nawapongeza Wakuu wa vyombo hivyo kwa umakini na utayari wao wa kukabiliana na majukumu yao ya kiulinzi na usalama kwa nchi nzima kwa weledi na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 [Kanuni za Kudumu za Bunge] naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2018 hadi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza katika kipindi cha pili

na cha mwisho cha uhai wa Kamati kwa kipindi cha miaka miwili na nusu iliyobaki ya uhai wa Bunge la 11, kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (7). Kwa kuzingatia hilo, naomba niwashukuru Wajumbe ishirini na tano (25) wa Kamati ambao katika kipindi cha takribani miezi tisa tangu kuundwa upya kwa Kamati wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni: -

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Salim Mwinyi Rehani, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb- "
4. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb- "
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb- "
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa, Mb-"
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb- "
8. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb- "
9. Mhe. Joseph Mkundi, Mb- "
10. Mhe. Joram Hongoli, Mb- "
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb- "
12. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb- "
13. Mhe. Bonnah Moses Kaluwa, Mb- "
14. Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb-"
15. Mhe. Dr. Suleiman Ally Yussuf, Mb- "
16. Mhe. Augostino Mayanda Masele, Mb-"
17. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb- "
18. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb-"
19. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb- "
20. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb- "
21. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb- "
22. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb- "
23. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb- "
24. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb- "
25. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb- "

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa kwa mara ya kwanza katika kipindi cha pili na cha mwisho cha uhai wa Kamati kwa kipindi cha miaka miwili na nusu iliyobaki ya uhai wa Bunge la 11, kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (7). Kwa kuzingatia hilo, naomba

niwashukuru Wajumbe ishirini na tano (25) wa Kamati ambao katika kipindi cha takribani miezi tisa tangu kuundwa upya kwa Kamati wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni: -

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019 na imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo: -

i. Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;
ii. Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
iii. Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
iv. Sehemu ya Nne ni hitimisho la Taarifa.

### 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019 na imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo: -

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 ikisomwa pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) ambazo ni: -

i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
ii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii ni: -

i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
iii. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati ina majukumu ya nyongeza matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni: -

i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na
v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

### 1.2 Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2017/2018 na 2018/2019. Njia zilizotumika ni: -

i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Vyama hivyo;
iii. Kuwataka Mawaziri kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;
iv. Ziara za kukagua utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;
v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018;
vi. Kutoa taarifa maalumu ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya masuala ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (17); na
vii. Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Serikali na Asasi za Kiraia.

## 1.3 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari 2018 - Januari, 2019 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo: -

### 1.3.1 Semina

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019, Kamati ilishiriki na kuongoza Semina tatu zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, chini ya Mradi wa Awamu ya Pili wa kuliwezesha Bunge *(Legislative Support Project II)* unaodhaminiwa na UNDP. Semina zilizofanyika zilihusu: -

i) Namna Bunge linavyoweza kufuatilia Utekelezaji wa malengo ya Maendeleo endelevu, Mei, 2018.
ii) Hatua za kuzingatia wakati wa uchambuzi wa Mikataba ya Kimataifa Juni, 2018;
iii) Umuhimu wa kujumuisha Masuala ya Jinsia katika Utekelezaji wa Majukumu ya Bunge Septemba, 2018;

**Mheshimiwa Spika**, naomba kukiri kuwa Semina hizo kwa kiasi kikubwa zimewajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala ya Jinsia, ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu (SDG) na uchambuzi wa Mikataba ya Kimataifa.

### 1.3.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, yapo masuala (hususan yanayohusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa) ambayo Kamati yaliyaandikia taarifa maalumu ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, yapo masuala mengine ambayo yalibainika na yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

### 1.3.3 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii

ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya Miradi Mitatu (3) ilikaguliwa katika maeneo manne (4) katika kipindi cha Mwezi Machi, 2018. Miradi hiyo pamoja na vifungu vyake ni ifuatayo:-

| SN | Fungu | Simbo ya Mradi | Jina la Mradi | Mahali Mradi ulipo | Thamani ya mradi (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 29 | 6308 | Ujenzi wa Magereza ya Wafungwa | Ruangwa, Lindi | 9,760,000,000.00 |
| 2. | 93 | 6301 | Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji | Lindi Mjini | 817,255,840.81 |
| 3. | 93 | 6301 | Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji | Mtwara Mjini | 1,596,360,224.79 |
| 4. | 57 | 6103 | Tathmini na Ulipaji wa Fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Kilwa, Lindi | 3,662,108,122.00 |

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi uliofanywa, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yalioathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

### 1.3.4 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua kwa kina Bajeti za Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

### 1.3.5 Kuchambua Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilishughulikia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za kibaolojia na Sumu pamoja na Uangamizaji wake (*The Convention on prohibition of development, production and stockpiling of bacteriological (Biological) and Toxins Weapons and on their Destruction*) wa Mwaka 1972. Kamati ilichambua kwa kina Mkataba huo na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

### 1.3.6 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge; na katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari 2018- Januari, 2019, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Bunge la Afrika (PAP) na katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.0 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari 2018 hadi Januari, 2019, sasa naomba kutoa taarifa

ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa.

## 2.1 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake katika kipindi kinachotolewa Taarifa, ilifuatilia pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali ambayo imekuwa ikiyasemea katika taarifa zake mbalimali hususan Taarifa za Mwaka za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hilo, Sehemu hii ya Taarifa itagawanyika katika sehemu ndogo mbili (2) ambapo sehemu ya kwanza itaongelea masuala ambayo Kamati imekuwa ikiyashauri mara kwa mara lakini bado hayajatekelezwa kikamilifu; na Sehemu ya Pili itaongelea masuala mengineyo ambayo Kamati imeyabaini katika kipindi kinachotolewa Taarifa.

### 2.1.1 Masuala yaliyotolewa ushauri lakini Utekelezaji wake si wa kuridhisha

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake katika kipindi cha Februari 2018 hadi Januari 2019, pamoja na mambo mengine, ilifuatilia utekelezaji wa masuala ambayo yamekuwa yakishauriwa na Kamati mara kwa mara lakini utekelezaji wake umekuwa changamoto sugu. Masuala haya yanajumuisha yale yaliyotolewa ushauri tangu Bunge la Tisa na la Kumi, lakini utekelezaji wake hauridhishi. Masuala hayo pamoja na hatua ya utekelezaji wake ni yafuatayo: -

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora-Tanzania (African Peer Review M echanism –APRM Tanzania) kutokuwa na hadhi ya Taasisi (Legal entity) | Kamati, kwa kipindi cha miaka mitano (5) mfululizo, imekuwa ikishauri Serikali kuipatia *APRM* hadhi ya Taasisi ambayo pamoja na mambo mengine, itaiwezesha *APRM* kuwa na Fungu lake la Kibajeti badala ya fedha zake kupitishiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kitengo cha *Africa Division,* jambo linalosababisha kitengo hicho kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. |
| 7. | Umiliki wa Chuo cha Diplomasia (Tanzania-Mozambique Centre for Foreign Relations); | Suala hili limekuwa likiripotiwa na Kamati tangu Mwaka 2017 hata hivyo Serikali bado haijafanya maamuzi ya dhati ya kukichukua Chuo hicho. Msumbiji bado inatambulika kisheria kuwa Mmiliki halali wa Chuo hicho pamoja na Tanzania, ilhali iliacha kuchangia Michango ya Chuo tangu mwaka 1982. Vilevile, Kamati ilibaini kuwa tayari Msumbiji imeanzisha chuo chake cha Diplomasia nchini humo. |
| 8. | Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania na Uendelezaji wa Viwanja vya Balozi | Tangu Bunge la Tisa, Kamati hii imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu wa kuyafanyia ukarabati majengo ya Balozi za Tanzania nje ya Nchi na kuendeleza viwanja vya Balozi zetu nje. Hata hivyo suala hili haijatekelezwa kwa ukamilifu jambo |

### 2.1.2 Masuala Mengine ambayo Kamati imeyabaini

#### 2.1.2.1 Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Usimamizi wake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliamua kukagua miradi iliyo katika Mikoa hiyo ili kujiridhidisha na utekelezaji wa miradi hiyo ambayo Kamati haijawahi kuitembelea wala kuikagua.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini kuwa pamoja na ucheleweshwaji au kutokupatikana kabisa kwa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji, usimamizi hafifu wa miradi hiyo ulikuwa ni changamoto katika utekelezaji wa miradi iliyotembelewa.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi matatu yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika**, kundi la kwanza ni miradi ambayo fedha zake zilitengwa na kutolewa kwa mtiririko mzuri lakini kasi ya utekelezaji wake si ya kuridhisha. Mfano wa Mradi huo ni **Mradi Na. 6308** kuhusu Ujenzi wa Mabweni ya Wafungwa na Mahabusu katika Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi uliotengewa Shilingi Bil 1.49 ambazo zote zilitolewa. Katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa fedha zilizotengwa zilitolewa zote tangu Mwezi Septemba, 2017 hata hivyo, hadi Kamati ilipofanya ziara yake Mwezi Machi, 2018, Shilingi 714,235,285.45 zilikuwa bado hazijatumika. Kamati ilipohoji kuhusu kutokutumika kwa fedha hizo, haikupata majibu ya kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la Pili ni miradi ambayo utekelezaji wake umesimama na Mkataba wa Ujenzi wake umesitishwa. Mfano wa Miradi huo ni **Mradi Na. 6301** kuhusu Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mtwara Mjini. Kamati ilipotembelea Mradi huu ilielezwa kuwa utekelezaji wa Mradi huo umesimama na Mkataba wake umesitishwa. Hata hivyo, Kamati ilipohoji haikuelezwa wazi kama Mradi huo ulisitishwa kutokana na ukosefu wa fedha au kutokana na kutoridhishwa na utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika ziara hiyo, Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi na Mikataba ya Serikali jambo ambalo lilisababisha Wakandarasi waliochukuliwa kwa ajili ya Ujenzi kutokuwa na sifa stahiki na malipo ya awali kwa wakandarasi kutolewa kwa dhamana ya Bima badala ya Dhamana ya Benki;

(ii) Uwezo mdogo wa kiufundi na kifedha jambo ambalo limesababisha Jengo hilo kwanza, kujengwa kwa ubora usioridhisha na pili ujenzi huo kusimama kwa muda mrefu;

(iii) Kutokuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya Mkandarasi na Mshauri elekezi jambo lililosababisha ujenzi huo kuwa chini ya kiwango;

(iv) Usimamizi wa miradi usioridhisha kwa upande wa Wizara jambo lililothibitishwa na Wasimamizi wa miradi hii kutokuwa na maelezo yaliyojitosheleza pale ambapo Kamati ilihoji kuhusu utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la tatu ni miradi ambayo haijatekezwa kutokana na kutokupelekewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wake. Mfano wa Mradi huo ni **Mradi Na. 6103** kuhusu Tathmini na Ulipaji wa Fidia ya Ardhi katika eneo la Ras Mshindo. Maelezo yaliyotolewa na Wizara yalibainisha kuwa katika

Mwaka wa Fedha 2017/2018 mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi **3,662,108,122/=** ambazo hadi Kamati ilipotembelea mradi huo fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kupokea na kutekeleza maoni ya Kamati kuhusu kutoa fedha hizo kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hilo, ambapo fedha hizo zilitolewa kwa ukamilifu wake mwezi Novemba 2018.

#### 2.1.2.2 Hali ya Ushirikiano wa Kikanda kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2018, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Hali ya Ushirikiano wa Kikanda wa Majeshi ya Wizara katika SADC na EAC. Wakati wa kujadili Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa pamoja na ushirikiano mzuri ulipo baina ya Majeshi yetu na majeshi ya nchi nyingine za SADC na EAC, baadhi ya Wawakilishi wa Majeshi hushindwa kuhudhuria vikao vya Kikanda kutokana na uhaba wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kutokuhudhuria vikao hivyo kunasababisha kukosekana kwa muendelezo wa ajenda zinazojadiliwa katika vikao hivyo vilevile kuondoa fursa ya Majeshi hayo kujadili kuhusu changamoto mbalimbali na kupata muafaka wa pamoja wa namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kuyawezesha Majeshi kushiriki vikao vya Kikanda kwa kutenga na kutoa fedha kwa ajili hiyo.

#### 2.1.2.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Vitambulisho- NIDA

**Mheshimiwa Spika,** mnamo mwezi Oktoba, 2018 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa- NIDA.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuijadili kwa kina Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa, Mamlaka kupewa ukomo (ceiling) wa Bajeti usiozingatia mahitaji halisi, upungufu wa vyombo vya usafiri, na uhaba wa watumishi ni baadhi ya changamoto zilizosababisha Mamlaka kushindwa kufikia lengo la usajili. Kwa mfano, Mamlaka ilijiwekea lengo la kusajili watu milioni 22.7 kufikia Mwezi Disemba, 2018 lengo ambalo halikufikiwa.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa, kasi ya uzalishaji wa vitambulisho inaathiriwa na uchakavu wa mashine unaotokana na kutofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto ya rasilimali watu, Kamati ilielezwa kuwa Mamlaka ilitumia vijana 200 wa JKT katika kusaidia zoezi la usajili. Kamati inapongeza juhudi hizi katika kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa na ni Rai ya Kamati kuwa vijana hao wapewe kipaumbele pale ambapo Mamlaka itapata kibali cha kuajiri kwa kuzingatia kuwa vijana hao tayari wana uzoefu wa kazi hiyo.

#### 2.1.2.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha Julai-Disemba, 2018

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo na Mafungu yake yote kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kujadili kwa kina kuhusu Taarifa hiyo, Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Ukusanyaji mzuri wa Maduhuli hususan kwa Fungu 51 la Wizara lililokusanya asilimia 78.6 ya lengo, Fungu 28 la Jeshi la Polisi ambalo limekusanya asilimia 131.6 ya lengo.

(ii) Upungufu wa nyumba za makazi na Askari Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji;

(iii) Upungufu wa sare za Maafisa na Askari wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;

(iv) Upungufu wa rasilimali watu katika Idara ya uhamiaji, Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Magereza ina upungufu wa askari na maafisa 12,203, Uhamiahi upungufu wa maafisa 16,517, Zimamoto upungufu wa maafisa 4893);

(v) Uhaba wa magari ya kuzima moto na maokozi, uhaba wa vituo vya zimamoto na uokoaji, na ukosefu wa visima vya kuhifadhia maji;

(vi) Ukomo wa bajeti (ceiling) usiozingatia mahitaji halisi ya matumizi ya Kawaida (OC) ya Wizara, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza;

(vii) Madeni ya Wazabuni. Kwa mfano, hadi kufikia Juni 30, 2018, kwa upande wa maji pekee, Jeshi la Polisi lilikuwa linadaiwa Shilingi Bilioni 9,078,216,936/36; Jeshi la Magereza Shilingi Bilioni 1,620,067,921.10 na Jeshi la Zimamoto jumla ya Shilingi 17,406,878.58.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, changamoto nyingi za Wizara pamoja na Mafungu yake zinasababishwa na ufinyu wa Bajeti ilhali maduhuli yanayokusanywa kwa Mafungu yote ni ya kuridhisha. Hata hivyo, kwa upande wa madeni, Kamati imejiridhisha kuwai Serikali inaendelea kuyalipa kwa hatua.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto ya makazi iliyoorodheshwa hapo juu, Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuendelea kujenga nyumba zao wenyewe kwa gharama nafuu.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitembelea nyumba za Jeshi la Polisi zilizopo Medeli, Dodoma na kuridhishwa na ujenzi wa nyumba zinazoendelea kujengwa kwa gharama nafuu. Hata hivyo, changamoto ya makazi kwa Jeshi la Polisi bado ni kubwa.

#### 2.1.2.5 Udhibiti wa ajali za barabarani

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kudhibiti ajali za barabarani ambapo katika kipindi cha Julai- Disemba, 2018 matukio 1,446,639 yaliripotiwa nchini ikilinganishwa na matukio 1,272,998 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Idadi hii ni pungufu ya matukio 193,641 sawa na asilimia 15.2.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada za Serikali katika kupunguza ajali za barabarani, Kamati imebaini kuwa lipo ongezeko la watumiaji wa barabara wasiotii Sheria za Usalama barabarani kama vile madereva wa bodaboda, ambao wanaendelea kusababisha ajali nyingi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kuwa, ili kufanikiwa zaidi katika kudhibiti ajali za barabarani, ni muhimu Serikali ikamilishe mchakato wa kuifanyia Marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ambayo inatarajia kugusa maeneo yote yenye upungufu ambayo yanachangia kusababisha ajali za barabarani.

#### 2.1.2.6 Udhibiti wa Msongamano wa Mahabusu na Wafungwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza kwa kipindi cha Julai-Disemba 2018, ilibaini kuwa uchache wa magereza, kuongezeka kwa idadi ya watu, upepelezi wa kesi unaochukua muda mrefu bila kukamilika, rufaa za kesi kuchukua muda mrefu bila kusikilizwa, na Mahakama kutegemea zaidi adhabu ya kifungo Gerezani, kumeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa msongamano Magerezani.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu iliendelea kuishauri mara kwa mara Serikali kutoa adhabu mbadala kama vile vifungo vya nje kwa wahalifu wenye makosa madogo; kutumia ipasavyo utaratibu wa *Parole,* na kuhakikisha kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi kutolewa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokutana na Wizara hii Mwezi Januari, 2019 ilielezwa kuwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati kuhusu kudhibiti msongamano wa wafungwa kwa kutumia: -

(i) Utaratibu wa *Parole* ambapo wafungwa 91 walinufaika katika kipindi cha Julai- Disemba, 2018

(ii) Utaratibu wa kifungo cha nje ambapo wafungwa 561 waliachiliwa kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2018; na

(iii) Jeshi kuendelea na ujenzi wa Magereza mapya katika Wilaya za Chato, Geita na Ruangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada hizo Kamati yangu inaendelea kuishauri Serikali kutoa adhabu mbadala kama vile vifungo vya nje kwa wahalifu wenye makosa madogo; kutumia ipasavyo utaratibu wa *Parole,* na kuhakikisha kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi kutolewa kwa wakati.

### 2.1.2.7 Jukumu la Magereza Kujitosheleza kwa Chakula

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipowasilisha Taarifa ya maoni na Mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na mambo mengine, ilishauri Jeshi la Magereza kuwa na Mpango Mkakati wa kujitosheleza kwa chakula.

**Mhesimiwa Spika,** katika kikao chake na Wizara hiyo katika kipindi cha Januari, 2019, Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Magereza limeandaa Mkakati huo unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao makuu ya chakula (Mahindi, mpunga na maharage) katika Magereza kumi (Songwe, Kiberege, Idete, Mollo, kitai, Kitengule, Pawaga, Nkasi, Ludewa na Arusha) ya Kimkakati. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa katika msimu wa kilimo 2018/2019, malengo ni kulima ekari 14,584 za mazao mbalimbali kwa matarajio ya kuvuna tani 12,306.6.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi hizo za Serikali, Kamati imebaini kuwa ushauri wake kuhusu Jeshi la Magereza kuwa na Mpango Mkakati wa kujitosheleza kwa chakula haujatekelezwa kwa ukamilifu kwani Jeshi limeshindwa kuonesha namna ambavyo Mkakati huo utatekelezwa pamoja na gharama za utekelezaji wa mkakati huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijiridhisha kuhusu Mikakati ya Majeshi ya Magereza ya Nchi nyingine hususan Ghana na Afrika Kusini na kubaini kuwa Mikakati yao imebainisha utekelezaji wake ikiwemo kutumia njia za umwagiliaji katika kilimo na uzalishaji wa chakula cha ziada kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya Jeshi la Magereza**.** (Ten – Year Strategic Plan 2015-2025, Ghana Prisons Serviceavailable at www.ghanaprisons.gov.gh)

#### 2.1.2.8 Shirika la Uzalishaji la Magereza (Prison's Corporation Sole)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magereza lilianzishwa mwaka 1974 kupitia *The Corporation Sole Act No. 2.* Shirika hili, pamoja na mambo mengine, lilianzishwa kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji katika Jeshi la Magereza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Shirika hili mwezi Agosti, 2018, ilielezwa kuwa Shirika linashindwa kuzalisha kwa tija kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kifedha kunakosababishwa na Shirika kudai Taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya Shilingi

Milioni 5,171,373,374.26 kwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula cha wafungwa (Sh. 4,591,738,983.73) bidhaa za viwanda vidogo vidogo (Sh. 185,467,976.54), na huduma za makandarasi (Sh. 394,166,413.99).

Aidha, pamoja na madeni hayo, Kamati ilielezwa kuwa Shirika linakabiliwa na uchakavu wa mashine, mitambo na nyenzo zilizopitwa na wakati ambazo zinapunguza uzalishaji na kushindwa kuwa na bidhaa za kutosha za kushindana katika soko.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto ya uwezo wa kifedha kuathiri utendaji wa Shirika, Kamati ilibaini kuwa Shirika linaendeshwa bila kuwa na Bodi kinyume cha matakwa ya Sheria iliyoanzisha Shirika hili, jambo linaloathiri usimamizi wenye tija wa majukumu ya Shirika.

Aidha, Kamati ilijiridhisha kuwa Sheria inayosimamia Shirika la Magereza (The Corporation Sole Act, 1974) ilipitishwa kabla ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992 na hivyo kulifanya Shirika hili ambalo ni la Umma kuendeshwa kinyume na matakwa ya Sheria ya Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto zinazolikabili Shirika, bado limeendelea kutekeleza majukumu yake. Kamati inalipongeza kwa kuwa moja ya Taasisi zinazojenga Mji Mpya wa Serikali Jijini Dodoma kwa gharama nafuu.

#### 2.1.2.9 Idara ya Uhamiaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uhamiaji mwezi Januari 2019, ilibaini kuwa ufinyu wa bajeti umeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Idara. Jambo hili limesababisha Idara kuwa na upungufu wa vitendea kazi na kuchelewa kuwaondoa nchini wahamiaji haramu wanaoshikiliwa katika magereza mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufinyu wa Bajeti, Kamati ilibaini kuwa uwepo wa wahamiaji haramu na usafirishaji haramu wa binadamu kuwa ni changamoto nyingine inayoikabili Idara. Hali hii inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo utandawazi, machafuko ya kisiasa na hali ya kiuchumi katika baadhi ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vyake na Idara ya Uhamiaji katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati imekuwa ikihoji kuhusu weledi wa Maafisa Uhamiaji katika ofisi za maeneo ya mipaka na katika viwanja vya ndege. Kamati ilibaini kuwa wapo Watumishi wachache ambao hawana ujuzi katika masuala ya huduma kwa wateja (customer services) na Diplomasia jambo ambalo linaathiri ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

### 2.1.2.10 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa kipindi cha Julai-Disemba, 2018

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwezi Januari, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti katika Kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Disemba, 2018 mafungu yote ya Wizara (Fungu 57- Wizara, Fungu 38 Ngome na Fungu 39 JKT) yalikusanya asilimia 58.55 ya makadirio. Kamati ilijiridhisha kuwa kasi ya makusanyo hayo ni nzuri na lengo linaweza kufikiwa hadi kufikia Mwezi June, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mafungu yote matatu, Kamati ilielezwa kuwa asilimia 49.78 ya fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zimetolewa. Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida Wizara ilipokea asilimia 49.8 ya fedha iliyotengwa na kwa upande wa Maendeleo, Wizara ilipokea asilimia 49.5.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa na mtiririko wa fedha wa kuridhisha katika nusu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati imebaini kuwa yapo maeneo ambayo yametengewa na kupelekewa fedha kwa kiasi kisichoridhisha licha ya kuwa ni muhimu katika sekta ya Ulinzi. Maeneo hayo ni pamoja na: -

i) Uendeshaji wa mafunzo kwa vijana wa JKT kwa mujibu wa Sheria ambapo posho ya chakula hailipwi kwa wakati hivyo kusababisha kuongezeka kwa madeni ya wazabuni;

ii) Fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makambi ya JKT;

iii) Ruzuku kwa mashirika ya Jeshi ya Nyumbu na Mzinga;

iv) Umiliki ardhi kisheria (Malipo ya fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi)

v) Tathmini ya miradi inayotekelezwa na Wizara;

vi) Kuendeleza programu za utafifiti katika Shirika la Nyumbu.

**Mheshimiwa Spika**, ipo haja kwa Serikali kuona umuhimu wa kutoa kipaumbele katika kutoa fedha kwa ajili ya maeneo hayo yenye tija katika sekta ya ulinzi.

### 2.1.2.11 Utekelezaji wa Majukumu ya Shirika la Nyumbu (TATC) na Mzinga

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2018, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mashirika ya Nyumbu na Mzinga.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Nyumbu, Kamati ilielezwa kuwa, changamoto za uchakavu

na Upungufu wa miundombinu ya teknolojia, Ukosefu wa Mafunzo kwa Wafanyakazi, na kupungua kwa fedha za Ruzuku ya Maendeleo kumeendelea kuathiri utendaji wa Shirika hilo. Kamati ilibaini kuwa, kwa muda wa miaka 25 tangu uhawilishaji wa teknolojia kutoka TTG – Ireland uliposimama Mwaka 1991, Shirika limepokea fedha za ruzuku ya Maendeleo kwa miaka nane (8) tu, jumla ya Shilingi 6,618,456,000/-. Kutokutolewa kwa fedha hizo kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na za kibunifu za Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati vilevile ilibaini kuwa Shirika la Nyumbu limeandaa Mpango Mkakati wake wa miaka kumi 2018-2028 ambao utekelezaji wake utagharimu Shilingi 137,984,000,000/=. Kamati inaamini kuwa, endapo fedha hizi zitatolewa, zitaliwezesha Shirika hilo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na hatimaye kuiongezea nchi kipato.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Mzinga, Kamati ilibaini kuwa Shirika linachangamoto za kibajeti zinazoathiri shughuli za kitafiti za Shirika hilo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Taasisi za Utafiti za Serikali, kama vile COSTECH bado hazijaonesha nia ya dhati ya kulisaidia Shirika la Mzinga katika kutoa fedha kwa Shirika hilo kwa ajili ya utafiti hata pale Shirika lilipowasilisha maombi yake.

#### 2.1.2.12 Utekelezaji wa Majukumu ya Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi- Monduli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Utekelezaji wa Majukumumu ya Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi- Monduli Mwezi oktoba, 2018, ilielezwa kuwa jukumu kubwa la Chuo hiki ni kufundisha Maafisa wanafunzi (Officer Cadets). Aidha, Dira ya Chuo ni kuwa Kituo cha ubora kitaaluma katika Kanda kwa kuwafundisha na kuwaelimisha Maafisa Wanafunzi kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa ili kuwa na weledi wa juu wa kijeshi, uongozi na usimamizi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho Kamati ilibaini mafanikio mbalimbali ya Chuo hicho ikiwa ni pamoja na:-

i. Tangu kuanzishwa kwake Chuo kimefanikiwa kutoa viongozi ambao wameshika nyadhifa za juu Jeshini na Serikalini ikiwa ni ndani na nje ya nchi; na

ii. Chuo kimeendelea kupokea Maafisa Wanafunzi kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Jambo hili linathibitisha imani kubwa ya nchi hizo kwa Chuo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazokikabili Chuo hicho ikiwa ni pamoja na: -

i. Uchakavu wa majengo ya Chuo yakijumuisha makazi ya Askari na Maafisa ambayo yamejengwa tangu mwaka 1972. Majengo hayo hayajafanyiwa ukarabati mkubwa tangu kujengwa kwake;

ii. Uvamizi wa maeneo ya Mafunzo unaofanywa na Wananchi wanaoishi pembezoni mwa mipaka ya Chuo. Uvamizi huo unatokana na uharibifu wa alama za mipaka kwa lengo la kupanua maeneo yao ya kilimo na ufugaji;

iii. Upatikanaji wa maji ambapo chanzo cha maji kinachotumika ni kilekile tangu kuanzishwa kwa Chuo licha ya kuwa maji hayo yanatumika katika maeneo mengine yanayokizunguuka Chuo hicho.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kikao hicho, Kamati ilibaini kuwa maeneo ya baadhi ya Kambi za Jeshi yanavamiwa na Wananchi kwa kudhaniwa ni mapori. Ni vema Serikali ikaendelea kuwaelimisha Wananchi kuwa maeneo hayo yametengwa kimkakati kwa ajili ya matumizi ya kazi za Jeshi na sio mapori yaliyokosa kazi.

### 2.1.2.13 Utekelezaji wa Majukumu ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi katika kusimamia Diplomasia ya Uchumi

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Oktoba 2018, Kamati yangu ilipitia na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu namna Balozi za Tanzania nje ya Nchi zinavyochangia Uchumi wa Taifa kupitia Ushirikiano wa Diplomasia ya Uchumi.

**Mheshimwa Spika**, katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa Tanzania ina Balozi 41 na Konseli kuu 3 katika nchi mbalimbali duniani ambazo zimegawanyika katika Kanda Nne za kijiografia ambazo ni Afrika, Mashariki ya kati, Asia na Australasia, Ulaya na Amerika.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Serikali yalielimisha Kamati kuwa Wizara kupitia Balozi zake kwa kushirikiana na Wadau wengine imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kidiplomasia yanayolenga kuchangia uchumi wa nchi yetu kupitia diplomasia ya uchumi. Haya yamefanyika kupitia kutangaza vivutio vya utalii, kuvutia wawekezaji; kutafuta fursa mbalimbali kama vile mafunzo, ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo ya kina ya Serikali kuhusu juhudi zinazotekelezwa na Balozi katika kukuza Diplomasia ya uchumi, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu ya Balozi zetu katika kukuza Diplomasia ya Uchumi. Changamoto hizo ni pamoja na: -

i. Upungufu wa Watumishi katika Balozi hususan wenye taaluma ya masuala ya uchumi;

ii. Baadhi ya Balozi kutekeleza Diplomasia ya Kisiasa kutokana na nchi ambazo Balozi hizo zipo kutokuwa na fursa za kiuchumi; na

iii. Serikali kutokutoa fedha za kutosha za uendeshaji (OC) jambo linalosababisha Balozi kushindwa kutekeleza vema majukumu yake hususan katika Nyanja ya Diplomasia ya Uchumi.

### 2.1.2.14 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2018

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Januari, 2019 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi cha nusu Mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa mtiririko wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni mzuri kwani hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 46% ya Shilingi 166,606,232,000 zilizokuwa zimetengwa kwa ajii ya Matumizi ya Kawaida. Vile vile, hadi kufikia mwezi Disemba, 2018, Wizara iliweza kukusanya asilimia 52.3 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli ya Shilingi 28,564,158,100.00 yaliyokuwa yamepangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati inaipongeza Serikali kwa mwenendo huu wa makusanyo ambao unadhihirisha kuwa Wizara itafikia malengo yake ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Disemba, 2018, Wizara ilikuwa haijapokea fedha zozote kutoka katika Shilingi 10,400,000,000/= zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto zinazosababishwa na kutopatikana kwa fedha za maendeleo kuwa ni pamoja na: -

i) Balozi nyingi kuendelea kutumia magari ya uwakilishi na huduma yaliyochakaa sana jambo linalochafua taswira ya nchi;

ii) Kuchelewa kujenga au kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo ya Ofisi na makazi jambo linaloisababishia Serikali kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kodi ya pango.

#### 2.1.2.15 Kuwasilisha Maoni kuhusu Azimio la Bunge

**Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliwasilisha Bungeni maoni na Ushauri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuzuia Uendelezaji, Uzalishaji, Ulimbikizaji wa Silaha za Kibaolojia na Sumu pamoja na uangamizi wake (The Convention on Prohibition of Development, Production and Stockpiling of Bacteriological (Biological) and Toxin Weapons and on their Destruction). Lengo la Mkataba huo ni kuzuia uendelezaji na uzalishaji wa silaha za kibaiolojia isipokuwa kwa sababu za kiusalama tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake, ilibaini kuwa Tanzania ilisaini Mkataba huo tarehe 12 Agosti, 1972 ikiwa ni miaka 46 iiyopita na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni wa Nchi tano (5) tu (Haiti, Misri, Somalia na Syria) ambazo zilisaini Mkataba huo lakini zilikuwa hazijauridhia hadi kufikia Mwezi Septemba, 2018, ingawa nchi nyingine 182 za Umoja wa Mataifa zilikuwa zimeshauridhia.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na sababu za msingi zilizotolewa na Serikali kuhusu ucheleweshwaji wa kuridhia Mkataba huo, Kamati inaona ni vyema Serikali ikashughulikia dosari ya kuchelewesha uridhiaji wa Mikataba na Itifaki zilizosainiwa kwa kuziwasilisha Bungeni ili ziridhiwe kwa ajili ya utekelezaji wake.

#### 2.1.2.16 Taarifa za Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Diplomasia ya Kibunge, Mabunge huwa na uwakilishi katika Mabunge na

Vyama mbalimbali vya Kibunge ili pamoja na mambo mengine, kuongeza ushirikiano miongoni mwa nchi mbalimbali na kuwakilisha vema wananchi wa nchi wanachama kwa kutetea maslahi yao kijamii, kiuchumi na kisiasa.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako, kupitia dhana ya Diplomasia ya Kibunge, ni miongoni mwa mabunge mengi duniani yanayoheshimu na kuthamini nafasi yake katika kuwezesha ushawishi mzuri wa mambo ambayo ni ajenda ulimwenguni vilevile kuchochea kasi ya kuridhia mikataba ya kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inalipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge, ambapo limeendelea kuwa na Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na kuwawezesha Wawakilishi hao kushiriki vikao katika Vyama na Mabunge mbalimbali, kwa maslahi ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo: -

**i) PAP**

**Mheshimiwa Spika,** Bunge la Afrika limeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 17 cha mkataba wa Umoja wa Afrika (Constitutive Act of the Africa Union) ambapo nchi 51 zimeridhia Mkataba huo. Bunge hili, pamoja na mambo mengine linalenga kutumika kama chombo cha kurahisisha uhimizaji wa utekelezaji bora wa Sera, Kanuni na taratibu zilizowekwa na Umoja wa Afrika katika kujiletea maendeleo kwa manufaa ya bara la Afrika, na kusaidia kuimarisha Amani, ulinzi na usalama katika Bara la Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Bunge la Afrika kwa kipindi cha Machi 2017 hadi Agosti, 2018. Kamati ilielezwa kuwa moja ya shughuli zilizotekelezwa na PAP, ni uchaguzi wa viongozi wa Bunge la Afrika, Mwezi Mei 2018 ambapo Mhe. Stephen Julius Masele, Mb alichaguliwa kuwa Makamu wa kwanza wa Rais na Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb alichaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Wabunge Vijana katika Bunge la Afrika. Kamati inawapongeza kwa uteuzi huo na inaamini kuwa wataendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Kamati ilielezwa kuhusu shughuli nyingine zilizotekelezwa ikiwa ni pamoja na kujadili migogoro ya Bara la Afrika, kujadili Mikakati bora ya kupambana na ukatiki kwa wanawake, kujadili Mikakati ya kuridhia Itifaki zilizopitishwa na Bunge hilo, na kujadili Umuhimu wa Vijana katika Maendeleo ya Bara la Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili taarifa ya wawakilishi hao, kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Bara la Afrika ikiwa ni pamoja na: -

a) Mashambulizi ya ugaidi ya mara kwa mara yanayoendeshwa na makundi ya Alshabaab, Boko Haram na Alqaeda; na mapigano ya kugombea madaraka katika baadhi ya nchi;

b) Idadi kubwa ya vijana wa Afrika kutokuwa na ajira jambo linalosababisha vijana hao kujihusisha na uhalifu, uhamaji haramu na vitendo vya kigaidi;

c) Nchi wanachama kutoridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali iliyopitishwa na Bunge la Afrika kwa mfano Itifaki inayounda Bunge la Afrika (Reviewed Protocol relating to the Pan African Parliament 2014) na Itifaki ya Umoja wa Afrika kuhusu masuala ya Uhalifu wa Kimtandao (African Union Convention on Cyber Security and Personal Data Protection, 2014) ambazo zote bado hazijaridhiwa na Bunge letu.

d) Ukatili dhidi ya wanawake ambapo wanawake wengi wanakosa haki ya kumiliki ardhi, kupata elimu na kushiriki katika vyombo vya maamuzi na uchumi.

**ii) Bunge la Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki kwa kipindi cha Disemba 2017 hadi Agosti, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Serikali kwa ujumla kwa kuwezesha Kikao cha nne cha Bunge la Nne la Afrika Mashariki kufanyika katika jiji la Dodoma na hususan katika viwanja vya Bunge kuanzia tarehe 10- 25 Aprili, 2018. Jambo hili si tu liliimarisha mahusiano kati ya Bunge lako na Bunge la Afrika Mashariki, bali pia liliongeza fursa za kiuchumi vilevile kulitangaza Jiji la Dodoma kimataifa ambalo kwa sasa ndio Makao makuu ya nchi. Ni rai ya Kamati kuwa, vikao vya Mabunge mengine kama vile vya Bunge la Afrika vipendekezwe na kukubalika kufanyika Dodoma ili kuendelea kulitangaza Jiji hili kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa ikijadili Taarifa iliyowasilishwa, ilibaini yafuatayo: -

i) Wananchi wengi bado hawajui fursa mbalimbali za kuchumi ambazo zipo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

ii) Baadhi ya vituo vya pamoja vya mipakani (One Stop Boarder Posts- OSBP) kama vile cha Rusumo na Kabanga havina huduma ya zimamoto na uokoaji;

iii) Kutokuanza kutumika kwa kituo cha Horohoro ingawa majengo yake yamekamilika;

iv) Kutokuwepo kwa Sera ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto zilizoainishwa hapo juu, Kamati ilibaini kuwa chanagamoto za upatikanaji wa michango kutoka kwa nchi wanachama kunaathiri utekelezaji wa mipango iliyokuwa imewekwa. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mchango wake wa 2017/2018 mapema, ikiwa ni Nchi ya kwanza kufanya hivyo na kuonesha mfano wa kuigwa na Nchi nyingine wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu changamoto za Wawakilishi wa Tanzania, Kamati ilibaini kuwa Wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika Mashariki bado hawana Ofisi kwa ajili ya kufanyia kazi wanapokuwa nchini. Jambo hili limekuwa likiratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo: -

#### a) Masuala ambayo yamekuwa yakitolewa Ushauri mara kwa mara lakini utekelezaji wake si wa kuridhisha

Kutokutekelezwa kwa muda mrefu kwa masuala kumi na tatu (13) ambayo yamekuwa yakishauriwa mara kwa mara na Kamati hususan kuhusu Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki, Umiliki wa Chuo cha Diplomasia, Ubovu wa barabara za mipakani, Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi, *APRM* kutokuwa na hadhi ya Taasisi pamoja na masula mengine yaliyoainishwa katika sehemu ya Pili, kipengele 2.2.2.1, ni kiashiria kuwa Serikali haijayapa uzito unaostahili masuala hayo.

Kamati, kwa mara nyingine, inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuyashughulikia masuala hayo muhimu kwa manufaa ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

**b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

i) Kutokufuata taratibu za kisheria na kikanuni katika kutekeleza miradi ya maendeleo hususan ya Uhamiaji katika Mkoa wa Mtwara kunasababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango na hivyo kupoteza fedha nyingi za walipa kodi ambazo zingeweza kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla;

ii) Kuendelea kutumika kwa Sheria ya Magereza ya mwaka 1974 kunaathiri ufanisi wa utendaji wa Shirika la uzalishaji la Magereza kwani halijiendeshi kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992;

iii) Shirika la Magereza kuendeshwa bila Bodi kunasababisha Shirika hilo kutokutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwani linakosa usimamizi ulioainishwa kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wake;

iv) Taasisi za Serikali hususan Jeshi la Magereza (Fungu 29) kutokulipa madeni yanayodaiwa na Shirika lake la Magereza kunaathiri uzalishaji wa Shirika hilo;

v) Kutokulipwa kwa madeni ya Wazabuni katika Majeshi na Taazisi zilizo chini ya Wizara ya mambo ya Ndani ya nchi kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Majeshi hayo na Taasisi za Wizara;

vi) Kucheleweshwa kutolewa kwa hukumu za kesi za mahabusu kunachangia msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani;

vii) Jeshi la Magereza kutokuwa na Mpango Mkakati madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula kunasababisha Serikali kuingia gharama kubwa katika kutoa huduma ya chakula kwa wafungwa na mahabusu;

viii) Ukomo (ceiling) wa bajeti usiozingatia mahitaji halisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa unaathiri utendaji wa Mamlaka hiyo hususan katika kufikia malengo ya vitambulisho vinavyokusudiwa kutolewa;

xi) Kutotumika ipasavyo kwa mpango wa *parole* na matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

**c) Wizara ya Ulinzi na JKT**

i) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;

ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (beacons) kunachangia uvamizi wa Raia wa kigeni katika baadhi ya maeneo ya mipaka jambo ambalo linaweza kuathiri ulinzi na usalama wa nchi;

iii) Madeni kwa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa Shirika hilo;

iv) Kukosekana kwa uzio katika baadhi ya Kambi za Jeshi kunasababisha migogoro ya ardhi kutokana na wananchi kuvamia maeneo hayo;

v) Wananchi kuvamia maeneo ya kufanyia shughuli za kimkakati za Jeshi la Wananchi yakidhaniwa ni mapori, inaathiri shughuli za majeshi vilevile ni hatari kwa usalama wa Wananchi;

vi) Wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya Wananchi na Vikosi vya Jeshi hilo;

vii) Uchakavu wa majengo ya Chuo cha mafunzo ya Kijeshi cha Monduli kunashusha hadhi ya Chuo hicho kinachotoa mafunzo ya Kimatatifa;

viii) Kutokutolewa kwa fedha za Maendeleo kwa Shirika la Nyumbu kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na za kibunifu za Shirika hilo.

**d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

i) *APRM* kutokuwa na hadhi ya kisheria (legal entity) ya kuwa Taasisi inayojitegemea kunasababisha Taasisi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;

ii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kunaikosesha nchi fursa ya kuvutia mikutano na maonesho ya kimataifa mengi zaidi kufanyika hapa nchini;

iii) *AICC* kutokuwa na majengo yakutosha kwa ajili ya shughuli za mikutano unakiondolea Kituo hicho ufanisi kwa kushindwa kushindana katika soko;

iv) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunasababisha Balozi zetu kutumia magari na majengo yaliyochakaa jambo linaloathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

v) Kukosekana kwa Sera ya Taifa kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki ni jambo la hatari katika mustakabali wa nchi; Serikali imekuwa ikitekeleza shughuli za Mtangamano wa Afrika Mashariki bila ya kuwa na mwongozo bora wa kisera;

vi) Mchakato wa kuifanyia marekebisho Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 unachukua muda mrefu jambo linaloifanya Sera hiyo kutoendana na kasi ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo sasa;

vii) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa na Itifaki zilizosainiwa kunachelewesha Nchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye Mikataba na Itifaki hizo;

viii) Serikali kutokutoa fedha za kutosha za uendeshaji (OC) kunasababisha Balozi kushindwa kutekeleza vema majukumu yake hususan katika Nyanja ya Diplomasia ya Uchumi.

## e) Vyama vya Kibunge

i) Ukosefu wa ajira kwa vijana katika Bara la Afrika bado ni changamoto kubwa ambayo kila nchi mwanachama wa PAP inatakiwa kuishughulikia. Ni vema Serikali ikaandaa mikakati mahsusi ya kuhamasisha vijana kujishughulisha na kilimo chenye tija ikiwa ni pamoja na kuanzisha mitaala ya kilimo na ufugaji kuanzia ngazi ya elimu ya msingi kama njia mojawapo ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana;

ii) Serikali iwasilishe Bungeni Itifaki na Mikataba yote iliyopitishwa na Bunge la Umoja wa Afrika ambayo inatija kwa Taifa letu ili iweze kuridhiwa kwa maslahi ya Taifa; itifaki hizi zijumuishe itifaki inayounda Bunge la Afrika, ili kuliwezesha Bunge hilo kuwa chombo cha kutunga Sheria;

iii) Upo umuhimu kwa Serikali kuweka na kuendeleza mikakati ya kuwashirikisha wanaume na wavulana katika kutatua changamoto zinazowakabili wanawake na wasichana hususan zile zinazohusu ubaguzi na uonevu wa kijinsia;

iv) Upo umuhimu wa nchi wanachama kuridhia Itifaki zinazohusu usalama na Amani katika bara la Afrika na kutekeleza Itifaki hizo;

v) Upo umuhimu kwa Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa mbalimbali za kuchumi zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

vi) Kutokuwa na Ofisi kwa ajili ya Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Kibunge ya Wawakilishi hao wanapokuwa nchini- nje ya vipindi vya Mikutano ya Bunge na Kamati.

### 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: -

#### i. Shirika la uzalishaji la Magereza

**Kwa kuwa** Sheria ya Shirika la Magereza ya Mwaka 1974 (The corporation Sole Act, 1974) ilianzishwa kabla ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992 hivyo kutoendana na matakwa ya Sheria ya Mashirika;

**Na kwa kuwa** kuendelea kutumika kwa Sheria ya Magereza ya Mwaka 1974 kunaathiri ufanisi wa Shirika katika kujiendesha kiushindani kwani linaendeshwa chini ya Uongozi wa Jeshi la Magereza;

**Kwa hiyo basi,** Sheria ya Magereza ya Mwaka 1974 ifanyiwe Marekebisho ili Shirika hili lijiendeshe kwa kujitegemea jambo ambalo litaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake**.**

#### ii. Mkakati wa Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula

**Kwa kuwa** Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Magereza halina Mpango Mkakati madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula;

**Na kwa kuwa** kutokuwa na Mkakati huo madhubuti kunasababisha Serikali kuingia gharama kubwa katika kutoa huduma ya chakula kwa wafungwa na mahabusu**;**

**Kwa hiyo basi,** Jeshi la Magereza liandae Mkakati madhubuti wa kujitosheleza kwa chakula, ikiwa ni pamoja na kutumia rasilimali za ardhi, nguvu kazi na zana za kilimo walizonazo katika kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi ya Magerezani na kwa ajili ya kuuza kwa lengo la kuliongezea Jeshi hilo kipato. Aidha, Mkakati huo ukamilike ndani ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

iii. **Migogoro ya Ardhi katika maeneo ya Jeshi**

**Kwa kuwa** baadhi ya maeneo ya Kambi na Vyuo vya Jeshi havina uzio kuzunguuka maeneo hayo;

**Na kwa kuwa** kukosekana kwa uzio katika maeneo hayo kunasababisha wananchi kuvamia maeneo hayo kwa ajili ya shughuli za kijamii zikiwemo za kilimo na ufugaji, jambo ambalo si tu husababisha migogoro pale wananchi wanapotakiwa kuhama bali pia linahatarisha ulinzi na usalama wa maeneo hayo;

**Kwa hiyo basi,** Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika makambi na vyuo vya Jeshi ili pamoja na kuondoa migogoro ya ardhi inayotokana na wananchi kuvamia maeneo hayo, kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo hayo.

iv. **Utekelezaji wa majukumu ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi**

**Kwa kuwa** baadhi ya Balozi za Tanzania nje ya nchi zina upungufu wa watumishi hususan wenye taaluma ya masuala ya uchumi;

**Na kwa kuwa** upungufu huo unaathiri shughuli za Balozi katika kutekeleza Diplomasia ya uchumi hususan katika kutangaza vivutio vya utalii na kutafuta fursa za ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya Nchi;

**Kwa hiyo basi,** Serikali ipeleke watumishi zaidi ambao wana taaluma ya masuala ya uchumi ili kuziwezesha Balozi

zetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii itengeneze Mkakati thabiti wa kuziwesha Balozi zetu kutangaza utalii. Mkakati huu ni pamoja na kutenga na kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza utalii nje ya nchi pamoja na kutumia watu mashuhuri (celebrities) waliowahi kutembelea vivutio vya Utalii nchini.

v. **Upungufu na Uchakavu wa Majengo ya Ubalozi**

**Kwa kuwa** Mkakati wa Miaka Kumi na Tano (2001/2003- 2016/2017) wa kuendeleza viwanja, kukarabati na kununua majengo ya Ofisi na makazi ya Watumishi Balozini haukutekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha;

**Na kwa kuwa** kutokutekelezeka kwa Mkakati huo kumesababisha Serikali kuendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kukodi nyumba za makazi na Ofisi;

**Kwa hiyo basi,** Serikali ione umuhimu wa kutumia mikopo ya muda mrefu lakini yenye riba nafuu (mortgage) katika kuendeleza viwanja vya Balozi zake ambavyo baadhi yake vimetelekezwa (abandoned) kama kilichopo London-Uingereza, Muscat- Oman na Nairobi- Kenya, pamoja na kuboresha majengo ya Ofisi na Makazi ya watumishi. Hii itasaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za walipa kodi zinazotumika kwa ajii ya kodi za pango, na fedha hizo kuelekezwa katika miradi mingine ya maendeleo.

vi. **Uendeshaji wa Chuo cha Diplomasia**

**Kwa kuwa** Serikali ya Msumbiji imeendelea kutochangia michango ya Chuo cha Diplomasia tangu Mwaka 1982 ilhali bado inatambulika kisheria kuwa mmiliki halali wa Chuo hicho pamoja na Tanzania;

**Na kwa kuwa** Serikali ya Msumbiji kutokuchangia michango hiyo kunasababisha chuo na Wizara ya Mambo

ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuendelea kubeba jukumu la kukiendesha na kugharamia shughui zote za Chuo;

**Na kwa kuwa** Serikali imeendelea kuitumia Tume ya Pamoja ya ushirikiano yaani *Joint Permanent Commission* katika kulipatia ufumbuzi suala la umiliki wa Chuo bila mafanikio;

**Kwa hiyo basi,** Serikali ifanye maamuzi ya kukichukua na kukimiliki Chuo hiki bila ya ubia na Msumbiji.

vii. **Utalii wa mikutano**

**Kwa kuwa** majengo ya kituo cha kimataifa cha Mikutano cha Arusha hayakujengwa rasmi kwa shughuli za mikutano;

**Na kwa kuwa** kutokuwa na majengo rasmi kwa ajili ya shughuli za mikutano unakiondolea kituo uwezo wa kushindana katika soko na hivyo kuathiri utalii wa mikutano;

**Kwa hiyo basi**, Serikali itekeleze mpango wake mahsusi wa kujenga kituo kipya cha mikutano cha *Mount Kilimanjaro International Convention Centre* (MKICC) ambacho pamoja na mambo mengine kitakuwa na eneo la kutosha la maonesho na huduma nyingine muhimu kwa shughuli za utalii wa mikutano. Aidha, Vituo mahsusi vya mikutano vianzishwe katika Mikoa ambayo ina fursa za kitalii kama vile Iringa, Zanzibar, Mwanza na vilevile katika Makao Makuu ya Nchi, Dodoma.

viii. **Ofisi za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki**

**Kwa kuwa** Wabunge wanaoiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki hawana Ofisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ikiwemo kukutana wawapo nchini;

**Na kwa kuwa** kutokuwa na Ofisi hiyo si tu kunaathiri utendaji kazi wa Wabunge hao bali pia ni fedheha kwa Wabunge hao na kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ndilo linalowakilishwa na Wabunge hao;

**Hivyo basi,** Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iharakishe upatikanaji wa Ofisi kwa ajili ya Wawakilishi hao hususan katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi wanapokuwa nchini.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2018 hadi Januari, 2019. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Kangi Lugola, (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Eng. Hamad Masauni, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

……………………………….
Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
06 Februari, 2019

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu wetu, ahsante sana Mwenyekiti. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15)

ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2018 hadi Februari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda sitaweza kusoma taarifa yote, hivyo naomba taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yetu imegawanyika katika maeneo manne, nikijielekeza kwenye majukumu ya Kamati, katika kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya Kikanuni kama yanavyoainishwa katika kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

(i) Kushughulikia bajeti ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini;

(ii) Kushughulikia Taarifa ya Mwaka ya Utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini; na

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia mbalimbali na njia hizo ni kama vile vikao kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara pamoja na taasisi zake. Kamati vile vile ilitumia semina mbalimbali zilizotolewa na wadau kwa ajili ya kujenga uelewa wa Kamati. Kwa nafasi hii nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau wote ambao walijitokeza kutoa semina kwa Kamati, kwani semina hizo zimejenga uelewa mkubwa na kuwezesha Kamati hii kutekeleza shughuli zake. Vilevile Kamati ilitekeleza majukumu yake kupitia ukaguzi wa miradi ya maendeleo ambayo jumla ya miradi

9 ilikaguliwa. Maelezo ya kina ya miradi iliyokaguliwa yanapatikana kuanzia ukurasa wa 2 - 12 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya taarifa ya Kamati imejikita katika uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha nusu mwaka (kuanzia Julai hadi Disemba 2018) na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2018 Wizara ya Nishati ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 275.4 sawa na asilimia 33 ya lengo la bajeti ya nusu mwaka, ambapo Wizara ilitarajia kupokea shilingi bilioni 846.14.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi bilioni 263.29 ni fedha za miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 32 ya fedha zilizopokelewa. Kwa upande wa matumizi ya kawaida shilingi bilioni 12.01 zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 88 ya fedha zilizotakiwa kupokelewa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ya Madini ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 16.5 sawa na asilimia 83 ya lengo la bajeti ya nusu mwaka 2018/2019 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kati ya shilingi bilioni 19.64 ambazo Wizara ilitarajia kupokea. Kwa miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha, mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Dodoma ndiyo mradi pekee ulipokea fedha ambapo ilipokea kiasi cha shilingi milioni 100. Hata hivyo, Wizara ilipokea ruzuku ya kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ya Madini katika Mji wa Serikali Ihumwa, Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika shughuli za Wakala wa Umeme Vijijini. Hadi kufikia Disemba 31, Wakala wa Umeme Vijijini ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 257.36 ikiwa ni zaidi ya matarajio ya kupokea shilingi bilioni 206.04; ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 125. Pamoja na upatikanaji mzuri wa fedha, Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa ni kikwazo katika

utendaji kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni kama vile:-

(i) Kuwepo kwa hali isiyoridhisha ya upatikanaji wa vifaa muhimu vya umeme vinavyozalishwa hapa nchini kama nguzo, nyaya na mashine umba, kufuatia kuchelewa kufunguliwa kwa Hati za Muamala yaani LC. Sambamba na hilo, kumekuwepo na tatizo la baadhi ya viwanda nchini kushindwa kuzalisha vifaa kama walivyokubaliana na wakandarasi; na halikadhalika viunganishi vinavyoagizwa nje ya nchi kuchukua muda mrefu kuwasili nchini.

(ii) Katika baadhi ya maeneo ya miradi kumekuwa na mwitikio mdogo wa wananchi kuunganishiwa katika umeme.

(iii) Usimamizi usioridhisha kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini; na

(iv) Baadhi ya maeneo yamekuwa yakirukwa kupelekewa umeme hasa katika maeneo muhimu kama shule, zahanati na maeneo mengine ya kijamii. *(Makofi)*

(v) Kumekua na mgogoro wa kodi na ushuru kwa wazalishaji wa nguzo katika Mkoa wa Iringa, mgogoro ambao umechukua muda mrefu kupatiwa utatuzi takriban miezi mitatu na hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa. Hadi kufikia Desemba 31, 2018 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa umefikia MW 1,565 ambapo MW 573 ni kutokana na nguvu ya maji, MW 892 ni kutokana na gesi asilia, MW 88 ni mafuta na MW 10 *biomass.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa mitambo hiyo umejumuisha mitambo ya wazalishaji binafsi ambayo

huchangia kwa asilimia 13.21. Aidha, Shirika linamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua umeme wa *MW* 36.46 na hivyo kufanya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia *MW* 1,602.18.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzalishaji wa umeme nchini ikiwa hivyo, mahitaji ya juu katika mfumo wa gridi ya Taifa umefikiwa kuwa *MW* 1,165 na mahitaji hayo yalifikiwa mwezi Novemba, 2018 ikilinganishwa na *MW* 1051 zilizokuwa zimefikiwa hadi mwezi Juni, 2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 6.21.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejiwekea lengo la kuzalisha umeme kiasi cha *MW* 5000 ifikapo mwaka 2020 na *MW* 10000 ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati, upo uwezekano mkubwa kwa nchi yetu kutofikia uzalishaji wa *MW* 5000 ifikapo mwaka 2020. Taarifa zinaonesha kuwa uwezekano uliopo ni kufikisha *MW* 2,780 na hii itategemea kukamilika kwa wakati kwa zoezi la uchambuzi wa zabuni unaoendelea sasa kupata Kampuni za wawekezaji binafsi zenye sifa ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme yenye jumla ya *MW* 950 ambako katika hizo *MW* 600 ni ya kutokana na Makaa ya mawe, *MW* 150 ni Umeme wa Jua na *MW* 200 ni Umeme wa upepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendana na kasi yetu ya ujenzi wa Uchumi wa Viwanda, Kamati yako inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji ya Mto Rufiji upewe kipaumbele cha juu katika kupelekewa fedha za kutosha na kusimamiwa kikamilifu ili ukamilike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kisheria *TANESCO* ndio mnunuzi pekee wa umeme nchini kutoka kwa wazalishaji, wawekezaji binafsi wamekuwa wa kipata wakati mgumu wa kufikia makubaliano na *TANESCO* katika bei za kuuziana umeme na wakati mwingine majadiliano hayo huchukua muda mrefu kuliko ilivyokusudiwa. Hivyo kuchangia

kwa kiasi kikubwa kuwakatisha tamaa wawekezaji binafsi wenye nia ya kuwekeza na kuendeleza uzalishaji wa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa *TANESCO* ihakikishe inaweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza na kuzalisha nishati ya umeme nchini. Aidha, Kamati inashauri uwepo mfumo madhubuti na unaoeleweka ambao utawezesha wawekezaji kufanya maamuzi ya kuwekeza nchini kwa kuzingatia vigezo vilivyo wazi na matakwa ya nchi yetu, bila kuiingiza *TANESCO* kwenye mzigo wa kununua umeme kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la *ZECO*, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa uamuzi wa kuifutia rasmi *ZECO* deni lililokadiriwa kufikia shilingi bilioni 22.8 lililotokana na kodi ya ongezeko la thamani kwa manunuzi ya umeme toka *TANESCO*; na vilevile kuifanya kodi ya ongezeko la thamani kuwa asilimia sifuri kwa umeme unaouzwa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili, Kamati inatambua mchango wako na inakupongeza sana kwa kulipa jambo hili uzito mkubwa ambao umesaidia Serikali kuharakisha kumaliza utata wa deni hili na kufikia maamuzi ya kuhakikisha mauzo ya umeme ya *ZECO* yanafanyika bila kutozwa kodi ya ongezeko la thamani kwa mujibu wa Sheria za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuleta Bungeni Muswada wa marekebisho ya Sheria ili maamuzi haya yaweze kupata nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini; Bunge lako liliidhinisha jumla ya shillingi bilioni 8.56 kwa ajili ya Tume ya Madini kwa matumizi ya kawaida pamoja na mishahara ya watumishi. Hadi kufikia Disemba, 2018, Tume ya Madini ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 8.32 ikiwa ni sawa na asimilia 94 ya lengo la nusu mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Tume kupokea kiasi kikubwa cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, Kamati imebaini fedha hizi kutokidhi mahitaji ya kuiwezesha Tume kama msimamizi wa shughuli zote za madini kutimiza majukumu yake kikamilifu. Kwa hali ilivyo sasa, Tume inakabiliwa na changamoto kubwa ya Sheria ya Madini kutokueleweka vyema kwa jamii ya wachimbaji, wafanyabiashara wa madini na umma kwa ujumla na hivyo kusababisha uwepo wa migogoro ya kutolipwa kwa baadhi ya tozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua na kuthamini Sekta ya Madini nchini, Kamati inapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Wizara ya Madini kwa kuandaa mkutano mkubwa tarehe 22 Januari, 2019 ambao ulijumuisha wadau mbalimbali wa sekta ya madini kwa lengo la kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali kuhusiana na sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mkutano huo, Kamati imenufaika kwa kusikia changamoto na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na wachimbaji, wauzaji na wachenjuaji wa madini nchini. Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia kazi kwa kina maazimio yote ishirini (20) ya mkutano huo. Kama yanavyoonekana kuanzia ukurasa wa 32 hadi wa 34 wa taarifa hii. Aidha, Kamati itaendelea kushirikiana na Wizara na wadau wote wa sekta ya madini ili kuweza kuangalia namna bora ya kushauri kutatua changamoto za sekta ya madini ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Ndogo ya Gesi, pamoja na kuwepo kwa wingi wa gesi asilia nchini bado matumizi yake ni madogo ukilinganisha na gesi iliyopo. Hivyo ni rai ya Kamati kwa Serikali kutafuta masoko ya kuuzia gesi asilia kwa matumizi mengine ya viwandani na majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kufanyia marejeo mikataba iliyopo ili kukidhi matakwa ya sheria ya

sasa. Nchi yetu kwa sasa ina Mikataba hai ipatayo 11 katika eneo la utafutaji na uendelezaji wa shughuli za Gesi Asilia hapa nchini ambapo katika hiyo mikataba mitatu ipo kwenye hatua za uzalishaji na mikataba nane ipo katika hatua ya utafutaji na ugunduzi. Mikataba yote hii iliingiwa kwa sheria za zamani na kwa msingi huo inakinzana na sheria zilizopo sasa yaani Sheria ya Petroli, Sura 392 ya mwaka 2015; Sheria ya Mapitio ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017; na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017. Mikataba hii imeinyima nchi fursa ya kunufaika kikamilifu na rasilimali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka katika kufanya majadiliano na wawekezaji ili kurekebisha vifungu/masharti yenye kasoro kwenye mikataba hiyo ili iendane na matakwa ya sheria zilizopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa majukumu na bajeti ya wizara kwa kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama yanavyoonekana kuanzia ukurasa wa 36 hadi ukurasa wa 37 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na kufanyika kwa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na kukutana na wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni ya jumla yanayoonekana kuanzia ukurasa wa 38 hadi ukurasa wa 40 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuainisha maoni ya jumla, Kamati inapendekeza Bunge liliridhie Maazimio ya Kamati kuwa Maazimio ya Bunge kama yanavyoonekana kuanzia ukurasa wa 41 hadi ukurasa wa 48 wa taarifa hii.

Hitimisho, katika kuhitimisha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge na kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa ushirikiano wenu, kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba watambuliwe, na majina yao yote yaingie kwenye *Hansard* kama yalivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati inapongeza Wizara ya Nishati chini ya Uongozi wa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mbunge; Naibu Waziri Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge Katibu Mkuu, Dkt. Khamis Mwinyimvua, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ujumla wao. Aidha, Kamati inaipongeza pia Wizara ya Madini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge, Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hivyo kuwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Steven Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati yetu. Pia namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto pamoja na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Felister Mgonja kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kama maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu, Mwenyekiti asante sana.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

______________________

**[*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*]**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2018/2019.

***1.1. Majukumu ya Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kiKanuni kama ilivyoanishwa katika kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini;
b) Kushughulikia Taarifa za Mwaka za Utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini pamoja na;
c) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

## *1.2. Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni vikao kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara pamoja na taasisi zake, semina mbalimbali pamoja na Ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Njia hizi ziliwezesha Kamati kufikia malengo ya utekelezaji wa majukumu yake.

### 1.2.1 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa fedha na ambayo haikutengewa fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2017/2018. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Mara (Musoma), Shinyanga, Tabora (Nzega na Igunga) pamoja na Singida.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo;

i. Miradi ya Umeme Vijijini, Mara.

ii. Mgodi wa Buhemba, Musoma (Mara).

iii. Mgodi wa mchimbaji wa kati, Musoma(Mara).

iv. Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv Iringa–Shinyanga (Backbone), Shinyanga.

v. Miradi ya umeme Vijijini, Shinyanga.

vi. Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).

vii. Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega, Tabora.

viii. Miradi ya Umeme vijijini, Singida.

ix. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, Singida.

***1.3. Maelezo ya Miradi pamoja na changamoto zake***

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya miradi pamoja na changamoto ambazo Kamati ilizibaini kwa kila mradi wakati wa ukaguzi:

**i) Miradi ya Umeme Vijijini, Mkoa wa Mara**

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa ambayo miradi ya umeme vijijini Awamu ya Tatu inatekelezwa, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Mradi huu unahusu miradi midogo ya *Densification*, Uendelezaji wa Gridi ya Taifa (Mizunguko ya I na II) na Mradi mdogo wa maeneo nje ya gridi (off-grid).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea vijiji viwili vya wilaya ya Butiama ambavyo ni Busegwe na Muriaza. Vijiji hivi vipo katika mradi wa ujazilizi (Densification). Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya ushirikishwaji mdogo wa wananchi pamoja na Viongozi wa maeneo husika na hivyo kusababisha maeneo muhimu na yenye watu wengi kutofikishiwa umeme kama inavyotakiwa. Aidha, changamoto hiyo imesababisha maeneo mengi katika vitongoji na vijiji kurukwa wakati wa upelekaji wa umeme huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini kuwa mashine umba (Transformers) zilizofungwa kwa ajili ya kusambaza umeme zina uwezo mdogo kulinganisha na mahitaji ya eneo husika, hali ambayo inapelekea maeneo hayo kutokuwa na umeme wa uhakika.

**ii) Mgodi wa Buhemba, Musoma (Mara)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mgodi wa dhahabu wa Buhemba unaomilikiwa na Serikali kupitia STAMICO. Serikali iliukabidhi mgodi huu kwa STAMICO mwaka 2011 kupitia **Leseni, Prospecting License (PL) namba 7132/ 2011** iliyotolewa mwezi Julai, 2011, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 8.18. Awali mgodi huu ulikuwa ukimilikiwa na Kampuni ya Meremeta Limited, ukijulikana kama *Buhemba Gold Mine Limited* kabla ya kufungwa rasmi mwaka 2007.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi sasa kiasi cha mashapo (indicated resources) yenye **wakia 441,772** kimethibitika kuwemo kwenye miamba migumu kutoka katika migodi ya wazi ya Buhemba 1, Buhemba 4, Kilamongo South na Kilamongo North. Hata hivyo, pamoja na kuthibitika kuwepo kwa mashapo ya kutosha hakuna shughuli yoyote ya uchimbaji inayoendelea katika mgodi huu kutokana na ukosefu wa fedha za kuendeleza Mgodi huo. Aidha, uvamizi unaofanywa na wachimbaji wadogo wanaozunguka eneo la Mgodi umesababisha uharibifu wa mazingira ya Mgodi, upotevu wa vifaa na kuhatarisha maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa ziara ya Kamati mgodini hapo, ilibainika kuwa Mradi unakabiliwa na madai ya mapunjo ya mafao

ya wafanyakazi wa zamani wa Mgodi walioachishwa kazi mwaka 2007; wakati Meremeta ilipokuwa mmiliki wa Mgodi huo. Madai hayo ya Wafanyakazi 129 yanadaiwa kufikia **shilingi milioni 89,021,324**. **Aidha, katika vikao vya Kamati vya mwezi Januari, 2019 Kamati ilifahamishwa na Wizara kuwa tathmini/uhakiki wa deni hili uliofanyika hivi karibuni umebaini kuwa kwa sasa deni hilo limeshuka na kufikia Shilingi milioni 40. Kushuka huku kunatokana na kuondoa gharama ambazo kimsingi mgodi ulizigharamia lakini zikajumuishwa kwenye madeni yanayopaswa kulipwa.**

**iii) Mgodi wa Mchimbaji wa kati, Musoma (CATA MINING)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia iliweza kutembelea mgodi wa mchimbaji wa kati katika kijiji cha Kiabakari mkoani Mara na kujionea uwekezaji katika mgodi wa dhahabu wa *Cata Mining.*

**Mheshimiwa Spika,** CATA inamilikiwa kwa ubia kati ya Mtanzania, na Mkanada, kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50. Aidha mwaka 2014, CATA ilipata leseni ya uchimbaji wa madini namba 483/2015 kwenye eneo la kilima cha Kataryo. Hata hivyo eneo hili halikuwa na dhahabu ya kutosha. Mwaka 2015 CATA iliingia makubaliano na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuchenjua mabaki ya mchanga yaliyoachwa na wachimbaji wa kikoloni. Tarehe 10 Agosti 2016, CATA ilipata leseni ya utafiti wa madini ya dhahabu **PL 10645/2015,** katika eneo la Mgodi wa Kiabakari baada ya kushinda zabuni iliyokuwa imetangazwa na Wizara ya Madini. Mgodi huo upo katika eneo la Kambi

ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kata ya Kiabakari, Wilaya ya Butiama. Mwezi Novemba, 2016, CATA iliingia mkataba na (JWTZ) ikiwa ni muendelezo wa mkataba wa mwanzo wa uchenjuaji, lakini makubaliano hayo yalikuwa ni kuruhusu CATA kufanya utafiti wa madini ya dhahabu katika mgodi wa Kiabakari. Mkataba huu uliitaka CATA kufanya utafiti na baada ya kugundua dhahabu iingie makubaliano mapya na JWTZ kuhusu uchimbaji na mgawanyo wa faida ya uchimbaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kukosa leseni ya umiliki katika eneo la Jeshi, Kampuni hii iliamriwa kufunga shughuli zake za uchimbaji toka mwezi Julai, 2017. Aidha, CATA ilitarajia katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2017, kuzalisha kilo 100 za dhahabu kwa kila mwezi, hivyo mpaka kipindi cha mwezi Machi 2018, Kampuni ilikua imepata hasara inayofikia **Dola 36.0 milioni**, kutokana na kusimama kwa uzalishaji zaidi ya miezi tisa. Aidha, Kampuni hii imeshindwa kuendelea na urejeshaji wa mikopo inayofikia **Dola 50.0 milioni**, kwenye mabenki ya hapa nchini. **Pamoja na Wizara ya Madini kutekeleza jukumu la kumpatia leseni mchimbaji huyu wa kati, bado shughuli za uchimbaji kwa mchimbaji huyu hazijaanza hadi sasa, kwakuwa bado hajafikia makubaliano na Jeshi. Ni Rai ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na mchimbaji kwa ajili ya kufikia muafaka wa jambo hili, ili apatiwe kibali cha kuchimba dhahabu na hivyo Wizara kukusanya mapato kutoka kwa mchimbaji huyu aliyefanya uwekezaji mkubwa.**

**iv) Mradi wa kusafirisha umeme wa msongo 400kv Iringa – Shinyanga (Backbone), Shinyanga**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mradi wa REA awamu ya tatu mkoa wa Shinyanga umepata miradi miwili, ambayo ni mradi wa REA – III (grid extension) na mradi wa kuvipatia huduma ya umeme vijiji vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovolti 400 (VEI/BTIP).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea vijiji vya Negezi na Bulimba ambavyo ni baadhi ya vijiji vya Mradi wa VEI/BTIP unaotekelezwa wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na miradi hii inayoendelea mkoani Shinyanga, changamoto kubwa ilionekana kuwa, bado vijiji vingi havijapata umeme kwa awamu ya kwanza ya mradi. Aidha, maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri za miji ya Kahama, Kishapu na Shinyanga bado hayajafikiwa na huduma ya umeme.

**v) Miradi ya Umeme Vijijini, Wilaya ya Nzega na Igunga (Tabora).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi ya REA inayotekelezwa katika wilaya ya Nzega kijiji cha Idala pamoja na kijiji cha Iborogero wilayani, Igunga.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu pia mkoa ulipata mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji 12 vilivyoko pembezoni mwa mkuza wa

njia kuu ya kusafirisha umeme (400KV) kwa wilaya ya Igunga katika mkoa wa Tabora na wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga. Pamoja na utekelezaji unaoendelea katika miradi hii, Kamati iliona changamoto ya maeneo mengi ya vijiji na vitongoji kukosa umeme. Aidha, utekelezaji ulionekana ni wa kusuasua kutokana na ukosefu wa Fedha na udhaifu wa ushirikishwaji wa viongozi wa wananchi wa maeneo husika katika uainishaji wa maeneo hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kurukwa kwa maeneo katika sehemu moja.

**vi) Chuo cha Madini Kampasi ya Nzega, Tabora**

***Mheshimiwa Spika,*** *Kamati yako ilitembelea chuo cha madini katika kampasi ya Nzega, mkoa wa Tabora. Chuo cha Madini kilikabidhiwa rasmi eneo lililokuwa linamilikiwa na Kampuni ya uchimbaji madini ya* ***Resolute (Tanzania) Ltd*** *na kuanzisha Kampasi ya Nzega tarehe 12 Desemba, 2014. Kampuni hiyo ilikuwa inamiliki Kitalu cha Uchimbaji (Special Mining Licence) namba SML 19/97 kilichopo katika Kata ya Lusu, Wilaya ya Nzega, kinachopatikana katika sehemu ya ramani (Quarter Degree Sheet – QDS) 80/1 chenye ukubwa wa kilomita za mraba 38.95. Hivyo eneo lote la QDS 80/1 lilikabidhiwa kwa Chuo cha Madini pamoja na rasilimali zake.*

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Kampasi ya Nzega ni kuongeza wataalam wa kada ya kati katika sekta ya madini. Hivyo pamoja na shughuli nyingine za taaluma Kampasi ya Nzega ni mahsusi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo katika fani za Jiolojia na Utafutaji wa Madini, Uhandisi Uchimbaji Madini,

Uhandisi Uchenjuaji Madini, Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini na Upimaji wa Ardhi na Migodi. Vilevile, lengo la pili ni kukipanua Chuo cha Madini ili kiweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi kwa sababu katika Kampasi ya Nzega kuna migodi (Pits) ambayo itawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo. Lengo la tatu lilikuwa ni kuifanya Kampasi ya Nzega kuwa Kitovu cha Mafunzo *(*Centre of Excellence*)* kwa ajili ya kutoa mafunzo ya rasilimali za madini na mazingira kwa wachimbaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na uwepo wa rasilimali hizi, Serikali inakabiliwa na changamoto ya ulinzi wa eneo linalozungukwa na chuo ukizingatia wachimbaji wadogo wamekua wakivamia eneo kwa ajili ya kutaka kuendeleza shughuli zao za uchimbaji. Aidha, Kamati ilijionea changamoto ya kukosekana kwa huduma nyingine za kijamii kama makanisa/misikiti n.k.

**vii) Miradi ya Umeme vijijini mkoa wa Singida pamoja na Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme 400kv Singida – Arusha, mkoani Singida**


**Mheshimiwa Spika,** mkoa wa Singida unapata umeme kutoka Gridi ya Taifa kupitia njia kuu za kusafirisha umeme za msongo wa Kv 400. Katika mradi wa REA awamu ya tatu, mkoa wa Singida umepata miradi miwili (2) ambayo ni mradi wa REA – III (Grid Extension) na mradi wa kuvipatia huduma ya umeme vijijini vilivyo ndani ya mkuza wa njia kuu ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kv 400.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea ofisi ya TANESCO ya mkoa na kuona kituo cha kupozea umeme (substastion) cha TANESCO kupitia mradi huu wa msongo wa umeme wa Kv 400. Aidha, Kamati ilitembelea kijiji cha Kisaki na kujionea hali ya upatikanaji wa umeme.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na miradi inayoendelea kwa mkoa huu bado kuna changamoto ya vijiji kukosa umeme. Aidha maeneo mengi yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Singida bado hayajafikiwa na huduma ya umeme. Vilevile kuna maeneo ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani hapo hayajapatiwa umeme kama vile mradi wa umwagiliaji maji.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yako, zilibainika changamoto mbalimbali zinazochangia kuzorota kwa utekelezaji wa Miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati**.** Changamoto kubwa katika ukaguzi wa miradi yote ni ukosekanaji wa Fedha za kutekeleza miradi. Kwa upande wa REA, changamoto ya ukosekanaji wa fedha umesababisha wakandarasi kucheweleshewa malipo hivyo kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati. Aidha, upatikanaji wa vifaa vya kutekeleza miradi ya REA kama nyaya, mashine umba (Transformers) na nguzo, umesababisha kwa kiasi kikubwa miradi hii kutekelezwa kwa kasi ndogo. Kamati pia ilibaini kuwa uhakiki wa mali za wananchi wanaopaswa kupisha mradi kuchukua muda mrefu na hivyo kuathiri mpango kazi wa utekekelezaji wa miradi. **Ni Rai ya Kamati kwa Serikali kuhakikisha inapeleka fedha za miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili miradi hiyo iweze kutekelezeka kwa ufanisi na kwa wakati.**

**MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2013/2014-2017/2018)**




*uwa Wizara ya*

***ekelezaji wa***
***Fedha 2018/***

a ya ukaguzi
a maoni

inakabidiliwa
upelekwaji wa
yosababisha
ekeleza miradi
o basi, Kamati
na kwa wakati
kwa kuwa fedha hizi zina wigo na ni tozo za wananchi.

ii. Katika kutekeleza miradi hii ya umeme vijijini, bado maeneo mengi ya vijiji na vitongoji yanarukwa. Kamati inaishauri Serikali, kuainisha maeneo kwa kuwashirikisha viongozi pamoja na kuongeza wigo kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii, ili wigo (scope) uwe ni wa kukidhi maeneo mengi ya vijiji.

iii. Miradi ya umeme vijijini bado inakabiliwa na changamoto ya baadhi ya maeneo kuendelea kufungwa Mashine umba (Transformers) zisizokidhi viwango na mahitaji ya maeneo. Kwenye baadhi ya maeneo Mashine umba zinazofungwa zimebainika kukosa ubora wenye kuaminika. Kamati inashauri Serikali kuzifanyia ukaguzi wa kina Mashine umba kabla wakandarasi hawajazifunga katika maeneo ya miradi.

iv. Kamati inashauri Serikali iendeleze jitihada zake za kukiendeleza Chuo cha madini kampasi ya Nzega ili kiweze kudahili wanafunzi kwasababu miundombinu ya chuo iko katika hali nzuri.

v. Kamati inashauri Serikali kuwa karibu na wachimbaji wadogo na wa kati ili kuweza kuchukua hatua za haraka katika kuwasaidia kutatua changamoto wanazokabiliana nazo.

vi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kulifanyia kazi pendekezo la kutafuta mbia wa kuweza kuendeleza mgodi wa Buhemba. Aidha, Kamati inashauri mchakato wa kumpata mbia huyu uharakishwe kuwezesha mbia kuanza kazi ndani ya mwaka huu wa fedha.

vii. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusiana na mazingira ya uchimbaji wao. Aidha, jitihada za makusudi zifanyike kuwatengea maeneo ambayo yatawasaidia kuendeleza shughuli zao za uchimbaji.

viii. Kamati inapendekeza pia wananchi kulipwa fidia zao kwa wakati hasa katika maeneo ambayo miradi mbalimbali inatekelezwa.

### *1.5. Semina kwa Wajumbe wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Januari 2019 Kamati iliweza kupata semina mbalimbali ambazo zililenga kuipatia fursa kufanya majadiliano ya kina na wadau mbalimbali katika sekta ya nishati na madini. Aidha, Kupitia Semina hizo Kamati yako ya Nishati na Madini imekuwa na uelewa mpana kuhusu sekta ya madini, mafuta na gesi asilia ambazo inazisimamia, hivyo kuelewa vyema mambo muhimu ya kuzingatia kama Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kushauri na kuisimamia vyema Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi katika kuhakikisha vibali vinapatikana kwa wadau wa nje pale ambapo wanahitaji kufanya majadiliano na Kamati yako. Ni dhahiri kwamba, unasimamia vyema Bunge hili na kutekeleza majukumu yako kikamilifu kwa kuzingatia misingi, Kanuni na miongozo ya kuendesha Bunge katika kutoa fursa mbalimbali.** Aidha, Maelezo ya kina ya semina zilizofanyika ni kama ifuatavyo;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati ya Madini ilikutana na kufanyiwa Semina na Taasisi ya Tanzania *Chamber of Mines* siku ya Jumatatu tarehe 7 Mei, 2018, Dodoma. Lengo la semina hiyo

kwa wajumbe wa Kamati ilikuwa ni kujadili maendeleo ya sasa katika sekta ya madini hususan wachimbaji wakubwa na watafiti wa sekta ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilikutana katika Semina na Wizara ya Nishati siku ya Jumamosi tarehe 12 Mei, 2018, Dodoma. Lengo la semina hiyo kwa wajumbe wa Kamati ni kujadili na kuongezewa uelewa kuhusu uendelezaji wa Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji ya mto Rufiji (Stigler's Gorge) pamoja na Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati ya Madini ilikutana na Taasisi ya *Tanzania Renewable Energy Association* (TAREA) siku ya Jumanne tarehe 4 Septemba 2018, Dodoma. Lengo la semina hiyo kwa wajumbe wa Kamati lilikuwa ni kuwajengea uwezo wajumbe katika eneo la uendelezaji na uzalishaji umeme kwa kutumia nishati jadidifu katika maeneo yaliyo nje ya gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilikutana katika Semina na Wizara ya Madini siku ya Jumamosi tarehe 25 Agosti, 2018, Dodoma. Lengo la semina hiyo lilikuwa ni kupokea na kujadili taarifa kuhusu muundo wa Wizara ya Madini na Tume ya madini, ukusanyaji wa maduhuli Mirerani na udhibiti wa utoroshwaji wa madini nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilikutana katika Semina na Shirika la WWF tarehe 11 Septemba, 2018 Dodoma. Lengo la semina hiyo kwa wajumbe wa Kamati lilikuwa ni kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za nchi hususani katika uendelezaji wa nishati jadidifu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati ilikutana katika semina na Wizara ya Nishati tarehe 08-09 Septemba, 2018, Dodoma. Lengo la semina hiyo ilikuwa ni kuwapitisha wajumbe wa Kamati katika taasisi zipatazo tisa zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, ili kuwawezesha kufahamu majukumu yao pamoja na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 8 Novemba, 2018, Taasisi ya Hakirasilimali ilikutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa lengo la kubainisha mapungufu ambayo wameyabaini katika Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji ya Mwaka 2015 [TEITA, 2015] ambayo wanaona mapungufu hayo yamekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Natural Resource Government Institute* (NRGI) ilikutana na Kamati yako mnamo tarehe 12 na 13 Novemba, 2018 Dodoma kwa lengo kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika sekta hizi muhimu za madini, mafuta na gesi. Semina hizo zimekuwa zikilenga kuwajengea uwezo wajumbe kuhusu Sheria mbalimbali zinazohusu udhibiti na ukusanyaji wa Mapato kutoka kwenye Sekta hizi kwa maendeleo ya uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati yako, Ofisi ya Bunge imekua na utaratibu mzuri wa uandaaji wa semina elekezi kupitia mradi wa *UNDP* (***Legislative Support Program***) kuhusu masuala ya kutunga Sheria pamoja na Kanuni mbalimbali za uendeshaji wa Shughuli za Bunge. Mafunzo haya yamekua muhimu sana katika kuongeza uelewa mpana kwa wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kibali chako, tarehe 20 Januari, 2019 Kamati yako ilikutana na Uongozi wa

kampuni ya *Globeleq* ambayo iliwasilisha taarifa ya utekelekezaji wa shughuli za kampuni ya SONGAS katika mradi wa kuzalisha umeme kwa njia ya gesi asilia. Kupitia kikao hicho, Kamati ilielezwa juu ya makubaliano ya kimkataba kati ya SONGAS na TANESCO katika kuuziana umeme, aidha, wajumbe walipata uelewa na kushauri vyema katika masuala ya mikataba na utekelezaji wa mradi kati ya SONGAS na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakupongeza wewe binafsi kwa kuunda Kamati maalum za Bunge za Tanzanite, Almasi, na Sekta ndogo ya Gesi. Taarifa za Kamati hizi zimesheheni mapendekezo ambayo yakifanyiwa kazi ipasavyo yataliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali tulizonazo. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hizi ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali zake.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### *2.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Ujumla*

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha nusu mwaka (kuanzia Julai hadi Disemba 2018) na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2018 Wizara ya Nishati ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 275.40** sawa na **asilimia 33** ya lengo la bajeti ya nusu mwaka 2018/19 ambapo Wizara ilitarajia kupokea **shilingi bilioni 846.14**. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa **shilingi bilioni 263.29** ni fedha za miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 32** ya fedha zilizopokelewa. Kwa upande wa matumizi ya

kawaida **shilingi bilioni 12.01** zilipokelewa ambazo ni sawa na **asilimia 88** ya fedha zilizotakiwa kupokelewa katika kipindi hicho.
Aidha, Wizara ya Madini ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 16.5** sawa na **asilimia 83** ya lengo la bajeti ya nusu mwaka 2018/19 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya **shilingi bilioni 19.64** ambazo Wizara ilitarajia kupokea. Kwa miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha ni mradi wa ujenzi wa ofisi za Dodoma pekee ndiyo ulipokea fedha kiasi cha **Shilingi milioni 100,** hata hivyo Wizara ilipokea ruzuku ya kiasi cha **shilingi bilioni 1** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ya madini katika mji wa Serikali Ihumwa, Dodoma. Aidha, taasisi zifuatazo ziliwasilisha taarifa kwenye Kamati na kujadiliwa:-

### 2.1.1 Wakala wa Nishati Vijijini ( REA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme vijijini (REA) kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme kwa awamu ya tatu pamoja na hali ya upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu ya miradi ya umeme vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba 31, 2018 Serikali kupitia Wakala ilipokea fedha zaidi ya matarajio. Wakala umepokea jumla ya **shilingi bilioni 257.36** kati ya matarajio ya **shilingi bilioni 206.04** ambayo ni sawa na **asilimia 125.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kufanywa na wakala wa nishati vijijini, Kamati ilijadili taarifa ya wakala na kubaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

a) Wakandarasi kucheleweshewa malipo yao hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi hii kwa wakati;

b) Hali isiyoridhisha ya upatikanaji wa vifaa muhimu vya umeme vinavyozalishwa nchini kama Nguzo, Nyaya, na Mashine umba(Transformers) kufuatia kuchelewa kufunguliwa kwa Hati za Muamala (LC), Sambamba na hilo, baadhi ya viwanda nchini vimeshindwa kuzalisha vifaa kama walivyowaahidi wakandarasi, na viunganishi vinavyoagizwa nje ya nchi kuchukua muda mrefu kuwasili nchini;

c) Viongozi wa maeneo ambayo miradi inatekelezwa bado hawashirikishwi ipasavyo katika kuamua wigo wa maeneo ya kutekeleza miradi;

d) Katika baadhi ya maeneo ya miradi kumekuwa na mwitikio mdogo wa wananchi kuunganishiwa umeme.

e) Usimamizi usioridhisha kwa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini;

f) Baadhi ya maeneo kurukwa kupelekewa umeme hasa katika maeneo muhimu kama shule, zahanati na maeneo mengine ya kijamii.

g) Baadhi ya maeneo kuwekewa mashine umba(Transformers) zenye uwezo mdogo ukilinganisha na mahitaji ya maeneo.

h) Mgogoro wa kodi na ushuru kwa wazalishaji wa nguzo katika Mkoa wa Iringa kuchukua

muda mrefu (takriban miezi mitatu) kupatiwa ufumbuzi na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya Umeme.

### 2.1.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la umeme TANESCO lenye jukumu la kuzalisha/kufua,kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao na Shirika la Umeme nchini (TANESCO) vilivyofanyika kwa nyakati tofauti, yalijitokeza malalamiko kuhusiana na Shirika la umeme la Zanzibar (ZECO) kuuziwa umeme kwa bei kubwa. Katika kufuatilia suala hili, maelezo ya Wizara kwa Kamati yalionesha kuwa TANESCO inaliuzia Shirika la Umeme la Zanzaibar (ZECO) umeme wa jumla (bulk supply) **MW 77.** Umeme huu husafirishwa kwenda Unguja kupitia njia kuu chini ya bahari yenye msongo wa **KV 132** na **MW 10** kwenda kisiwa cha Pemba kupitia njia kuu ya **KV 33**. Aidha, usambazaji wa umeme Zanzibar ni jukumu la Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO). Ilielezwa kuwa, katika kuuziana umeme ZECO iligoma kukubaliana na ongezeko la bei ya umeme wa KWh na KVA kutokana na EWURA kupandisha bei ya umeme kwa kiwango cha jumla kwa nyakati tofauti. Deni lililotokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) lilikadiriwa kufika shilingi bilioni 22.8. Jitihada kubwa zilifanywa na Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge kwa ujumla kuhusu kumaliza utata wa deni kati ya ZECO na TANESCO.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa uamuzi wa kufuta rasmi deni lililokuwa likitokana na ongezeko la thamani kwa ZECO; na vilevile kuifanya tozo ya ongezeko la thamani kuwa asimilia sifuri kwa umeme unaouzwa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika, Katika jambo hili, Kamati pia inatambua mchango wako na inakupongeza sana, umelipa jambo hili uzito mkubwa ambao umesaidia Serikali kuharakisha kumaliza utata wa deni hili na kuuza umeme kwa Shirika la Zanzibar bila kuwatoza kodi ya ongezeko la thamani kwa mujibu wa Sheria ya Muungano.**

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua kubwa sana kwa Serikali yetu, kwani imeheshimu na kulinda muungano wetu ili sasa wananchi waweze kunufaika kwa kupata umeme wa gharama nafuu na wa uhakika kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuleta Bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ili maamuzi haya muhimu yaweze kupata nguvu ya kisheria.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu na hali ya upatikanaji wa fedha kwa Shirika la Umeme (TANESCO) kwa kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa Fedha wa 2018/19 ambapo hadi kufika Disemba 31, 2018 fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ni **shilingi bilioni 76.00.** Hata hivyo, katika kipindi hicho Shirika limefanikiwa kuuza umeme wa **shilingi bilioni 757** sawa na **asilimia 94** ya Lengo la kuuza umeme wa **shilingi bilioni ni 806.** Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2018 shirika limekusanya jumla ya **shilingi bilioni 775** sawa na **asilimia 91** ya lengo la kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 853** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Shirika kukusanya mapato juu ya malengo, na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Shirika, changamoto zifuatazo zilibainika:-

a) Uhitaji mkubwa wa Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika;

b) Upotevu wa umeme kutokana na uchakavu wa mifumo na usafirishaji na usambazaji wa umeme;

c) Gharama kubwa za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta hasa katika maeneo ambayo hayajaunganishwa katika gridi ya Taifa;

d) Gharama kubwa ya fidia kwa ajili ya upatikanaji wa ardhi;

e) Kuharibika kwa Mitambo ya kufua umeme kunakosababisha mitambo hiyo kuzimwa kwa muda mrefu, na hivyo kuligharimu shirika na Taifa kwa ujumla kwa kukosekana kwa umeme wa uhakika katika maeneo mbalimbali hapa nchini;

f) Upotevu wa umeme kutokana na uchakavu kwa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; na

g) Uharibifu na wizi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.

### 2.1.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini. Pamoja na mafanikio yaliyopo hasa kutokana na kugundulika kwa gesi nchini bado manufaa yake kwa wananchi hayajaonekana kwa kiasi cha kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2018, TPDC imeweza kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 282.25** sawa na **asilimia 104**

ya malengo ya nusu mwaka ya kukusanya **shilingi bilioni 272.15.** Makusanyo haya yameongezeka kwa shirika baada ya Kinyerezi II kunganishwa, pamoja na gawio la SONGAS kuongezeka, Pan African Energy kutoa *profit share*, na ada za leseni kuongezeka kwa kipindi cha nusu mwaka.

Hatahivyo, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na shirika hili katika ukusanyaji wa mapato, bado linawadai wateja wake wakubwa jumla ya **shilingi bilioni 527. 096.** Miongoni mwa wadaiwa ni TANESCO, SONGAS, PAET, Ndovu Resources Ltd na Kilimanjaro Oil Ltd. Kutolipwa kwa fedha hizi kwa wakati kunalifanya shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, sambamba na changamoto hii, TPDC inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

a) Kutoanza kutolewa kwa Fedha za maendeleo kutoka kwenye mfuko wa mapato yatokanayo na mafuta na gesi asilia (Oil and Gas Fund);

b) Kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia hivyo kutovutia wawekezaji wa mkondo wa juu;

c) Bei ya gesi asilia kwa ajili ya viwanda vya mbolea kuwa chini ya bei ya soko (bei inayoombwa na wawekezaji ni USD 2.6/ mmBTU wakati gharama halisi za gesi ni USD 5.36/mmBTU).

### 2.1.4 Tume ya Madini

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya madini ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Madini yenye jukumu la kusimamia shughuli za madini nchini. Lengo kuu la kuundwa kwa Tume ni kuboresha usimamizi na udhibiti katika

ukaguzi wa uzalishaji na biashara ya madini kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako liliidhinisha jumla ya **shillingI bilioni 8.56** kwa ajili ya Tume ya madini kwa matumizi ya kawaida pamoja na mishahara ya watumishi. Hadi kufikia Disemba 2018 Tume ya Madini ilipokea jumla ya shilingi **bilioni 8.32** ikiwa ni sawa na **asimilia 94** ya lengo la nusu mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Tume kupokea kiasi kikubwa cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu, Kamati imebaini fedha hizi kutokidhi mahitaji ya kuiwezesha Tume kama msimamizi wa shughuli zote za madini kutimiza jukumu lake kikamilifu. Kwa hali ilivyo sasa, Tume inakabiliwa na changamoto kubwa ya sheria ya madini kutokueleweka vyema kwa jamii ya wachimbaji, wafanyabiashara wa madini na umma kwa ujumla na hivyo kusababisha uwepo wa migogoro na kutolipwa kwa baadhi ya tozo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mijadala mbalimbali na wachimbaji madini, Kamati imebaini kuwa katika kuendeleza shughuli za uchimbaji nchini, kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa wachimbaji wadogo kama vile, Kodi ya Ongezeko la Thamani **(VAT 18%),** kodi ya zuio **(withholding tax 5%),** tozo ya ushuru wa halmashauri **(service levy 0.3%),** tozo ya ukaguzi **(inspection fee 1%)** na mrabaha wa madini ghafi ya vito **(6%)** kiuhalisia ni kubwa na ni nyingi sana kwa wachimbaji. Aidha, kutokana na tozo kuwa nyingi wachimbaji wamekuwa wakifanya utoroshaji na kutafuta mianya ya kuepuka kulipa kodi hizo hivyo Serikali kupoteza mapato kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Wizara ifanye mapitio ya mfumo wake wa bajeti ili iweze kuainisha mahitaji halisi ya kifedha ya Tume ya madini ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake**

**kikamilifu hususan katika kuendelea kutoa elimu kwa umma na wachimbaji. Aidha, ipo haja ya kuangalia namna ya kufanya marekebisho ya sheria za kodi mbalimbali ili kuimarisha mazingira mazuri ya wachimbaji kulipa kodi kwa Serikali bila kukwepa.**

### 2.1.5 Uendelezaji wa Jotoardhi nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa Fedha katika Kampuni ya uendelezaji wa jotoardhi nchini. Kampuni ya uendelezaji wa jotoardhi (TGDC) ilianzishwa mwezi disemba 2013 na kuanza kazi Julai 2014. Kampuni inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali kupitia TANESCO. Jukumu kuu la kampuni ya TGDC ni kuendeleza rasilimali ya jotoardhi iliyogunduliwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako liliidhinisha kiasi cha **shilingi bilioni 46.32** kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na matumizi ya kawaida kwa kampuni hii. Hadi kufika Disemba 2018, TGDC walikua wamepokea kiasi cha **shilingi bilioni 4.56** zikiwemo fedha za maendeleo zilizopokelewa kwa **asilimia 100** ya lengo. Aidha, pamoja na kupokea bajeti kulingana na kazi zilizopangwa kufanyika kwa nusu mwaka, TGDC inakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo kwa Sheria mahsusi ya jotoardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kuwa Wizara ya Nishati ihakikishe yanakuwepo mazingira bora yatakayowezesha utekelezaji na uendelezaji wa miradi ya jotoardhi ili Taifa liweze kuwa na nishati mchanganyiko katika uzalishaji wa umeme nchini. Katika hili Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa mchakato wa kupatikana kwa sheria ya Jotoardhi. Aidha Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha TGDC inapatiwa leseni ya eneo la Songwe ambalo hivi sasa limemilikishwa kwa wawekezaji binafsi na hivyo kukwamisha utekelezaji mradi wa

kuzalisha umeme ambao una manufaa mapana kwa watanzania wote.

**2.1.6 Chuo cha Madini Dodoma**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Madini Dodoma kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu, ushauri na utafiti katika sekta ya madini. Aidha, kwa sasa chuo hiki kina kampasi mbili kwaajili ya kutoa mafunzo. Moja ni kampasi ya Dodoma na nyingine ni kampasi ya Nzega.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2018/19 Chuo cha Madini (MRI) kiliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.004** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.). Aidha, chuo hiki hakikupangiwa fedha za Miradi ya Maendeleo kwani kinapaswa kujiendesha kutokana na udahili wa wanafunzi. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2018 Chuo cha madini kilipokea jumla ya **Shilingi milioni 467,046,400** kwa ajili ya O.C.

Pamoja na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati ilielezwa, changamoto kubwa zifuatazo zilibainika:-

a) Uhaba wa wakufunzi katika Chuo;

b) Fedha za makusanyo kurudishwa mfuko mkuu wa Serikali kunakwamisha uendelezaji wa miradi chuoni;

c) Gharama za ulinzi hasa kwa kampasi ya Nzega ambayo eneo ni kubwa na limekuwa likizungukwa na wachimbaji wadogo ambao wanataka kuendelea kuchimba katika mashimo ya migodi yalioachwa wazi;

d) Idadi ndogo ya madarasa ya kufundishia;

**2.1.7 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa jiolojia hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali

za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimbali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi asili n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2018/19 GST iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 5.082** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 2.761** ni mishahara na **Shilingi bilioni 2.321** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.). Aidha, GST haikuwa na fedha za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2018 GST ilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 2.236** ambapo **Shilingi bilioni 1.199** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 1.037** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, GST imetekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya ugani na kuboresha ramani za jiolojia za madini za kila mkoa ambapo taarifa za madini kwa kila mkoa zimekusanywa. Wakala pia umeendelea kuchakata takwimu katika vituo mbalimbali vya kupimia matetemeko ya ardhi. Aidha, wakala pia umeendelea katika utoaji wa huduma za maabara na kufanya uchunguzi mbalimbali katika sampuli za madini.
Pamoja na majukumu haya mazito waliyonayo GST changamoto zifuatazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu yake:-

a) Uhaba wa bajeti katika kutekeleza miradi mbalimbali;

b) Upungufu wa vifaa mbalimbali vya kisayansi vya kufanyia kazi; na

c) Uhaba wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Wakala.

### 2.1.8 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Shirika hili la madini limepewa jukumu la kusimamia maslahi ya Serikali katika sekta ya madini kwa kufanya tafiti na uwekezaji katika migodi ya madini kama zilivyo kampuni zingine kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19 Shirika lilitengewa **shilingi bilioni 8.9** kwa ajili ya kuendeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni kuendeleza mradi wa uchenjuaji mabaki ya mchanga wa dhahabu Buhemba, mradi wa kuchimba makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira na mradi wa kuchimba kokoto wa Ubena Zomozi. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba 2018, Shirika halikupokea fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, fedha zilizokusanywa na Shirika katika kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2018 ni **shilingi bilioni 1.99** sawa na **asilimia 29.0** ya matarajio ya **shilingi bilioni 6.81** katika kipindi cha nusu mwaka. Aidha, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 1.38** zimetokana na ruzuku kutoka Serikalini na **shilingi milioni 609.53** zimetokana na vyanzo vya ndani vya Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika limejitahidi kwa kiasi kikubwa kuendeleza baadhi ya miradi yake kama vile mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira (Kabulo) pamoja na mradi wa dhahabu wa STAMIGOLD – Biharamulo ambao sasa umeanza kuzalisha dhahabu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Shirika kujitahidi kuendeleza miradi mbalimbali na usimamizi wa maendeleo ya sekta ya madini, changamoto zifuatazo ziliripotiwa katika Kamati;

a) Ufinyu wa mtaji wa kuendeleza miradi ya maendeleo hivyo kuchelewesha Shirika kufikia malengo liliyojipangia katika mwaka wa fedha 2018/19;

b) Uhaba wa watumishi hasa katika ngazi za uongozi katika kufanya maamuzi ya kimkakati sambamba na kusimamia mikakati ya kutekeleza majukumu ya Shirika;

c) Kusimama kwa mradi wa ubia wa *TanzaniteOne* kutokana na majadiliano ya maboresho ya mkataba wa ubia pamoja na kutokuanza kwa uchimbaji wa dhahabu katika mradi wa ubia wa *buckreef* na;

d) Malimbikizo ya madai ya watumishi katika miradi ya Shirika ambayo ni pamoja na mradi wa Buhemba na kiwira;

### 2.1.9 Sekta Ndogo ya Mafuta na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara ya Nishati kuhusu sekta ndogo ya mafuta pamoja na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa lengo la kuratibu na kusimamia mfumo wa uagizaji mafuta nchini ili ununuzi wa mafuta yanayoingizwa nchini ufanyike kwa ufanisi, na kujihakikishia upatikanaji wa mafuta nchini kwa wakati wote na hatimaye Taifa kwa ujumla lipate manufaa ya kiuchumi. Licha ya jitihada hizi, bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

a) Wapokeaji wa mafuta kushindwa kukamilisha taratibu za ulipiaji wa mafuta kwa wakati

kama inavyoelekeza katika mikataba na makubaliano;

b) Kutokuwepo kwa maghala ya kutosha ya kuhifadhia mafuta kumepelekea kwa kiasi kikubwa wakala kushindwa kuanza uagizaji wa gesi za kupikia majumbani (LPG) na mafuta mazito (HFO) kupitia mfumo wa uagizaji wa pamoja;

c) Makampuni ya ndani kushindwa kushiriki kwenye zabuni kama *Suppliers* kutokana na kutokuwepo na uwiano sawa wa gharama za mitaji na uagizaji baina yao ambapo makampuni mengi ya nje yanapata fursa ya kupata mitaji rahisi toka mabenki ya nje halikadhalika yanafanya biashara kutoka kwenye nchi zenye mfumo wa *Tax Free Zone*, makampuni ya ndani hayapati fursa hiyo na hivyo kushindwa kushindana na makampuni ya nje;

d) Upotevu wa mafuta unaotokana na miundombinu duni na mapungufu ya kiuadilifu wa wafanyakazi;

e) Marekebisho kwenye nyaraka za malipo (LC ammendments) yanaweza kuchelewa kuhakikiwa na hivyo kufanya mafuta kutopokelewa kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika, Kutokana na Changamoto hizo, Kamati yako inaona ni vyema Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuharakisha kukamilisha majadiliano yatakayowezesha kuanza kwa mfumo wa kupokelea mafuta sehemu moja "Single Receiving Terminal" ili kupunguza *demurrages* pamoja na upotevu wa mafuta.**

## 2.2 *Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini*

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la umeme nchini linaendesha mfumo uliounganishwa na gridi ya Taifa wenye mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji, gesi asilia na mafuta. Hadi kufikia Disemba 31,2018 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa ulifikiwa **MW 1,565** ambapo **MW 573.70 (36.64%)** nguvu ya maji, **MW 892.72 (57.02%)** gesi asilia, **MW 88.80 (5.67%)** mafuta na **MW 10.50 (0.67%)** *Biomass.* Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia **asilimia 13.21**.
Aidha, Shirika linamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua **MW 36.46** na hivyo kufanya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia jumla ya **MW 1,602.186**. Mahitaji ya juu katika mfumo wa gridi ya Taifa yamefika **MW 1,116.58** (yalifikiwa Novemba 30, 2018) ukilinganisha na **MW 1,051.27** zilizokuwa zimefikiwa hadi mwezi Juni 2018. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 6.21**. Hivyo basi, kutokana na taarifa hizo, kwasasa hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imejiwekea lengo la kuzalisha umeme kiasi cha **MW 5000** ifikapo mwaka 2020 na **MW 10,000** ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati, upo uwezekano mkubwa wa kutofikisha **MW 5000** ifikapo mwaka 2020. Taarifa zinaonesha kuwa uwezekano uliopo ni kufikia uzalishaji wa **MW 2780**, na hii itategemea kukamilika kwa wakati kwa zoezi la uchambuzi wa zabuni unaoendelea sasa kupata Kampuni za wawekezaji binafsi zenye sifa ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme yenye jumla ya **MW 950** (Makaa ya mawe **MW 600**, Umeme wa Jua **MW 150**, Umeme wa upepo **MW 200**); ili uzalishaji huo uweze kuanza mwaka 2019 kama inavyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika, ili kuendana na kasi ya uchumi wetu wa Viwanda, Kamati yako inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji ya Mto Rufiji unapelekewa fedha za kutosha na kusimamiwa kikamilifu ili ukamilike kwa wakati.** Sambamba na hilo, TANESCO ihakikishe inaimarisha miundombinu ya kusambaza umeme nchini kwa kubuni na kujenga miundombinu imara inayodumu kwa muda mrefu na kuongeza ufanisi wa Shirika ili kupunguza kero kwa wateja. Aidha, katika kuendelea kupata nishati ya uhakika nchini, TANESCO inapaswa kujikita pia katika kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo vingine vya Nishati, kama vile umeme wa Upepo, ambao kwa takwimu imebainika kuwa zaidi ya **MW 850** zinaweza kuzalishwa kutoka katika chanzo cha nishati ya upepo katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa na wawekezaji wengi wenye nia ya kuwekeza katika nishati jadidifu, bado kumekuwa na urasimu mkubwa katika makubaliano na wawekezaji kuhusu bei ya kuuza umeme baada ya wazalishaji binafsi kuzalisha umeme huo. Kwakuwa TANESCO ndio mnunuzi pekee nchini wa umeme, wawekezaji binafsi wamekuwa wakishindwana katika kukubaliana bei za mauziano na TANESCO na wakati mwingine majadiliano ya makubaliano yanachukua muda mrefu kuliko ilivyokusudiwa hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwakatisha tamaa wawekezaji binafsi wenye nia ya kuwekeza na kuendeleza uzalishaji nishati hii ya umeme.

**Mheshimiwa Spika, Ni rai ya Kamati kwa TANESCO kuhakikisha inaweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza na kuzalisha nishati ya umeme nchini.** Aidha, TANESCO ihakikishe unakuwepo mfumo madhubuti na unaoeleweka ambao utawezesha wawekezaji kufanya maamuzi ya kuwekeza nchini kwa kuzingatia matakwa yetu

bila kuiingiza TANESCO kwenye mzigo wa kununua umeme kwa gharama kubwa. Vilevile, Shirika linapaswa kujikita katika kujiendesha kibiashara pamoja na kuleta ushindani wenye tija ili Taifa linufaike na uwepo wa umeme wa uhakika nchini.

## 2.3 *Sekta ya Madini*

**Mheshimiwa Spika,** hadi sasa mchango wa Sekta ya madini ni **asilimia 4.8%** katika Pato la Taifa. Wizara ya Madini pamoja na Tume ya Madini, inapaswa kuendelea na usimamizi na udhibiti wa utoroshwaji wa madini yote nchini, kwa kuimarisha ulinzi kwa maeneo yenye migodi mikubwa na ya kati ili madini yetu yawe na manufaa kwa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya madini iliundwa kwa lengo kuu la kuboresha usimamizi na udhibiti katika ukaguzi wa uzalishaji na biashara ya madini na kuhakikisha utekelezwaji wa Sera, Sheria, Kanuni na taratibu unafuatwa ipasavyo ili kuongeza Pato la Taifa katika Sekta ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2018, Tume ya madini ilitoa jumla ya **leseni 3697** za uchimbaji mdogo (PMLs), **leseni 33** za uchimbaji wa kati (MLs), **leseni 695** za utafutaji wa madini (PLs), leseni kubwa za biashara **522** (DL), leseni ndogo za biashara **930** (BL) na leseni **21** (PCLs) za uchenjuaji wa madini. Hata hivyo, Pamoja na Tume ya Madini kutoa leseni zote za uchimbaji na utafiti wa madini bado Serikali haina mfumo rasmi wa kuwatambua wachimbaji wadogo hali ambayo inapelekea kukosekana kwa takwimu rasmi za mapato ya wachimbaji wadogo katika kulipa tozo mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua na kuthamini Sekta ya Madini nchini, Kamati inapenda kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.

John Pombe Magufuli pamoja na Wizara ya Madini kwa kuandaa mkutano mkubwa tarehe 22.01.2019 ambao ulijumuisha wadau mbalimbali wa sekta ya madini kwa lengo la kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali kuhusiana na sekta ya madini. Kutokana na mkutano huo, Kamati imenufaika kwa kusikia changamoto na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na wachimbaji, wauzaji na wachenjuaji madini nchini. Kamati inaishauri Serikali kuyafanyia kazi kwa kina maazimio yote ishirini (20) ya mkutano huo. Aidha mapendekezo hayo ni;

(i) Madini ghafi yaruhusiwe kusafirishwa nje ya nchi ili kuondoa ushawishi wa kutorosha kwenda nje;

(ii) Kodi na tozo mbalimbali; kodi ya **(VAT 18%)** ifutwe, kodi ya zuio **(withholding tax 5%)** ipunguzwe hadi **asilimia 3**, Tozo ya ushuru wa halmashauri **(service levy)** ya **asilimia 0.3** iongezwe hadi **asilimia 1,** *Inspection and clearance* fee ya **1%** iondolewe, mrabaha wa madini ghafi ya vito upunguzwe kutoka **asilimia 6 hadi 3**;

(iii) Kuanzishwa kwa benki ya madini ili kuwezesha kupata mikopo na mitaji;

(iv) Maeneo yenye leseni za utafiti wa madini ambayo hayafanyiwi utafiti yafutwe na yatengwe kwa shughuli za uchimbaji;

(v) Kuwepo kwa maafisa madini/afisa migodi katika maeneo ya uzalishaji wa madini ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(vi) Serikali itoe ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini;

(vii) Taasisi ya *Tanzania Gemstone Industries* irudishwe kutokana na umuhimu wake katika ununuzi, ukataji na utafutaji wa madini;

(viii) Madini yanayotoka nje ya nchi yaingizwe bila tozo yoyote ila yanapotoka nchini yalipiwe tozo zote zinazotakiwa;

(ix) Mamlaka ya utoaji wa vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi ikasimishe kwa maafisa Madini wa Mikoa;

(x) Ada za leseni kwa malipo ya eneo la uchimbaji kwa hekta 1 ipunguzwe kutoka shilingi 80,000 hadi shilingi 50,000 Aidha, Ada ya mwaka ya leseni za uchenjuaji ipunguzwe kutoka USD 1,000 hadi Tsh 500,000;

(xi) EPP itambuliwe na NEMC kwa madhumuni ya kukidhi masharti ya EIA kwa wachimbaji wadogo wa madini;

(xii) Maombi ya leseni kwa wachimbaji wadogo kupitia *online* siyo rafiki kwa wachimbaji wengi Aidha, leseni ziongezwe muda kutoka miaka 7 hadi miaka 15;

(xiii) Ufanyike ulinganishi/uwiano kwa tozo na kodi kwa nchi za maziwa makuu. Aidha zilipwe mara moja na kwa taasisi moja;

(xiv) Bei elekezi za masoko ziendane na uhalisia wa eneo (bei ya soko);

(xv) Utunzaji wa Mazingira;

a) Vibali vya mazingira vitolewe wakati leseni za madini zinapotolewa;

b) EPP isimamiwe na madini, halmashauri wataarifiwe kuzitambua taarifa hizo;

c) EPP na EMP ziendelee kusimamiwa na Wizara ya madini na NEMC kuzipitia upya Sheria husika za kuzuia miradi ya wachimbaji wadogo kwa kulazimisha kuandaa EIA;

d) Kwa miradi ya kati na mikubwa, gharama za EIA zipungue.

(xvi) Adhabu kwa watoroshaji;

a) Kwa wamiliki wa leseni, inashauriwa leseni na mali zao zitaifishwe aidha, wachukuliwe hatua za kisheria kama wahujumu uchumi;

b) Kwa wasiokuwa na leseni, wachukuliwe hatua za kisheria kama wahujumu uchumi na kufilisiwa.

b) Uhaba wa watumishi has

(xvii) Uwepo wa bei elekezi zenye uhalisia kwenye madini ya ujenzi na viwanda;

(xviii) Kuwepo kwa miundombinu kwenye maeneo ya machimbo;

(xix) Tozo na ada kwa wachimbaji wadogo wa madini zilipwe kwa shilingi ya Tanzania;

(xx) Kuwepo kwa mikataba ya kazi katika shughuli za uchimbaji wa madini ya Tanzanite katika maeneo ya mchimbo ya Mirelani.

**Aidha, Kamati itaendelea kushirikiana na Wizara na wadau wote wa sekta ya madini ili kuweza kuangalia namna bora ya kushauri kutatua changamoto za sekta ya madini ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali hii muhimu.**

## 2.4 *Sekta Ndogo ya Gesi*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, TPDC ina wajibu wa kutekeleza shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambambazaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa maeneo ambayo gesi asilia imeshaanza kuvunwa yaani Mnazi bay na Songosongo, kiasi ambacho kimehakikiwa ni futi za ujazo **Trilioni 1.96.** Hadi kufikia Disemba 2018, gesi asilia iliyokuwa ikitumika katika uzalishaji umeme, viwandani, na matumizi mengine kwa mwaka ni **futi za ujazo Trilioni 0.63.** Hii inaonesha kuwa kwa mwaka gesi inayotumika ni sawa na **asilimia 4.18** ya gesi iliyohakikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa wingi wa gesi asilia nchini bado matumizi yake ni madogo ukilinganisha na gesi iliyopo. **Hivyo ni rai ya Kamati kwa Serikali kutafuta masoko ya kuuza gesi asilia kwa matumizi mengine ya viwandani na majumbani.**

**Mheshimiwa Spika,** kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuendeleza matumizi ya gesi asilia nchini imekuwa ndogo sana. Mfano, Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Lindi, Dar es salaam na Mtwara bado upo katika hatua za chini mno za utekelezaji kutokana na ufinyu wa bajeti.

## 2.5 *Umuhimu wa kufanyika kwa marejeo ya mikataba iliyopo ili kukidhi matakwa ya sheria za sasa;*

Kwasasa nchi yetu ina Mikataba hai ya gesi katika eneo la utafutaji na uendelezaji wa shughuli za gesi asilia hapa nchini ipatayo kumi na moja, ambapo

katika hiyo mikataba mitatu ipo kwenye hatua za uzalishaji, na mikataba nane ipo katika hatua ya utafutaji na ugunduzi. Mikataba yote hii iliingiwa kwa sheria za zamani na kwamsingi huo inakinzana na sheria zilizopo sasa **(Sheria ya Petroli, sura 392 ya mwaka 2015, Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017, na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017)**. Mikataba hii imeinyima nchi fursa ya kunufaika kikamilifu na rasilimali zake. **Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka katika kufanya majadiliano na wawekezaji ili kuboresha masharti yenye kasoro kwenye mikataba iliyopo ili iendane na masharti ya sheria zilizopo sasa.**

**Mheshimiwa Spika,** Kuendelea kuwepo kwa mikataba hasi ambayo masharti yake hayana tija ni jambo ambalo linapaswa kuto fumbiwa macho. Ni vyema kwa kutumia sheria za sasa za rasilimali, Serikali iangalie namna ya kufanya majadiliano na makampuni yaliongia mikataba hiyo ili kuboresha masharti hasi hasa katika mikataba ya gesi kati ya TANESCO, TPDC, SONGAS na PAET. Mfano hai ni jinsi ambavyo mikataba hii imesababisha TANESCO kuelemewa na mzigo wa madeni makubwa; ambayo hadi kufikia Januari 2018 TANESCO ilikuwa ina deni litokanalo na ununuzi wa umeme wa gesi asilia la takriban **shilingi bilioni 630.8** ilizokuwa ikidaiwa na SONGAS, PAET, na TPDC. Aidha kwa TANESCO kushindwa kulipia ankara za Gesi Asilia kwa TPDC kwa muda mrefu kumeisababishia TPDC kushindwa kujiendesha kibiashara na kuendeleza uwekezaji katika sekta ndogo ya Gesi Asilia, hata hivyo, TPDC inashindwa kulipa Ankara za ununuzi wa Gesi Asilia kwa wakati kwa makampuni ya mkondo wa juu hali ambayo imesababisha wakati mwingine Makampuni ya Mkondo wa Juu kusitisha kuuza Gesi Asilia kwa TPDC kutokana na deni kuwa kubwa.

### 2.6 *Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa majukumu na bajeti za wizara kwa kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa Fedha 2018/2019*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na hali ya upatikanaji wa Fedha za maendeleo kwa kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Disemba 2018, Wizara ya Nishati ilikua imepokea jumla ya shilingi **bilioni 263.39** sawa na **asilimia 32** ya fedha zilizopangwa kupokelewa kwajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, hadi kufikia Disemba 2018 Wizara ya Madini ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi milioni 100** kati ya **shilingi bilioni 19.92** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo Wizara ilipokea ruzuku ya **Bilioni moja** kwajili ya ujenzi wa ofisi za madini katika mji mkuu wa Serikali Ihumwa, Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** miradi mingi bado haijatekelezwa kutokana na ukosefu wa Fedha, Upungufu wa watumishi mbalimbali, ukosefu wa vitendea kazi kwa baadhi ya taasisi. Aidha, katika utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu, ukosefu wa vifaa kwa wakati ulikwamisha wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kwa muda ambao ulipangwa. Miradi ya REA inatekelezwa nchi nzima na inagusa wananchi wengi hivyo kutokutekelezwa kwake kunakwamisha shughuli mbalimbali za wananchi ambao wana matumaini makubwa na mradi huu. **Hivyo basi, ni ushauri wa Kamati kuwa bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati kwani kutokutolewa kwa kiasi kikubwa kunasababisha miradi kutokutekelezwa. Aidha, kuhusu upungufu wa watumishi katika Wizara na baadhi ya taasisi zake, Ni vyema Serikali ikatoa**

**vibali vya kuajiri watumishi katika kada mbalimbali, pamoja na kuwathibitisha kazini kwa wakati watumishi wanaokaimu nafasi mbalimbali ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi. Hatahivyo, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati kwa maendeleo ya Taifa.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### *3.1 Maoni ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao;

a) Upatikanaji wa Fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwenda kwenye Wizara na Taasisi zake bado ni changamoto kubwa. Hali hii inakwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali kutekelezwa, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kupeleka fedha zilizo idhinishwa na Bunge kwa wakati;

b) Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inaendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa wakati wote nchi yetu inakuwa na mafuta ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi nchini na kujihakikishia usalama wa nchi yetu. Aidha, umefika wakati sasa kama taifa tuwe na mkakati wa makusudi kuhakikisha makampuni ya wazawa hususan TPDC yanajengewa uwezo ili kuweza kushiriki katika uagizaji wa mafuta;

c) Kasi ya utekelezaji wa Mradi wa REA III hususan *Grid extension Round* I imekuwa ndogo mno kutokana na kukabiliwa na changamoto nyingi tangu kuanza kwake. Hivyo Serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wa miradi ya REA awamu ya tatu kwa kuzingatia wigo wa maeneo, ubora wa vifaa na upatikanaji wake, pamoja na malipo ya wakandarasi kwa ujumla, kwani maeneo mengi hayajafikishiwa umeme kama ilivyotarajiwa, na maeneo mengine utekelezaji wake ni kama umesimama;

d) Ucheleweshaji wa ulipaji fidia kwa wananchi waliokuwa wanafanya kazi katika migodi mbalimbali nchini pamoja na wananchi walioachia maeneo yao kupisha utekelezwaji wa miradi mbalimbali ya Serikali mfano mradi wa LNG Lindi umeendelea kuwa tatizo sugu. Serikali ichukue hatua za haraka kukamilisha zoezi la ulipaji fidia ili kuwaondolea wananchi kero;

e) Uchimbaji wa madini ukiachwa ufanyike kiholela unaweza kuleta athari kubwa za kimazingira. Ni vyema kuanzia sasa Serikali ikawa na mfumo wa kutoa Elimu kwa wachimbaji kuhusu athari za madini mbalimbali kwa mazingira kabla ya kuwapatia leseni;

f) Serikali iongeze kasi katika kuendeleza miradi ya nguzo za zege kutokana na ukweli kwamba nguzo za zege zinadumu kwa muda mrefu, na pia ni rafiki kwa mazingira na gharama zake ni nafuu.

g) Kwakuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya nishati, Serikali ione umuhimu wa kuweka msukumo katika matumizi ya

nishati jadidifu katika kuzalisha umeme na kutoa fursa kwa wawekezaji binafsi kuwekeza katika kuendeleza miradi ya aina hii;

h) Serikali inapaswa kuwa na utaratibu wa haraka katika kushughulikia vibali vya utoaji wa ajira na uidhinishaji wa miundo ya Taasisi zake. Hii itasaidia kuondokana na tatizo la kuwepo kwa ombwe la taasisi zenye majukumu makubwa kuchelewa kuanza kufanya kazi ambazo zilikusudiwa kufanywa na taasisi hizo.

i) Ipo haja kwa Serikali kuhakisha tatizo la *flow meters* katika bandari zote zinazopokea mafuta kwa pamoja linapatiwa ufumbuzi wa haraka. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa ukarabati wa miundombino mingine muhimu katika bandari zetu unafanyika ili kuiepusha Serikali na upotevu wa mapato unaosababishwa na upotevu wa mafuta;

j) Serikali inapaswa kujipanga vizuri zaidi katika kuwezesha matumizi ya gesi asilia kwa kuhakikisha wananchi wengi wanaunganishwa katika nishati hii, kwani takwimu zinaonesha matumizi ya nishati ya mkaa na kuni nchini yapo katika kiwango cha juu sana jambo ambalo lina athari kubwa kwa mazingira yetu;

k) Mchango wa wachimbaji wadogo ambao wanakadiriwa kufikia milioni 6 ungeweza kuwa mkubwa zaidi kama Serikali ingekuwa na mfumo madhubuti wa kuwezesha kuwatambua, na kuwa na takwimu zao za uhakika za ulipaji wa mapato ya Serikali hivyo Serikali ijipange vyema katika eneo hili.

l) Katika udhibiti wa Rasilimali ya Madini, Serikali inapaswa kuimarisha mahusiano yake na jamii, ili kushirikiana kwa pamoja kulinda rasilimali zetu. Aidha, Serikali inapaswa kuwekeza katika wataalam wabobezi katika masuala ya madini, ili wawe na taaluma kubwa ya udhibiti na waweze kuishauri vyema Serikali juu ya kuziba mianya ya utoroshaji.

m) Serikali ifanye tathmini ya kina ya wataalam kwenye sekta ya Gesi nchini, katika kipindi cha sasa, muda wa kati, na muda mrefu ujao na kuzihusisha taasisi za kielimu nchini kuwa na mitaala stahiki ili kukidhi mahitaji ya soko ya wataalam wabobezi katika sekta ya gesi.

n) Serikali iweke mfumo madhubuti wa kudhibiti gharama za miradi ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia kwani miradi hii hugharimu fedha nyingi na wawekezaji wanaweza kutumia udhaifu wa mfumo kuongeza gharama za uwekezaji kwa lengo la kukwepa kodi.

### *3.2 Ushauri na Mapendekezo ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuainisha maoni ya jumla ya Kamati kuhusu masuala ya msingi yaliobainika katika Sekta ya Nishati na Madini kwa ujumla wake, naomba kutoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Wakala wa Nishati vijijini (REA)

**a) Ucheleweshwaji wa Fedha za kutekeleza miradi ya REA kwa wakati;**

**KWA KUWA**, Fedha za miradi ya REA zimekuwa zikichelewa kupelekwa kwa wakati hivyo kuchangia kuzorota kwa utekekezaji wa miradi;

**NA KWA KUWA**, kuchelewa kukamilika kwa miradi hupelekea kuongezeka kwa gharama za Miradi husika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo fidia kwa wakandarasi na kupanda kwa thamani ya dola hapa nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge lako liazimie kuwa Fedha za miradi ya REA zipelekwe kwa wakati katika kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka husika, ili kuipunguzia Serikali gharama ya kulipa fidia wakandarasi wanaocheleweshewa malipo yao.

**b) Hali ya Upatikanaji wa Vifaa vya kutekeleza miradi ya REA**

**KWA KUWA** Serikali iliazimia vifaa vinavyotekeleza miradi hii vitengenezwe hapa nchini,

**NA KWA KUWA,** makampuni haya yanayotengeneza vifaa hapa nchini yanachelewesha wakandarasi kupata vifaa hivi kwa wakati;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha vifaa vya kutekeleza miradi hii vinapatikana kwa wakati na vikiwa na ubora stahiki, ili miradi iweze kutekelezwa na kuendana na mpango wa utekelezaji wa kumaliza miradi hii.

**c) Ushirikishwaji wa Viongozi wa Wananchi katika maeneo ya miradi**

**KWA KUWA,** maneno mengi ya kijamii na kiuchumi katika vijiji na vitongoji vingi yalirukwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya awamu ya kwanza na ya pili,
**NA KWA KUWA,** hali hiyo ilisababishwa na ushirikishwaji mdogo wa viongozi wa vijiji na

vitongoji, hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya mradi na kuleta kero kwa wananchi hasa kwenye maeneo yaliyorukwa,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuhakikisha inawashirikisha kwa kiasi kikubwa Viongozi wa wananchi katika uainishaji wa maeneo ya kupelekewa umeme ili maeneo muhimu ya kijamii na kiuchumi yapewe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu.

### 3.2.2 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

#### a) Shirika la TANESCO kujiendesha kibiashara

**KWA KUWA,** Shirika limeonesha jitihada za kujiendesha lenyewe kwa kufanya makusanyo mbalimbali ya fedha katika vyanzo vyake vya ndani;

**NA KWA KUWA,** ili shirika liweze kufikia azma yake ya kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; wateja wanapaswa kulipa ankara kwa wakati ili TANESCO iweze kukusanya mapato yake;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liishauri Serikali kupitia TANESCO kuwachukulia hatua za kisheria wateja wote wasiolipa ankara kama inavyostahili. Aidha, shirika lijiendeshe kibiashara kwa kutoa fursa kwa wawekezaji binafsi wenye nia ya kuzalisha umeme wa bei nafuu.

#### b) Uchakavu wa Miundombinu ya kufua, kuzalisha na kusafirisha umeme

**KWA KUWA,** Mitambo mingi ya kuzalisha na kusafirisha umeme imekuwa ikiharibika na kushindwa kufanya kazi kutokana na uchakavu

wake na kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati,

**NA KWA KUWA**, kuharibika kwa mitambo hiyo mara kwa mara husababisha kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini jambo linaloigharimu TANESCO na Taifa kwa ujumla,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri kuwa Bunge liitake Serikali kuliwezesha Shirika la TANESCO kwa kutenga Fedha za kutosha ili kuweza kufanya matengenezo ya mitambo hii na hivyo kuliepusha Taifa na tatizo la kukosekana kwa Umeme wa uhakika.

**c) Utoaji fursa kwa wawekezaji wenye nia ya kuzalisha umeme**

**KWA KUWA,** Wawekezaji wengi binafsi wenye nia ya kuzalisha umeme kwa kutumia njia nyingine za uzalishaji kama upepo, makaa ya mawe, nishati ya jua, wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kutofikiwa kwa makubaliano na TANESCO katika ununuzi wa umeme wanaozalisha;

**NA KWA KUWA**, kutofikiwa kwa makubaliano hayo kwa wawekezaji na TANESCO, imesababisha usumbufu kwa wawekezaji binafsi kushindwa kuwekeza kwa wingi katika uzalishaji wa nishati jadidifu;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuhakikisha kuwa muongozo wa uwekezaji katika Sekta ya Nishati unakamilishwa haraka ili masuala yote muhimu ikiwemo bei elekezi ya kuuza umeme kwa TANESCO yawe wazi kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa umeme.

### 3.2.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

**a) Mpango wa usambazaji wa gesi asilia majumbani**

**KWA KUWA,** TPDC ina mpango wa usambazaji wa gesi asilia majumbani kutokana na kuwa na uwezo wa kuzalisha gesi nyingi zaidi ya soko lililopo kwa sasa, ila shirika hili linakabiliwa na changamoto ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi hii majumbani,

**NA KWA KUWA**, changamoto hiyo inatokana na ukosefu wa Fedha za kujenga miundombinu hiyo, jambo linalochangia kuifanya TPDC kushindwa kujiendesha kibiashara kama ilivyo kusudiwa kutokana na kushindwa kufikia wanunuzi wa gesi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuwezesha utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi katika mikoa mbalimbali kwa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi kwa watumiaji ili sasa gesi asilia iweze kuwanufaisha watanzania.

**b) Mpango kabambe wa matumizi ya Gesi Asilia wa mwaka 2016 (NGUMP 2016)**

**KWA KUWA,** TPDC ina mpango kabambe wa matumizi ya gesi asilia wa mwaka 2016,

**NA KWA KUWA**, mpango huo unatoa dira ya matumizi bora ya gesi asilia nchini pamoja na mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ndogo ya umeme wa mwaka 2016 ambao pamoja na vyanzo vingine umeainisha miradi ya umeme utokanao na gesi asilia,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuipatia TPDC bajeti ya kutosha ili kuiwezesha kutekeleza

majukumu yake ya msingi na kufuata utekelezaji wa mpango kabambe wa usambazaji wa gesi asilia ili kwenda sambamba na malengo hayo katika kuleta maendeleo katika Taifa letu.

### 3.2.4 Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

**KWA KUWA,** Chuo cha Madini ndio chuo pekee kinachotoa mafundi mchundo na mafundi sanifu katika sekta ya Madini nchini na Chuo hiki kina kampasi mbili kwa sasa, Dodoma na Nzega;

**NA KWA KUWA,** makusanyo ya Fedha za udahili ya Chuo yanapelekwa kwenye mfuko mkuu wa Hazina hivyo Chuo kinakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa Fedha, uhaba wa vifaa na uchakavu wa miundo mbinu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liazimie kwa Serikali kukiwezesha chuo hiki kifedha kwa kuacha makusanyo ya Chuo kubakia chuoni ili chuo hiki kiweze kujiendesha chenyewe, kufanya ukarabati wa miundo mbinu pamoja na kuajiri walimu wa kutosha.

### 3.2.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)

**KWA KUWA,** Wakala wa Jiolojia nchini amepewa jukumu muhimu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza taarifa mbalimbali za kijiosayansi kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya ardhi;

**NA KWA KUWA,** Wakala huu una jukumu la kutoa taarifa mbalimbali lakini unakabiliwa na uhaba wa bajeti hivyo kupelekea kukwama kwa utekelezaji wa majukumu yake kikamilifu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kutenga na kupeleka fedha kwa Wakala wa Jiolojia nchini ili

wakala uweze kufanya tafiti mbalimbali za kisayansi kama ilivyojipangia ili Taifa linufaike katika kutoa maamuzi sahihi wakati wa utafutaji na uchimbaji wa rasilimali zake nchini.

### 3.2.6 Sekta Ndogo ya Mafuta

#### a) Utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)

**KWA KUWA,** Wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) ndio imepewa jukumu la kuwa wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja nchini;

**NA KWA KUWA,** mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja umeleta uhakika na usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini lakini Wakala unakabiliwa na changamoto ya kutorasimishwa kwa muundo wa utekelezaji wa majukumu yake hivyo watumishi wake hawana ajira za kudumu hivyo kuathiri ufanyikaji wa maamuzi mbalimbali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali kuharakisha kumaliza taratibu za kupitisha muundo rasmi wa utekelezaji na majukumu ya Taasisi hii kwani bado haujapitishwa rasmi na Serikali. Hatua hiyo itaiwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hata watendaji wake kuthibitishwa na kuajiriwa kwa ajira ya kudumu ili kuhakikisha Wakala huu unatekeleza majukumu yake kwa ubora na ufanisi.

#### b) Uwepo wa Sehemu moja ya Kupokelea mafuta

**KWA KUWA**, Serikali ilishaanza taratibu za kutengeneza eneo moja la kupokelea mafuta yaani *Single receving Terminal*;

**NA KWA KUWA,** kuwepo kwa sehemu moja ya kupokelea mafuta kutapunguza *demurrages* pamoja na upotevu wa mafuta;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuhakikisha Msajili wa Hazina anakamilisha kwa haraka mapitio ya mfumo ili taratibu za uanzishwaji wa utaratibu wa kupokea mafuta sehemu moja uweze kuanza na hivyo kupunguza hali ya upotevu wa mafuta na ukosefu wa mapato kwa Serikali.

### 3.2.7 Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia (TEITI)

**KWA KUWA**, Taasisi ya Uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia (TEITI) iliundwa kwa lengo la kusimamia utekelezaji pamoja na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasimali madini, mafuta na gesi asilia;

**NA KWA KUWA,** maeneo ya uwazi yalilenga katika ukusanyaji wa mapato, mgawanyo wa mapato na matumizi, utoaji wa leseni na mikataba ya uchimbaji wa madini, hata hivyo bado taasisi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha za ndani pamoja na upungufu wa watumishi kulingana na majukumu

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kupeleka fedha kwa taasisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake. Vilevile Serikali iangalie namna ya kuajiri watumishi mbalimbali ili waweze kukamilisha majukumu ya kusimamia uwazi na uwajibikaji wa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia nchini.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

### *4.1 Shukrani*

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dr. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
5. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
6. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
7. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
8. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
9. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
10. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
11. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
12. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
13. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
14. Mhe. Ajari Rashid Akbar, Mb
15. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
18. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
19. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb
20. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
21. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
22. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb

24. Mhe Hamida Mohamed Abdallah, Mb
25. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb

**Mheshimiwa Spika,** pia Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati chini ya uongozi wa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani (Mb), Naibu Waziri Mhe. Subira Khamis Mgalu (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ujumla wao. Aidha, Kamati inaipongeza pia Wizara ya Madini chini ya uongozi wa Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Katibu Mkuu Prof. Simon Msanjila pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, hivyo kuwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai kwa ushirikiano wake na Kamati yetu. Pia namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Katibu wa Kamati hii, Ndg. Felister Mgonja kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

### *4.2 Hoja*

**Mheshimiwa Spika,** sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
06 Februari, 2019

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hizo ndiyo taarifa mbili za Kamati ambazo tutazifanyia kazi siku ya leo na niwapongeze Wenyeviti hawa kwa sababu hakuna hata mmoja aliyegongewa kengele hata moja nadhani wameonesha mfano mzuri sana wa namna ya uwasilishaji taarifa, zinazoletwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeshaletewa orodha na vyama vilivyoko hapa Bungeni kwa ajili majina ya wachangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Shally Raymond, wachangiaji wa CCM, wanachangia kwa dakika kumi na tano, wachangiaji wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo wanachangia dakika kumi isipokuwa Upendo Peneza ambaye atachangia dakika tano, wachangiaji wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kila atakayeitwa anachangia dakika tano. Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Kigua, Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai na nafasi tuliyopata sisi Wabunge kuzungumzia mambo ya maendeleo ya nchi yetu katika jengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wangu, amewasilisha ripoti ambayo ni nzuri kabisa, ripoti ambayo tuliijadili na ripoti ambayo inazungumzia mambo mengi. Nimesimama kuweka msisitizo katika mambo machache tu ambayo labda naona ni vyema kama wote, tukayafahamu na tukaweza kuyafafanua zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze sana Amiri Mkuu ambaye ni Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuvisimamia vyombo hivi na kuviimarisha na hata tukawa na amani katika nchi yetu, amani inayotuwezesha sisi tukae hapa, tuweze kuzungumza kwa nafasi bila wasiwasi,. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina amani kwa vile Wizara ya Ulinzi na Usalama na Wizara zote nyingine zinazohusu mambo hayo ziko vizuri, Wizara ya Mambo ya Ndani, ikisimamiwa na Waziri wetu Kangi Lugola na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikisimamiwa na Waziri wetu, Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati hatukuona tatizo sana, kwa hela za matumizi kutoka kwa wakati, hela ambazo zilikuwa zina shida ni hela za maendeleo. Inapokuwa kwamba hela za maendeleo haziendi kwa wakati kama ilivyoandikwa kwenye ripoti yetu, inakwamisha mambo mengi na hapa nitaanza sasa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, haikuweza kupata hela za maendeleo kwa wakati muafaka na hivyo kufanya majengo yetu yaliyo katika Balozi kuwa katika hali ambayo siyo nzuri. Wakati Balozi zetu haziko kwenye hali nzuri, inaonesha taswira mbovu kwa nchi, majengo yale yanaonekana yamekaa tu na kwa hivyo basi, kwa vile hatukupata pia nafasi sisi Wabunge, kwenda kutembelea yote nitakayozungumza hapa ni kwa nadharia kwa yale tuliyoelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba kwa kuwa ni ngumu sana kuendelea kulipia kodi ya pango katika maeneo mengi kwenye Balozi zetu, ni vyema sasa, Balozi zetu zikawezeshwa, zikajenga majengo yake, zikaweza kupangisha zikanufaika kwa kodi na pia ikaonesha jinsi ambavyo sisi tunajali heshima ya kuwa na Balozi katika maeneo husika. Sioni sababu ya kutaja yote lakini, niseme ni mengi, imekuwa hivyo, kwa hiyo naweka msisitizo kuwe na *mortgage finance* ambayo itasaidia Balozi hizo, kwa sasa na kwa muda ujao wakaweza kupata kipato lakini pia wakawa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hayo tu, hata magari yaliyoko kule, naamini nitatoa ushuhuda kwa magari yaliyo India kwa sababu niliwahi kwenda matibabu *New Delhi*

nikaliona gari la Balozi na zile fujo za uendeshaji India, gari hilo limegongwa kila upande huku na huku, lakini sio rahisi sana, pia wakawa na magari kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali ione umuhimu wa kuonekana kwa sababu wanasema ni vyema muonekano ukawa mzuri, yaani *halo effect*, mara moja na mtu akaku-*judge* kwa muonekano mpaka akaja kukuangalia ndani inakuwa ni jambo la baadaye sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Nje, ni ile *(APRM) African Peer Review Mechanism* haijaweza kupata nafasi yake katika nchi yetu. *African Peer Review Mechanism* inaiweka nchi katika mizani na nchi nyingine na sisi tunaamini Tanzania tuna utawala bora, tunaamini Tanzania tuna uongozi mzuri, tunaamini Tanzania sasa hivi, tuko vyema. Ni kwa nini basi, *African Peer Review Mechanism* isiwezeweshwe ili tukapimwa, tukalinganishwa na nchi nyingine za Afrika wakaweza kweli, kutupa tathmini, wale *eminent persons* wanaofanya tathmini hiyo, imeshafanyika mara moja, miaka ya nyuma, lakini wakati muafaka, eneo hilo limepauka, ofisi hiyo imebidi wamrejeshe, Bibi Rehema Twalibu aendelee kukaa kaa pale tu lakini sio kwa hali ambayo inakubalika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua huku Bungeni kuna mwakilishi ambaye anatuwakilisha kule, lakini hela wanazopata zinapitia Wizara ya Mambo ya Nje, wangeweza wenyewe kupata fungu lao na wao wakaweza kupangilia na hivyo basi tukaweza kufanyiwa tathmini vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa, kwenye uwakilishi wetu, katika Balozi katika kutafuta biashara. Hivi majuzi yamekuweko mazungumzo na pia hali halisi kwamba kuna mizigo iliyokuwa inakwenda Congo, lakini imekwama kwa sababu au ni ya mahusiano, au ni jinsi ambavyo hatujaweza au Wizara yetu haijaweza kusimamia vizuri, naomba kupitia Bunge hili, sasa Wizara ya Mambo ya Nje, ifanye mkakati maalum ili hata ile mizigo iliyokwamba Tunduma itoke mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba sisi, misimu yetu ya kilimo inafahamika wazi, ni wakati gani tunalima, wakati wa masika, ni wakati gani tunavuna, ni wakati gani tunauza, mara nyingi na imekuweko hata juzi, hata jana, tumezungumza kwamba bidhaa zetu, yakiwemo mahindi hayana soko, lakini kama Wizara hii, ingezungumza na Wizara nyingine za Mambo ya Nje, mahindi haya yangetoka yakapitia Zambia, yakaenda kuuzwa, sioni kwa nini tuna Wizara ambayo inahusika na bado mambo hayo hayatekelezeki kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati wa kupitisha maazimio ya hii ripoti yetu ya Kamati, jambo hilo likafikiriwa na likazungumziwa sana ili tupate masoko mengi, kote, ili bidhaa zetu, ziweze kuuzwa kwa haraka na wakati muafaka, hela hiyo iweze kurejeshwa kwa wananchi wetu na sisi wenyewe tuendee kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Majeshi yetu yameendelea kuimarika kila wakati na niseme tu, kuna mambo machache ambayo yakiwekwa vizuri, hata majeshi haya yatakuwa hayalalamikiwi na mambo haya sijui kama yanahusu sana haya majeshi moja kwa moja au yanahusu Wizara ya Fedha kwa sababu ni madeni ya nyuma ya majeshi yetu kulipa katika vyombo vinavyotoa huduma, vikiwemo vyombo vinavyotoa huduma ya maji na vyombo vinatoa huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumeingia Bunge hili tumekuwa tukiomba sana madeni ya maji yalipwe kwenye mamlaka za maji. Kuna maeneo ambayo ni nyeti, huwezi kwenda kukata maji; na hapa eneo la uhakika na la karibu sana ni Chuo cha Polisi Moshi. Kuruta wanapoingia pale wanaingia wengi kwa mara moja, maji yale yana madeni ya siku za nyuma ambayo ni makubwa yanakwenda kwenye takriban bilioni mbili. Kwenda kukata maji kwa kuruta haiwezekani na wala haieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, kwa sasa wanakwenda vizuri kulipa *current bills* lakini basi Wizara ya

Mambo ya Ndani izungumze na ione kwamba italipaje madeni ya nyuma ili ile Mamlaka ya Maji kule Moshi *(MUWASA)* isifunge shughuli nyingine na wala watu wasichukie watakapoona kwamba wamepeleka pendekezo la kupandisha maji, watadhani kwamba ni kwa ajili ya ile bili kubwa ya *CCP* ndiyo maana wananchi wanapandishiwa maji. Hapa naweka msisitizo tunaomba sana madeni ya nyuma yalipwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme pia walizungumzia, lakini niseme kwamba ni vyema basi vyote hivyo vikafanyika kwa pamoja ili tuweze kujua kwamba kama tunavyoamini majeshi na msemo unaosema hilo jeshi mambo yake na vitendo vyake sawasawa, viwe sawa hata kwenye ulipaji madeni ili wote waweze kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba napongeza ile hali ya vyombo vetu vya majeshi kuweza kuwa na kandarasi zao; ujenzi wa nyumba za polisi wanajenga wenyewe sasa. Hata hivyo, naomba basi pamoja na kwamba wanajenga wenyewe, wajenge nyumba za kwenda juu; na hizi nyumba za kupanga *bungalows* zinachukua nafasi kubwa. Ni wazi kwamba kwa sasa Mungu haumbi tena nchi, alishaumba, ni sisi wenyewe tutumie vizuri. Kwa hiyo nitoe rai yangu kwamba majengo yanayojengwa sasa polisi na kwingineko yaende juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nipongeze vyombo hivyo vyote na niwaombee kwa Mungu tuendelee kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Kigua atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa pili kwenye

taarifa ya Kamati hizi mbili. Awali ya yote nichukue fursa hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukutana na wachimbaji wadogo wadogo. Mimi niupongeze uamuzi huu nikiamini ulikuwa ni uamuzi wa busara na nikiamini kabisa moja ya maeneo ambayo yanaweza kutusaidia kuongeza pato la Taifa ni kwenye sekta ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hii ya madini, wachimbaji wadogo wadogo hawa wamekuwa hawapewi kipaumbele. sasa kutokana na Mheshimiwa Rais kukutana na wachimbaji wadogo wadogo maana yake tunaona kabisa dhamira ya Serikali kuwatambua wachimbaji wadogo wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili zipo changamoto mbalimbali na moja ya changamoto hizo Mheshimiwa Rais ameweza kuzizungumzia na majuzi nimemsikia Waziri mwenye dhamana akizungumzia kwamba wapo watu wenye maeneo ambayo wameyashikilia kwa muda mrefu na hawajayafanyia kazi. Ushauri wangu, Waziri mwenye dhamana na eneo hili afanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja tu, katika eneo langu la Wilaya ya Kilindi, kwenye Kijiji cha Kwafumbili, Kata ya Negelo, kuna mwekezaji mmoja ana maeneo mengi sana, ameyashikilia maeneo haya hajayafanyia kazi, lakini wachimbaji wadogo wadogo ambao wangeweza kupewa eneo hili wangeweza kuhakikisha kwamba wanafanya shughuli hizi na Serikali ingeweza kupata mapato ya kutosha. Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo mafupi katika eneo hili sasa naomba nichangie katika eneo la sekta ya gesi. Kwa kweli kwanza nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana ya nishati hususan katika eneo la *REA,* amefanya kazi kubwa sana. Ameweza kupita katika maeneo mbalimbali na ameweza kutusikiliza shida zetu. Naamini kabisa umeme huu utakaposambaa katika Vijiji

vyetu vyote maana yake wananchi wetu wataweza kupata maendeleo. Ukizingatia dhamira ya Serikali ya nchi ya viwanda, hatuwezi kuendesha viwanda bila kuwa na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri eneo hili lipewe umuhimu wa hali ya juu lakini pia wakandarasi hawa ambao wamepewa kusambaza umeme vijijini, wamepewa maeneo makubwa sana. Tuangalie namna ambavyo wanaweza kupunguziwa mzigo huu ili dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kwamba kila kijiji kinapata umeme, iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye eneo la sekta ndogo ya gesi na nikizungumzia eneo la *SONGAS*. Eneo hili nimzungumzie mtu anayeitwa *Pan African Energy*. Huyu mtu *Pan African Energy* alikuja kwa jina la *Ocelot;* hii ni kampuni ambayo ilikuwa inatokea Canada. Watu hawa walikuja kama wawekezaji kwa ajili ya kusaidia suala la umeme, ikaanzishwa kampuni ya *SONGAS* ambayo tunasema ni *special purpose vehicles.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiiangalia kampuni hii na muundo wake unasikitisha sana. Unasikitisha kwa sababu *SONGAS* yenyewe ambayo ni *special purpose vehicles* ukiangalia umiliki wake watu wa *TANESCO* wana asilimia 9.0, *TPDC* asilimia 28 na huyu *Globeleq* ana asilimia 54. Sasa unajiuliza huyu *Globeleq* huu mtaji aliouwekeza mpaka akapata asilimia 54 ameupata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza sana ni kwamba hakuna kampuni iliyosimamia kufanya tathmini, yaani kwamba *TANESCO* ana asilimia tisa, *TPDC* asilimia 28 ni nani alisimamia tathmini hizi? Ukiangalia na maelezo ya kutoka kwa watu wa *Globeleq* wanakwambia kwamba eneo lile la *SONGAS* ambapo lilikuwa ni eneo la *TANESCO* thamani yake ilikuwa ni dola milioni moja. Sasa ni nani alisimamia uthamini ambao umehakikisha kwamba Serikali inapata asilimia tisa peke yake? Maana yake unaona kwamba kuna matatizo makubwa sana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda mbali zaidi unaangalia eneo la *TPDC*. *TPDC* wana visima vinne na visima hivi vinne ndivyo ambavyo vinatoa gesi; lakini vinatoa gesi thamani yake imethaminishwa kwa asilimia 28 tu, huu ni wizi mkubwa sana. Naishauri Serikali iangalie namna gani inaweza ikalisimamia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo kuna mambo ambayo yana upungufu mwingi sana na moja ya upungufu ambao upo katika mkataba huu ni eneo ambalo *Globeleq* katika taarifa zake za pesa anaonesha mkopo wake mwanzoni ulikuwa unaonyesha kama ni *preferential,* lakini sasa hivi inaonesha kama ni *debit note. Debit note* maana yake ni kwamba anapotaka kulipa madeni atapunguza gharama zake zote mwishoni ndio atalipa deni. Mkataba huu una upungufu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema eneo hili kwa sababu naamini kabisa Serikali inapoteza mapato mengi sana; na hii ni kinyume kabisa na mikataba ya madini ya nishati/petroli ya mwaka 2015. Naomba Serikali ilipitie eneo hili vizuri sana na nina uhakika Mheshimiwa Naibu Waziri mwenye dhamana na eneo hili ananisikiliza na atalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mbalimbali ambao nimeuona na ambao Mwenyekiti wa Kamati ameuzungumzia na naamini Serikali itaufanyia kazi. Moja ya upungufu huo ambao nadhani ni mikataba hasi ni suala la *TANESCO* na *Pan African Energy. PAET –Pan African Energy (PAET)* wao wanatoa vipaumbele vya kwenye kuwauzia gesi kwanza wanawauzia *SONGAS* pili viwanda 32 na wa mwisho anakuwa ni *TANESCO*. Jambo hili halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu mwingine ambao upo katika mikataba hii ni suala la tozo ambalo *TANESCO* wanatozwa. Katika Mkataba huu kuna kipengele kinachosema kwamba *TANESCO* asipoweza kununua kiwango cha juu na cha chini anatozwa faini; eneo hili limekaa vibaya na kwa taarifa yako ni kwamba hadi kufikia

Januari, 2018 *TANESCO* wanadaiwa bilioni arobaini na milioni mia tatu. Mkataba huu haujakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lina upungufu na ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo linahusu *Production Sharing Agreement.* Huu ni mkataba ambao Serikali iliingia na watu wa *Pan African Energy*. Moja ya upungufu mkubwa ni kwamba watu wa *Pan African Energy* wao wana-*operate* kwenye mikondo yote mitatu kwa maana *upstream, midstream* na *downstream,* kitu ambacho sio sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Petroli, inaruhusu *Pan African Energy* ku-*operate* kwenye *upstream.* Tafsiri yake ni kwamba gharama za *midstream* na *downstream* zote wanazipeleka juu, maana yake wanaiibia Serikali; Serikali lazima iangalie katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi ni kwamba *Pan African Energy* katika *Production Sharing Agreement* wameiwekea sharti *TPDC* kwamba ili aweze kushiriki katika shughuli za uzalishaji ni kwamba lazima aweze kuweka dhamana na dhamana hiyo lazima ipitiwe na *Pan African Energy.* Hili jambo ni mkataba hasi na ni lazima Serikali iweze kupitia eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi utaona kwamba suala la *Pan African Energy* kuna upungufu makubwa sana, niiombe Serikali...

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Yosepha Komba.

**T A A R I F A**

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuongezea anachokiongea mzungumzaji *Pan*

*African Energy* wamepewa *exemption* ya *withholding tax* wanapouza *share* zao. Kwa hiyo, bado matatizo ni mengi kwenye *Pan African Energy.* Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea lakini ina upungufu kimsingi, hoja ninazozizungumzia ni kubwa zaidi kuliko hiyo anayoizungumza yeye. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kwamba *TPDC* wao hawaruhusiwi kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji mpaka waweke dhamana, lakini dhamana hiyo haiwezi kuwa na thamani yoyote ile mpaka iwe imekubaliwa na *Pan African Energy*. Kimsingi utaona kwamba kuna matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi niseme Mkataba wa *Pan African Energy* au *Production Sharing Agreement* una matatizo makubwa sana. Ushauri wangu kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, naomba wakae chini waone namna gani ambavyo wanaweza kuhakikisha kwamba tunakaa chini kwa sababu Serikali inapoteza mapato mengi. Pamoja na hayo mkataba huu umekwenda vibaya zaidi, unaisha 2024, sasa kwa nini tusubiri mpaka 2024? Nashauri kwa kupitia njia zile tulizoptia kwenye madini basi tuweze kutumia njia hiyo hiyo kwenye sekta ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo machache, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima, muda ukituruhusu tutamaliza na Mheshimiwa Kiza Mayeye.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kwa masikitiko makubwa sana nikutaarifu

tu kwamba taarifa ambayo umesomewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Wajumbe wa Kamati hatujapata fursa ya kuipitia; na sijajua lengo hasa ni nini, taarifa tumekuja kukutana kama ambavyo wewe umeisikia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama mbele ya kiti chako kwa dakika kumi ambapo dakika zote hizi kumi nakwenda kuzungumzia suala moja tu na suala hili leo ninazungumza ni mara ya tano na sio lingine ni juu ya *SONGAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa ni kwa nini suala hili limekuwa ni gumu sana kuchukuliwa hatua. Nashindwa kuelewa ni kwa sababu gani Serikali imekuwa ikisuasua kuchukua hatua kwenye suala hili la ubadhirifu wa rasilimali za wananchi wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge nafikiri hawajapata fursa ya kuelewa vizuri suala hili ndiyo maana wanashindwa kujua uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi sana, utafutaji wa gesi asilia kwenye visima vya *SONGAS* ulianza mwaka 1969, mpaka kufikia mwaka 1990 Serikali ilikuwa imeshatumia zaidi ya dola milioni 150. Baada ya tafiti kuonesha kwamba gesi inaweza kutumika kuzalisha umeme, Serikali kwa haraka sana ikatangaza zabuni na wakampata mzabuni ambaye ni *SONGAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpaka hatua ya mzabuni kupatikana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia *TPDC* ilikuwa inamiliki visima vitano vya gesi ikiwepo kisima namba tatu, nne, tano, saba na tisa. Pia *TPDC* walikuwa wanamiliki mitambo ya kuchakata gesi ambayo pia ilikuwa ni mali ya Serikali. *TANESCO* walikuwa wanamiliki mitambo ya kuzalisha umeme ambayo yalikuwa ni majenereta manne, yapo pale Ubungo Dar es Salaam. Pia eneo la Songosongo ambapo visima hivi vinapatikana, lilikuwa ni eneo ambalo lipo chini ya *TPDC* kwa maana hiyo lilikuwa ni eneo la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi, Serikali ikaona ili mradi uweze kuanza ikaenda kuchukua mkopo kutoka *World Bank* Dola za Kimarekani milioni 216, sasa viini macho vinaanzia hapo. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwapa *SONGAS* visima vyake vyote vitano bure bila gharama yoyote kulipwa! Kiini macho namba mbili, Serikali iliwapatia *SONGAS* mitambo ya kuchakata gesi bure bila gharama yoyote kulipwa. Kiini macho namba tatu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwapatia *SONGAS* zile jenereta nne za *TANESCO* ambazo zipo pale Ubungo bure bila gharama yoyote kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile asilimia tisa ambayo kwenye mkataba inaonesha kwamba ndio hisa za *TANESCO* walikisia tu kwamba tathmini ya eneo zima lile la *TANESCO* ni dola milioni moja, huu ni wizi wa mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hisa ambazo zinamilikiwa na *TPDC* asilimia 29. Hisa hizi wamefanya makisio bila kuwa na *evaluation report*. Wanasema eneo la Songosongo na njia yake ya kupitisha bomba la gesi linakadiriwa kuwa na thamani ya dola milioni tatu lakini ukiuliza *evaluation report* iko wapi, haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiini macho cha mwisho, japokuwa mitambo na kila kitu *SONGAS* walipatiwa na Serikali, lakini bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia *TANESCO* tunawapa fedha za fidia *SONGAS* na wakati katika uwekezaji Serikali ndiyo imewekeza kwa kuwapa mitambo na kila kitu kwa maana ya *capacity charge* tunatoa sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote, ningependa Serikali ituambie, kwamba dola milioni 60 za kwenye *ESCROW* akaunti zimekwenda wapi? Hii ni kwa sababu Serikali pamoja na mbia wakati wanakubaliana kufanya mradi huu, walikubaliana kuweka dola milioni 60 kwenye akaunti ya *ESCROW* ilikuwa ni kama kinga kwamba ikitokea mradi usipotekelezeka, basi mwekezaji hiyo pesa anaichukua. Hii pesa ilitokana na kodi ambayo walikuwa

wanakatwa wananchi wa Tanzania kwenye petroli na dizeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpaka hivi ninavyozungumza na wewe hizi fedha kwenye akaunti hazipo na kibaya zaidi unapowauliza wahusika wanasema kwamba zimetumika kununua mtambo namba tano na vielelezo hawana. Sasa unaweza ukaona ni kwa namna gani katika mradi huu wa *SONGAS* kuna wizi mkubwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti ya *Songas* ilipata fursa ya kukutana na Kamati. Niliona kwenye taarifa ya Gazeti la *The Citizen* la tarehe 2 ambalo linaonesha Katibu Mkuu wa Nishati na Madini anaelezea kwamba mapendekezo yaliyokuwa yanatolewa na Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika, yameshaanza kufanyiwa kazi miezi miwili iliyopita. Huu ni uongo uliopindukia. Kwa sababu baada ya kukutana na wahusika, Menejimenti nzima ya *Songas* wanakiri, wanasema hata hiyo ripoti hawajawahi kuisikia wala hawaijui. Sasa ni bahati mbaya tunakuwa na aina ya watumishi Serikalini ambao wanakuwa wanatoa taarifa za uongo bila hata kuwa na aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ni kitu gani...

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** ...ni kitu gani ambacho...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa kuna taarifa. Mheshimiwa Subira Mgalu.

Hii hoja ni ya Kamati, siyo hoja ya Serikali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu, atakayehitimisha hoja hapa ni Mwenyekiti wa Kamati na sio Mawaziri. Kwa hiyo, yeye hapo ni kama Mbunge mwingine kwenye hili. Mheshimiwa Subira Mgalu.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Jesca, Mjumbe wa Kamati yetu, kwamba taarifa ile ambayo ilitolewa na Kamati ya Bunge iliyoundwa na Mheshimiwa Spika ya kuhusu masuala ya gesi iliwasilishwa mbele ya Umma katika viwanja vya Bunge. Kwa maana hiyo, kwa vyovyote vile hata *Songas* aliona hizo *findings* kupitia taarifa iliyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, moja ya mapendekezo na hata Kamati ya Nishati na Madini imesema kwamba Serikali ifanye mapitio ya mikataba mbalimbali kuhusu Sekta ya Gesi. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kazi hiyo imeanza kufanyika na sisi kama Wizara tumewasilisha mikataba yote Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kazi inaendelea. Kuisema Serikali kwamba haifanyi chochote, siyo kweli katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile siwezi kupokea taarifa hii, maana hata Wabunge humu ni mashahidi. Hakuna mtu mwenye uwezo wa kuwa na *access* na hiyo taarifa. Uwezekano wa kupata taarifa hiyo na kuipitia ni mgumu kuliko kawaida. Nami niseme tu, kama tutaendelea kuwa humu ndani na kuendelea kudanganyana kwamba taarifa imekabidhiwa kwenye Umma na kwa hiyo, mambo yanaenda sawasawa, tunakuwa hatutendei haki nafasi zetu kama viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea.

**TAARIFA**

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Jesca Kishoa kwamba *Songas* anayoizungumzia ipo Jimbo la Ubungo na *Songas* ilijenga vibanda vya walinzi kwa thamani ya shilingi bilioni 40. Mbao za vibanda hivyo walizinunua Abu Dhabi, mafundi wa kujenga waliwaleta kutoka Abu Dhabi. Kwa hiyo, Kampuni ya *Songas* inanuka ufisadi, mali ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono yote miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu mkubwa unaoonekana kwenye mikataba ni sawasawa na baba ameshikwa na mtoto wake, amefungwa mikono na miguu, halafu mtoto anamwita jirani amcharaze viboko baba yake. Hicho ndicho ambacho kimefanyika. Watoto wa Tanzania...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa malizia dakika moja, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja tu na ninaomba popote pale alipo Mheshimiwa Rais anaposikia sauti hii, achukulie hatua suala hili, kwa sababu Serikali yoyote inayojinasibu kama ni Serikali inayopinga ufisadi, haiwezi kwa namna yoyote ikaruhusu mkataba wa *Songas* ukaendelea kuwepo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hasna Mwilima, halafu Mheshimiwa Kiza Mayeye, ajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hizi tatu; kwa maana ya Mambo ya Ndani, Ulinzi na Usalama, pamoja na Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kikao chake alichofanya tarehe 22 pale Dar es Salaam, kuitisha wachimbaji wadogo na kusikiliza kero zao. Ni jambo zuri na kwa kweli wachimbaji wote Tanzania nzima wamempongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Wizara ya Mambo ya Ndani. Ukurasa wa 11, Kamati imezungumzia kuhusu migogoro mbalimbali baina ya wananchi pamoja na Jeshi la Polisi na Magereza. Naomba nizungumzie kuhusu suala la migogoro ya wananchi pamoja Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Ilagala tunalo Gereza, lakini ni miaka mingi sana wananchi wa Ilagala wamekuwa wakipiga kelele kwamba Gereza limehodhi maeneo yao na Ofisi ya *DC* pamoja na Mkurugenzi waliunda Kamati na ikabaini kwamba ni kweli Gereza lilihodhi maeneo ya wananchi bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua nia njema ya Serikali na Wizara kwamba wanahitaji Magereza wawe na maeneo kwa ajili ya kulima kutosheleza chakula cha wafungwa; lakini kwa kuwa Magereza wamechukua karibu ekari 10,000 na kitu, tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, awaambie wananchi wa Ilagala: Je, wameamua ni ekari ngapi zitarejeshwa kwa wananchi ili na wananchi wapate maeneo ya kulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, nitajikita sana kwenye suala la madini. Nimeona hapa Sekta ya Madini inachangia asilimia 4.8 tu kwenye Pato la Taifa. Hii

ilinishawishi niingie kwenye mtandao kuangalia kwenye *East Africa* nchi nyingine zinafanyaje *especially* kwa wachimbaji wadogo? Nikaangalia kwa mfano, wenzetu Kenya wanazungumzia tu kwenye Kijiji cha Usiri. Kijiji hiki ile *revenue per year* kwenye *local economy* tu, kinaingiza Dola za Kimarekani *1.9 million.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hivyo, *Migori District,* kwenye madini ya dhahabu tu; nataka tu kutoa mfano, madini ya dhahabu tu, Migori wanaingiza 37 *Million USD per year*. Ukienda Rwanda ambayo ni nchi ndogo sana, unaona kwamba wachimbaji ambao wamewa-*formalized* pamoja wanaingiza *39.5 million per year,* lakini wanakwambia kwa mwaka mzima kusafirisha madini nje kwenye nchi ya Rwanda ni sawasawa na asilimia 20 inaingiza mapato ya Serikali ya Rwanda kwa maana ya hii *foreign exchange. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka nizungumzie suala la madini. Tuliwasikia wachimbaji wakati wanaongea na Rais, walimwomba Mheshimiwa Rais Wizara ya Madini isijikite tu kwenye masuala ya dhahabu, *tanzanite* na *gemstones*, wajikite vilevile kwenye *industry minerals* kama vile *gypsum,* chokaa na madini mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, kwa sababu gani? Wachimbaji hawa wanaochimba madini ya ujenzi, Serikali kupitia Wizara ya Madini wangeweza kuwaangalia vizuri, kuwasimamia ili wajiunge wawe na utaratibu mzuri, Serikali ingepata mapato mengi sana kwenye madini ya ujenzi, tofauti kama wanavyong'ang'ania dhahabu na madini mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hata ile *withholding tax* ile 5%, mimi nipo kwenye Kamati ya Bajeti, tuliomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuitoa ile kuishusha iende mpaka 3%. Naona Kamati kwenye ukurasa wa 32 nao wamependekeza hivyo hivyo, *withholding tax* itoke 5% iende mpaka 3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mheshimiwa Rais wakati anaongea na wachimbaji alionesha kwamba anaridhia na alitoa tamko kwamba Wizara ya Fedha na Wizara ya Madini ikae chini na ione namna gani ya kupunguza hii *withholding tax* pamoja na tozo nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, madini ya chokaa yana namna mbili; tuna namna ile kwamba madini yameshakuwa *processed* kwa maana ya ile *lime powder* ambayo unaweza ukauza hapa hapa nchini, lakini tuna ile *limestones* ambayo tunasafirisha nje. Sasa ukienda ukurasa wa 33, mimi naungana kabisa na Kamati kwamba Wizara itoe vibali vya kusafirisha madini nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema madini yasitoke nje, madini yanatofautiana. *Tanzanite* sawa utai-*process* hapa utaipeleka nje lakini *limestone* tunasafirisha. Mimi ni mdau, tunasafirisha ikiwa imepondwapondwa kama kokoto, tunapeleka kwa *tons* tunazisafirisha nje kwa maana ya Kongo, Burundi, Rwanda na nchi nyingine. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu haya mapendekezo ya ukurasa wa 33 tunaomba ayafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wachimbaji wadogo wanachajiwa ekari moja Sh.80,000/=. Ni mchimbaji gani anaweza? Unakuta mchimbaji ana-*own* ekari 30, anatakiwa alipie Sh.80,000/= kwa ekari. Naona Kamati nayo imetoa mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la *NEMC,* wachimbaji wadogo wanatakiwa walipe shilingi milioni moja na nusu, wachimbaji wakubwa ndiyo shilingi milioni 4.5. Sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atoe tamko zuri ili tuweze kuelewa Serikali yetu na kama Rais wetu alivyo na nia njema katika kuhakikisha hii Sekta ya Madini inakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia *NEMC;* wachimbaji wa chokaa wao wanachoma kwa kutumia kuni,

sasa hivi wanajipanga kuchukua makaa ya mawe ambayo wanayatoa Mpanda. Wananunua tani moja shilingi 145,000 na kule Mpanda hawaruhusiwi kununua tani moja mpaka waanzie tani tano. Kwa hiyo, unakuta shilingi 145,000 mara hiyo tani tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema hivi, wachimbaji wa chokaa mfuko mmoja wa chokaa ambayo imeshakuwa *processed* wanailipa Halmashauri shilingi 500 kwa mfuko. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, hilo aliangalie. Wanailipa Wizara ya Madini, kwa maana ya Ofisi ile ya Madini shilingi 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanaomba angalau hiyo shilingi 500 kwa mfuko iteremke mpaka kwenye shilingi 250 ili waweze kukidhi na angalau Serikali muweze kupata mapato zaidi kuliko kuweka kiwango kikubwa ambacho mnawasababishia watafute njia za panya kutorosha chokaa zao badala ya kuilipa Serikali na Serikali iweze kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru sana Serikali, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwajali wachimbaji wadogo wadogo wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kiza Mayeye, dakika tano.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika ripoti hii ya Kamati. Kwanza kabisa, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nishati pamoja na Waziri wa Madini kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze katika suala la *REA,* bado kumekuwa na changamoto kubwa Mheshimiwa Waziri katika suala la *REA III.* Vijiji vingi katika maeneo mengi bado umeme haujafika. Kwa mfano tu, katika Mkoa wangu wa Kigoma kuna Vijiji kwa mfano Msimba na Kamara umeme

umepita katika eneo moja lakini eneo lingine umeme haujafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji kwa mfano, Kamanyangwe, Kihinga, Kalongolonge na Kingungo, bado hawajapata umeme lakini umeme umepita barabarani. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri ambayo mnaifanya, lakini mhakikishe kwamba vijiji vyote vinaweza kupata umeme huu wa *REA III. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tena suala la gridi ya Taifa. Sote tunajua kwamba Mikoa ya Kigoma na Katavi mpaka sasa hatujaingia katika gridi ya Taifa. Tunatumia umeme huu wa *Diesel TANESCO* ambao ni gharama kubwa na kusababishia Serikali yetu hasara kubwa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tayari mmeanza sasa mchakato, basi hiyo Februari, 2020 gridi ya Taifa iweze kukamilika katika Mikoa hii ya magharibi, Kigoma na Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tena suala la mradi wa Mto Malagarasi. Nniseme kwamba wananchi wa Kigoma tumeupokea vizuri mradi huu na tunaunga mkono juhudi za Serikali kwa kuanzisha mradi huu wa Malagarasi Megawati 45 kutoka Malagarasi kwenda Kidahwe. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri pesa ziende kwa wakati, Wakandarasi wamalize kazi kwa wakati. Wananchi ambao wamepisha mradi huu, waweze kupewa fidia zao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati akaniambia tayari wameanza kuthaminisha. Naomba sana wananchi hawa kwa sababu wamejitoa na kupisha mradi huu waweze kupatiwa fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie katika suala madini. Wachimbaji hawa wadogo wa madini, wengi ni vijana wa Kitanzania ambao wameamua kujiajiri kwa kufanya kazi, lakini bado wamekuwa na changamoto kubwa, kwamba

kwanza hawana elimu ya kutosha, lakini hawana vifaa na hata pesa hawana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Doto awaangalie hawa wachimbaji wadogo kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tozo nyingi sana za ushuru. Tumeona hapa katika ukurasa wa 22 wa Kamati, kuna *VAT* asilimia 18, *withholding tax* 5%, *service levy* 0.3, *inspection* 1% na mrahaba wa madini ghafi ya vito 6%. Michango hii imekuwa ni mingi. Tozo zimekuwa nyingi kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, kama tozo zitakuwa ni nyingi bado hatutaweza kuepuka tatizo hili la wachimbaji kutorosha madini. Naomba Serikali iangalie iweze kupunguza hizi tozo kwa wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiona kwamba wachimbaji hawa wadogo wadogo mara kwa mara vifo vimekuwa vikitokea katika maeneo yao. Najua ni kwa sababu hawana uelewa wa kazi ambayo wanaifanya. Naiomba sana Wizara itoe elimu ya kutosha kwa wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kuondokana na madhara haya ya vifo ambayo wamekuwa wakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nizungumzie suala la *GST.* Hawa wanajiolojia ni watu muhimu sana ambao wanaweza kutusaidia kutambua madini mbalimbali katika maeneo mbalimbali, lakini wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kukosa bajeti na fedha za kutosha. Naiomba sana Serikali iwapatie watu hawa pesa waweze kuzunguka katika maeneo mbalimbali, waweze kutuambia ni madini gani yanapatikana katika maeneo hayo hususan ukiwepo Mkoa wangu wa Kigoma ambao naamini kuna madini ya chokaa na hata dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia ni kidogo hatutaweza kuwa na Mbunge mwingine

anayeweza kuchangia. Niwataje Wabunge wachache ambao wapo katika orodha ya wachangiaji wa mchana. Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Hamida Abdallah, Mheshimiwa Abdallah Mtolea na wengine tutaendelea kuwataja tutakavyoendelea na michango ya mchana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano tutaanza uchangiaji na Mheshimiwa Oliver Semuguruka, atafuatiliwa na Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na pia kuwa mchangiaji wa kwanza katika Bunge lako Tukufu jioni hii. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya katika Taifa letu. Pia nazipongeza Kamati zote mbili pamoja na Mawaziri na Wizara husika kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kuchangia hoja zote mbili zilipo mbele yetu. Kwanza kabisa nianze na ripoti ya Nishati na Madini. Nianze kumshukuru Waziri wa Nishati kwa kuwezesha kupata umeme katika Wilaya yetu ya Ngara, lakini kuna vijiji ambavyo havijapata umeme, namwomba Mheshimiwa

Waziri wa Nishati na Madini, nasikitika kwa kuwa simuoni humu ndani, lakini Naibu Waziri yupo, naomba alisikize hili. Kuna kaya ambazo hazijapa umeme katika Wilaya yetu ya Ngara, naomba wajitahidi wamalizie ili waweze kupata umeme. Kwa mfano, unaweza ukakuta kuna kaya mimi nina umeme, Mheshimiwa Matembe hana umema, Mheshimiwa Kangi ana umeme, ndiyo ilivyo. Kwa hiyo naomba kila Kaya wapate umeme, kwa kweli wanafanya kazi nzuri na nampongeza sana Mheshimiwa Rais, bila yeye hata tusingeweza hata kupata umeme huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika mradi wa Kabanga *nickel*, ambao uko Wilaya ya Ngara. Mradi wa Kabanga *nickel* umesemwa muda mrefu sana, pindi niko shule ya msingi, mpaka sasa hivi nazeeka unaitwa ni mradi tu wa Kabanga *nickel*, lakini hakuna kitu ambacho tunakiona. Kwa hiyo, ninaomba, naishukuru sana Serikali kwa kurudisha leseni ya Kabanga *nickel* Serikalini, lakini naomba Mwekezaji wanayemtafuta Serikali awe ni mwekezaji kweli, kwa sababu kuna wawekezaji ambao ni makanjanja. Nimesema tangu niko *primary* wanakuja wawekezaji wanatafuta *research* kwamba kuna madini ya Kabanga *nickel* wakifika wanaondoka, hamna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati niko shule ya msingi nilikuwa naona ndege zinapita, unaambiwa zinaenda Kabanga *nickel* kuangalia madini yanavyoendelea. Baada ya muda wale watu wana *disappear,* hiyo *research* gani inayofanyika? Kweli mimi mpaka nafika umri huu, hiyo ni *research* kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru kwamba Mheshimiwa Rais ameweza kuliona hili na kurudisha leseni Serikalini. Naomba iwe kweli kweli, sababu wananchi wa Wilaya ya Ngara wanahitaji kunufaika na mgodi ule, kwa sababu bila kunufaika na mgodi ule, wanaishia tu kuona majengo, kuna majengo yamejengwa na pale na Kabanga *nickel*, ukienda pale ni Kabanga *nickel*. Kwa hiyo ni vema zaidi tuweze kupata ushirikiano na Serikali walete Mwekezaji

wa kweli, asiwe Mwekezaji wa uongo uongo ili tuweze kunufaika na hayo madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini haya yanapatikana Ngara mpaka Congo, Congo yapo nafikiri kwa asilimia 65, pia yaani huo mkondo unaanzia Ngara mpaka Congo. Sasa kwa nini Congo waendelee kunufaika sisi Tanzania tusinufaike au ni kwa sababu tuko mpakani. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Madini na Naibu wake wanisikilize kwa makini, kuna ujenzi wa reli ya kati, tunapenda ikitokea tuweze kunufaika na hii reli ya kati, tupate kusafirisha haya madini yetu ili yaweze kununuliwa huko nje, lakini sasa hakuna hakuna kinachoendelea.*(Makofi)*

Naomba niongelee pia Jimbo la Kyerwa; madini ya *tin*, naiomba Serikali ifanye haraka kukamilisha taratibu za kuruhusu kusafirisha *tin* kwenda kwenye masoko ya nje. Wananchi wa Kyerwa wanasubiri kwa hamu sana ili waweze kunufaika na hayo madini ya Kyerwa. Pia naomba wananchi wapate mafunzo ili wanufaike katika mgodi ule kwa sababu kuna ambao wanaenda kuchimbia vijembe, akifika kule mara unaporomoka udongo umemuua, kuna vifo vingi vimetokea. Jamani hivi kweli hatuwezi kuangalia hili kwa jicho la huruma?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kyerwa wanapenda sana wanufaike na haya madini ya *tin*, lakini hakuna mafunzo yanayotolewa kwa wananchi. Pia wachimbaji hawana vitendea kazi, ndiyo kama huo mfano nilioutoa, vitendea kazi anaenda na kajembe kake amekaweka begani, kajembe ka kawaida, hawezi kuambiwa kwamba kuna kitu hiki kinatakiwa kifanyike uchimbe hivi uende urefu fulani hivi, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwona pale Naibu Waziri wa Madini, naomba mtusaidie ili tuweze wale wachimbaji wadogo wadogo wa Kyerwa waweze kupata elimu ya kuweza kujua hapa nikienda kuchimba na haka kajembe hakatanisaidia au mwisho wa siku atafariki, ataacha familia yake inateseka*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba sana sana Wizara ya Madini iangalie kwa jicho la huruma mradi, mgodi wa Kabanga nickel na mgodi wa Kyerwa, kwa kweli nawaomba sana sana. Mheshimiwa Rais wetu mpenzi anasaidia wanyonge, sasa hawa wachimbaji wadogo wadogo na wale watu wa hali ya chini, tulisipowasaidia inaleta ukakasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna ripoti mbili za Kamati ziko mbele yetu. Naomba nijielekeze katika ulinzi na usalama. Wilaya yetu ya Ngara, mimi ni mzaliwa wa Ngara japo ni Mbunge wa Mkoa Kagera Viti Maalum, lakini wahamiaji haramu wako wengi. Hao wahamiaji haramu wanatokea Burundi, wanapita njia za panya, njia za chocho, kwa hiyo wakipita njia za panya wanakuja kutudhuru sisi Watanzania ambao tuko mpakani. Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie kupata magari mapya na mafuta ya kutosha ambayo yatafanya doria, masaa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema ilikuwa ni mwaka juzi, 2017, kuna Afisa wa Uhamiaji alipata ajali na akafariki kwa sababu ya gari bovu na alikuwa anaenda kwenye doria katika hizo njia za panya za uhamiaji. Sasa naomba tuweze kupata magari ya kutosha mapya na tuweze kupata mafuta ya kutosha ili hata wale Maaskari wa Uhamiaji waweze kufanya kazi zao bila kipingamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi Karagwe, ni mpakani pia tunapakana na Uganda, Rwanda na Burundi yaani kuna Ziwa linazunguka. Naomba upande wa Karagwe barabara siyo rafiki kabisa, barabara ni za shida sana. Naomba Wizara hii ya Usalama na Mheshimiwa Kangi, babu yangu ananisikia, watuwekee barabara rafiki ili hata mtu akienda kufanya doria aweze kufika. Katika hilo naomba sana sana kwa Mheshimiwa Kangi, Waziri wa Mambo ya Ndani atusikilize na atuangalie kwa jicho la huruma; kule Karagwe kuna maziwa mfano Ziwa Ngoma, Buligi, Kavunjo, Nyamlebe, tunaomba kupatiwa boti ili doria ziweze kufanya kazi kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba kuwepo kwa boti kutasaidia kupambana na biashara haramu zinazofanyika majini kwa sababu ile Karagwe imezungukwa na ziwa. Kwa hiyo, tusipopata boti ndiyo hivyo wahamiaji haramu wanatusumbua wanatoka, Uganda, Rwanda na Burundi hakuna tunachofaidika. Kwa hiyo Mheshimiwa Kangi, babu yangu Waziri wa Mambo ya ndani, naomba ulifanyie kazi tupate boti kwa ajili ya kusadia wananchi ambao wako Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda Misenyi, Wilaya ya Misenyi kwenye Kituo cha Ushuru wa Pamoja na Uganda yaani tulijiunga Kituo cha Ushuru Uganda na Tanzania. Kile kituo kazi kinafanya kazi *twenty four hours*, lakini Maaskari wa Uhamiaji ni wachache, hawatoshi, yaani mtu anaweza aka-*overnight,* akaja akashinda, hivyo. Kwa hiyo hatafanya kazi kwa ufanisi, naomba tuongezewe Maaskari wa Uhamiaji, pale ni mpakani, ukitoka tu pale Mutukula unaingia Uganda. Kwa hiyo wanaotoka Uganda kuja Tanzania wengi ni wahamiaji, sasa tutawajuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tuliyonayo Maaskari wa Uhamiaji ni wachache, mtu mwingine anaweza akachoka hata asiweze kufuatilia aanze kuangalia pasipoti imetoka wapi na inaenda wapi. Kwa hiyo, tukipata Maaskari wa kutosha wa kuwa wanapeana *shift* itatusaidia hata sisi. Kwa hiyo naomba sana sana Mheshimiwa Kangi babu yangu atusaidie katika hilo. Tangu mwaka jana 2018 ndiyo huo muungano ulifanyika Uganda na Tanzania, lakini ndugu zetu wa kule Uganda wana Maaskari wa kutosha wa Uhamiaji *why* kwetu tusipate wale Maaskari wa uhamiaji wa kutosha? Ni kwamba hawapo au ni ile kutokupanga kwamba ukiambiwa uende Kagera ni mpakani huko, kama changamoto tunazozipata kwamba ukienda huko kuna Wanyarwanda, kuna Wahutu, utauawa *no* siyo hivyo, mimi nimezaliwa Ngara lakini kuna shida hizo za wahamiaji, lakini wakitusaidia katika kuleta Maaskari yanaisha. Kwa hiyo naomba hilo lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, gari la uhamiaji la Misenyi ni chakavu chakavu yaani halifai katika kufanya doria, hivi kweli tuko Tanzania na tuko mpakani mwa Uganda? Yaani Maaskari wa Uganda ndiyo wanasaidia kwamba huyu ni mhamiaji kutoka Uganda, huyu ni Mganda amekujaje Tanzania yaani ni aibu, kwa hiyo naomba sana sana, waweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tishio la usalama mpakani, kama madawa ya kulevya ni ngumu sana kubainika sababu mbwa aliyepo pale Misenyi amezeeka, hata akifundishwa hawezi kufundishika. Sasa tunafanya kitu gani? Kwa hiyo naomba wahusika watulee mbwa ambaye bado ni kijana sijui niseme yaani ambaye anaweza kufundishika akaelewa. Kwa hiyo naomba sana sana, Wizara ya Mambo ya Ndani muweze kutuangalia kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naona dakika zimeisha nilikuwa nayo mengi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nadhani ameshakusikia hapo Kabanga *nickel.* Mheshimiwa Ruth Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Saada Mkuya ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na naunga mkono moja kwa moja hoja iliyowasilishwa hapa mezani. Nitazungumzia maeneo matatu, nitazungumzia suala la Magereza, *economic diplomacy* na *diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwenye Kamati kwamba Magereza yetu yana msongamano mkubwa sana na ilipofika Desemba, 2018 Gereza la Segerea lina wanaume 1,723, lakini wafungwa ni 158 tu wafungwa, kwa hiyo walioko rumande ni 1,565. Wanawake wako 313 na waliofungwa ni

66, kwa hiyo rumande wako 247. Kwa hiyo tuseme jumla pale Segerea kuna Mahabusu 1,812. Hii ni namba kubwa sana kwa watu ambao wako Mahabusu, upelelezi unaendelea haujakamilika, wako Mahabusu wanatumia pesa za walipakodi kula, wako Mahabusu badala ya kuweko uraiani wakifanya kazi na kuongeza juhudi za kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kubwa sana sasa Serikali ya Awamu ya Tano kuangalia mfumo wa kutoa haki, ukianzia na TAKUKURU, ukija na *DPP* mpaka na Polisi kuhakikisha kwamba upelelezi unafanyika kwa wakati kusudi hawa Mahabusu waweze kuhukumiwa watoke, kwa sababu wanapoendelea kukaa Mahabusu huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu na si sahihi na hata Mungu hapendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba upelelezi ukamilike kwanza kabla ya kupeleka watu Mahakamani, wapelekwe upelelezi ukiwa umekamilika, kesi inasikilizwa, wanatoka na endapo kuna umuhimu wa kumweka mtu Mahabusu, tunayo *best practice* Zanzibar ambapo Zanzibar unakaa Mahabusu tu miezi tisa kama upelelezi haujakamilika unaachiwa huru. Kwa hiyo, hili jambo ni jambo la kufanyia kazi na namshauri sana Mheshimiwa Waziri, liweze kufanyiwa kazi...

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Kabisa ili haki iweze kutendeka....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel kuna taarifa, Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimpe taarifa mchangiaji kwamba kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai hata kwetu Tanzania Bara ni siku 60, kama upelelezi haujakamilika. Kwa hiyo

asione kwamba Sheria ya Zanzibar iko bora zaidi ya yakwetu, Sheria zote ziko sawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, unaikubali taarifa hiyo?

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siipokei hiyo taarifa, naomba aende Segerea, aende Keko akaangalie halafu aje na *data* hapa. Watu wanakaa mpaka miaka mine, miaka sita upelelezi unaendelea, hiyo siyo sahihi, hata mbele ya Mungu si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi kesi zingine ambazo pia zinakalisha sana watu Magerezani, ni hizi kesi za utakatishaji fedha. Nashauri Serikali ya Awamu ya Tano iangalie tena hii sheria kwa sababu watu wabaya wanaweza kutumia huu mwanya kubambikizia watu kesi za utakatishaji pesa kwa makusudi, kusudi waweze kuendelea kukaa upelelezi unaendelea miaka na miaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo liweze kuangaliwa na kufanyiwa kazi, tukienda kwenye suala hili maana yake tunasema kwamba kama ikiwa watu wanakaa muda mrefu, kesi zao hazisikilizwi, upelelezi unaendelea, tunasema *justice delayed is justice denied*. Kwa hiyo mtu hajapewa nafasi ya kusikilizwa na saa nyingine anaachiwa hata kufidiwa hafidiwi, anakuwa amepoteza miaka yake jela, mahabusu, amepoteza watoto, amepoteza mke na kila kitu. Kwa hiyo hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja pia kwenye suala la *economic diplomacy*. Kwa *trend* ya hivi karibuni hata kwa miaka mingi Ubalozi inakuwa kama ni zawadi au ni adhabu unasukumwa ukakae huko usionekane. Inabidi sasa kubadilisha huu utaratibu kusudi Ubalozi uwe ni shughuli ambayo mtu anakwenda kuifanya na waweze kupata elimu *either trade* au *marketing* au uwezeshaji kusudi wanapokwenda kule kwenye zile Balozi waende na utaalam ambao watakwenda kuutumia kutafuta miradi, fursa na mitaji kwa ajili ya kuiendeleza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumesikia Dokta mmoja anapelekwa Cuba, huyu ni mtaalam mzuri sana nafikiri wa *anesthesia* anajua *economic diplomacy* ni kitu gani? Atakwenda kufanya nini kule? Kwa hiyo, inabidi watu wapate elimu waweze kujua wanapokwenda kule siyo kugonganisha *glass* za *wine,* ni kutafuta fursa, fedha na mitaji kwa ajili ya nchi hii. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA:** Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

**MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kumpa taarifa mchangiaji kwamba huyo ambaye ameteuliwa kwenda Ubalozi wa Cuba anasema ni Daktari na sisi lengo la kuweka Daktari tunataka tufungue Ubalozi Cuba kwa sababu tunalenga hasa kutumia utaalam wao kwenye mambo ya udaktari na tunao wanafunzi wetu wengi ambao wanapelekwa kule kwenda kusomea mambo ya udaktari. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, hawa Mabalozi wanapoteuliwa kuna mpango na programu maalum inayofanywa na Wizara katika kuwajengea uwezo kwenye *economic diplomacy. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Pia katika kupeleka Mabalozi nje ya nchi kuwepo na vigezo vya kuweza kupima utendaji wao wa kazi na upimaji wao utakuwa ni kuweza kuleta mitaji, fursa za biashara na wale ambao wanashindwa warudishwe...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba aliyempa taarifa mwanzo alikuwa ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mhehimiwa Ruth Mollel, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza katika ku-*strengthen* hii *carrier* ya *diplomats* katika mambo ya *economic diplomacy* hata mitaala ya Chuo Kikuu ya *Political Science* na *International Relations* iingizwe watu waweze kutoka kule wakijua kwamba sasa tunakwenda kuingia kwenye uchumi wa nchi na kuboresha maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kulikuwa na Siku ya Mabalozi ambayo sidhani kama siku hizi ipo. Siku hii ilikuwa muhimu ambapo Mabalozi walikuwa wanakutana na kubadilishana uzoefu na kusaidia katika kutafuta mitaji kwa ajili ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala pia la *Diaspora,* tukubali kwamba tunao Watanzania wengi sana ambao wako nje ya nchi wanafanya kazi kule. Kulikuwa na ajenda ya kutengeneza kanzidata ya *Diaspora,* napenda Waziri atakapokuja kuzungumza hapa atuambie kwa mfano kule *Diaspora* tuna Watanzania wangapi. Kwa nini nasema hivyo?

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya kuona ni jinsi gani ya kuwawezesha kuleta mitaji na pesa nyumbani ili kuongeza nguvu ya uchumi na kupunguza umasikini nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia katika nchi zingine, kwa mfano, kwa mujibu wa *statistics* za Benki ya Dunia, kwa mwaka Kenya wanaingiza *2 billion USD* kwa mwaka kutoka *Diaspora;* Uganda wanaingiza *1.2 billion USD*; Somalia wanaingiza *1.4 billion USD;* Nigeria wanaingiza *21 billion USD,* Tanzania tunaingiza ni milioni 456 USD. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mollel kengele imegonga kwa mara ya pili. Mheshimiwa Mollel mwingine, Dkt. Mollel kwa sababu muda wake umeshakwisha hauwezi kumpa taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, Mheshimiwa Maftah Nachuma dakika tano atafuatiwa na Mheshmiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa dakika hizi chache nilizozipata. Kwanza naomba kuunga mkono hoja hizi za Kamati zote mbili lakini nitaongea haraka haraka sana kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, Kamati ya Nishati na Madini imezungumza mambo mengi sana ya msingi na miongoni mwa mambo ambayo nimeyapenda sana ni suala zima la kudhibiti utoroshwaji wa madini

ambapo imeweza kuipongeza Serikali. Nami pia nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kitendo cha kujenga ule ukuta wa Mererani ambapo tanzanite ilikuwa inatoroshwa kwa kiasi kikubwa sana. Wakati wa Kamati Maalum tuliweza kupewa taarifa kwamba miji mingi ya Kenya ukiwemo Mji wa Naivasha umeendelea kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya madini ya tanzanite yanayotoroshwa kutoka Mererani Tanzania, leo ni mji bora kabisa kule Kenya. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kitendo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo bado kuna uhafifu katika kudhibiti madini mengine yakiwemo madini ya *blue sapphire* ambayo yanapatikana kule Tunduru, Mkoani Ruvuma. Kule Tunduru kuna watu wa Sri Lanka wengi sana ambao wananunua madini haya na wanayapeleka kwao wanayaunganisha wanasema haya madini yanatoka Sri Lanka, *blue sapphire* inatoka Tunduru. Niitake Serikali kama kweli tunahitaji kudhibiti sekta hii ya madini ambayo imenufaisha nchi nyingi duniani basi tudhibiti madini ya *blue sapphire* kule Tunduru yasiweze kutoroshwa hovyo hovyo na kupelekwa Sri Lanka na zaidi kuweka *label* ya Sri Lanka kwamba yanatokea pale Sri Lanka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nizungumzie suala la miradi hii ya gesi. Nisikitike kwamba Kamati imesema ni sekta ndogo ya gesi na sekta ndogo ya madini. Nashangaa, kwa nini iitwe sekta ndogo? Kwa sababu kama kweli tunahitaji kuitumia gesi sawasawa, nchi za wenzetu kwa mfano, Qatar na nchi zingine zimeweza kuendelea kwa kutumia uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali tuwekeze katika miradi ya gesi ambayo ilianza kuwekezwa miaka sita, saba iliyopita. Kule Mtwara na Lindi kuna ule mradi wa *LNG,* nashangaa kwamba Serikali iko kimya sana, haiendelezi mradi ule. Ule mradi ulikuja kuleta ajira nyingi sana kwa wananchi wa Mikoa ile ya Kusini, wananchi wa Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftah kuna taarifa, Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mchangiaji kwamba mradi wa *LNG* uwekezaji wa kisima kimoja ni dola bilioni 15. Kwa sheria alizoleta Mheshimiwa Kabudi hakuna mtu atakuja kuwekeza pesa zake zaidi ya shilingi trilioni 30 kwenye *LNG* watakwenda kuwekeza sehemu nyingine. Nampa tu taarifa ili aelewe kwamba hata wale wanaodai fidia hawatalipwa tena. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, inavyoonekana ulikutana nao hao wote wakasema hawaji, siyo? Mheshimiwa Maftaha, unaipokea taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika sana na maelezo yake na kwa kawaida huwa nazungumza mambo ambayo nina uhakika nayo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Taarifa.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa inabidi akishachangia mtu akishapewa taarifa aipokee kwanza ile taarifa aanze kuzungumza ndiyo anapewa taarifa nyingine. Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu amesema pale kwamba Mheshimiwa Kabudi alileta sheria humu ndani, sheria hii ililetwa na Serikali siyo Mheshimiwa Kabudi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa sababu muda wangu ni mchache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nazungumza hapa ni kwamba sekta ya gesi na mafuta ni muhimu sana, haziwezi kuitwa ni sekta ndogo. Naamini kama kweli kwa sababu taarifa ya Kamati imezungumza hapa kwamba Serikali ina mpango wa kuongeza *megawatts* za umeme na mipango ya Serikali inasema ikifika 2020 basi tuweze kuwa na *MW 5,000* lakini taarifa ya Kamati inasema mpaka 2020 tutakuwa na *megawatts* zisizozidi 2,780. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwa sababu tuna sekta ya gesi Mikoa ya Kusini, mpango ule wa kujenga zile *plant* za Lindi, kuendeleza zile *plant* za Mtwara, tujenge *plant* ya umeme Kanda ya Kusini ili tuweze kuziongeza hizi *megawatts* Taifa hili liweze kuondokana na tatizo hili la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango ya Serikali ya kujenga *Stigler's Gorge,* ni mipango mizuri kwa sababu lazima kama Taifa kuwe na miradi ya kielelezo lakini bado ikifika 2020 hatutakuwa na *megawatts* zile ambazo tunazihitaji. Kwa hiyo, kwa kuwa miradi ya gesi iko tayari maeneo ya Kusini, Serikali ijenga *plant* za umeme kwa kutumia hii gesi yetu ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki. Bahati njema kwamba Mikoa ya Kusini hivi sasa tayari Serikali imeshaiunganisha katika gridi ya Taifa. Tukijenga *plant* Mtwara na Lindi tutaweza kusafirisha umeme mwingi tukaingiza katika gridi yetu ya Taifa na tukaondokana na tatizo hili la kukosa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumzie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Saada Mkuya atafuatiwa na

Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

**MHE. SAADA M. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja za Kamati zetu mbili ambazo zimewasilishwa hapa na tunaendelea kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu leo kwanza nataka nitumie *forum* hii ya Bunge kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Magufuli pamoja na Baraza lake la Mawaziri kuona umuhimu mkubwa uliopo wa kuondosha tozo ya Ongezeko la Thamani kwa umeme ambao *ZECO* wananunua kutoka *TANESCO.* Tunashukuru sana sana na kutokana na jambo hili tunaona *spirit* kubwa iliyopo katika Serikali ya Awamu ya Tano kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo katika Muungano wetu. Kwa hivyo, tunamshukuru sana na naamini Wazanzibari wamefurahi sana kwenye hili na wanaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na shukurani hizo, vilevile naomba kuzishukuru Kamati zetu za Bajeti na Kamati yetu ya Nishati na Madini kwa sababu kwa pamoja walitoa uzito mkubwa kuona kwamba Serikali inalitatua tatizo hili kwa haraka zaidi. Tunazishukuru sana Kamati hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, naomba nitoe shukurani hizi kwa Mheshimiwa Spika kwa sababu alipobaini jambo hili hakusita kulipa uzito unaostahiki na hatimaye limekwenda kutatuliwa. Tunawashukuru sana pia Wabunge wote ambao walikuwa wamelichangia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na *VAT,* kiukweli *VAT* ni jambo moja dogo katika mambo mengi ambayo yanaikabili Shirika letu la Umeme la Zanzibar *(ZECO)* wakati linaponunua umeme kwa *TANESCO.* Lazima nikiri, Waziri wa Nishati na Naibu wake wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana na kwa nia hasa ya dhati inaonekana.

Nikiongea na Mheshimiwa Waziri ananipa *commitment* ambayo inatoka kabisa moyoni kwake kwamba wanajitahidi kuhakikisha hata zile gharama nyinginezo ambazo zimeonekana ni mzigo mkubwa sana kwa *ZECO* ambazo zinakwenda kwa wananchi wanaotumia umeme kule Zanzibar, amekuwa akinipa *comfort* na *commitment* ya hali ya juu. Tunataraji sana, sana, sana hili jambo litafanyika kwa uharaka zaidi ili kuona kwamba tunakwenda kupunguza ule mzigo wa gharama ya umeme ambao unanunuliwa na *ZECO* kutokea *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo hili nadhani tunapata mafunzo ya mambo mawili; kwanza ni kuhakikisha ama ni kuona kwamba hata katika zile sekta ambazo hatuzioni ni za Muungano lakini tunajua katika utekelezaji wa *activity* zetu zina athari katika pande mbili za Muungano. Kwa mfano, kama utaangalia tozo hizi ambazo zinatozwa utaona kwamba Zanzibar wanaweza tu wakanunua lakini kuna athari kubwa katika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ambapo vilevile kuna wananchi wa Tanzania nao wanatumia. Kwa hivyo, hilo ni funzo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini funzo la pili, ni kuona ushirikishwaji wa taasisi zetu hata kama siyo za Muungano. Kwa vile tuko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna umuhimu mkubwa hata katika sekta zile ambazo siyo za Muungano kufanya kazi kwa pamoja ili kuona kwamba hali hii ambayo inaweza tu ikatokea ikaleta mgogoro *somewhere* inaondoka. Kwa hivyo, hata tunapokwenda katika bajeti tunaomba *consideration* ya taasisi ambazo zinafanya kazi zinazofanana zifanye kazi kwa pamoja ili kuona kwamba manufaa yanayopatikana yanakuwa ni ya pande mbili za Muungano. Tunaipongeza sana Serikali, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri, tunampongeza sana Naibu Waziri kwa sababu tunaona kwamba ile *commitment* ni ya dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeoimba sana Serikali kuona ule mchakato ama yule *consultant* ambaye anafanya kazi ya kuangalia gharama nyinginezo aweze

kuharakisha. Vilevile tunapokwenda huyo *consultant, of course,* amepewa *terms of reference* lakini nadhani hajui kwa dhati jinsi gani hasa hasa hizi sekta mbili zinavyofanya kazi yaani sekta moja lakini katika pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ingewezekana sisi kama wananchi ama watu wetu wa ndani hata kama ni *consultant* awe ni mtu wa ndani ambaye anajua kiundani *operations* za Serikali zetu mbili. Kama tunatafuta mtu mwingine ambaye hata hajui *operation* yenyewe inavyofanya kazi hataweza kujua kiundani tatizo lililopo na yeye ataangalia katika *business level.* Hiyo inaweza kabisa kuleta utata katika mapendekezo ambayo atayatoa na pengine sana azimio ambalo tumeazimia lisiweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna *doubt* kwamba umeme ni nyenzo kubwa sana katika uchumi wa Taifa hili. Kwa upande wangu unajua *sometimes* unaweza ukawa unashangaa mtu anapinga mradi wa umeme kwa mfano wa *Stigler's Gorge*. Sasa hivi Tanzania tuna uhaba wa umeme na Serikali inafanya *initiatives* kwa ajili ya kutafuta umeme. Wenzetu pengine walioko nje ambao kwa namna moja ama nyingine wanahisi kutakuwa kuna maslahi wao wanaangalia katika *aspect* ya mazingira lakini tunaojua hitaji hasa la changamoto hii ni sisi Watanzania. Kwa hiyo, kwenye suala kama hili la kitaifa tukiacha tofauti zetu za kisiasa na kimtazamo, nadhani kuna umuhimu mkubwa wa kui-*support* Serikali yetu kwenda kuangalia jinsi gani tunaweza kupata umeme wa uhakika na wa kutosha ili kuona kwamba uchumi wetu unapaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tukiangalia tuko katika tuko hiyo *development stage* tukiwa tunaangalia uchumi kukua, tunakua katika kiwango ambacho bado hatujakua vizuri lakini kinaweka miundombinu ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa uchumi wetu uweze kubeba *development* za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo tunaomba wenzangu hata katika maeneo kama haya ya kitaifa ni lazima tuwepo pamoja na ni lazima tuungane pamoja tuone kwamba tunai- *support* Serikali kwa nguvu zote kuona kwamba inakwenda kutekeleza jambo hili. Mtu mwingine atakuwa anaangalia kwa mawazo yake mengine, *of course* tunajua kwamba kuna *choice* baina ya ukuaji wa uchumi na mazingira, lakini sisi kwa sababu ni Taifa ambalo linaloendelea tunahitaji *development*, tunahitaji uchumi wetu ukue, lazima *choice* tuangalie lile ambayo utaleta *impact* kwa wananchi wengi walio maskini *rather than* kuangalia hasara kidogo ya upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeze sana Serikali na tunatarajia kwamba hizi *process* ambazo zinaendelea zinakamilika kwa haraka zaidi ili kuona kwamba *stiegler's gorge project* ile inafanikiwa na tunataka kuzalisha umeme ili umeme ufaidishe wananchi mmoja mmoja. Naamini *the more* umeme utakapokuwa unapatikana Tanzania Bara pengine inawezekana hata ile *multply effect* ikaenda mpaka Zanzibar. Kwa hiyo, kwenye suala la maendeleo hakuna budi lazima tuungane kwa pamoja, tuone kwamba hili jambo linapatiwa ufumbuzi wa haraka na tunaweza kufaidi matunda ya uhuru wetu kama vile ambavyo tumekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali vilevile kuona kuna umuhimu wa kuanzisha Balozi kule Cuba. Hili suala nadhani tumelisema sana humu ndani na limejadiliwa kwa mapana, lakini kwa sababu Serikali yetu ni Serikali sikivu imeona kuna umuhimu sana wa kufungua ofisi kule Cuba na tunatarajia sana mafanikio yale ambayo tunayo sasa yataendelea kuleta athari chanya zaidi katika uchumi wetu kutokana na kazi ambazo Balozi atakuwa anazifanya kule Cuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa John Heche ajiandae.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kusudi niweze kuchangia katika hotuba za Kamati zetu mbili Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Taifa lolote ulimwenguni linapimwa uwezo wake na nguvu zake kutokana na nguvu za kiuchumi na nguvu za kiulinzi na usalama. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika Taifa letu vimefanya kazi kubwa kwa uhakika na tunaendelea kupata heshima ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu kutokana na uzalendo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiambie Serikali tu kwamba kuna jambo moja ambalo linajitokeza ambalo si jema sana la ugomvi baina ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na wananchi hasa katika suala zima la ardhi. Migogoro ya ardhi imekuwa inatia doa amani yetu na kwa maana hiyo naishauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Magereza na vyombo vingine vyote vya Ulinzi na Usalama ikiwemo Jeshi la Polisi ardhi zake zipimwe na zijulikane kabisa kwamba hairuhusiwi raia yoyote kusogea na kujenga karibu na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeonekana wazi kwamba vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimekuwa vikichukua maeneo makubwa muda mrefu lakini raia kutokana na kwamba tunazidi kuongezeka, tumeendelea kuwa tunasogea kwenye maeneo haya na kuchukua maeneo na hatimaye kuanzisha mizozo isiyokuwa na umuhimu. Kwa maana hiyo naiomba Serikali itenge pesa makusudi kabisa ili kusudi maeneo yetu vyombo vya Ulinzi na Usalama yapimwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na *beacon*, ni alama ambazo zinaonyesha ramani yetu au mipaka yetu ikoje katika mustakabali wa usalama wa Taifa letu na kwa maana hiyo kwa sababu kuna *beacon* ni mbalimbali zimeng'olewa katika mipaka yetu na nchi jirani ambazo zinatuzunguka, basi ni jambo la muhimu kuhakikisha kwamba Serikali kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nchi za Nje pamoja na Wizara ya Ardhi wafanye jitihada kuhakikisha kwamba *beacon* zetu zinarejeshwa mahali ambapo zilikuwepo hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la diplomasia ya uchumi, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada ambazo ameendelea nazo za kufufua Shirika letu la ndege. Diplomasia ya uchumi isingewezekana kama kusingekuwa na jitahada mahususi za Mheshimiwa Rais wetu za kuhakikisha kwamba tunakuwa na Shirika la Ndege ambalo litakuwa linatuunganisha na Mataifa mengine ya nje. Kwa maana ya kwamba wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza nchini kwetu hata kama wangekuwa wanapatikana huko nje ingekuwa ni tatizo zaidi kuwafikisha katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata watalii vilevile wanaweza wakaja pamoja na kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unaendelea kuimarika kutokana na kwamba mchango wa shirika hili utaendelea kuonekana. Niiombe sasa Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama muda wote vipatiwe pesa zake kwa wakati hasa katika masuala mazima ya miradi yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la nishati na madini, niipongeze Wizara yetu ya Nishati kwa jitihada nzuri na za makusudi ambazo zimeendeelea kuonekana na hasa kwa jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kuzionyesha na kwa kuthubutu kuhakikisha kwamba mradi mkubwa wa *Stiegler's gorge* unaanza kutekelezwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata jana tumeshuhudia uendelezaji wa mradi wa Rusumo katika Mto Kagera mradi ambao utaendelea kutuletea huduma ya umeme wa megawati karibu 27 ambazo zitakuwa zinagawanywa katika Taifa na sisi tutanufaika kwa utaratibu huo. Kwa maana hiyo nchi yetu itakapokuwa inaendelea katika sera yake ya kukuza viwanda na kuwa Tanzania mpya ya viwanda ninaamini kwamba matarajio hayo tunaweza kuyafikia muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimeendelea kuwa na mashirika yake ya uzalishaji mali ikiwemo Shirika la SUMA JKT na hata Magereza, Jeshi la Ulinzi na Usalama linayo Mashirika yake ya Mzinga na Nyumbu. Vyombo hivi vimekuwa vikifanya kazi zake nzuri na kwa maana hiyo naiomba Serikali kwa makusudi mazima ihakikishe kwamba inaviongezea nguvu kuhakikisha kwamba vinashiriki katika uzalishaji mali na kuweza kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima linalohusiana na suala la vitambulisho vya Taifa. *NIDA* wamekuwa ni wakala wa kuzalisha hivi vitambulisha vya Taifa, lakini kimsingi wameshindwa kufikia malengo kutokana na kwamba wanapungukiwa pesa pamoja na vitendea kazi vingine zikiwemo mashine za kuzalisha hizo kadi za vitambulisho vya Taifa. Kwa maana hiyo naomba Serikali kwa makusudi mazima ijipange vizuri kuhakikisha kwamba *NIDA* wanawezeshwa ili kusudi waweze kuvitoa vitambulisho hivyo ambavyo ndio vitakuwa vinaonesha uraia halali wa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiendelea kuiona kwamba nchi yetu inasonga mbele, tuwe katika utaratibu unaokubalika kwa kuhakikisha kwamba vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinakaa katika utaratibu unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika Wizara ya Madini, kwanza niishauri tu kwamba katika kile kikao cha

wadau cha tarehe 22 na tarehe 23 naomba Wizara iyatekeleze maazimio yote ambayo yaliazimiwa na kikao hicho cha wadau. Pendekezo lingine ninalotaka kulitoa kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba Mataifa mengine yaliyoendelea yamekuwa yakishindana katika uzalishaji na kulimbikiza silaha za maangamizi. Naishauri Serikali yangu ya Tanzania yenyewe ijitahidi katika kuhakikisha kwamba tunalimbikiza vitu vya thamani ikiwemo dhahabu na Benki yetu Kuu ihakikishe kwamba inanunua dhahabu na kuiweka katika Hazina ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati zote mbili. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Lucy Mahenga ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kwa mwaka huu uliopita. Kipekee kabisa nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe kwa jinsi ambavyo wameweza kuandika ripoti nzuri nimeisoma, kwa kweli na ushauri ambao wameutoa ni ushauri muhimu sana katika sekta hii kwa ajili ya kuipeleka mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Sekta ya Madini, nianze kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa miaka mitatu, lakini kikubwa zaidi tarehe 22 Januari, 2019 ambapo aliweza kukaa na wadau wa madini Mkoani Dar es Salaam, kwa kweli inaonyesha nia ya dhati kabisa kuweza kuondoa changamoto na kero mbalimbali zilizopo kwa wananchi hasa wachimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niunge mkono kabisa Kamati ambayo imependekeza kwamba yale

mapendekezo ya wachimbaji wadogo walivyokutana kule Dar es Salaam, Serikali iweze kuyachukua na kuweza kuyafanyia kazi. Kwa kunukuu yanapatikana katika ukurasa wa 32, 33 na 34. Kwa msisitizo zaidi nikianza na pendekezo la pili ambalo ni kuondoa baadhi ya kodi tumegundua kwamba wachimbaji wadogo na wachimbaji wanazo kodi nyingi ambazo wakati mwingine zinawarudisha nyuma kabisa katika shughuli zao za uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kutokana na ushauri ambapo wachimbaji wadogo wenyewe wadau wa wachimbaji walivyokutana, nilikuwa naishauri Serikali kipekee kabisa iweze kuangalia na kupunguza hizi kodi ambazo zinakuwa ni kodi zinazokandamiza wachimbaji wadogo wa madini na wachimbaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ushauri ambao aliutoa kwamba wanahitaji kuanzisha benki ya madini, niunge mkono kabisa kwamba Serikali iangalie namna ya ku-*support* kuweza kuanzisha benki ya madini ili wachimbaji hasa wale wadogo ambao hawana uwezo wapate fursa ya kuweza kukopeshwa yaani kwa riba nafuu ili waweze kumudu shughuli zao za uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna eneo ambalo pia walizungumzia kwamba katika maeneo mengi ambayo yamepewa leseni za utafiti wa madini unakuta maeneo mengi sana yanachukuliwa kwa ajili ya utafiti wa madini. Lakini maeneo hayo wachimbaji wanakuwa hawaruhusiwi kufanya shughuli zao zozote zile. Kwa hiyo, niunge mkono mapendekezo hayo kwamba Serikali iangalie maeneo haya ambayo mengi yalikuwa yamepewa kwa ajili ya shughuli za utafiti wepewe wachimbaji hasa wadogo waweze kufanya shughuli za kiuchumi hatimaye waweze kuchangia pato la Taifa. Kwa sababu wachimbaji hawa watakapoweza kufanya shughuli zao za uchimbaji wataweza kupata fedha na mwisho wa siku wataweza kuchangia kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la ruzuku kwa wachimbaji wadogo, niombe Serikali suala hili ni muhimu sana. Siku za nyuma Serikali ilikuwa inatoa ruzuku, lakini hivi karibuni hatuoni tana wachimbaji wadogo kupewa ruzuku. Niiombe sasa Serikali iangalie siri kwa macho mawili, ile benki kama vile wakulima wanavyopewa ruzuku hata wachimbaji wadogo tuangalie namna ya kuwapa ruzuku ili hatimaye waweze kuwekeza zaidi katika shughuli zao za uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala muhimu kabisa ambalo wamelizungumzia, ni suala la tozo na ada mbalimbali kwa wachimbaji wadogo wa madini ambazo wamekuwa wakilipa kwa dola. Kwa hiyo, niombe pia hata mimi nashauri kwamba Serikali iangalie tozo hizi zilipo kwa shilingi ya Tanzania, kama ambavyo tunasisitiza hata watu wengine wageni wakiingia ndani ya nchi walipwe kwa shilingi hata katika wachimbaji wa madini pia tuangalie namna ya tozo hizi kulipwa kwa shilingi za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda pia kusisitiza kuna baadhi ya maeneo ambayo yalichukuliwa kwa ajili ya uanzishaji wa shughuli mbalimbali za madini likiwemo lile eneo la Lwamgasa ambapo wamechukua kwa ajili ya kuanzisha shughuli mbalimbali za uchimbaji lakini kwa ubia na watu wengine. Watu hawa kwa muda mrefu sana eneo hili limechukuliwa lakini hawajapewa fidia. Kwa hiyo niiombe Serikali pia iangalie namna watu hawa wapewe fidia, miezi sita imepita hakuna chochote, ni mwaka sasa hakuna chochote kinachoendelea na sheria tunavyoijua ni kwamba kwa muda wa miezi sita kama wameshafanyiwa tathmini hawajalipwa Serikali inatakiwa kufanya tathmini upya tena ili waweze kulipwa haki zao za msingi. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie sasa namna ya kuweza kuhakikisha hawa ambao wanahitaji kulipwa fidia wanalipwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa hawarusiwi kufanya shughuli zozote za kiuchumi katika maeneo yale. Sasa kwa sababu mtu hatumruhusu kufanya

shughuli yoyote anapataje uchumi wake kama humruhusu kulima, haruhusiwi kufanya kitu chochote katika eneo lake. Kwa hiyo, naomba sana katika Sekta ya Madini Serikali iangalie namna zaidi ya kuangalia mapendekezo ambayo wachimbaji wa madini na wadau mbalimbali wa madini wameweza kuyapendekeza na kuweza kuiomba Serikali iweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Sekta ya Umeme, Sekta ya Nishati nianze kipekee kabisa kupongeza Serikali hasa Wizara ya Nishati kupitia Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa hakika wanafanya kazi kubwa sana kwenye hii Wizara, kila wakati Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanapita sehemu mbalimbali kukagua miradi mbalimbali ya umeme hata kwenye Jimbo langu wamefika, niwapongeze sana kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya kupeleka umeme kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *REA III*, katika awamu ya kwanza yake, ni kweli wamefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata umeme. Niombe sasa zile nguzo ambazo pengine tunapopeleka umeme labda kwenye kijiji fulani, unakuta nguzo zinakuwa chache sana wanaoweza kupata huo umeme ni wachache ukilinganisha na mahitaji. Watanzania sasa hivi wanahitaji kupata umeme kwa sababu umeme ndio maendeleo kupitia umeme watakuwa na uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi, wengine watatumia kwa ajili ya viwanda. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri hebu tuangalie kuongezea nguzo za umeme hasa kwenye maeneo ambako wanapeleka umeme huu wa *REA,* watu wanahitaji umeme sana . *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatolea mfano tu kwenye Jimbo langu, pale Nyakagomba wamepeleka kweli umeme wa *REA III,* katika awamu ya kwanza, lakini kila siku hata hivi leo natumiwa meseji sasa Mbunge mbona nguzo hazitoshi, watu wengi tunahitaji umeme? Kwa hiyo, nitumie fursa hii

kuomba kabisa kwamba hebu tuangalie kuongeza nguzo kwa sababu wananchi wanapenda umeme kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niishukuru Serikali kwa mradi mkubwa sana wa Rufiji ule wa *Stiegler's Gorge,* ni mradi wa kimkakati, naipongeza sana Serikali kwa kufanya maamuzi hayo. Tuna uhakika kwamba baada ya muda mfupi Tanzania itaondokana na tatizo la upungufu wa umeme. Kwa hiyo, niombe tu Serikali iendeleze huo mradi kwa sababu ni mradi mkubwa wa kimkakati ili tuweze kufikia azma ya Serikali ya viwanda. Hakika umeme wa *Stieglers Gorge* utatusaidia kuweza kufikia hiyo azma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna miradi mingine ya umeme, kwa mfano katika Mkoa wetu wa Geita kuna ule mradi wa *220 KV*. Ni kweli Mheshimiwa Waziri amezindua huu umeme lakini hatujaona kinachoendelea. Tuombe hii miradi Serikali iendelee kuwekeza nguvu ili iweze kufanya kazi kwa wakati. Wananchi kama ambavyo nimetangulia kusema wanahitaji umeme... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa Hamida Abdallah ajiandae.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye kamati hizi kwa mwaka huu. Kabla sijaanza kuzungumza, juzi kuna propaganda imesemwa hapa na

tunajua Bunge hili ni chombo cha wananchi na lina heshima kubwa. Sasa kama propaganda inaweza ikaja mpaka humu na ikaacha kujibiwa matokeo yake inaweza kuaminika na ikaleta uchafuzi. Ni bahati mbaya sana kwamba propaganda hiyo ilizungumzwa na kiongozi mwenyewe wa mhimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tarime hatujawahi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche subiri kidogo. Hayo maneno yalizungumzwa humu ndani na Kikanuni kama Mheshimiwa Mbunge ana shida na kilichozungumzwa na Kiti hapa, utaratibu uko kwenye Kanuni ya 5. Kwa hivyo, Mheshimiwa Heche endelea na mchango wako, usizungumzie yale ambayo Kiti kilisema kwa sababu Kanuni zetu zimeweka utaratibu. Kama kuna jambo lilizungumzwa na Kiti hapa Mbunge hakuridhika nalo Kanuni ya 5 inatoa maelekezo ya nini cha kufanya. Kwa hiyo naomba ujielekeze kwenye mchango wako na sio yale ambayo yalizungumzwa na Mheshimiwa Spika.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu huo mkubwa uliouchukua. Nazungumza kwa sababu tuko kwenye Kamati ya Nishati. Cha kwanza kama Mbunge wa Tarime nataka kusema hatujawahi kupewa pesa yoyote bure na mgodi, haijawahi kutokea. Pesa ambazo Halmashauri ya Tarime inapewa au iliyokusanya ni pesa zinazoitwa *service levy. Service levy* ipo kwa mujibu wa sheria; na kwa miaka mitatu tukizijumlisha ndiyo tumepata bilioni 9.3. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuna taarifa, ukae upokee taarifa hiyo. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu Mheshimiwa Heche anasema hawajawahi

kupokea fedha, lakini alichokisema Mkuu wa Mkoa alisema ni bilioni 9.5, Mwenyekiti wa Halmashauri yake, rafiki yake akasema sio bilioni 9.5 ni bilioni 9.3. Sasa kati ya yeye na Mwenyekiti wa Halmashauri nani anajua kwamba, fedha zimeingia kwa sababu tayari Mwenyekiti wake wa Halmashauri amekiri wamepewa, lakini ni bilioni 9.3 siyo 9.5? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fundisheni watu kuwa maana ya Wabunge wa Chama Tawala, mjiheshimu kama mnaoongoza nchi ili tujadiliane mambo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa tulizopokea ni pesa za *service levy* ambazo ni kodi; na kodi ya *service levy* ina sheria yake ya matumizi. Sheria inasema unapokuwa umepokea pesa hizo *60 percent* inakwenda kwenye *development, 40 percent* inakwenda kwenye uendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Tarime tumepeta hizo pesa tukasema hatuwezi kupeleka *60 percent,* tukapeleka *development 80 percent,* tofauti na wengine wote. Nataka nikutajie miradi michache tuliyofanya ili mjue Tarime ni Wilaya. Pesa za vijana na walemavu tumepeleka shilingi 1,219,000,000, *TARURA* tumepeleka milioni 700, madarasa kwenye vijiji... *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna Taarifa Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi nitoe Taarifa. Naomba nimpe Taarifa mzungumzaji, mdogo wangu Mheshimiwa Heche, sioni kwa nini atoe pumzi kubwa sana ya kupinga jambo hilo wakati bajeti yake sio hii. Mwenyekiti wa Halmashauri yake na mhasibu wa Halmashauri na Mkurugenzi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Sawa, Mkurugenzi wa Halmashauri, Mwenyekiti wake na Mhasibu wake asubuhi ya leo wanasema wamepelekewa Kamati ya Ukaguzi na Mkuu wa Mkoa wa Mara na wako tayari kupokea Kamati hiyo na kufanya ukaguzi. Sasa anachokifanya hapa Mheshimiwa Heche sijui kama anapinga ukaguzi au anapinga nini? Sielewi anachotaka kupinga hapa saa hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuwe tunakuwa na uvumilivu wa kusikiliza wengine wanasemaje na wanalindwa na kanuni, tuwe na uvumilivu. Mheshimiwa Heche unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama ni kuhusu utaratibu au ni taarifa? Mimi nasema maendeleo tuliyoyafanya; madawati Tarime tumetengeneza 12,500 hakuna mtoto anakaa chini. Vituo vya afya tumetengeneza saba kwa miaka mitatu, vingine hamjaleta Madaktari, zahanati 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwa kifupi tu na mengine mengi. Kwa kumalizia *CAG* ametoa hati safi mara tatu mfululizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inayoongozwa na CHADEMA, Tarime chini ya Mbunge Heche. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye *REA.* Serikali ya CCM walisema wao ni Serikali ya wanyonge na

kwenye wanyonge tulisema tuwapelekee maji na umeme. Kwenye maji wammeshindwa kwa sababu, Mheshimiwa Silinde alitoa hapa takwimu, sasa mimi nakuja kwenye umeme. *REA* Awamu ya Tatu iliyoanza mwaka 2017/2018, 2018/2019 tulipanga kupeleka umeme kwenye vijiji 3,559, leo tunavyozungumza vijiji vilivyopelekewa umeme ni 322 chini ya asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipanga kuunganishia wananchi laki moja na themanini...

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Tulieni dawa iingie.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Mheshimiwa Heche ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, lakini naomba nimpe taarifa anapoisemea miradi ya *REA* Awamu ya Tatu iko ya aina mbalimbali, kuna ujazilizi, kuna *off-grid,* kuna *REA* yenyewe ya *grid*. Katika utekelezaji wa miradi hiyo kuanzia tarehe 1/1/2017 mpaka tunavyozungumza sasa jumla ya vijiji ambavyo vimefikiwa ni 1,393. Kwa hiyo anaposema vijiji 322 akizungungumzia *grid extension* asisahau kwamba, miradi yote hiyo, asisahau kusema Makambako Songea anajua taarifa, asisahau kusema ya Iringa, Shinyanga, asisahau kusema na miradi ya ujazilizi, kwa hiyo, nilikuwa nampa taarifa tu Mheshimiwa Mjumbe wa Kamati yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachangia. Kwanza *grid extension* au *densification*

anaijua ambayo wao wanasema mabeberu, walikuwa wanawatukana mabeberu, yote *grid extension* inafadhiliwa na Norway ambao ni mabeberu anayoizungumza yeye pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulilenga kuunganishia umeme wananchi 180,766, waliounganishiwa hivi tunavyozungumza ni wananchi 7,300 peke yake chini ya asilimia tatu. Hizi pesa mfadhili wake ni nani? *Financer* wa pesa za *REA* na ninyi wote ni Wabunge, kama mnataka kurudi humu lazima muwe wakweli. *Financer* wa pesa za *REA* ni wananchi wenyewe wanaonunua mafuta, wanaonunua umeme na hizi pesa zilikuwa *ring fenced.* Sasa nataka watwambie, Mheshimiwa Waziri atwambie hapa, je, hizi pesa ndio wamechukua wakaenda kununua watu au wakaenda kujenga miradi mingine ambayo haikukusudiwa kufanyika? Kwa sababu, pesa za *REA* ziko *ring fenced* na zinaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo kama tumewaunganishia wananchi umeme asilimia 3.8 peke yake; na Mheshimiwa Waziri namsikitikia, kwa sababu ukihesabu vijiji, kuna vijiji tumeenda, mimi ni Mjumbe wa Kamati, umeme umepelekwa kijijini lakini umepita kwenye nyumba nne tu kijijini, nyumba nne peke yake; halafu wanahesabu tu vijiji, wanakimbia wanahesabu vijiji. Sasa kama leo ni miaka miwili ya *REA Phase III wa*meunganisha vijiji 322 kati ya 3,500, wanafaa kuendelea kuongoza nchi hii? Wanafaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye *Stieglers Gorge.* Kwanza kuna watu wanaimba humu *Stieglers Gorge! Stieglers Gorge!* Wamekuwa kama makasuku. *Stieglers Gorge Gorge* kupata umeme wake ni mwaka 2027…

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** …kwa sababu, kuna wengine wanafikiri utawaka kesho umeme wa *Stieglers Gorge.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Keissy.

**TAARIFA**

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Naibu Spika, afute kauli yake kutuita kasuku, sisi sio kasuku hapa. Tuna busara kuliko yeye mara tatu, mara nne, afute kauli yake mara moja, hamna kasuku humu ndani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, hilo neno lilishawahi kusemwa na huko nje likaleta ukakasi kidogo. Naomba ulifute hilo utafute neno lingine, uendelee na mchango wako.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niondoe, wanaimba vyovyote wanavyoimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa *Stiegler's* ni bilioni 700; hivi tunavyozungumza pesa ambazo zimekwenda ni bilioni 26...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** ...sasa kama umeme huu kujenga hili bwawa ni trilioni 7.1, trilioni 7.1 kwa bilioni 700 tunahitaji miaka 10 kujenga...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuna taarifa nyingine. Mheshimiwa Dokta Mollel.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mhesimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa kaka yangu Mheshimiwa Heche kwamba, chama ambacho yeye ni mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati Kuu ambaye Kamati Kuu aliingizwa baada ya yeye kuanzisha maandamano ya kumpindua Mwenyekiti kwa sababu ya matumizi ya zaidi ya bilioni mbili

na ukipiga mahesabu ni zaidi ya bilioni kumi na mbili, pesa zilizopatikana kwenye chama mpaka leo hawamiliki hata choo. Sasa tulinganishe ukasuku kati ya watu ambao umeme umepelekwa kwa kiwango...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** ...tulinganishe ukasuku ni upi kati ya maelezo aliyoeleza...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mollel, neno kasuku limeshafutwa, neno kasuku limeshafutwa Mheshimiwa Mollel. Mheshimiwa Heche unaipokea Taarifa hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Unampa mtu mmoja mara mbili, si ndiyo? Haya, sawa.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa mbili kwa mtu mmoja...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, unafanya, una-*allow* Kikao cha Bunge kiwe soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi *Stiegler's Gorge* pesa zilizotengwa ni *700 billion,* pesa zilizokwenda ni bilioni 27. Kampuni iliyopewa tenda ya *Arab Contractors* ni kampuni inayohusika kujenga nyumba, haijawahi kujenga bwawa popote duniani, haijawahi. Kampuni hii imetafuta mtu wa kum-*subcontract* inayetaka kumpa *80 percent* ya mradi, watu wanakataa wanaiambia nipe kazi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii nchi ni ya kwetu...

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** ...na sisi tunasema...

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *source* nyingi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuna Kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Subira Mgalu, Kanuni inayovunjwa?

**MBUNGE FULANI:** Aitaje.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anayezungumza amevunja amevunja kanuni...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** ...Nataja, nataja Kanuni. Kanuni ya 64(1)...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba mtulie, amepewa nafasi Mheshimiwa Subira Mgalu kuzungumza, naomba mtulie, Mheshimiwa Haonga nazungumza tafadhali. Mheshimiwa Subira Mgalu endelea; Mheshimiwa Halima Mdee tafadhali! Mheshimiwa Halima! Mheshimiwa Subira Mgalu endelea.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa taratibu Kanuni ya 64(1) kwamba Mheshimiwa Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nithibitishe Mheshimiwa Mbunge 1(a) kwamba, Mheshimiwa Heche

amesema uongo kwamba Kampuni ya *Arab Contractors* imetafuta mbia; Kampuni ya *Arab Contractors* ilivyoshiriki tenda ya kujenga Mradi wa *Stiegler's Gorge* ilikuja ilikuwa na *JV* ya *El Sewedy Electric* Kampuni ya Misri na hakuna mpaka sasa hajatoa asilimia 80 ya kazi alizopewa. Kwa kulitaarifu Bunge lako tarehe 14 tunamkabidhi *site.* Kwa hiyo naomba afute kauli yake au alithibitishie Bunge kwa sababu mimi nina uhakika na nasema ninavyosema.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuthibitisha.

**MBUNGE FULANI:** Sio wewe sasa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namsaidia Mheshimiwa Heche kuthibitisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona uthibitishe ya Ujiji! Ujiji! Halmashauri ya Ujiji thibitisha!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a). Fasili ya (2) ya Kanuni hizi inamtaka Mbunge anayetaka kusimama kuhusu jambo hili atasema Kuhusu Utaratibu na ndicho alichokifanya.

Mheshimiwa Subira Mgalu anasema mchangiaji, Mheshimiwa Heche, anatoa taarifa Bungeni ambazo hazina ukweli na ukisoma Kanuni yetu ya 63, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane; na huwa nawakumbusha siku zote ni vizuri kusikiliza ili kanuni hizi tuzifahamu. Hii ni 2019 na bado nasikitika kuna Wabunge wa mara nyingi kabisa ambao wako humu ndani na wao bado wanataka kuonesha kana kwamba kanuni hizi hawazijui. Mheshimiwa Halima Mdee nasikia kila kitu.

Waheshimiwa Wabunge Kanuni yetu ya 63 inakataza kusema uongo Bungeni, jambo ambalo Mheshimiwa Subira

Mgalu limemsimamisha ni kuhusu maneno aliyoyazungumza ama taarifa anayoizungumza Mheshimiwa Heche kuhusu kampuni hii ambayo imepewa kazi ya kujenga Mradi ama Bwawa la *Stieglers Gorge,* kwamba kampuni iliyopewa haina uwezo wa kujenga na imetoa asilimia 80 ya kazi zake kwa kampuni nyingine. Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kutumia Kanuni ya 64 anasema kwamba kampuni hiyo wakati ikiomba kazi haikuomba peke yake, iliomba pamoja na kampuni nyingine ndiyo maana ya *joint venture.*

Kwa namna hiyo, kwa matakwa ya Kanuni ya 63 inayokataza kusema uongo maana yake ni kwamba Mheshimiwa Subira ameonesha uongo uko wapi kwa masharti ya Kanuni ya 63. Kwa sababu Kanuni ya 63 inataka Mbunge anayesema mwingine anasema uwongo ndiye anayepaswa kuthibitisha. Katika mazingira haya Mheshimiwa Heche kwa kuwa huo mkataba mimi siko nao hapa; muwe mnasikiliza. Mheshimiwa Haonga, upo hapa huu ni mwaka wa nne, wewe sio Mbunge mgeni tena, unazifahamu kanuni. Nikisimama, usizungumze tafadhali.

Kwa masharti ya 63, Mheshimiwa Subira Mgalu ambaye anatoka Wizara yenye dhamana na jambo hili, naye anao uwezo wa kuleta mkataba hapa ili tuweze kuendelea na mjadala huu. Kwa sasa kwa kuwa mkataba naweza kuletewa hapo, nimtake Mheshimiwa Heche kuchukua utaratibu huu alioomba Mheshimiwa Subira, nami natakiwa kutoa maamuzi, nikuombe hayo maneno uyatowe ili tuendelee na mjadala. Kwa sababu tukifika mahali pa kuleta mkataba ukaonekana una *joint venture* mnafahamu kanuni zetu zinavyotaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Heche tuendelee na mjadala, ondoa hayo maneno ya asilimia 80.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie; na ilifaa utafute *Hansard* uone nilichosema. Kampuni ya *Arab contractors,* haina uzoefu wa kujenga mabwawa, nimesema hivyo. Nimerudia kusema na sitatoa neno langu, inatafuta ma-*subcontractors* wa kuingia kujenga bwawa. Ndicho nilichosema.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angellah Kairuki, naomba ukae kwanza tumalize hili la utaratibu. Mheshimiwa Heche.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Anadanganya.

**MHE. JOHN WEGESA HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siondoi neno langu hata moja.

**MBUNGE FULANI:** Iletwe *Hansard*.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, nimetoa maelezo marefu, sikusudii kuyarudia. Kwa mujibu wa Kanuni ya 63 na hiyo Kanuni ya 64 Mheshimiwa Subira Mgalu nitakutaka utuletee mkataba. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Heche, wakati huo naye atatuthibitishia, tukishapata huo uthibitisho kwamba nani anasema uongo? Kwa sababu hiyo, mchango unaohusu *Stiegler's Gorge* na mjenzi aliyepata hiyo kazi kuhusu asilimia anazoweza kufanya kazi na uwezo wake wa kufanya kazi, mjadala huo hautaendelea mpaka hili jambo litakapokwisha. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Heche ataendelea na mchango wake ukiondoa hilo jambo la utendaji kazi wa mjenzi wa *Stiegler's Gorge* na uwezo wake wa kazi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisaidie Taifa kwa mambo mengine. Bomba la gesi ambalo tulikopa na tukajengea, mpaka sasa hivi *utilization* ni *seven percent* peke yake. Mtwara, alikuwa anazungumza hapa Mbunge wa Mtwara, tuna uwezo wa kupata umeme wa *megawatt 300*, Ruhunji tuna uwezo wa kupata Megawatt 350 na Kinyerezi *III megawatt* 350.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hizi pesa *in total* ambazo tungeweza kupeleka na tukapata umeme mwingi kweli kweli na wa haraka, kwa sababu umeme wa *Stiegler's Gorge* ni mpaka 2027. Tunaweza tukapata umeme na wa haraka na wa bei nafuu, tumezichukua tunakwenda kuzi-*dump* sehemu ambazo hatuwezi kuzipata matokeo leo na tunakwenda kuharibu mazingira kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, *LNG*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, naambiwa ni kengele ya pili.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Siyo mimi ninayetunza muda, muda unatunzwa mezani Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Mayenga, atafuatiwa Mheshimiwa Hamida Abdallah na Mheshimiwa Upendo Peneza ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu kwenye taarifa hii ya Kamati. Naomba kwa nafasi ya kipekee, kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika suala zima la kusimamia Sekta ya Madini hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kikao ambacho amekifanya tarehe 22 Januari, kwa uamuzi aliouchukua kuongea na wadau kusikiliza matatizo yao. Vile vile, tumeweza kuona kwamba Mheshimiwa Rais anaumia sana na suala zima la kutaka

wananchi wake tuwe na maisha mema, kiasi ambacho amekuwa akiingilia hata hizi sekta nyingine licha ya kwamba yeye ni Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi ninazisema, lakini vile vile Mheshimiwa Rais wetu ni msikivu sana. Nilisimama hapa kwenye Bunge la mwezi Tisa, nikaomba kwamba Mheshimiwa Rais aweze kusaidia kuhamisha *TIC* kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Rais na baada ya wiki moja alifanya hivyo. Namshukuru sana na ninampongeza sana, kwa sababu kwa uamuzi huo sasa ina maana tutakuwa tunaanza kuzungumza lugha moja kwenye masuala mazima ya uchumi na hasa kwa kutegemea kituo chetu cha uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 31wa taarifa hii ya Kamati, inasema hivi, naomba kunukuu: "Hadi sasa mchango wa Sekta ya Madini ni asilimia 4.8." Taarifa hii inasema kwamba, "Wizara ya Madini pamoja na Tume ya Madini inapaswa kuendelea na usimazi na udhibiti wa utoroshwaji wa madini yote nchini kwa kuimarisha ulinzi kwa maeneo yenye migodi mikubwa na ya kati."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wazo langu na ushauri. Ninaomba Serikali, niseme wazi kwamba siyo Tume ya Madini wala siyo Wizara yenye uwezo wa kudhibiti utoroshwaji wa madini hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema namna hiyo? Kwa sababu biashara ya madini kwanza kabisa inafanana sana na madawa ya kulevywa. Nasema hivyo kwa sababu ni biashara ambayo inahusisha pesa nyingi sana; ni biashara ambayo *crime* yake huwa ni *very organized* kiasi ambacho Tume ya Madini au Wizara peke yake haitakuwa na uwezo wa kufanya *control*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni nini? Naomba Serikali iweze kuunda Mamlaka ya Udhibiti wa utoroshwaji wa madini hapa Tanzania, pamoja na usimamizi wa kodi. Kwa sababu lazima tujiulize, hawa watu kwa nini

wanatorosha madini? Maana kutorosha madini ni suala lingine na kuweza kuwadhibiti ni suala lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye biashara hii ya madini, kuna kodi nyingi sana. Hizi kodi ndizo zinazofanya watu hawa waweze kutorosha. Kuna *VAT, Withholding Tax,* kuna vitu vingi, kuna *Service Levy*, kuna vitu vingi sana kama *inspection fees* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na haya, mtu anaona akipata madini, kuliko aende Serikalini kulipa kodi zote hizo, bora kutorosha. Kwa binadamu yeyote kwenye suala linalohusu pesa, tutalaumiana, tutafukuzana, tutafanyiana kila aina ya vitu, lakini inabidi nasi, hasa Serikali, tuweze kubadilika jinsi ya kuweza ku-*deal* na watu wanaofanya biashara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi, yapo mambo ambayo tunafanya kama maamuzi lakini baadaye yanakuja kututokea puani. Suala la ku-*declare* dhahabu umeitoa wapi? Huu ni uamuzi ambao siyo wa busara. Naomba suala hili Serikali iweze kuangalia upya. Kwa sababu kama tunavyofahamu kule kwetu Shinyanga na maeneo mengine huko Usukumani, mtu amepata dhahabu yake, anakwenda Serikalini ili aweze kukadiriwa kodi. Akifika kule, anaanza kuhojiwa kwanza utueleze ulipoitoa hii dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu utaratibu kwa kweli naomba Serikali iangalie upya, kwa sababu mtu huyu huyu akitoka hapo, akivuka *border* tu pale Sirari akapita Kenya, anaenda kuisajili kama dhahabu ambayo imetoka Kenya. Wenzetu wanamaliza hapa, wanakwenda kuuza nje kama vile dhahabu ambayo imetoka Kenya. Matokeo yake Tanzania kuna madini mengi sana, migodi mingi sana lakini ukiangalia takwimu za uuzaji wa dhahabu nje, zinasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasisitiza sana uundwaji wa hii mamlaka. Ninafahamu kwamba mamlaka hii itafanya kazi kama ilivyo Mamlaka ya Udhibiti wa

Madawa ya Kulevywa ili tuweze kupata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tuweze kuangalia mashine zetu (*scanners)* kwenye maeneo ya *Airport*, Bandarini na na kadhalika, zina uwezo kiasi gani? Watu wanatorosha madini. Hata juzi kuna mshiriki mmoja wa kile kikao cha Mheshimiwa Rais, aliweza kusema jinsi wanavyotorosha madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-*declare interest,* mimi nimekuwa Mjumbe wa *Williamson Diamond for nine years,* kwa hiyo, najua kinachofanyika. Ukichukua dhahabu ukafunga na hizi karatasi za sigara, ukaweka katikati *sponge* ya nusu inchi au ya inchi moja, hakuna mashine ina-*detect.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wamekuwa wakifanya hivi. Vile vile, lazima tuweze kuangalia kwamba kama watu hawa wanaweza kuwa na mbinu kama hizi, ingawa wengine taarifa zinapelekwa wanakamatwa: Je, Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Serikali kununua dhahabu. Naomba Serikali kabla haijafikia uamuzi wa kununua dhahabu, iweze kukaa chini na kupitia mfumo mzima, tangu mtu anavyoanza kuchimba dhahabu mpaka kufikia kwenye mauzo. Nasema hivyo kwa sababu wachimbaji wadogo, tujiulize, pesa wanatoa wapi? Watu hawa siyo mitaji yao, mitaji inatoka Uarabuni, India na kadhalika. Wanapokuja kupata fedha ndiyo wanaingiza kwenye biashara hii. Wakiingiza kwenye biashara hii hawawezi kuuza dhahabu Serikalini hata mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu watu hawa sasa hivi pesa zinaingia, ingawa tuna Sheria ya *Money Laundering,* ndiyo maana nimesema kwamba Serikali lazima ikae ijipange sana. Hata hii Mamlaka ya Kudhibiti Utoroshaji wa Madini naomba sana ihusishe vyombo vya ulinzi na usalama, ihusishe wataalam kwa maana ya Maprofesa na kadhalika, vile vile ihusishe wale ambao ni wachimbaji

*local* kabisa, ili muunganiko wao huu, wale ambao ni wako kabisa, waweze kutoa *experience* wa kile ambacho wanakifanya *on the ground.* Tusikae kutegemea tu kwamba ni wataalam peke yao watakaa chini, wao watakuwa wanafanya *experience* ya makaratasi wakati *on the ground* mambo ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie pia *airports* zetu jinsi zilivyojengwa. Maofisi ya Maafisa katika *airports* zetu. Unaingia kwenye Ofisi ya Afisa wa *Airport,* una uwezo wa kutoka kwenye ndege ukapita kwenye Ofisi ya Afisa bila kupita kwenye *scanner.* Naomba *Airport* ya Mwanza iangaliwe na *airport* nyingine zote ziangaliwe. Hii ndiyo mianya ambayo inasababisha madini yetu yanatoroshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine Mheshimiwa Heche alikuwa analizungumzia hapa kwamba tunafaa kuongoza au hatufai, naomba kumwambia Mheshimiwa Heche, yeye mwenyewe anapumulia mashine, hali yake ni mbaya sana. Akae tu avumilie, milango tulishaifunga. Yeye mwenyewe alishakaa akasema anataka kurudi huku lakini mambo yamekuwa magumu. Asubiri ikifika mwakani, aende nyumbani kwake apumzike. Maana kuna watu wakikaa, kila siku Serikali haifanyi kazi, Serikali haifanyi hivi; Serikali inajitahidi, lakini ninyi wenyewe mkikaa, mna matatizo lukuki! Hayo matatizo yenu ambayo yanasababisha mpaka mnafikia hapo mlipo...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Lucy Mayenga. Mheshimiwa Mwakajoka, muda wa kuchangia umeisha. Mheshimiwa Hamida Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Peneza na Mheshimiwa Ally Keissy ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia taarifa za Wizara hizo mbili, ambazo zipo mezani. Kwanza nianze kwa kuunga mkono taarifa hizo.

Mheshimiwa naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi ambazo anaendelea nazo za kukutana na makundi mbalimbali katika kuendelea kuimarisha ili nchi yetu iendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa nzuri ambazo anazifanya za kuendelea kuimarisha katika kutoa huduma mbalimbali, lakini kwa dhamira njema ya kuhakikisha tunafikia malengo ya kuzalisha *Megawatt* 5000 katika kuhakikisha sasa Tanzania tunakwenda katika uchumi huo wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia ni mpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto kwa kuteuliwa kwake na kuwa Waziri katika Wizara hii ya Madini. Ni Wizara mpya lakini ni Wizara ambayo inakwenda vizuri, tunafanya nayo kazi vizuri. Kwa kipindi kifupi tumeona jitihada kubwa sana wanazozifanya katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie upande wa *REA* ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wameuzungumzia. Upande wa *REA* kwanza naipongeza nchi yetu kwani tumeweza kuwashawishi wawekezaji kuja kufungua viwanda vya uzalishaji wa nyaya, uzalishaji wa *transformer*, LUKU na vifaa mbalimbali pamoja na nguzo za umeme na kufanya kazi ya usambazaji wa umeme kuwa rahisi na kutumia muda mfupi katika utekelezaji wa usambazaji huu wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kwamba Wakala wa Umeme Vijijini kwa kutumia fursa hii wa uwepo wa viwanda ndani ya nchi, wangeweza kufanya kazi kwa

*speed* ambayo tuliitarajia ya kusambaza umeme katika vijiji vingi nchini Tanzania. Tunajua kwamba mradi huu wa *REA* ndiyo mkombozi kwa wanyonge kule vijijini. Tumeona maeneo ambayo tayari umeme huu umefika, namna ambavyo vijana wamefurahia na wanahangaika kujiajiri katika kuendesha shughuli mbalimbali zinazotumia umeme. Kwa hiyo, umeme wa *REA* umekuwa ni mkombozi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa sababu tumetenga fedha kwa ajili ya mradi wa *REA,* lakini ukiangalia kiwango cha mafuta tunachoagiza na kuingizwa nchini na kiasi cha mafuta kinachouzwa: Je, kinalingana na ile fedha ambayo *REA* wanaipokea? Kwa hiyo, tunayo changamoto ya upatikanaji wa fedha ya kusukuma miradi hii ya *REA* kuhakikisha Watanzania umeme unawafikia. Pia tungeongeza Wakandarasi ili kusukuma hizi kazi ziweze kwenda kila kona na kuhakikisha umeme unafika kwa wakati kwa wananchi kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Baraza na Mawaziri na kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo wameweza kuondoa *VAT* katika umeme kule Zanzibar, wamefanya jambo la kiungwana sana. Kwa kweli hoja hii ilikuwa ina manung'uniko mengi sana, hata sisi Wanakamati tulikuwa tunajiona kwamba hatuna amani. Kwa hiyo kwa uamuzi ambao Serikali imeufanya kwa kweli tumefarijika sana, kwa sababu tumeona tunaendelea kuimarisha Muungano wetu ili twende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie upande wa *TANESCO,* kwanza nilipongeze shirika kwamba linakwenda, totauti na pale zamani. Shirika hili sasa limeanza kulipa madeni kwa *TPDC,* kwa hiyo ni hatua nzuri sana kwa sababu sasa wanaweza kwenda. Shirika linaonesha sasa linajiimarisha. Rai yangu kwa Serikali, zile ofisi za Serikali ambazo zina madeni makubwa ziungane kwa pamoja kuhakikisha tunawaunga mkono *TANESCO* kwa kuwalipa madeni yao, ili sasa waweze kujiimarisha katika kuhakikisha wanatoa huduma iliyokuwa bora kwa wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia kwa hatua mbalimbali ambazo wamezifikia, leo Watanzania tunanunua umeme kupitia simu zetu, wametupunguzia mzigo mkubwa tofauti na zamani, imeleta tija sana lakini pia imepunguza madeni, imeweza kufunga umeme wa LUKU, haya ni maeneo makubwa kwa Shirika hili la *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo kubwa ambazo wanazifanya kulikuwa na wizi wa umeme lakini wamejitahidi katika kudhibiti wizi ule wa umeme ambao ulikuwa unatokea. Kwa hiyo wote kwa pamoja tuungane katika kuhakikisha tunaendelea kulilinda shirika hili kwa kuwasaidia panapotokea tunaona katika maeneo umeme unabiwa, basi tuweze kutoa taarifa ili mara moja watu hao washughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nipongeze juhudi kubwa zinazofanya na Serikali kupitia Wizara hii, tumeweza Serikali kupanua bandari pale Dar es Salaam kupunguza msongamano lakini Bandari ya Tanga na kule Mtwara ili kuweza kusogeza huduma kwa wananchi, ni maendeleo makubwa sana, kwa sababu kama wananchi wa Mikoa ya Kusini wanapata mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kule Mtwara, kwa kweli ni faraja kubwa sana na ni maendeleo kwetu kwa sababu yanaweza kuongeza ajira katika sekta mbalimbali. Kwa hiyo nipongeze juhudi ambazo zinafanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie upande wa *LNG;* tunajua yanayoendelea Serikalini ya kukamilisha mazungumzo mpaka hapo mwaka 2023/2024. Naiomba sana Serikali katika eneo lile ambao inakwenda kutekeleza mradi *LNG* wapo wananchi ambao wanaishi pale na kwa kipindi kirefu sasa karibu miaka mitano walishaambiwa kwamba wasiweze kujiendeleza pale, kwa maana tumewambia maendeleo yao yakae likizo kwa muda fulani , naiomba sana Serikali yangu kwa kipindi karibu cha miaka mitatu mfululizo fedha inatengwa kwa ajili ya kuwapa fidia hao wananchi lakini fedha hiyo haitoki. Sasa ningependa wakati Waziri ana *wind up* aniambie ni kwa nini fedha hii

haitoki kwenda kupewa fidia wananchi wale wa Kata ya Mbanja, Kijiji cha likong'o.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie upande huu wa madini, nimshukuru sana Waziri wa Madini na Naibu wake, kwa kweli walitoa ushirikiano katika kuhakikisha tozo mbalimbali kwa wazalishaji wa chumvi hasa wale wa Lindi ambao walikuja hapa Dodoma tukakaa nao pamoja na kuona baadhi ya tozo ziondolewe ili kuwafanya wazalishaji wa chumvi waweze kuingia katika ushindani wa masoko, lakini tuweze kuwa na viwanda vya chumvi nchini Tanzania. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Dotto pamoja na Naibu wake, lakini hata wakati ule dada yangu Mheshimiwa Angella Kairuki alifanya kazi kubwa ya kutusaidia na hatimaye wananchi wale wanaendelea vizuri katika uzalishaji wa chumvi, lakini kuna Halmashauri ambayo

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamida kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Upendo Peneza dakika , atafuatiwa Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ukiangalia katika ripoti ya Kamati, Kamati katika vitu ambavyo vimependekezwa, katika ripoti yake ukurasa wa 22 kwamba maeneo ambayo wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakipata shida na wao kutorosha madini kupeleka nje ya nchi. Kamati imetaja matatizo ni kodi ambazo ziliwekwa na kodi hizi ni kodi ya ya ongezeko la thamani (*VAT* 18%), kodi ya zuio *(ithholding tax* 5%), tozo ya ushuru *(service levy* 0.3%), tozo ya ukaguzi kwa maana ya *(inspection free* ya 1%) na mrabaha wa madini katika maeneo mbalimbali ambao wachimbaji hao wadogo wanatozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais Magufuli alifanya kikao na wachimbaji wadogo na kukubaliana kwamba Serikali itafanya utaratibu wa kuondoa kodi hizi zinazowakabili wachimbaji wadogo, lakini ndani ya Bunge hili kuanzia mwaka 2017, tulipokuwa tukijadili *Finance Bill* ndani ya Bunge hili tatizo la *withholding tax* lilijadiliwa ndani ya Bunge hili na Mheshimiwa Mbunge wa Kahama pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Nzega ambao na wenyewe ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na kuonyesha kwamba hili ni tatizo na Serikali isikubali kupitisha kodi hizi ambazo zinaenda kuwakaba hawa wachimbaji wadogo wadogo. Hata hivyo, hatukuweza kusikiliza, leo miaka miwili baada ya kupitisha hiyo *Finance Bill,* tunarudi tunakaa na wachimbaji wadogo ili kuweza kuzifuata kodi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba nchi hii sasa tumekuwa na matatizo mengi, kwa sababu hatusikilizi ushauri au hatuongei na wadau kabla ya kufanya maamuzi. Tulipokuwa tunaanza Bunge hili tulipata shida kwa Serikali kuweka kodi katika huduma za bandari. Serikali imepoteza fedha nyingi sana kwa watu kuhama kusafirisha mizigo kupitia bandari yetu, Bunge hili hili lilipitisha vilevile kwa Serikali kung'ang'ania wakati Wabunge wanashauri, Bunge likapitisha tena kwa maana ya watalii kutozwa *VAT* katika huduma ambazo wanazozitoa. Kila mwaka, mwaka unapita, ndipo tunapokuja kufanya mabadiliko, huku watu na kodi zimeshapotea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Upendo Peneza, kuna taarifa. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE.JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji, mdogo wangu Mheshimiwa Upendo Peneza kwamba, atakubalina nami kwamba Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwamba ni Rais msikivu na anasikiliza sana ushauri unaotolewa na

Wabunge na kwamba sasa tozo mbalimbali zilizokuwa zinatozwa kwenye madini ikiwa pamoja na *withholding tax* tayari ameshaanza kuzifanyia kazi wakati huu alipokuwa amewaita wale wafanyabiashara wa madini na wachimbaji wadogo wadogo, amekaa nao na kuzungumza nao ili kupata muafaka wa jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Upendo Peneza, uanipokea taarifa hiyo?

**MHE. UPENDO PENDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bandari mwaka mmoja baadaye tukafanya marekebisho, suala la Utalii mwaka mmoja baadaye tukafanya marekebisho, mapato tumeshapoteza na leo kwenye suala la wachimbaji wadogo miaka miwili baadaye. Watu wa Geita ni kati ya watu ambao wamewekwa ndani kwa sababu utoroshaji wa madini. Ni kwa sababu wakipiga mahesabu, wakifanya shughuli zao za uchimbaji mpaka wakauze, faida hawaioni. Kwa hiyo, naongea kwa sababu sehemu ya wananchi waliopo Geita ndio waliokamatwa kutokana na kadhia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nchi inabidi ifanye ni suala la kuzingatia ushauri kwa muda, ni suala la muda, kwa sababu katika utawala hakuna kujaribu, ndio maana nadhani hata Urais mwenye sifa anayegombea miaka 40, la sivyo wangeruhusu vijana wenye miaka 18 au 25, hata Tume ya Jaji Warioba walikataa kwa sababu tunategemea watu wanaotuongoza ni watu wenye *experience,* ni watu ambao wapo tayari kusikiliza ushauri wa watu, watu walioko tayari kuangalia *impact* kabla ya kufanya maamuzi ambayo tunaendelea kuyafanya ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Geita watu wengine wanaopata leseni ni watu wanaopata leseni za uchenjuaji ambayo kwa Kiingereza wanasema *processing* and *smelting,* ni watu ambao wanachukua mchanga ambao umeshafanyiwa kazi na mtu mwingine, anauchukua anauozesha kwenye sumu aina *cyanide* na *mercury* kwa ajili

ya kupata dhahabu tena. Watu hawa wanaofanya shughuli za uchenjuaji wana tozo nyingi sana zinazowakabili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pendo Peneza kengele imeshagonga. Mheshimiwa Ally Keissy atafautiwa na Mheshimiwa Mwakajoka na Mheshimiwa Abdallah Mtolea ajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie hizi Kamati zote mbili na naziunga mkono. Kwanza kabisa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli kwa uwezo na ujasiri wa kufanya bwawa la Rufiji kwa ajili ya umeme. Ni ajabu kabisa Wabunge wote wakikaa wanadai umeme kwenye vijiji vyao, wadai maji kwenye vijiji vyao, maji huwezi kupata bila umeme, hakuna chochote kinachofanyika kwenye kijiji chako bila umeme, wanadai *REA* awamu ya tatu kwamba wanataka vijijini umeme, vitongojini umeme, sasa bila ujasiri wa Rais Magufuli kupata umeme, nyie mtapata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Ethiopia wanachanga pesa wanakata mishahara kwa ajili ya kujenga bwawa kubwa wapate umeme. Nyie Wabunge tukisema tuanze kuchanga pesa mtaanza kuruka ruka. Nchi nzima Ethiopia na umaskini wao wanachanga pesa kujenga bwawa kubwa la umeme, je, tukiamua watu hapa tuanze kuchangia bwawa la Rufiji kule mtakubali nyie?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anakubali kutoa fedha kujenga bwawa la umeme tupate umeme nchi nzima mpaka vijiji vyenu, leo mnakaa mnapiga kelele, mazingira, Marekani ndio baba wa Taifa kwa viwanda, anakataka kutia mkataba kwa ajili ya mazingira, mbona hamumchukulii hatua? Mnapiga kelele, Mheshimiwa Zitto, Kigoma hakuna *grid* ya Taifa kama kwangu Nkasi, tuache kelele tupate *grid* ya Taifa katika vijiji vyote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa unaitia hasara *TANESCO* umeme hautoshi mnatumia majenereta na mnachafua mazingia moshi kule kwenu. Ndugu zangu lazima tumtie nguvu Rais ajenge bwawa, kelele za hawa jamaa...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mwenzangu, miradi hiyo mikubwa tulipokuwa nao kule tulishaiuza kwa wale wajamaa ili waingie wao ili wapate pesa, sasa kwa sababu Magufuli anaingia kwenye mradi ambao waliuuza nje, ndio maana sasa wanalalamika kwa sababu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kessy, unapokea taarafa hiyo?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo mimi nawafahamu. Ukiona mti wako hauzai, ujue ni hatari kata panda mwingine, sasa ndugu zangu hawa wanapungua siku hadi siku, Madiwani wamepungua, Wabunge wanapungua mpaka ifike 2020 hali ni ngumu, tumuache Rais afanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia habari ya mkataba wa *SONGAS* na Serikali yetu. Hapo fungueni masikio vizuri sana, hapo tuelewane huu mkataba, ujasiri wa Rais auvunje, hatuweeze kwenda nao mpaka 2024, tutakufa. Huu mkataba ni adui mkubwa wa nchi hii, ni wizi wa hali ya juu na namwomba Rais walioshiriki wote Mkataba huu wakamatwe mara moja kuanzia sasa.

Mkataba huu Serikali yetu ilichangia 73% dola bilioni 285 milioni, hawa jamaa wa *SONGAS* walichangia dola 106.3 milioni, sawa na 27%, bado haikutosha, hizi pesa sio zao, Serikali yetu ilikwenda *World Bank* kukopa na kuwapa. Badala ya wao watulipe sisi, lakini sisi ndio tunawalipa wao, jamani ndugu zangu ni hatari kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu kiningine kibaya katika *Shareholder* wakati sisi tuna 73% wenyewe 27% sisi tukapata 46% wenyewe 54%, ndugu zangu! Kingine cha ajabu, tukaingia mkataba nao kwa ajili ya kuweka *capacity charge* dola milioni tano kwa mwezi, sawa na shilingi kwa sasa 11, 475, 000,000 wakati sisi tuna 73% tunapunjwa kila mwezi *capacity* charge tunapunjwa 8,668,750,000.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy kuna taarifa, Mheshimiwa Ally Keissy.

*(Hapa Mheshimiwa Ally K. Mohamed aliendelea kuzungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy *microphone* yako ilikuwa imezima kwa hiyo yatakuwa hayajaingia hayo uliyosoma baada ya kipaza sauti kuzimwa. Mheshimiwa Kubenea taarifa na Mheshimiwa Ally Keissy itabidili hayo uliyokuwa unasema urudie ili yaingie kwenye *Hansard*.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa tu Mheshimiwa Keissy kwamba mkataba huu wa *Songas* ulifungwa katika Serikali ya Awamu ya Tatu, chini ya Chama cha Mapinduzi na Serikali iliyoko madarakani sasa hivi ni ya Chama cha Mapinduzi na mikataba yote hii sisi hatuhuisiki nayo, wanayohusika nayo ni wao wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona Mheshimiwa Kubenea hanielewi, mikataba mibovu

tunazungumzia yote na wewe mwenyewe labda ulikuwa chama mtumishi wa Vyama vya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia haikuingia kwenye *Hansard,* nyamazeni

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma muache Mheshimiwa Keissy achangie kidogo ndio unaweza ukasimama kwenye taarifa, la sivyo utakuwa unampa Mheshimiwa Kubenea. Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongee taratibu, nazungumzia mkataba wa *SONGAS* na Serikali. Huu mkataba ni ufisadi wa hali ya juu, namuomba Rais anisikilize na waliopo wakamwambie mkataba huu haufai kuanzia leo waufute. Huu mkataba Serikali ilichangia dola 285.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy kuna taarifa nyingine huko.

**MHE.JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi ni Mjumbe wa Kamati na Mheshimiwa Keissy ni Mjumbe mwenzangu, taarifa hizi anazozizungumza tulikutana nao tarehe 25 Januari na kama Kamati tuliona kulikuwa na upungufu na namshukuru Mheshimiwa Kubenea amesema huu mkataba ulifungwa Awamu ya Tatu na kipindi hicho Waziri Mkuu alikuwa mzee *zero,* kwa hiyo tulikubaliana kabisa, *Mr zero* Mheshimiwa Sumaye ambaye wamechukua na wao wako naye huko.

Kwa hiyo, tulikubaliana kama Kamati kwamba mikataba hii iende kawa *AG* ipitiwe upya ili tuweze kuangalia jinsi ya kwenda nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa hiyo waliotufikisha kwenye matatizo ni Sumaye ambaye ndio baba yake na Mheshimiwa Kubenea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Musukuma moja kwa moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy naomba ukae kidogo, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 64 kutokutumia lugha ya kuudhi; mzungumzaji aliyekuwa anampa taarifa Mheshimiwa Keissy amezungumza kuwa nchi hii imewahi kuwa na Waziri Mkuu anayeitwa *zero.* Kwa kumbukumbu zangu nchi hii haijawahi kuwa na Waziri Mkuu anayeitwa *zero* na tumefunzwa kuheshimu viongozi wetu, naomba ndugu yangu Mheshimiwa...

*(Hapa baadi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kama ni lugha ya Kibunge kusema kwamba nchi hii imewahi kuwa na Waziri Mkuu *zero*. Naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, naomba ufute hilo neno *zero*.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Subhana Allah,* Mungu tusaidie, waliyemwita *zero* si ni ninyi kina Zitto. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, naomba ufute neno *zero* tuweze kuendelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuta lakini dhambi zinawarudia waliolitunga hilo jina. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy endelea na mchango wako.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea. Hawa Songas *capacity charge* wakati sisi *TPDC* tumechangia asilimia 73 wanachukua 100% *capacity charge* wakati sisi tungepata asilimia 73 *capacity charge* na wenyewe wangepata asilimia 27. Wakati huo huo mitambo ikiharibika gharama ya kutengeneza mitambo yote ni juu ya *TANESCO*. Mpaka sasa *TANESCO* wameshagharamia matengenezo ya mitambo shilingi bilioni 3.22 pamoja na *VAT* shilingi bilioni 90 wakati wale Songas wamekaa starehe huko kwao wanakula tu zile *capacity charge*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi hao Songas na *PanAfrica*; *PanAfrica* wenyewe wamekaa katikati hata kodi hawalipi. Tangu Awamu ya Nne tumesema sisi hapa Bungeni kuhusu *PanAfrica* kulipa kodi, kodi walikuwa hawalipi, wanachukua *net* pesa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichunguza mikataba *TANESCO* haiwezi kupata chochote na itaendelea kufifia. *Songas* amechukua baadhi ya Watanzania ambao walikuwa madarakani *TPDC* na kuingia mikataba hii mibovu, ndiyo Wakurugenzi wake. Baadhi ya viongozi wa Serikali waliokuwa Wakuu wa Mikoa ndiyo washauri wake. Juzi walikuja kwenye Kamati niliwahoji ninyi kweli ni wazalendo? Mzungu alibadilika rangi. Nikawauliza ninyi ni wazalendo kuangamiza nchi namna hii? Mpaka tarehe ya leo wametudhulumu shilingi trilioni 1.3 73 ya asilimia zetu 73.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu zangu tunakalia kudai watu nyanya sokoni kule ushuru na mambo madogo madogo wakati hela zinakwenda kuliwa na Wazungu. Nilimwambia yule Mzungu kama Tanzania kwa wajanja mnaifanyia hivi, je, DRC Congo kule? Belgium imekaa inanyonya DRC Congo inakuwa tajiri mpaka watupe masharti ya ajabu ajabu tuoane ndiyo watupatie pesa wakati hawana chochote si lolote, wananyonya nchi za Kiafrika mchana kweupe tena ni Mabeberu wana ndevu ndefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu mambo ya nje, tuelekeze nguvu zetu DRC Congo, tuweke jicho letu DRC Congo. Congo ni nchi ambayo imekaa kitajiri kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Tuienzi DRC Congo tupeleke macho yetu DRC Congo. Tunakaa chini ya ua la waridi, Congo itatusaidia sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *tunapitwa na nchi kama Rwanda inayoegamia Congo leo inasifika dunia nzima kwa kupora Congo.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, jicho letu tupeleke Congo. Nashangaa wanasema wameshindwa kupeleka mahindi kule kupitia Zambia wakati Lake Tanganyika kuna barabara ya kutosha kwenda DRC Congo kupitia Ziwa Tanganyika. Ndugu zangu tubadilike, tuwe na wachumi na wafanyabiashara katika Serikali yetu.

**MBUNGE FULANI:** Kabisa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Tuondokane na mambo ya ajabu ajabu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa kitu kimoja, Rais Magufuli aliwaita Wachungaji, Mashekhe na Maaskofu badala ya kuzungumza mambo ya maana

akatokea jamaa mmoja akamwambia wewe mzee wakikushauri kuongeza muda usikubali, alitumwa na nani? Ukienda kila sehemu wanataka Rais Magufuli bila Rais Magufuli ndugu zangu nchi ilikuwa imeoza, tukubaliane kabisa nchi ilikuwa imeoza. Wabunge wanasafiri kama wakimbizi kwenda nchi za nje na *impact* hakuna leo, Rais kawabana wanabaki wanatapatapa wanahangaika. Hilo wazo alimtuma nani kwenda kumwambia Rais kwamba asiongeze muda, mlimtuma nyie. Wenyewe Wachungaji, Maaskofu na Mashekhe wana muda wa kuongoza, Shekhe ni mpaka achanganyikiwe akili au afe.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, kuna taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Haya, nipe taarifa nikujibu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa Mheshimiwa Keissy kwamba ni kweli kabisa Taifa hili lilikuwa limeoza chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka yote tangu tumepata Uhuru na bado limeendelea kuoza kwa takwimu anazozitoa za Taifa hili kuendelea kuumizwa na mabeberu. Taarifa yangu ni hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesema lilikuwa limeoza siyo sasa limeoza, hiyo taarifa sipokei, napokea nusu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia habari ya *TANESCO*, mpaka leo *TANESCO* inadaiwa zaidi ya bilioni 600 na hao jamaa wa Songas. Songas wanawauzia umeme

*TANESCO* senti sita, *TANESCO* wanauza senti 11, tukamuuliza anasema eti mimi nauza bei ya chini sana, wewe unauza huna gharama kama *TANESCO*. *TANESCO* wanagharamia kusambaza umeme nchi nzima wewe Songas una gharama gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa tunawaogopa vipi hawa *Songas*, tunawaogopa nini hawa *PanAfrica*? Lazima tuongoze kijasiri ili kujikomboa, tunaibiwaje shilingi trilioni 1.3 halafu tunaenda kuwaomba tena hela Wazungu? *Hicho ni kitu cha ajabu mpaka Rais wa Marekani na mke wake wakaenda kutembea pale Ubungo, hamkusikia au mlisikia?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**WABUNGE FULANI:** Tulisikia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** *Ni kwa sababu ya maslahi yake*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujasiri Rais Magufuli namwomba anisikilize aingilie upya mikataba hii ya Songas, asilale usingizi, awatafute wote waliotia saini kwanza awalundike magereza mara moja. Kama walipata mali kwa njia ya rushwa kuingia mikataba ya namna hii, mali zao zitaifishwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita nilizungumza mara nyingi watu kama hawa ndugu zangu wanaoingia mikataba mibovu dawa yao ni kuwanyonga. Leo ukiwanyonga watu 200 Muhimbili wanazaliwa 500 kuna hasara gani? *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy muda wako umekwisha, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Frank Mwakajoka atafuatiwa na Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ajiandae.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, mwongozo unaombwa kama hakuna aliyesimama, Mheshimiwa Mwakajoka ameshasimama. Mheshimiwa Mwakajoka endelea.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia taarifa hizi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita sana kwenye Kamati ya Nishati na Madini lakini nataka nizungumzie sana kuhusiana na sekta ya madini. Kila mmoja wetu anajua kabisa kwamba sekta ya madini ni eneo muhimu sana na rasilimali kubwa sana katika Taifa hili. Tulitegemea kabisa katika Serikali hii Awamu ya Tano tulitegemea labda ingeweza kuchangia fedha nyingi sana katika pato la Taifa. Ukweli tu ni kwamba mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa bado uko chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukijaribu kuangalia katika kipindi cha mwaka 2017/2018 tumeona sekta ya madini imechangia asilimia 4.8 lakini mwaka 2015 sekta ya madini ilichangia karibuni asilimia 5.8. Kwa hiyo, inaonyesha ni jinsi gani ambavyo sekta ya madini sasa hivi inazidi kushuka na haiwezi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu nyingi za msingi zinazosababisha sekta ya madini iendelee kushuka. Tusitegemee miujiza kama sekta ya madini inaweza ikafikisha asilimia 10 kama ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017/2018, Serikali iliweza kutenga fedha za maendeleo na tukazipitisha ndani ya Bunge hili shilingi bilioni 20 lakini zilizokwenda kufanya kazi kwenye miradi walipeleka Sh.1,183,000,000, tusitegemee miujiza hapo. Mwaka 2018/2019 fedha za maendeleo zilitengwa Sh.19,621,000,000 na fedha ambazo zimekwenda sasa hivi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa muda wa miezi sita ni Sh.100,000,000 peke yake, hapa tunategemea nini? Kama tuna dhamira ya kweli ya kuinua sekta ya madini katika Taifa hili miezi sita sekta ya madini imeweza kupata Sh.100,000,000 kati ya Sh.19,621,000,000, hapa tunategemea kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusitegemee miujiza katika kuinua sekta ya madini na tusitegemee kabisa kama sekta hii ina uwezo wa kuchangia asilimia 10 ambayo mnazidi kuzungumza ndani ya Bunge hili. Hili jambo haliwezekani kwa sababu mnatenga fedha, tunafanya maigizo ndani ya Bunge halafu hampeleki fedha kwenda kutekeleza miradi hii. Kwa hiyo, tunategemea kwamba tutaendelea kushuka mwaka hadi mwaka kwa sababu hatuoni ni namna gani Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba sekta ya madini inakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo lingine, kuna taasisi inaitwa *TEITI* ambayo inasimamia uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini. Mwaka 2017/2018 taasisi hii iliweza kufanya ukaguzi wa taasisi mbalimbali kwenye sekta ya madini na baadaye ikatoa majibu. Kati ya taasisi 1,230 walikwenda kukagua taasisi 55 ambazo walikuta kuna upotevu wa fedha karibuni shilingi bilioni 30. Taasisi hii ilishindwa kukagua taasisi zote kwa sababu ilikosa fedha za kutendea kazi katika kipindi chote hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hivi, kama hawawezi kutoa fedha kwenye maeneo muhimu kama eneo hili la *TEITI* tafsiri yake ni kwamba kuna ufisadi na kitu kinafichwa ndani yake ili tusiweze kutambua. Tunahitaji mashirika haya yote yaweze kukaguliwa katika kipindi kinachohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine, uko mradi wa *Tanzanite One* pale Mererani. Ule mradi tulipata taarifa kwamba tayari Serikali inataka kubadilisha mkataba, iko kwenye mazungumzo na kampuni ambayo ni wabia na Serikali. Kilichotokea huwezi kuamini sasa ni mwaka wa tatu bado mazungumzo yanaendelea na pia Wizara ya Madini haina taarifa mazungumzo yale yamefikia wapi. Tunasikia tu kwamba Mheshimiwa Kabudi bado anafanya mazungumzo wakati miaka mitatu tunapoteza fedha na kodi. Ni mazungumzo gani ya miaka mitatu hayo? *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, kuna taarifa, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji anayechangia ni mjumbe mwenzangu wa Kamati. Kuna neno analitumia najaribu kufikiria siijui hiyo taasisi inaitwa TEITI, pengine labda atuambie kirefu chake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa siyo maswali. Mheshimiwa Frank Mwakajoka, endelea.

**MHE. FRANK MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema siwezi kumjibu muhuni huyo namuacha tu.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, usimuite Mbunge mwenzio muhuni, futa hilo neno halafu uendelee kuchangia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalifuta neno hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwamba Serikali itafanya majadiliano kwa haraka ili

kuhakikisha kwamba Mradi huu wa Tanzanite unainufaisha nchi lakini pia wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi katika mradi huu waweze kupata haki zao. Cha kushangaza ni kwamba mradi huu mpaka sasa umesimama sasa ni miaka mitatu, tunasikia tu Kabudi, Kabudi, Kabudi yuko kwenye mikataba, hivi Kabudi ndiyo Serikali? Tunataka kujua mikataba hii itatoa majibu lini na wananchi waweze ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, ni Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Profesa Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanavyosikiliza tunavyozungumza Profesa Kabudi wanashangaa sana kwa sababu walikuwa na matarajio makubwa kwamba akipewa nafasi hii angeweza kuisaidia nchi sasa tunaona hali ni mbaya zaidi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank, kuna taarifa nyingine, Mheshimiwa Kakunda.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa ndugu yangu Mbunge anayechangia, ni kwamba yeye na sisi wote tulishawahi kupitisha Sheria ya Majadiliano ya Mikataba mwaka 2017 mwezi Julai. Kwa hiyo, anaposema miaka mitatu iliyopita si kweli. Naomba aendelee baada ya kupokea taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, akumbuke kwamba kwanza sisi huku tulikataa. Huku si tulisema hapanaaa, ndicho tulichokisema, huko wakasema ndiyo. Pamoja na hayo, Waziri wa Madini hajui majadiliano

yanaendaje anayejua ni Kabudi, hivi kweli kuna usalama namna hii? Sisi kwenye Kamati yetu tunakutana na Mheshimiwa Waziri na tukisoma taarifa yake hapa inaeleza kabisa tumemuuliza kwenye kikao anasema hajui wanaendelea na mazungumzo, sasa sisi tunakuwa na wasiwasi. Kama kweli Serikali hii na viongozi ambao mmepewa madaraka mtakuwa hamna uchungu na maisha ya Watanzania na uchumi wa Taifa hili miaka mitatu mazungumzo yanafanyika ya kampuni moja tu na huyo mtu ni mbia, Profesa Kabudi inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunachotaka kusema ni kwamba lazima mjadala huu uishe mapema na Serikali ianze kupata fedha. Pia tunataka tujue wafanyakazi wa *Tanzanite One* ambao ni zaidi ya 400 hali zao zikoje na Serikali imejipanga namna gani namna ya kuwalipa wananchi wale kwa sababu wanadai madai yao kwenye mgodi ule. Sasa hivi hawana kazi, familia zinakufa, watoto wanakufa, wameshindwa kupeleka watoto shuleni mnasema mko kwenye majadiliano. Yaani mnajadili fedha kwa taratibu namna hiyo, uchumi mnaweza mkajadili kwa utaratibu namna hiyo? Kama ni hivyo Mheshimiwa Profesa Kabudi atakuwa ameshindwa na amefeli kwenye mjadala huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine la mapunjo ya wafanyakazi kwenye Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira ambao jumla yao ni 800 ni miaka mingi imepita hawajalipwa. Mwaka 2015, Serikali imefanya majadiliano na kuhakiki madeni imekuta wanadai karibuni Sh.1,800,000,000, wafanyakazi wale wamefanya kazi miaka mingi lakini Serikali mpaka leo haijawalipa na hakuna mpango wowote wa kuwalipa kwa sababu hata bajeti ya mwaka jana hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi hawa. Tunaomba Waziri anavyokuja hapa aeleze ni lini wafanyakazi wa Mgodi wa Kiwira watalipwa fedha zao ili waweze kufuta jasho kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine la makinikia. Watanzania bado wanajiuliza sana makontena 277 ambayo yalikuwa yamekamatwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na wakasema yale makinikia yatakwenda kuuzwa na wakiyauza inawezekana kila mmoja Tanzania akapata *Noah*. Watanzania wamesubiri *Noah* hawajaziona. Mpaka sasa hivi Watanzania wamesubiri *Noah* hazionekani. Juzi watu wameanza kupunguza wanasema kama Serikali imeshindwa kuwapa *Noah* basi hata Balimi tatu tatu wataridhika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya majadiliano yote ni Mheshimiwa Profesa Kabudi anaendesha majadiliano ya namna hii. Kwa hiyo, tunaona ni jinsi gani ambavyo Mheshimiwa Profesa Kabudi alivyoshindwa kabisa kuweka vizuri mambo haya na zile kontena sijui kama bado ziko bandarini au zimeshatambaa na maji, hatujui. Tunaomba kujua pia Waziri akifika hapa atueleze haya makontena yako wapi na ni lini tutapata *Noah* moja moja au Balimi tatu, ijulikane hiyo. Kwa hiyo, hakuna namna ni lazima tujue ni mali ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna fedha walisema wale Mabeberu wanaleta mpaka leo hizo fedha kishika uchumba hakionekani. Jamani hii nchi kweli kila siku tutakuwa tunadanganywa? Ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma siku moja alichachamaa kwenye kikao baada ya kuona haoni *Noah* wala Balimi hazionekani lakini akawa hana namna yoyote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunaendelea na mjadala niwakumbushe tu moja, hoja zinazojadiliwa hapa ni hoja za Kamati.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo kama ni maswali maana yake yatajibiwa na Mwenyekiti wa Kamati, lakini pia unapopewa taarifa kikanuni unatakiwa kuikubali au kuikataa. Ukiiacha tu hivi Taarifa Rasmi za Bunge zinahesabu wewe umeikubali, kwa sababu hakuna mahali ulipoikataa. Kwa hiyo, lazima muweze kujibu unapoulizwa kama taarifa unaikubali ama kuikataa. Mheshimiwa Mlinga.

**MWONGOZO**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako kuhusiana na jambo lililotokea Bungeni mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tamaduni zetu za kidunia, majina maarufu yanakubalika, wazungu wanaita *(a.k.a),* yanakubalika na ndio maana Mheshimiwa Mwinyi alikuwa anaitwa Mzee wa Ruksa na lilikubalika. Mheshimiwa Rais wetu Magufuli anaitwa Tingatinga, limekubalika. Mheshimiwa Sugu ni Mheshimiwa Mbilinyi, linakubalika. Mheshimiwa Dkt. Mollel wa upande wetu anaitwa Dkt. Shika, limekubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwege limekubalika. Sasa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu Mstaafu zero kwa nini lisikubalike? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Mlinga.

**MBUNGE FULANI:** Wanaokubali waseme ndio!

**NAIBU SPIKA:** Lakini hilo neno lilishafutwa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa hiyo sina haja ya kulitolea mwongozo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo, Mheshimiwa Amina Mollel

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru ahsante. Pamoja na mchango mzuri uliotolewa na Mheshimiwa Ally Keissy, lakini kuna baadhi ya maneno ambayo alitumia kwa mfano aliposema Rwanda wananufaika na dhahabu ya Congo DRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ajili ya mahusiano mazuri ya kidiplomasia ningeomba tu mwongozo kwamba, je, ni sahihi au kama sio sahihi basi ingekuwa ni vyema yaondoke katika *Hansard* ili mahusiano mazuri tuliyonayo na jirani zetu yaendelee kuwepo. Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Achana naye.

**MBUNGE FULANI:** Aaah hujapewe nafasi.

**MHE. ALLY K. MOHAMED**: Mheshimiwa Naibu Spika, namjibu, mimi nakaa jirani...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Amina Mollel kuhusu mchango aliochangia Mheshimiwa Keissy. Wakati mwingine kunakuwa na kelele nyingi sana hapa ndani, lakini inavyoonekana alisema maneno yanayoashiria kwamba nchi zetu jirani mahusiano yake yako namna fulani na kuibiana rasilimali zao. Kama hizo taarifa ndivyo zilivyo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, tunatakiwa humu ndani ukitumia mfano wa nchi nyingine unatumia kwenye habari chanya. Kwenye habari zilizo hasi huwezi kutumia humu ndani kwa sababu hizo ambazo sote tunazifahamu na tulishaelezana huko nyuma. Sasa hivi muda wetu hautoshi kuanza kuzieleza hizo zote. Kwa sababu hiyo naagiza watu wa Taarifa Rasmi za Bunge,

katika eneo hilo kwenye mchango wa Mheshimiwa Keissy uondolewe.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani labda kama ni kwenye hoja hii kama ni hoja nyingine miongozo ije baadaye tuendelee na mjadala.

**MHE. ALLY K. MOHAMED**: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo. Mimi nina ushahidi kila kitu asiniletee, mimi nina ushahidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy mbona unafanya vurugu! Mheshimiwa Ally Salum, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Abdallah Mtolea nadhani. Mheshimiwa Abdallah Mtolea atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Salum.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kusema machache katika taarifa hizi za Kamati mbili zilizowasilishwa hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimejifunza jambo leo na hili ni kuonesha ni kwa kiasi gani sasa kazi nzuri zinazofanywa na Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, zinakubalika pande zote, kwamba hata wale ambao hapo awali walikuwa wakibeza yale makubwa anayoyafanya sasa unaona wameanza kuyakubali kwa njia nyingine tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijakuja hapa nilipitia *Hansard* za Bunge kuona maoni ya Wabunge wakati wa mjadala wa *IPTL* ulipokuwa ukijadiliwa hapa Bunge. Yalikuwa ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba tuachane na miradi midogo midogo ya kutengeneza umeme nchini tuje na miradi mikubwa, hata kama nchi itasimama kufanya

shughuli nyingine kwa miaka mitano, lakini ikitatua tatizo la umeme, huo utakuwa uamuzi wa basara sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yes! Yes!

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikarudi nikaangalia *Hansard* za Bunge la Bajeti mwaka jana. Waliotoa maoni hayo wakati Serikali imeanza kuzungumzia suala la *Stiegler's gorge,* wakaanza kusema kwamba mradi huo si sahihi kwa sababu unaharibu mazingira. Leo tumekuja hapa tena tunasikia hoja zinazidi kubadilika ninachomaanisha kwamba mradi huo sasa sio sahihi mkandarasi aliyepewa hana uwezo wa kujenga. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inakuja hoja nyingine mpya kwamba mradi huo Watanzania wasiutegemee kesho au kesho kutwa nani alisema mradi mkubwa kama huu unaweza ukajengwa ndani ya mwaka mmoja? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mmmh!

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaweza kuona ni kwa namna gani Watanzania wanaanza kukubali na kuzielewa kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Sasa hili ni jambo zuri kwa sababu umeme ambao unakuja kujengwa kwenye nchi hii, unakwenda kuondoa matatizo mengi ambayo yamekuwa yakiisumbua nchi kwa muda mrefu. Wakati mradi huu ukiendelea miradi mingine ya kuimarisha umeme inaendelea kufanywa ili Tanzania isiwe gizani wakati wa kusubiri mradi huu. Watanzania wanaelewa kwamba tunakoelekea sasa tunakwenda kulitatua tatizo hili moja kwa moja. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa maamuzi haya magumu wanayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa suala hapa pia la *LNG* na kuna msemaji mmoja alitoa taarifa kwamba wananchi wasahau kuhusu *LNG* kwa sababu baada ya sheria mpya za kutunza rasilimali za nchi hii

zilizotungwa mwaka 2017, hakutokuwa na mtu atakayetamani kuja kufanya miradi ya *LNG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri haya masuala ya gesi ni masuala *sensitive* sana si kila mmoja anaweza kuyasema yana *technicalities* zake. Taifa halikuwa likitafuta Mkandarasi kwa ajili ya kujenga *LNG*, lakini waliokuwa wakifanya kazi ya gesi kwenye Kitalu *Block one* na *Block two* baada ya kugundua gesi nyingi wakasema hii gesi huwezi kuiuza hapa ndani ni lazima itengenezewe *plant* za *LNG* iuzwe nje. Serikali ikawaambia badala ya *Block one* kujenga *LNG* yake na *Block two* kujenga *LNG* yake, shirikianeni mjenge *plant* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana kwamba *Equinor* ambao zamani walikuwa wakifahamika kama *Statoil* wakishirikiana na *ExxonMobil* ambao ndio wako *block one* washirikiane na *Shell* ambaye ndio alinunua hisa za *British Gas (BG)* ambaye na yeye anashirikiana na *Ophir Energy* na *Pavilion Energy* kwamba hawa washirikiane kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati *Statoil* ambao ni *Equinor* leo wanahangaika na hili *Shell* alikuwa *busy* na *Plant* ya Msumbiji, kwa hiyo wakawa hawashirikiani vizuri. *Equinor* wakaamua kupambana kuishauri Serikali iwaruhusu wajenge *plant* yao wenyewe na mwezi wa Disemba Serikali imeridhia kwamba nyinyi *Equinor* mnaweza kuendelea na *plant* yenu. Leo mtu akisema hapa wananchi washukuru Mungu kuhusu *LNG* maana yake anazungumza jambo asilolijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niishauri tu Serikali hapa sasa kwa sababu mradi wa *LNG* ni mkubwa na kwa kuwa mmewaruhusu *Equinor* kuendelea na *LNG* basi kiundwe kitengo maalum cha kushughulika na hiyo *LNG* kama ilivyofanywa kwenye *Stiegler's gorge.* Kwamba kumekuwa na kitengo maalum kinashughulikia uendelezaji tu wa *Stiegler's gorge* na kwenye *LNG* vile vile kiundwe kitengo cha namna hiyo ili hawa *Equinor* wawe na mtu ambaye wanadili naye moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya mambo ya gesi usipoyajua kwa kweli yatakusumbua na ndio maana mtu anaweza kuja hapa akahoji, bomba kubwa la gesi mpaka leo *utilization* yake ni *7%* tu, hiyo ndio sahihi kwa sababu bomba lile halikujengwa ili lijae ndani ya miaka miwili. Kwa sababu kama lingejaa ndani ya miaka miwili ndio ingekuwa hasara. Lile bomba linatakiwa lisijae hata ndani ya miaka 20. Kwa hiyo, kama leo liko *7%* maana yake ujenzi ule uliona mbali zaidi na tuna sababu ya kuipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Watanzania waanze kuzoea vitu vikubwa vinavyojengwa kwa fedha za ndani, yale mengi ambayo tulikuwa tukiamini huko nyuma kwamba hayawezi kutekelezeka ndani ya Awamu ya Tano yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye Kamati nyingine ya Ulinzi na Mambo ya Nje…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea kengele imeshagonga.

**MBUNGE FULANI:** Aaaa, jamani shule.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ali Salim Khamis dakika tano na Wabunge wengine wote waliosalia kwa sababu ya muda imebidi wagawane muda. Kwa hiyo wote watachangia dakika tano tano. Mheshimiwa Ali Salim Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mheshimiwa Gerson Lwenge ajiandae.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami ya kuweza kuchangia mawili/matatu. Nataka nijielekeze zaidi katika masuala haya ya mafuta na gesi. Ripoti ya Kamati imeelezea wazi juu ya matatizo ya kisheria ambayo yanalikabili Taifa katika

masuala ya miradi hii ya gesi ya *SONGAS*. Pia tatizo hilo hilo lipo katika suala baina ya Zanzibar na Bara kuna tatizo kama hilo ambalo liko katika mikataba hiyo ya *SONGAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, nyongeza ya kwanza, suala la mafuta na gesi ni suala la Muungano na kwenye Ibara ya 34 inaeleza wazi na Ibara ya 64 pia nayo inaeleza jinsi ya masuala ya mafuta na gesi ambayo ni mambo ya Muungano. Kama hiyo haitoshi mwaka 2015, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Mafuta kuonesha kwamba nani hasa anastahiki kusimamia mafuta na gesi katika Tanzania. Sasa kilichojitokeza kwanza mwaka 2009 Baraza la Wawakilishi liliazimia kwamba suala la mafuta litolewe katika mambo ya Muungano, kwa sababu suala hili liliingizwa katika masuala ya Muungano mwaka 1968 katika Katiba ya muda ambayo kimsingi liliingizwa bila ridhaa ya Wazanzibari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiendelea Zanzibar sasa hivi imetunga sheria yake, Sheria Na.6 ambayo inasema kwamba mafuta ni mali ya Zanzibar na Zanzibar wao ndio wenye mamlaka ya kuchimba mafuta na Katiba ya Zanzibar iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 imeeleza wazi mipaka ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia katika sheria hii ya mwaka 2015 Kifungu cha 47, kimeleta marekebisho kumpa mamlaka Waziri wa Nishati wa Bara kwamba ndiye ambaye atatoa maelekezo jinsi masuala yote mazima ya mafuta. Pia Zanzibar nao katika sheria mpya ambayo imetungwa ya mwaka 2016, Sheria Na. 6 nayo vile vile imempa mamlaka Waziri wa Nishati wa Zanzibar kusimamia masuala ya mafuta. Sasa niombe kutokana na mkanganyiko huu wa kisheria na kikatiba nafikiri sasa ni wakati muafaka kuleta mjadala wa katiba ili suala hili la mafuta Zanzibar washughulike na masuala yao ya mafuta na Bara na wao washughulike na masuala yao ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika,Leo ukiangalia masuala haya mafuta huko mbeleni yataleta mgogora sana. Matatizo

haya haya ndio matatizo ambayo yanaikabili miradi hii mikubwa ya gesi sasa hivi, ukiangalia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haipati kitu katika suala zima la masuala ya gesi. Ndio maana leo kila mtu analizungumzia hapa kwamba mikataba ina shida, kwa hiyo sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bunge hili imetengeneza sheria kama zile ambazo wametengenezewa wao na *SONGAS*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeandika kwa maandishi pia mchango wangu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratias Ngalawa atafuatiwa na Mheshimiwa Gerson Lwenge na Mheshimiwa Ajali Akbar ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kujadili Hotuba za Kamati ya Nishati na Madini, pamoja na Ulinzi na Mambo ya Nje. Kwangu nijikite tu kidogo kwa sababu ya muda niongelee tu kidogo kuhusu suala la *Stiegler's gorge.* Tunapokuwa tunaongelea *long term investment* haiwezi kuwa ni kitu ambacho kinaweza kuzuka tu katika kipindi kifupi, tunayo *short term plan,* tunayo *medium* na zile *long term.* Wakati tunajadili suala la *long term plan* wakati huo *short term plan* zile zinaendelea. Kwa hiyo, unaponiambia kwamba huu mradi utakamilika baada ya miaka saba ni kipindi kifupi sana hasa kwa sisi ambao tunaona kuna faida kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri pia watu ambao wanatoa hoja hizi wakawa wanasubiri na kusikiliza wenzao wanaweza kuzipangua vipi zile hoja zenyewe. Kwa sababu unazungumzia suala la *MW* 300, hata hivyo, sasa

hivi Taifa halipo kwenye *crisis,* Taifa tayari linao umeme wa kutosha na pengine ni wa ziada. Kwa hiyo tunapoongelea mipango mikubwa, ni lazima tuongelee mipango mikubwa ya miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea gesi lazima useme hii gesi ya *MW* 300 *life span* yake ni ya muda gani? Inaweza ikawa kumbe ina *life span* ya miaka 20, lakini unapoongelea *Stiegler's gorge* vile vile na yenyewe uende uone kwamba ina *life span* ya miaka mingapi? Kwa hiyo huwezi ukavilinganisha vitu ambavyo unaweza ukavifanya kwa *short term plan, medium plan* na *long term plan.* Kwa hiyo, wakati mwingine tunapokuwa tunaizungumzia hii miradi na hasa miradi mikubwa, kwa sababu tayari Taifa limeshajipambanua, tunaenda kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni lazima tupate nishati ya kutosha, kwa hiyo hata ingekuwa huu mradi unaanza baada ya miaka 15 tunachokiangalia ni *viability* ya *business* yenyewe na tunachoangalia ni *sustainability* ya *business* yenyewe. Kwa hiyo, mwisho wa hapo ndio unaweza ukazijenga hoja zako vizuri. Sisi hatuna *crisis* kusema kwamba kesho ni lazima tufanye ili niweze kuja ku-*support* kwenye viwanda ambavyo tunataka kuviendeleza.

Kwa hiyo, kuna tabia ya kuwa sisi Wabunge tunajenga hoja unapotaka kujibiwa wewe unakuwa haupo, matokeo yake sasa *next time* unakuja unalijadili tena suala lile lile kitu ambacho si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niende kwenye madini. Tunalo suala la Liganga na Mchuchuma. Kwa kweli nimeona Wabunge wengi walikuwa wameizungumzia, lakini kuna haja Serikali ikaweka *concentration* kubwa na kama kwenye mpango wa maendeleo ilivyokuwa imezungumzwa kwamba kuna haja ya kujenga kiwanda cha kufua chuma pale Liganga. Ningeomba Serikali ijikite kwa sababu hadithi hii imekuwa ni hadithi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nina imani Serikali ya Awamu ya Tano itaweka *concentration* kubwa na nina imani kwamba ni Serikali sikivu hiki Kiwanda cha kufua Chuma pale, kitakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye suala la *REA, REA* wanafanya kazi nzuri, japo upo upungufu wa hapa na pale lakini kazi inayofanywa ni nzuri na ni kubwa. Sisi wote tunatoka kwenye majimbo, tunaona jitihada zinazofanyika za kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vingi vinapata umeme na vita-*stimulate* uchumi wa maeneo ambayo sisi tunafika. Kwa hiyo tuipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya na tujaribu kuitia moyo na kuwatia nguvu ili waweze kuzidisha mapambano na hatimaye tukaondoa ule umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la ulinzi. Kule maeneo ya Ziwa Nyasa hakuna doria yoyote ambayo inafanyika, hatuna boti la kiulinzi. Niiombe Serikali itupatie ulinzi kwenye maeneo yale na maeneo ya maziwa mengine ili kuweza kuondoa sintofahamu ambazo zinatokea hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Gerson Lwenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Ajali Akbar na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Nianze kwa kutoa masikitiko yangu makubwa; kwanza nitoe pole nyingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa mauaji ya kikatili ya watoto ambayo yametokea. Kihistoria kabisa kwa Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Njombe unajulikana ni mkoa wa amani na kwa miaka mingi hatujawahi kusikia vitu kama hivyo. Kwa kweli naomba sana, kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri, kwamba wamejipanga vizuri kuweza kukomesha jambo hili. Naomba nitoe wito kwa wananchi watoe ushirikiano wa kutosha, kufikia watu wote ambao walikuwa na mipango ya kutaka kuchafua Mkoa wetu wa Njombe,

mkoa ambao ni wa amani, ambapo tunawakaribisha wawekezaji waje kuendeleza mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Kamati ya Ulinzi, Mambo ya nje na Usalama; niseme tu naiunga mkono kwa sababu mimi ni mjumbe pia na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, hasa wa Mambo ya Ndani kwa namna alivyotoka kwenye uninja na kwenda kuwa kamanda. Waziri Kangi Lugola, anafanya kazi nzuri na Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri na vyombo vyote vya ulinzi na usalama. Tuviunge mkono, tuweze kushirikiana nao ili kusudi wafanye kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa upande wa Nishati, niipongeze sana taarifa ya Kamati. Katika ukurasa wa 11 wamezungumzia maoni ya aina tatu; kuna suala la upelekaji wa fedha za mradi, kuna suala la vijiji vinavyorukwa na tatu kuna suala la kufungwa mashine umba zile *transformer* ambazo hazikidhi viwango. Kwa kweli Waziri wa Nishati na Naibu wake wanafanya kazi nzuri sana na pia ni wasikivu. Hata hivyo, nataka kusema pamoja na hiyo Wabunge tunapotoa ushauri tunataka wafanye vizuri zaidi ili ikifika mwaka 2020 basi tuwe na vijiji hivi vilivyolengwa kupatiwa umeme viwe vimepata; maana ukikuta mpinzani anakusifia, basi wala ujue kabisa huyu anakukebehi, lakini ukikuta, wa CCM anakusifia basi ana maana kweli umefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana, katika changamoto ambazo zimeelezwa na Kamati, kitu kikubwa watumishi wa *REA* wanapokwenda vijijini, hawapiti kwa viongozi wa vijiji. Kwa hiyo unakuta wanaleta orodha ya vijiji lakini unakuta vijiji vinaandikwa ni vijiji lakini halisi ni vitongoji. Sasa vitu kama hivi ni kwa sababu hawafiki pale; halafu pili wananchi wanashindwa kujua taarifa ya ratiba ya mradi. Kwa mfano, ukichukulia Wilaya ya Wanging'ombe; nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amefika, ameona kabisa kasi ya utekelezaji wa mradi ule si nzuri. Tuna miaka miwili lakini ni vijiji saba tu na vitongoji ndivyo vimewashwa umeme, kati ya vijiji 38 vilivyolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba zile changamoto ambazo zinafanya utekelezaji uwe hauendani na kasi Wizara izichukue na kuzifanyia kazi na pia hii changamoto ya vijiji na vitongoji kuwa kuchanganywa ni kwa sababu tu hawaendi kwa viongozi wa vijiji, basi naomba jambo hili lirekebishwe ili kusudi tutakapokuja kwenye *REA phase III,* awamu ya pili, turekebishe yale maeneo ambayo yamerukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *REA Phase III* unakuta vijiji vile ambavyo vilikuwa na umeme tangu awamu ya kwanza hawajanufaika na hii ya kulipa Sh.27,000. Kwa hiyo ili wanufaike na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi naomba kwamba katika mzunguko wa pili hata vile vijiji ambavyo vilikuwa vimepata umeme kidogo, basi nao waingizwe kwenye mradi wa REA ili nao wanufaike na hii tozo ya Sh.27,000; kwa sababu hayo ndiyo niliyoona kuwa ni malalamiko ya wananchi wengi kule vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikubaliane na hoja za Kamati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ajali Akbar atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Hussein Amar ajiandae.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi naona dhamira ya Serikali ya *REA III* kwa kweli ni nzuri, isipokuwa kuna *challenge* ndogondogo ambazo sisi kama Wanakamati baada ya kutembelea tumekutana nazo. Kwa mfano ukosefu wa nguzo, nyaya, mashine umba; haya ndiyo matatizo ambayo yamejitokeza kwa wingi sana wakati tulipotembelea miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hii haitoshi kuna kurukwa kwa vijiji kama ambavyo Wajumbe wengi wamezungumza. Kwamba vijiji vingi vimerukwa kutokana na kukosekana kwa *scope of work*. Kwa hiyo, niiombe tu kwamba Wizara ifanye jitahada ya kuhakikisha kwamba sasa hili tatizo la kurukwa vijiji kutokana na kukosekana kwa

*scope of work* lisirudiwe tena, maana yake liende hatua kwa hatua, kama Mheshimiwa Waziri anavyokuwa akizungumza siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu hawa Mawaziri wetu; Mawaziri wote kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi. Mawaziri wa Nishati wamekuwa wakijitahidi sana kufanya kazi kwa kiasi kikubwa sana, Mawaziri wa Madini wamekuwa wakifanya kwa kiasi kikubwa sana; kwa kweli *production* inaonekana sasa hivi. Kwa mfano, leo unaweza ukachukulia hoja ya *TANESCO*. *TANESCO* leo wana uwezo, wao wenyewe wanajikimu wao, wenyewe wana uwezo wa kulipia bili zao za umeme. Hii ni jitihada kubwa kwa sababu *TANESCO* haikuwa kufikia hivyo. Ina maana kwamba kuna watu ambao wanafanya kazi ndiyo maana mpaka leo *TANESCO* inafanya kazi kiasi hicho na ina maana hawa vijana wanajitahidi kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye makusanyo, maduhuli yamekuwa yakionekana kwa kiasi kikubwa sana kwa upande wa madini, ina maana kwamba watu wa Madini, wamekuwa wakifanya kazi kwa kiasi kikubwa na ndio maana maduhuli, yamekuwa yakionekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tulikuwa tunazungumzia, ni kuhusu Jeshi letu. Hili Jeshi letu lilikuwa la wapigania uhuru wakati ule wa enzi za Mwalimu Nyerere. Siku moja niliwahi kuongelea kwamba tuangalie namna gani sasa hivi hili jeshi letu linaweza likageuka likawa jeshi la kiuchumi, lisiwe jeshi tu ambalo sasa hivi linakwenda kwenye korosho huko Mtwara, badala yake tulitumie Jeshi hilo Kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamchukulie Mheshimiwa Keissy alivyozungumza, kwamba tulitumie lile jeshi kiuchumi, ina maana kwamba watu wote ambao tumewaondoa kwenye mikono ya mabeberu sasa hivi ni wakati wao wa kurejesha zile fadhila ambazo tulikuwa tumewaondoa katika mikono hiyo maana hakuna hata mtu mmoja anayekuja kutushukuru. Sasa kama tuna nguvu kazi ya kutosha, tuna

vijana wa kutosha, kwa nini na sisi tusiwe kama wanavyofanya mabeberu wengine wa Ulaya? Kwa hiyo tuangalie, namna gani hawa vijana wetu ambao wana nguvu za kutosha tunaweza tukawabadilisha likawa ni jeshi la kiuchumi ili sisi tuishi maisha mazuri kama wanavyoweza kuishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeliona ni kuwapongeza, pamoja na ukwasi ni kwamba hii, *Stiegler's Gorge* hii, kwa kweli umeme tunauhitaji. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwapa vijana kazi hii na hawa vijana waendelee kuchapa kazi, haiwezekani moja kwa moja wewe ukawa unafanya kazi usisikie kelele, haiwezekani; maana mti unapopolewa ndio ambao una matunda huo. Kwa hiyo wakiona kwamba wanapigwa mawe basi wajue kwamba chochote wanachokifanya, waweke jitihada ili kuhakikisha kwamba hili bwawa la *Stiegler's Gorge* linafanya kazi na linazalisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu ule mradi ambao tulikuwa tumekubaliana katika Kamati, kwamba zile *megawatt* 400, Serikali ifanye jitihada na yule Mkandarasi aanze kazi ili kuhakikisha kwamba zile *megawatt* 400 pale Mtwara zinajengwa kwa haraka sana; ili kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa wakati kama vile ambavyo tumekubaliana na kama vile ambavyo wananchi wengi wana uhitaji umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagongwa Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika majadiliano haya. Kwanza nipende kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya katika taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana, naamini Watanzania walio wengi wanaona; na katika kazi hizi Mheshimiwa Rais lengo lake ni kupunguza matatizo ambayo yalikuwepo ambayo yalikuwa yakileta changamoto mbalimbali katika sekta ya madini na sekta mbalimbali ambazo ziko ndani ya nchi yetu. Juzi tumeona amekutana na wadau wa madini nchini, amejadiliana nao na ameona changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kuona hata baadhi ya wadau ambao wameweza kuchangia wameweza kuchangia, wameweza kuionesha Serikali sehemu ambazo kuna mianya inavyopoteza mapato katika nchi yetu. Hata kule Tanga wameweza kuzungumza habari ya maeneo yenye migodi ambayo watu wanaitumia migodi ile kwa ajili ya kujinufaisha binafsi. Vilevile pia wameonesha namna gani ambavyo baadhi ya watumishi wetu katika Serikali hawawajibiki ipasavyo. Kwa hiyo mimi binafsi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya na hatuna sababu ya kuacha kumpongeza kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kuzungumzia; ni kuzipongeza Wizara za Nishati na Madini, kazi kubwa sana wanazifanya pia. Tumeweza kuona hata Wizara hii ya Nishati kupitia Mheshimiwa Medard Kalemani pamoja na Mheshimiwa Subira Mgalu, wanapambana sana ili kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vinapata umeme. Katika maeneo yetu, tumeona wakitembelea vijiji. Mimi binafsi kwa kweli nisiseme uongo, wamekuja mpaka jimboni kwangu mara mbili, mara tatu. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, hata Kamati ilifika maeneo ya vijiji vyetu na

baadhi ya vijiji vimeanza kupata umeme katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo zipo jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vinapata umeme. Zipo changamoto ambazo zimezungumzwa hapa. Katika utekelezaji wa miradi ya aina yoyote changamoto huwa hazikosekani, tuangalie namna gani ya kuweza kutatua hizi changamoto zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hizo changamoto lakini miradi inatekelezwa vizuri na mambo yanakwenda, hata kama zipo lakini ni ambazo zinaweza kuzungumzika na kuweza kutekelezeka. Kwa mfano, niishauri tu Serikali, kwamba itoe fedha kwenye Wizara hii ya Nishati ili iweze kutimiza kazi zake kwa wakati. Wanapotoa fedha hizi zitakwenda kulipwa hawa wakandarasi ambao wanatekeleza miradi hiyo, wakandarasi wataweza kupata fedha ambazo zitawasaidia kununua vifaa ambavyo vitakuja katika utekelezaji wa umeme vijijini. Jitihada kubwa zinafanyika, lakini niiombe Serikali iweze kuongeza fedha katika miradi mbalimbali inayotekelezwa ikiwa chini ya Wizara hii ya Nishati. Kwa hiyo hilo nilikuwa napenda kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ipeleke fedha katika taasisi zake, kwa mfano *TANESCO, TPDC, STAMICO*, wawape fedha ili waweze kuhakikisha kwamba yale malengo waliyokuwa wemejiwekea waweze kuyatekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naliona, Serikali iangalie namna ya kuongeza rasilimali watu. Rasilimali watu imekuwa ni changamoto sana katika taasisi mbalimbali za Serikali na hii inasababisha kupunguza uwezo wa Serikali kukusanya mapato kwa wakati. Tunaweza kuona katika sekta za madini, gesi pamoja na mafuta. Kwa hiyo niiombe Serikali iweze kuongeza rasilimali watu ili

waweze kuhakikisha kwamba majukumu ambayo Serikali imejiwekea yaweze kutimizwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningependa kuchangia ni katika suala zima ambalo Kamati imezungumzia; masuala ya *flow metres.* Tunaweza kuona *flow metres* zetu katika maeneo yetu ya bandari. Kuna bandari ya Mtwara, bandari ya Tanga, lakini kuna Bandari hazina *flow metres.* Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba tunapata mafuta ambayo hayapo katika utaratibu mzuri wa mahesabu. Kwa hiyo tunapofunga *flow metres* zetu inatusaidia kuweza kupata *exactly figure* ambayo itatusaidia kupata mapato katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Wizara na pia Serikali ihakikishe kwamba inafunga *flow meters* katika maeneo ambayo yana uhitaji hasa kwa sababu ni faida kwa Taifa letu. Kwa hiyo walichukulie kama sehemu ya mojawapo ya kudhibiti kuingizwa kwa mafuta pasipo kupata *data* kwa sababu wanaweza kuchakachua taarifa ambazo zinakuwa zimeandikwa japo zinaandikwa na watumishi wetu. Sasa tukipata *flow meters* zitatusaidia kurekodi na kupata *amount* sahihi ya mafuta yanayoingia na vile vile itatusaidia kupata kipato, ambacho nchi inahitaji kukipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo...(Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Hussein Amar atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ajiandae.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja

zilizoko mbele yetu. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi kwa kuipata nafasi hii, nafasi adhimu kabisa. Nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukubali kukaa na wadau wa sekta ya madini, nami pia ni mdau, mchimbaji mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite kwanza kwenye ushauri, kwa sababu dakika tano ni chache. Kwanza niipongeze Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuyapitia yote tuliyoyapendekeza kwenye kikao tarehe 22; kwa kweli kazi nzuri wameifanya, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, naomba Serikali iyafanyie kazi haraka yote ambayo yamependekezwa na Kamati ili kuepusha utoroshwaji wa dhahabu na madini mengine. Kwa mfano ucheleweshwaji wa utoaji wa leseni. Ucheleweshwaji wa utoaji wa leseni unachangia sana utoroshaji wa madini kwa sababu kuna watu wanaifanya kazi bila kuwa na leseni Serikali haiwatambui, wanatorosha madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali ifanye haraka sana kuwatambua hawa wachimbaji wadogo wadogo na kuwarasimisha, kuwapatia leseni ili iweze kuwatambua na kuweza kukusanya kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni kwamba *NEMC, OSHA,* ZIMAMOTO na Madini waweze kukaa pamoja ili kuweza kurahisisha taratibu zote za kuweza kutoa vibali. Leo vibali vimekuwa na matatizo, *NEMC* anakuja kivyake, *OSHA* anakuja kivyake, Madini anakuja kivyake; leseni zinachelewa kutoka na zikitoka pia ni kwa gharama kubwa. Naiomba Wizara ya Madini ilishughulikie hili ili waweze kuweka *center* moja ya kuweza kuyashughulikia haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni kwamba, kuna maeneo mbalimbali; kwa mfano Wilaya

ya Nyangh'wale, kuna maeneo makubwa ambayo yanafanyiwa uchimbaji mdogo mdogo lakini wachimbaji hawajarasimishwa mpaka hivi sasa. Nina maeneo kama manane ambayo wachimbaji hawa wadogo wanachimba kiholela, wanaharibu mazingira na pia Serikali haipati mapato. Naiomba Wizara iyarasimishe maeneo hayo ili kuweza kuwapa wachimbaji wadogo wadogo na kuwapatia leseni na kuwatambua ili Serikali iweze kukusanya mapato. Leo hii dhahabu nyingi inatoroshwa kwa sababu udhibiti haupo, Serikali inapoteza mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana alikuwa akijipambanua hapa Mheshimiwa Wizara wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kingwangalla, anasema anachangia asilimia 27 kwenye Pato ya Taifa, lakini dhahabu na madini mengine yakiwekewa utaratibu mzuri, naamini kabisa itakuwa ni sekta ya kwanza kuchangia mapato makubwa sana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu rasilimali watu pamoja na vitendea kazi; Wizara hii ya Madini iongezewe, Serikali itoe pesa kuongezea hii bajeti ili iweze kupata hawa watendaji pamoja na vitendea kazi vya kutosha kama vile magari ili kuweza kuzunguka maeneo mbalimbali. Kwa mfano, ukiangalia leo Geita ina gari mbili ambazo nazo hazifai, lakini pia ina wafanyakazi 20 tu, lakini Geita inaongoza kwa uchimbaji wa dhahabu. Je, wale watumishi 20 watawazungukia vipi wale wachimbaji wadogo na kuweza kukusanya maduhuli ya Serikali? Naiomba Wizara iongezewe pesa ili sasa waweze kuajiri watu wengi na pia kuweza kupata vitendea kazi kama vile gari na vifaa vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nitoe ushauri, kwamba Wizara itengewe pesa ili iweze kujenga maabara katika Mkoa wa Geita, kwa sababu Mkoa wa Geita ni kitovu cha dhahabu, ijengwe maabara kubwa na kuweka vifaa mbalimbali kwa ajili ya upimaji wa dhahabu na mambo mengine mbalimbali yanayohusiana na masuala

ya dhahabu. Kwa hiyo naiomba Serikali itenge fedha ili kuweza kujenga maabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho niliomba nichangie muda mrefu, sasa dakika tano hazitoshi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI**: Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, ngoja tumalize, utaomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Joram Hongoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani na Mheshimiwa Doto Biteko ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja za Kamati hizi mbili. Nianze kwa kusema kwamba Kamati zimeandaa taarifa nzuri sana. Napongeza Kamati zote mbili; Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama lakini pia Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru sana Serikali kwa hoja waliyoitoa asubuhi kwa maana ya kauli ya asubuhi juu ya mauaji yaliyokuwa yanaendelea kule Njombe. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri kwa namna wanavyoshughulikia hili jambo kwa ujirani mwema kabisa na kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba mauaji Njombe yanatokomezwa au yanadhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri, yeye aliweza kushiriki pia katika misiba kule Njombe, hasa ya wale watoto watatu pamoja na kuongea na wananchi

na kutoa maelekezo mbalimbali kwa Jeshi la Polisi na viongozi wengine ili kwa pamoja kuweza kutokomeza mauaji yaliyokuwa yanaendelea kule Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba nichangie kidogo kwenye nishati ya madini, hasa juu ya umeme vijijini kwa maana ya umeme wa *REA.* Kwanza, napongeza kazi zinazofanywa na Wizara hii, wanafanya kazi kubwa na tunaona matokeo; vijiji vingi vinaendelea kupata umeme na maendeleo kupitia umeme yanapatikana na viwanda vingi vinafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo ambako hii miradi inaendelea kwa sasa, bado kasi yake siyo kubwa, ni ndogo hasa tukiangalia kwenye mikoa yetu, hasa kwenye Jimbo langu, kasi ya usambazaji wa umeme ni ndogo. Naomba Serikali ijitahidi kuwapa Wakandarasi fedha ili waweze kuhakikisha kwamba wanasambaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo tayari kusambaza umeme lakini ukiwauliza tatizo kubwa linakuwa ni fedha, wanashindwa kupata fedha kwa ajili ya kununua nguzo na vifaa mbalimbali kama nyaya na *transformer*. Pia kuna tatizo la uzalishaji wa hivi vifaa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, wajitahidi kuhakikisha kwamba wale wazalishaji wa vifaa na fedha zinakwenda kwa wakati ili maeneo yote ya vijijini yaweze kupata huu umeme wa *REA.* Ni muhimu sana na nina uhakika kabisa itatubadilisha Tanzania baada ya muda siyo mrefu Tanzania haitabaki kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo juu ya Shirika la *TANESCO.* Shirika hili pia linakabiliwa na madeni mengi kama walivyoeleza Wajumbe na inavyoeleza taarifa, lakini ulipaji wake wa madeni hayo bado unakwenda kwa kasi ndogo. Naomba Serikali ilipe madeni kwenye shirika hili ili liweze kujiendesha. Ilivyo sasa hivi, inapotokea kuna tatizo ambalo linahitaji vifaa, wanunue *transformer* au vifaa kwa ajili ya kurejesha umeme kwenye eneo fulani, inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine, kwa mfano, Nyanda za Juu Kusini, maeneo yetu yana mvua nyingi, kwa hiyo, umeme umekuwa ukiathiriwa, *transformer* nyingi zimekuwa zikiunguzwa na radi. Kwa hiyo, inapotokea *transformer* imeungua, inakuwa ni vigumu; na inachukua muda mrefu sana kurejesha umeme katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, alikuja kwenye eneo langu akakuta tatizo kubwa sana la umeme kwenye maeneo ya muhimu; ya hospitali na maeneo ya vijiji kwenye Kata moja ya Ikuna, lakini alipofika alitoa kauli na akaleta ile *transformer*. Nashukuru sana kwa Wizara nzima, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuleta hii *transformer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo sasa, mpaka leo hii ile *transformer* haijafungwa, sijaelewa wanakosa vifaa gani? Kwa hiyo, naomba mwezeshe hili Shirika la *TANESCO* ili liwe na uwezo wa kurejesha huduma haraka, kwa sababu linapochelewesha huduma, madhara yanakuwa makubwa. Viwanda vinasimama kufanya kazi na huduma haziwezi kuendelea kwa sababu umeme haupo. Likiwezeshwa vizuri litaweza kujitegemea na kuhakikisha kwamba umeme unarejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo haya ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu kuna radi nyingi, napendekeza kama inawezekana, tutumie ule mfumo wa Shirika kama la *CEFA* ambalo wanajenga *transformer* zinajengewa ndani na sijawahi kusikia *transformer* ya *CEFA* imepigwa radi. Kwa hiyo, kwenye maeneo ya mvua tunaweza tuka-*adapt* ule utaratibu wa *CEFA* ili *transformer*...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, ajiandae.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika mada muhimu ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kuwapongeza sana Kamati ya Kudumu kwa mapendekezo waliyoyatoa. Sisi kama Serikali tumeyachukua tutayafanyia kazi na kufanya maboresho zaidi. Kwa hiyo, napenda sana kumshukuru Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, wametoa michango mizuri, mingi na yenye ushauri. Bado naendelea kusema, kama Serikali, tutaichambua tutaifanyia kazi na kufanya maboresho ambapo lazima pafanyike maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nami basi niseme machache kuhusiana na ajenda ya leo. Kuhusiana na mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa *megawatt* 2,115, bila shaka Watanzania wote tunashuhudia, ni mara ya kwanza Tanzania kuingia kwenye ulingo wa kidunia kuwa na miradi mikubwa ya kuzalisha umeme. Kwa hiyo, tuipongeze sana Serikali yetu kupitia kwa Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu Watanzania na wananchi kupitia Waheshimiwa Wabunge; miradi mikubwa duniani inahesabika mnapokuwa na mradi wa kuzalisha umeme wa kuanzia *megawatt* 2,000. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeingia katika miradi mikubwa 70 duniani, nasi ni wa 60 duniani. Kwa hiyo, napenda tuwapigie makofi Watanzania wote walioshiriki katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, hata Kiafrika tulikuwa hatusomeki kwenye miradi mikubwa ya kuzalisha umeme. Leo tunaongelea *Stiegler's* yenye uwezo

wa kuzalisha *Megawatt* 2,115, ni mradi wa nne Afrika kwa ukubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana Wakandarasi ambao wanatekeleza mradi huu ambao ni *Arab Contractor* kutoka *Egypt* pamoja na *El Sewedy* wanatoka katika nchi ambazo zipo katika nchi tano za kuzalisha umeme mkubwa duniani. Walioshiriki sana kwenye kuzalisha umeme wa *Aswan Dam* wa *Megawatt* 2,100 kule *Egypt.* Kwa hiyo, hatuna mashaka na Wakandarasi na hatuna mashaka na maamuzi ya Kiserikali yaliyofanyika. Ni matumaini yetu mradi utatekelezeka vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwaambia Watanzania kwamba utekelezaji wa mradi huu ndiyo unaanza. Tumesaini mikataba mwezi uliopita, kwa hiyo, hatutarajii Mkandarasi kuwa amelipwa hela nyingi kwa sasa kwa sababu ndiyo kazi zinaanza. Kwa hiyo, ni matumaini yetu tunakokwenda tutamlipa Mkandarasi kulingana na kazi zinavyofanyika. Ndiyo maana kwenye taarifa umeona shilingi bilioni 26 tu kati ya shilingi bilioni 700 za utekelezaji wa kazi hii. Kwa hiyo, ni matumaini yetu, wala hatuna mashaka na wenzetu wa Hazina wataendelea kulipa vizuri kadri utekelezaji wa mradi utakavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutaja umuhimu wa mradi huu. Pamoja na kutekeleza miradi mchanganyiko ya kuzalisha umeme, kama ambavyo tunaendelea kuzalisha umeme wa *megawatt* 300 ambao tumeanza kuutekeleza sasa kule Mtwara kupitia *JICA,* wenye uwekezaji wa takribani Dola za Marekani milioni 395 ambao ni *megawatt* 300, mradi huu tunaanza kuutekeleza kuanzia Julai mwaka huu na utakamilika Juni, 2022 ambao utatuzalishia *megawatt* 300 za gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kweli kwamba tumeacha miradi mingine ya kuzalisha umeme. Umeme huo tutausafirisha kwenye gridi ya Taifa kutoka Mtwara, umbali wa kilometa 512 kwa kuingizwa kwenye rridi yetu ya Taifa. Bado tunatekeleza Mradi wa Kinyerezi

na mingine. Hii inaonesha kwamba Watanzania tunaamua kwenda na umeme mchanganyiko. Kwa hiyo, kutekeleza Mradi wa *Stiegler's* hakuna maana kwamba tunaondoa utekelezaji wa miradi mingine ya kuzalisha umeme. Naomba Watanzania tuendelee kuunga mkono, tushirikiane mradi utekelezeke ili tuondokane na changamoto ya umeme hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa leo tunapoongea hapa, tuna umeme wa ziada *megawatt* 278, matumizi yetu ya leo ni *megawatt* 979, lakini haina maana kwamba hatuhitaji kuendelea kuzalisha umeme. Unatutosha leo, lakini kwa kesho hautatoshi. Kwa hiyo, hatuna budi kuzalisha umeme mkubwa ili kujihakikishia ujenzi wa uchumi wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya *REA,* kwanza kabisa, napenda naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, mnatuunga mkono sana kwenye miradi hii. Tunapokwenda kwenye miradi yenu, huko kwenye Majimbo yenu mnatupa ushirikiano mkubwa. Nitoe rai tu kwa Wakandarasi kwa sababu limesemwa hapa, kwamba utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ni mradi shirikishi. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuagiza Wakandarasi kwamba popote walipo wasiingie kwenye maeneo ya Wabunge bila kuwashirikisha Wabunge au uongozi ulioko kule ili utekelezaji uwe na tija zaidi. *(Makofi)*

Leo tunapoongea, tunapeleka umeme vijiji takribani 6,212. Mwaka 2015 tulipeleka umeme vijiji 1,927 tu, kwa hiyo, ni zaidi ya asilimia 300 kwa miaka hii mitatu tumetekeleza mradi huu wa kupeleka umeme vijijini. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, mwendelee kutuunga mkono ili tufanye kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Heche alivyosema; juzi tu alituomba tumpelekee umeme Susuni, tukapeleka; tumepeleka Kerenge, tumepeleka Nyamwaga, Nyanungu na Nyurito. Ndugu yangu Mheshimiwa Heche anataka nini? *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Taarifa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza miradi kwa ufanisi sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Heche na Wabunge wengine, mradi huu ni wa miaka minne iliyobaki, mwaka...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana, kwa hiyo, sitaruhusu taarifa kwa sasa. Mheshimiwa Dkt. Kalemani endelea.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Niwape tu taarifa Waheshimiwa Wabunge, tunachukua michango ambayo wamesema kuhusiana na utekelezaji wa miradi hii, lakini tumejipanga vizuri kwa upande wa vifaa, sasa hivi Wakandarasi wameshaanza kupeleka vifaa *site.* Ni matumaini yetu kuanzia mwezi ujao *speed* itaongezeka zaidi ili kufikisha umeme kwenye vijiji ambavyo tumepanga kuvitekeleza kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikataba ya *Songas;* kwanza nikupongeze kupitia Kiti chako kwamba mwaka 2018 kupitia kwa Mheshimiwa Spika wakati ule, Waheshimiwa Wabunge waliunda Kamati Maalum ya kupitia mikataba hii ya kuzalisha gesi, mafuta pamoja na biashara. Kwenye mapendekezo ya Kamati, ilipendekezwa mikataba yote ipitiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ni sikivu sana, imeanza kupitia upya mikataba yote ukiwemo Mkataba wa *Songas.* Kwa hiyo, suala la kwamba mkataba ufutwe, urekebishwe ufanyiwe

maboresho, itatokana na mapendekezo ya Kamati ambayo sasa marekebisho na mapitio ya mikataba hiyo yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu matokeo ya kupitia mikataba yatakuja na mapendekezo ya kuboresha ambayo nia ya Watanzania ni kuhakikisha kwamba stahili ya Watanzania kwenye mikataba hii inapatikana. Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa vile mikataba inapitiwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni matumaini yetu mapitio hayo yataboresha zaidi, siyo kwa upande wa mkataba wa *Songas* tu, lakini mikataba yote ya kuzalisha gesi pamoja na utafiti wa gesi na mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kuhusiana na Mradi wa Kinyerezi. Tunayo miradi mingi sana. Mradi wa Kinyerezi wa *megawatt* 185 hivi karibuni utakamilika. Bomba la gesi ambalo Waheshimiwa Wabunge wanataja, ni kweli kabisa huwezi kuona mahitaji makubwa ya gesi kwa sasa kwa sababu viwanda vingi vya gesi vitaendelea kujengwa. Tutakuwa na mradi wa Kinyerezi Na. 1 unaoendelea *extension,* tutakuwa na Kinyerezi *No. 3* wa *megawatt* 600 pamoja na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mahitaji na matumizi ya gesi yataongezeka zaidi. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali walivyofanya kujenga bomba kubwa ambalo leo tunaona matumizi yake ni madogo, siyo vibaya kwa sababu tuna miaka mingi, zaidi ya 100, kuendelea kutumia bomba hili. Kwa hiyo, kutumia asilimia ndogo wala isiwatishe, tutaendelea kutumia kwa sababu miradi mikubwa itaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *LNG* ni kati ya miradi mikubwa sana duniani. Mradi huu mnatambua kwamba uwekezaji wake siyo chini ya Dola za Marekani bilioni 35. Hata hivyo, Serikali imeanza kuutekeleza mradi huu. Tunaposema ujenzi wa uchumi wa viwanda, ndiyo viwanda vya *LNG* tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge na nitoe taarifa; mradi huu haujakwama na hautakwama na tumeanza kuutekeleza. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema, tumeanza majadiliano na mmoja mmoja, tumeanza na *Equinor,* lakini wadau wote ambao wanashiriki kwenye kuzalisha, tunajadiliana nao na sasa tunaongeza kasi ili maeneo ambayo yameshapitiwa, yakamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge wa eneo anakotoka kule Likong'o kwamba tathmini ya fidia ya wananchi imeshafanywa na imeshakamilika. Kinachofanyika sasa hivi ni kufanya uhakiki. Taratibu za uhakiki zikikamilika, wananchi watalipwa fidia na mradi utaendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kusema mengi katika miradi hii, lakini jambo la msingi pia ni umeme wa gridi Kigoma pamoja na Katavi. Katika mradi huu tunatekeleza miradi mikubwa miwili; wa kwanza, ni mradi wa kutoka Iringa, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi ambao umeanza kutekelezwa kwa *portion* ya kuanzia Iringa mpaka Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua za haraka ili tuwapelekee umeme wa gridi wananchi wa Kigoma pamoja na Katavi, Serikali kuanzia Desemba mwaka 2018 tumeanza kutekeleza mradi wa kusafirisha umeme wa kilovoti 132, umbali wa kilometa 391 kutoka Tabora, Urambo mpaka Kidahwe, Kigoma. Mradi huu tumeshatenga fedha, Dola za Marekani bilioni 81. Mradi utatekelezwa kama tulivyosema na utakamilika Februari, 2020. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Katavi...

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Dkt. Kalemani. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Doto Biteko atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola na Mheshimiwa Dr. Mwinyi, ajiandae.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mungu kwa nafasi hii na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani aliyonipatia na kuniteua kuwa Waziri wa Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru sana mtangulizi wangu, Mheshimiwa Angellah Kairuki ambaye amekuwa Mwalimu wangu mzuri sana kwenye nafasi hii. Wakati nikihudumu kama Naibu Waziri wa Madini, amekuwa Mwalimu mwema, aliyenifundisha, aliyeni-*expose* kwa kweli kwa kila namna ya kujifunza namna ya kusimamia Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru vile vile Mheshimiwa Nyongo ambaye pia ni Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa ambao walinipatia wakati nikiwa Naibu Waziri mwenzake na hata sasa ambapo tunaendelea kushirikiana pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, kama walivyoanza wengine, nami naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Makamu wake, Mheshimiwa Mariam Ditopile pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa maelekezo ambayo kwa kweli wanatupa kila wakati tunapokutana nao kwenye vikao vya Kamati na kwenye mashauriano mbalimbali wanapoona kuna mambo yanayohitaji kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, binafsi naona fahari kubwa kufanya kazi pamoja na Kamati hii kwa sababu ya umakini wao na ubunifu wao, lakini vilevile kujali kwao na kufuatilia mambo mbalimbali ambayo yako kwenye Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau nami niseme naunga mkono hoja iliyoletwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Nami nitoe mchango mdogo tu kwenye mambo mbalimbali ambayo yamezungumzwa kwenye taarifa lakini vilevile na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, itashangaza sana kama nitasema hakuna changamoto kwenye Sekta ya Madini. Changamoto zipo na hazikuwepo leo, zimekuwepo kwa muda mrefu. Ninyi mnafahamu kwamba hapa Afrika Sekta ya Uvunaji wa Madini sisi tumeanza miaka ya 1990 kwa kuleta mitaji mikubwa kutoka nje. Huko nyuma waliokuwa wanachimba madini walikuwa wachimbaji wadogo. Ukianza mwaka 1987 mpaka mwaka 1997, miaka kumi ile wachimbaji wadogo peke yao ndio walikuwa wanachimba kwa asilimia 94, hapakuwa na mtaji wa mgeni hata mmoja, tulikuwa sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuja wenye mitaji miaka hiyo ya 1990 na hapo sasa Sekta ya Madini ikawa ndilo jambo linalojadiliwa. Bunge hili linafahamu, kama kuna sekta ambayo imeundiwa Kamati nyingi mno ni Sekta ya Madini. Kamati za Ushauri za Bunge ziliundwa kwenye Sekta ya Madini, Kamati za uchunguzi ziliundwa kwenye Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2002 iliundwa Kamati ya Kipokola, mwaka 2004 ikaundwa Kamati ya Masha; mwaka 2006 ikaundwa; zimeundwa Kamati nyingi na hata Bunge hili na lenyewe limeunda Kamati mbalimbali. Nia ilikuwa moja tu, kuondoa changamoto zilizomo kwenye Sekta ya Madini; na Serikali imekuwa ikifanya hivyo hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunavyoendelea kufanya kazi ya kusimamia Sekta ya Madini, tunagundua changamoto zilizomo, tunatafuta mbinu za kuziondoa. Namna mojawapo ya kuondoa changamoto hizo, ipo kwenye sheria. Ndiyo maana mnaona Sheria ya Madini imekuwa ikibadilika miaka hadi miaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1998 ilibadilika, mwaka 2010 ilibadilika na baadaye 2017 tukafanya marekebisho makubwa sana ya mwelekeo wa Sheria yetu ya Madini. Nia ni kuleta tija kwa nchi kwenye Sekta hii ya Madini. Bado tunaendelea kukabiliana na hizo changamoto pamoja na kwamba tumeshapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge hapa na nianze kueleza mchango mdogo tu ambao umeelezwa na ndugu yangu, Mheshimiwa Frank Mwakajoka, sijui ni kwa nia njema au ni kwa sababu ya kunogesha, anasema Sekta ya Madini mchango wake umeshuka. Naomba niweke taarifa sahihi kwenye Bunge hili; mchango wa Sekta ya Madini kwenye nchi ya Tanzania toka tumeanza kuchimba haujawahi kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitampa rekodi kidogo hapa; mwaka 2013, Sekta ya Madini ilikuwa inachangia asilimia 3.3; mwaka 2014, Sekta ya Madini ilikuwa inachangia asilimia 3.7; mwaka 2015, ilichangia kwa asilimia 4.0; mwaka 2016, imechangia *constantly* na mwaka uliofuata 2017, kwa asilimia 4.8. Haijawahi kuchangia kwa asilimia tano na ikashuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukuaji wa Sekta yenyewe ya Madini ni ule ambao ni *very promising.* Mwaka 2013, ukuaji wa Sekta ya Madini ulikuwa asilimia 6.9; mwaka 2014, ukuaji wake ulikuwa asilimia 9.4; mwaka 2015, ulikuwa asilimia 9.1. Mwaka juzi, mwaka 2017, sekta iliyoongoza kwa ukuaji katika sekta zote sio mchango wa sekta, ni Sekta ya Madini, ilichangia kwa asilimia 17.5. Nadhani tusivunjane moyo, tutiane moyo, tuna safari kubwa ya kufanya. Kazi ya kudhibiti madini kutoroshwa sio kazi ya mtu mmoja, Wizara

ya Madini, ni kazi ya Watanzania wote. Leo nataka niwaambie tunapokamata wanaotorosha madini hatukuti wageni peke yao, tunawakuta na Watanzania wenzetu wamo wakisaidia utoroshaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Serikali iwe yenyewe peke yake bila Watanzania wenyewe kutengeneza *mindset* ya kuwa na wivu na rasilimali zao. Naomba nipaze sauti kwenye Bunge hili kuwaomba Watanzania; madini tuliyonayo kuna siku yataisha, lazima tuone wivu, tuyalinde kwa nguvu zote. Wanaokamatwa wote wawe wenyeji, wawe wageni, ukienda utakuta aliyetengeneza huo mchongo ni Mtanzania mwenzetu aliyekuwa anachimba nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba nieleze vilevile, wameeleza hapa Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa wachimbaji wadogo waanze kurasimishwa na wameeleza maoni waliyoyatoa kwenye mkutano tulioufanya, tukamwalika Mheshimiwa Rais, kwamba tuyasikilize. Naomba niwaondoe wasiwasi; mapendekezo yao yote yako 22, yote tunayafanyia kazi kama Serikali, yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo waliyoyatoa yanayohusiana na sharia, Serikali inayafanyia kazi lakini yapo mengine ya kiutendaji kwa mfano kuwapatia maeneo ya kuchimba; baada ya wiki inayokuja nitatoa taarifa ya leseni ngapi tunazifuta kwa sababu tunazo leseni nyingi kwa kweli, zaidi ya 2,038, zimeshikiliwa na watu ambao hata humu nchini hawamo. Zinadaiwa fedha zaidi ya dola milioni 42, zimekalia maeneo wachimbaji wadogo wakienda kule wanafukuzwa, tunakwenda kuzifuta zote hizo tuwapatie wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo limeelezwa hapa juu ya *TEITI,* kwamba *TEITI* haijafanya kazi yake; naomba niweke rekodi sawasawa, ni kweli kwamba *TEITI* kazi inayofanya ni *reconciliation* kati ya kile kilichotolewa kwenye mgodi na kile kilichoingia Serikalini, hakuna fedha yoyote

iliyopotea. Kinachofanyika makampuni yanayoshughulika na Sekta ya Madini na Gesi, mafuta, ni makampuni 2,087. Wao wakatengeneza utaratibu wa kuyachambua baadhi kama sampuli, wakachukua yale yenye *threshold* ya mtaji wa milioni 300 ndiyo yakafika hayo 50. Sio kweli kwamba tulipaswa kukagua 2,000 sasa tumekomea 50, hapana, ni wale *MCG* waliamua wenyewe kuchambua kwamba tukague wale ambao wana mtaji mkubwa kuanzia dola milioni 300, ndiyo tukapata kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo fedha anayozungumza imepotea sio fedha iliyopotea, ni *reconciliation,* kwamba ukienda kwenye mgodi unakuta anakwambia nimelipa shilingi 10, ukija huku Serikalini unakuta pengine hiyo hela haijawa *recorded* au unakuja huku Serikali unakuta kuna fedha fulani haijawa *recorded,* ukienda kwenye mgodi unakuta hiyo fedha. Kwa hiyo, hiyo kazi unachukua hizo *anomalies* zote, unampelekea *CAG* ili aweze kuhakiki kujua kama kweli kuna fedha zimepotea, kwa hiyo hakuna pesa iliyoibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati njema Mheshimiwa Mwakajoka ni Mjumbe kwenye Kamati, majibu haya tulimpatia kwenye Kamati, lakini kwa sababu ni lazima tunogeshe, ruhusa tunaendelea, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwakajoka; hakuna mtu ataiba fedha kwenye Sekta ya Madini akabaki salama, hakuna mtu atatorosha madini kwenye Sekta ya Madini atabaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wamelalamikia kodi, wamelalamikia masoko. Nilikuwa na mkutano hapa juzi wa Wakuu wa Mikoa yote Tanzania, tumeshaanzisha maeneo na kuyatenga kwa ajili ya masoko ya madini. Hata ule utaratibu wa kusema mtu anayetaka kuleta madini hapa nje awe na mlolongo mrefu, mlolongo huo tumeuondoa, sasa watu wanaotoka Congo, Msumbiji, wale wanaotaka ku-*trade* madini yao ndani ya nchi, ruhusa, ilimradi waseme kwamba tunataka kuja kufanya biashara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Doto Biteko, muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliobaki na kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5), naongeza nusu saa na fasili ya tano haihitaji niwahoji maana kuna watu mtaanza hapa kuzungumza habari ya hoja.

Kwa hiyo sasa aendelee Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu kwenye hoja za Kamati, hususan kwenye taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Zungu pamoja na Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameifanya na kuweza kuainisha maeneo yenye changamoto na kutoa maoni pamoja na mapendekezo. Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati yake, nataka niwahakikishie kwamba maoni na mapendekezo waliyoyatoa katika Wizara yangu mara moja nitaanza kuyachambua na kuyashughulikia moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya tangu amekuwa Rais wa nchi hii. Mambo yote ambayo aliyaahidi kwenye Ilani hii ya CCM na hususan kwenye eneo la Ibara ya 4 na Ibara ya 146 inayohusu vyombo vya ulinzi na usalama. Nataka niwathibitishie Watanzania kwamba Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano wamewahakikishia Watanzania kwamba wamekuwa na

amani, wamekuwa na usalama, wamekuwa na utulivu, mali zao zinalindwa pamoja na maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba kuna baadhi ya Watanzania ambao wanabeza, wanakejeli juhudi za Mheshimiwa Rais, nataka nimthibitishie kwamba hao hawajitambui na hawajui kwamba yeye yuko na Mungu. Isaya 54, mstari wa 17 inasema: "Kila silaha itakayonyanyuliwa juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa," kwa sababu Mheshimiwa Rais yuko na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Katika uchambuzi wa Kamati, ukurasa wa 20 wamezungumzia masuala mbalimbali, lakini moja ambalo nitakwenda kulitolea ufafanuzi ni lile linalohusu kuchelewesha upelelezi wa kesi na hivyo wakati mwingine kusababisha magereza kuwa na mrundikano hasa wa mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango uliotolewa na Mheshimiwa Ruth Mollel ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati, ameelezea sana kwa hisia na uchungu mkubwa kwamba kesi nyingi zinachelewa, zingine miaka minne mpaka sita kwa mifano aliyoitoa. Nakubaliana naye, lakini sababu zinazosababisha kuchelewa kwa upelelezi wa kesi sio sababu moja, ni sababu nyingi kadha wa kadha. Kuna sababu zingine ni kutokana na kesi yenyewe jinsi ilivyo, inahitaji utaalam, wakati mwingine inahitaji kusafiri, tunahitaji fedha. Hata hivyo, pia nakubali kwamba, upelelezi mwingine unachelewa kwa sababu ya uzembe wa askari, kwa sababu ya askari kutowajibika na hivyo kuchelewesha upelelezi wa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ambayo ni kubwa na naomba Mheshimiwa Ruth Mollel anisikilize vizuri, pamoja na upande huo wanisikilize vizuri, kuna kesi ambazo zinachelewa upelelezi wake kwa sababu ya kutelekezwa. Baadhi ya kesi ambazo zinatelekezwa, nitolee mfano wa kesi maarufu ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Kesi ya Mheshimiwa

Tundu Lissu imetelekezwa. Katika mazingira ya kawaida kesi inapotelekezwa Jeshi la Polisi hawana namna nyingine ya kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tukio lile lililotokea tarehe 7 Septemba, 2017, lile gari lilikuwa na watu wawili tu. Baada ya tukio lile, sisi wapelelezi na uendeshaji wa kesi kuna wale tunaowaita *key witnesses; key witnesses* ni pamoja na *victim,* Mheshimiwa Tundu Lissu na yule dereva aliyekuwa kwenye gari. Katika mazingira ya kutatanisha na ambayo mpaka sasa hatuelewi; ni kwa nini dereva ameitelekeza kesi hii na kutotoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...ili atueleze hao ambao waliwafuatilia walikuwa ni watu wa aina gani?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...wembamba, wanene; warefu, wafupi, walivaaje ...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, analipotosha Bunge, taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ... ili kusaidia Jeshi la Polisi liweze ku...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, taarifa nilishazikataa tangu Mheshimiwa Stanslaus Mabula aliposimama, kwa hiyo naomba ukae tafadhali; Mheshimiwa Kangi Lugola.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema wakatulia ili niwape darasa la mambo ya upelelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukosa ushirikiano wa *key witness* ambaye ni dereva mpaka sasa, kesi hiyo tumeshindwa kuendelea nayo katika mazingira ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namba mbili; niendelee kutoa maelezo kwa nini kesi zinachelewa. Mheshimiwa Tundu Lissu baada ya kutoka hospitali tulitarajia kwamba angekuja kwa uchungu wa kesi yake ili aje atoe maelezo kusaidia Jeshi la Polisi ili tuweze kuchunguza na kuanzisha ushahidi ambao tunaweza tukapeleka kesi mahakamani. Kwa hiyo katika mazingira ya namna hiyo tunashindwa kuendelea na baadhi ya kesi kwa sababu wanaohusika wanatelekeza kesi zao na wanashindwa kutoa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu na niwaombe Watanzania wote ambao mnakuwa na kesi zenu za jinai, lazima mtoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, lazima kesi hizi muwe na uchungu nazo ili kuondoa lawama kwa Jeshi la Polisi kwamba wanachelewesha kupeleleza ilhali ninyi mnatelekeza kesi zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa mchango wangu... ninyi ndio mnaumiza Jeshi la Polisi kutoendelea kupeleleza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, naomba utulivu tafadhali.

Mheshimiwa Selasini nimekutaja tena, naomba utulivu na wewe ndio *Chief Whip* kwa sasa, naomba utulivu.

*(Hapa Mheshimiwa Selasini aliendelea kuhitaji nafasi ili atoe mwongozo)*

**NAIBU SPIKA:** Siwezi kukupa nafasi kwenye miongozo wakati nimekataa.

Mheshimiwa Kangi Lugola, ongea na Kiti.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye kipengele hicho kwamba katika mazingira ambayo mashahidi muhimu hawatoi ushirikiano kwa Serikali, wasitumie ndimi zao kupotosha wananchi kwamba Serikali inahusika katika vitendo kama hivyo ilhali wao hawataki kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la wahamiaji haramu; Waheshimiwa Wabunge wametoa michango yao juu ya wahamiaji haramu hasa katika Mikoa ya Kigoma, Kagera pamoja na Katavi. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inawahakikishia Watanzania kwamba wahamiaji haramu, hasa ambao wanatoka kwenye Nchi za Congo, Burundi, Rwanda pamoja na Uganda, kupitia Uhamiaji tunaendelea kufanya misako pamoja na doria na kuwabaini wahamiaji haramu wote wengine tunawarudisha kwao wengine tunawashtaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika kushughulika na suala hili la wahamiaji haramu, kuna maeneo mengine yana changamoto kubwa kama ambavyo Mheshimiwa Oliver Semuguruka amezungumzia maeneo ya Kyerwa kule. Nilipokwenda kule Isingiro, nikaenda Ruambaizi, pia kuna lile ziwa ambalo amelizungumzia ambapo wahamiaji haramu wanapenda kutumia mitumbwi na kuvuka kuja upande huu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Uhamiaji tutaendelea kufanya doria ikiwa ni pamoja na kutafuta uwezekano wa kuwa na boti katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala la wahamiaji haramu Serikali imeielekeza Idara ya Uhamiaji kuhakikisha kwamba wanasirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa hiyo niliyoitaja kuhakikisha kwamba

wanafanya operesheni maalum ya kuwabaini na kuwachukulia hatua mahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la vitambulisho vya Taifa ambavyo vinatolewa na *NIDA* kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wametoa michango yao. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa wanaendelea kubaini na kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa na wale ambao hawajafikiwa, wale ambao hawajapata vitambulisho wasiwe na wasiwasi, vitambulisho hivi lazima kila Mtanzania ambaye ana miaka 18 na kuendelea atapata na vitambulisho hivi vinatolewa bure. Kwa hiyo wale ambao hawajafikiwa wasidhani kwamba kuna ukomo na kwa sababu hajapata kitambulisho kwa hiyo sasa hatapata kitambulisho.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi, muda wako umwekwisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naipongeza Kamati, nawashukuru sana kwa ushirikiano wanaotupa mimi pamoja na watendaji wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kulikuwa kuna hoja ya kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini ambayo inaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa, napenda niliarifu Bunge lako kwamba tatizo hili sasa limekwisha. Kwa muda mrefu tulikuwa hatuna hii sera kwa sababu hakukuwa

na maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Napenda niliarifu Bunge lako kwamba maoni hayo sasa yamepatikana, mchakato unaendelea ndani ya Wizara ili kuikamilisha sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi *(beacons)* kunachangia uvamizi wa raia wa kigeni katika baadhi ya maeneo ya mipaka, jambo ambalo linaweza kuathiri ulinzi na usalama wa nchi. Nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba na eneo hili nalo limeanza kufanyiwa kazi kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka yetu upande wa Kenya na upande wa Uganda tayari *beacons* zimeanza kurudishiwa, upande wa Kenya tayari tuna kilometa zipatazo 172 kati ya 760 ambazo tayari wameshaudishia *beacons* kuanzia kwenye Ukanda wa Ziwa Victoria kuelekeza Ziwa Natron. Kwa hiyo zoezi hili linaendelea na tumeanza upande wa Kenya na Uganda, tutaendelea katika maeneo mengine, lakini nia na madhumuni ni kurudisha *beacons* hizo ili kuwepo na uhakika wa kwamba mipaka kati yetu na nchi jirani inajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni kwa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa shirika; tunakubali kwamba Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) lina madeni mengi hususan ule mrdai wao wa matrekta. Nataka nitoe taarifa hapa kwamba toka Mheshimiwa Rais ametoa agizo la wale wote wanaodaiwa waweze kurudisha fedha zile, shirika limeweza kukusanya Sh. 2,900,000,000 na tunaendelea na mchakato huo na baada ya hapo kuna Kampuni maalum ya SUMA JKT ya *auction* ambayo itachukua hatua za kisheria dhidi ya wale wote ambao watakuwa wameshindwa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa uzio katika baadhi ya Kambi za Jeshi kunasababisha migogoro ya ardhi kutokana na wananchi kuvamia maeneo hayo; ni kweli kwamba maeneo mengi ya Jeshi hayana uzio na hayawezi kuwa na uzio kwa sababu ni maeneo makubwa

sana. Tunachokifanya sasa hivi ni kwamba kuna maagizo kwa kila Mkuu wa Kikosi kuhakikisha kwamba wanaweka alama katika *borders* zao na hususan yale maeneo makubwa sana, wapande miti na waweke mabango yanayoonesha kwamba haya ni maeneo ya Jeshi, nia na madhumuni ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa mipaka ilipo na hawaingiliwi katika maeneo hayo. Baadhi ya maeneo hayo ni ya mazoezi, kwa hiyo wananchi wakiingia huko wanaweza kupata athari kubwa kutokana na dhana zinazotumika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya wananchi na vikosi vya Jeshi. Hapa ni kama nilivyosema, migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi ipo ya aina kadhaa; moja ni pale wananchi wanapovamia maeneo ambayo tuna uhakika ni ya Jeshi kwa sababu ya ufinyu wa ardhi ya kulima na kufuga, hao hakuna hoja, ni kuwaondoa tu kwa sababu lazima Jeshi libaki na maeneo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo maeneo yaliyotwaliwa kweli na wananchi hawa wanastahili fidia, tumeweka katika bajeti ya mwaka huu shilingi bilioni 20 na mpaka sasa hivi tumeshapokea karibu shilingi bilioni 3 ambazo tumeanza na kulipa eneo la Kilwa ambapo tunaweka *base* ya *Navy*. Kwa maana hiyo, kila fedha hizi zitakapoendelea kutolewa wananchi hawa wenye stahili za kulipwa fedha kwa sababu walihamishwa katika maeneo yao wataendelea kulipwa ili migogoro hiyo iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni uchakavu wa majengo ya Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi cha Monduli kunashusha hadhi ya chuo hicho kinachotoa mafunzo ya kimataifa. Tumekuwa na jitihada mbalimbali za kukiendeleza na kukiboresha chuo kwani ni cha muda mrefu na baadhi ya majengo yake yamechakaa. Nataka nieleze kwa mfano makazi, katika ule mradi wetu wa nyumba 6,064 pale Monduli wamepata nyumba hizo kwa ajili ya Askari na

kuna baadhi ya majengo mapya yamejengwa mfano mzuri ni maktaba, kuna maktaba mpya pale lakini tunaendelea kukarabati Ofisi na maeneo mengine kwa awamu kadri bajeti inavyoruhusu. Tunaelewa kwamba chuo hiki sasa ni cha kimataifa kinachukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya *SADC* na *East African Community* kwa maana hiyo kuna kila sababu ya kukiboresha ili kiwe na hadhi inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la kutotolewa kwa fedha za maendeleo kwa Shirika la Nyumbu na Mzinga kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na ubunifu wa shirika hilo. Ni sahihi kwamba kwa kipindi kirefu Mashirika haya ya Nyumbu na Mzinga yamekuwa hayapati bajeti inayostahili na kwa maana hiyo kazi zao zimeendelea kupungua. Nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba tayari kuna mpango mkakati maalum kwa mashirika yote mawili haya ambayo yana bajeti na mpango huo tunaupeleka Serikalini ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zikipatikana basi mashirika haya yanaweza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine iliyotolewa ya ubovu wa barabara za mipakani. Hapa nataka nilieleze suala hili kwamba mpaka sasa hivi sera iliyopo haiweki barabara hizi chini ya Wizara ya Ulinzi au Jeshi la Wananchi, barabara hizi bado ziko kwenye mamlaka ya Halmashauri za Wilaya. Ndiyo maana tunapata tatizo kwa sababu zinakuwa siyo za kipaumbele chini yao matokeo yake ni kwamba barabara nyingi hazina hadhi inayotakiwa. Tunaweza kushauri hapo baadaye tutakapokutana kati yetu sisi, TAMISEMI na wenzetu wa Ujenzi kuona kwamba ni muhimu tukatafuta mpango maalumu kwa ajili ya barabara hizi. Hizi ni barabara za kiulinzi zinatakiwa zipitike muda wote kwa sababu huwezi kujua tatizo litatokea lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, tunapokea ushauri wa Kamati, tutakaa na wadau wote ili tuone njia nzuri zaidi. Tukiwezeshwa kibajeti hata Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wanaweza wakazitengeneza

barabara hizi ili ziweze kupita wakati wote pale zitakapohitajika ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge mmoja alielezea suala la Jeshi kugeuka kuwa la kiuchumi. Nataka nieleze tu kwamba Jeshi lina matawi ya kiuchumi. Suma JKT, Nyumbu na Mzinga ni sehemu za Jeshi na mashirika yote haya yanafanya biashara. Kwa maana hiyo, siyo kwamba wakati huu wa amani Jeshi limekaa tu kuna biashara kubwa zinazofanyika mfano mzuri ni Suma JKT. Suma JKT wana viwanda vingi tu ikiwemo kiwanda cha maji, kiwanda cha ushonaji, kiwanda cha kutengeneza viatu, wako kwenye kilimo na ufugaji na wana miradi mingi mbalimbali. Nia na madhumuni ni wapate fedha ili kutatua matatizo ya Jeshi ambayo yako nje ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nichukue fursa hii niwataarifu wenzetu wa Kamati kwamba mapendekezo yao tumeyapokea, tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa. Sasa nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru lakini niwashukuru Wabunge wote na Mawaziri wa Kamati yetu ambao wamefanya kazi ambayo ilikuwa mimi ndiyo niifanye. Niwashukuru kwa majibu mazuri, sahihi

na wamechukua muda mzuri kunipunguzia kazi yangu mimi hapa leo kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza machache tu na la kwanza ni la kesi kuchelewa mambo ambayo hayakuzungumzwa humu ndani. Hivi karibuni Waheshimiwa wote mmeona kuwa Mheshimiwa Rais amechagua Majaji wapya wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ili ku-*speed up* kesi za watuhumiwa mbalimbali. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tulishauri kwenye Kamati Waziri aanze sasa kutumia *Mobile Court* ambayo leo imezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais. Mahakama hii itasaidia kwa haraka sana kupunguza msongamano wa mahabusu wenye kesi zile ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwa vile Waziri wa Mambo ya Nje hakuwepo ni suala nililozungumza sana kuhusu gharama za kodi za nyumba ambazo Serikali inagharamia sasa hivi. Nimezungumza kwenye *speech* yangu kwa takribani miaka kumi sasa tunatumia zaidi ya shilingi bilioni 216 kulipia kodi za mapango. Serikali sasa iingie kwenye utaratibu wa *mortgage financing*, utarabu ambao utapunguza gharama kubwa sana ya ujenzi kwani badala ya pesa kwenda huko zitafanya kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo ni jengo letu la Msumbiji. Sasa hivi tuna ghorofa tisa pale Msumbiji, tuna majengo New York na maeneo mengine ambayo ni mali ya Serikali ya Tanzania. Maeneo haya sasa yamesababisha hata maduhuli kuwa mengi kutokana na kodi ambayo tunaikusanya katika majengo hayo na katika nchi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo machache, niwashukuru Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na wewe pamoja na Sekretarieti ambayo imesaidia Kamati yetu kutekeleza kazi kwa mujibu wa sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maana ya taarifa na mapendekezo yote yaliyotolewa.

*(Hoja ilitolea iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa kwanza kuishukuru sana Kamati pamoja na Mwenyekiti kwa kazi nzuri waliyoifanya iliyotuwezesha sisi kama Bunge kuweza kuijadili taarifa hii lakini pia kuweza kutoa mapendekezo mablimbali kwa kadri walivyokuwa wameifanya kazi yao. Niwatakie kila la kheri Serikali, Mheshimiwa Waziri hapa imeahidi kuyachukua yale yote ambayo Bunge limeazimia siku ya leo.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba katika kuutekeleza yale ambayo Bunge limeshafanyia maamuzi basi tunaweza kwenda vizuri katika kushughulika na changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziona, wamezichangia kwenye Kamati lakini pia wamechangia humu ndani na sasa haya ni maamuzi ya Bunge, kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ili aweze kuhitimisha hoja yake, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja yangu. Nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Bunge ambao wamepata fursa ya kuichangia hoja hii na kutoa mchango wa mawazo. Hoja hii imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 27, katika hao Wabunge 25 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi. Katika hao wanne waliochangia kwa maandishi lakini vilevile walizungumza, kwa hiyo, tunabaki na Waheshimiwa Wabunge wawili ambao walichangia kwa maandishi. Kwa hiyo jumla ni Waheshimiwa Wabunge 27.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hizi karibu kila Mheshimiwa Mbunge ameunga mkono hoja ya Kamati yetu. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa kuunga mkono hoja za Kamati hii. Vilevile kwa niaba ya Kamati, nichukue fursa hii kuwashukuru kwa pongezi mlizotoa kwa kazi iliyofanywa na Kamati, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamefanya kazi kubwa ya kujibu sehemu kubwa ya hoja zilizokuwa zimetolewa. Zipo hoja ambazo zilikuwa ni nje ya hoja ya Kamati, kwa hiyo, sitarajii kuzijibu lakini tunazichukua kama rejea ya Kamati kwa ajili ya kuzifanyia kazi kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitajikata katika maeneo manne yaliyojitokeza kwa upana ambayo Waheshimiwa Wabunge kwa uwingi wao waliyagusia. Eneo ya kwanza ni eneo la *REA*. Waheshimiwa Wabunge wameonesha kwamba Mradi wa kupeleka Umeme Vijijini ni hitaji la kila Mtanzania na kwamba kama Taifa tuna kila

sababu ya kuhakikisha tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tunakamilisha utekelezaji wa miradi hii kwa wakati. Kamati iliainisha changamoto kadhaa ambazo bahati nzuri na Waheshimiwa Wabunge wamezitolea maelezo. Niishukuru Serikali imekubali kufanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza upande wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni umeme wa Mto Rufiji. Namshukuru Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo ya kina sana katika eneo hili. Mradi huu kama tunavyofahamu utachukua miezi 36 ya utekelezaji. Mradi huu ulitiwa saini Desemba, 2018 na baada ya kutiwa saini miezi sita itakuwa ni kipindi cha mkandarasi kuji-*mobilize* kabla ya kuanza kuutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati tunasema mradi huu ni wetu. Kwa hiyo, kama Taifa kwetu sisi mradi huu ni wa kufa na kupona. Tulipofika sasa siyo sehemu tena ya kuzodoana na kurudishana nyuma, tulikofika sasa ni kusema tunafanya vipi vizuri zaidi ili mradi huu, hiki chetu kiweze kufanikiwa vizuri. Ndiyo maana katika mapendekezo yetu kama Kamati tumeiomba Serikali ihakikishe kwamba tunasimamia vizuri utekelezaji wa mradi huu na kwamba fedha za utekelezaji mradi huu zitolewe kwa wakati ili usiweze kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine linagusa mapendekezo ya wadau wa sekta ya madini. Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumza wameonesha ipo haja kubwa ya kuwawezesha wachimbaji wadogo. Wameonesha nia na matarajio kwamba tukiisimamia vizuri sekta hii basi mchango wake utakuwa mkubwa kwa uchumi wa Taifa letu. Hicho ndicho ambacho sisi katika Kamati tulikiona na ndiyo maana tumependekeza yale mapendekezo yote ya mkutano wa wadau yafanyiwe kazi. Nafurahi kwamba Mheshimiwa Waziri wa sekta husika ameonesha utayari wa kuyafanyia kazi maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa kwa mapana na kwa hisia tofauti ni mradi wa *Songas* na mikataba yake. Mazungumzo yalivyoendelea hapa ndani yalijikita zaidi kwenye mradi Songas lakini sisi tuliiangalia sekta nzima ya gesi nchini tukifanya rejea ya Kamati ndogo iliyoundwa na Mheshimiwa Spika ya kuishauri Serikali jinsi Taifa linavyoweza kunufaika na mapato ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tunampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa ujasiri na umakini mkubwa alioufanya kwa kuunda Kamati ile. Namshukuru Mungu nilipata fursa ya kupata nafasi ya kuongoza Kamati ile. Ni Kamati iliyokuwa na watu wa makini, ushauri uliotolewa sina hofu na mashaka hata kidogo kwamba ukifanyiwa kazi utatutoa hapa tulipo ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, rai yetu kama tulivyoonesha kwenye mapendekezo yetu ni kwamba jambo lile lifanyiwe kazi ili tuweze kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Nafurahi kusikia kwamba Serikali inasema imeanza kufanyia kazi jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, lipo jambo lilijaribu kusemwa mwanzo hapa kwamba taarifa hii pengine siyo matokeo ya kazi ya Kamati. Napenda niwahakikishie taarifa hii ni matokeo ya mchango wa mawazo ya Kamati. Kamati ilikutana tarehe 24 kujadili rasimu ya kwanza ya taarifa ya Kamati, wakatoa mapendekezo. Kamati ilikutana tarehe 25 kujadili mapendekezo waliokuwa wameyatoa mwanzoni. Kumbukumbu za vikao hivyo ninazo hapa, ukihitaji tutaweza kuziweka Mezani. Ndiyo maana hata mapendekezo yaliyotolewa na wasemaji yalishabihiana moja kwa moja na kile ambacho Kamati ilikipendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sasa Bunge lako liridhie na kuidhinisha maoni na mapendekezo ya Kamati ili yawe ni maamuzi ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, lakini kabla sijawahoji, ninayo hapa mapendekezo ya mabadiliko ya maazimio ya Kamati, sehemu ya 3.2.4, ukurasa wa 45, kuna mapendekezo hapo ya Mheshimiwa Ester Michael Mmasi. Sasa nimuite aseme kuhusu mapendekezo yake, tusikie Mwenyekiti anasemaje? Mheshimiwa Ester Michael Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hiii nami niwezi kuboresha mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kama ilivyotolewa mbele yetu na sisi tumeona ni vyema sasa tupate nafasi katika muktadha huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyotoa mwongozo, tukiangalia sehemu ya 3.2.4, sehemu ya tatu, ukurasa wa 45 ya ripoti hii inayohusiana na masuala mazima ya Chuo cha Madini cha Dodoma (*MRI),* napenda kutoa azimio na mapendekezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwenye *section* hii inayohusiana na Chuo cha Madini cha Dodoma Bunge, maneno yanayosomeka kwamba 'Bunge liazimie kwa Serikali kukiwezesha chuo hiki kifedha kwa kuacha makusanyo ya chuo kubakia chuoni ili chuo hiki kiweze kujiendesha chenyewe, kufanya ukarabati wa miundombinu pamoja na kuajiri walimu wa kutosha' yafutwe na badala yake yawekwe maneno 'Bunge liazimie kwamba Serikali ikiwezeshe Chuo cha Madini Dodoma kifedha kwa kukipa fedha kwa wakati kama inavyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu'.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu imejikita katika misingi mikuu mitatu. Kwanza napenda kuongelea utaratibu

wa uendeshaji wa shughuli za taasisi ya elimu lakini pia sheria ambayo inaongoza maoni haya ya Kamati ambayo tuliitunga sisi wenyewe hapa Bungeni yaani *Finance Act* ya mwaka 2017 na napenda kueleza nafasi ya sisi Wabunge katika kujenga hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Bunge lako Tukufu na haswa ni-*declare interest* katika ajira yangu ya miaka tisa niliifanyia Chuo Kikuu cha Dar es Salam nikiwa na-*head* masuala mazima ya *payroll section* yaani ulipaji wa Chuo Kikuu cha Dar es Salam na hivyo nitapenda ku-*share experience* kwenye hili. Ni kweli kabisa katika uendeshaji wa shughuli hizi za taasisi za elimu ni kwamba mapato ya ndani mathalani masuala ya ulipaji wa ada, *examination fee* na hata mapato ya ndani mara nyingi yanakuwa hayako *budgeted* kwa maana nyingine hayaletwi kwenye bajeti ya Serikali ama ikama ya Serikali ya taasisi hiyo Bungeni. Tunaposema hivi ni kwamba ukija kuangalia masuala ya usimamizi ni sawa na kusema fedha hizi zinakuwa hazina wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga hoja yangu nisingependa sana tukumbuke *University swaga* haswa tunaporejea Mradi wa Mlimani *City*. Pia nisingependa tukumbuke masuala mazima ya uwekezaji kwenye taasisi mbalimbali mfano *NSSF,* tumeona *white elephant* nyingi zimemea katika Tanzania yetu pasipo kuwa na jicho zuri na lenye tija katika mustakabali mzima wa kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposimama hapa na ninapoitoa hoja hii tutakumbuka Wabunge wengi tulikuwa tukilalamikia usimamizi mbovu wa fedha za ndani na matumizi mabovu. Ni sisi Wabunge tuliomba Serikali iwe na jicho la pekee na kwa muktadha huu Serikali ilikuja na *policy* au mwongozo mzima wa *retention strategies* kwamba mapato yote ya taasisi yapelekwe kwenye Hazina Kuu ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurejea *Finance Act* ya mwaka 2017 kwa kifupi sana haswa napoangalia

Ibara ya 44.6A(1) inayosema: "*For the porpose of section 8, all public moneys shall be collected through Government e-payment Gateway system or its acronomy "GePG"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo *other instrument,* napojaribu kuangalia *speech*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Ester, kengele imegonga, dakika moja malizia.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu pia iko *speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya tarehe 8 Juni 2017, Bunge nitaomba mrejee ilieleza wazi umuhimu wa sisi kutumia mfumo huu. Kama hiyo haitoshi, ukiangalia kwenye nafasi yetu ya Kibunge zipo sehemu nyingi tunaweza kushauri suala hili. Tukiangalia kwa mfano masuala ya mishahara tuna *PE* ambayo inakuja Bungeni kupitia bajeti ya Serikali Kuu. Pia ukiangalia masuala ya ukarabati wa ujenzi tunayo *Capital Development Grants* ambayo inakuja Bungeni na sisi Wabunge nafikiri tuna nafasi nzuri ya kuchangia katika hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa muktadha naomba kutoa hoja na naomba Wabunge wenzangu wote waniunge mkono. Ahsante sana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kuhusu mapendekezo haya.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokiona sisi ni chuo kutokuwa na fedha za kutosha za kujiendesha. Sina tatizo na mapendekezo haya kama Bunge litaridhia kwamba

mapendekezo haya yanakwenda kuliondoa tatizo la chuo kutokuwa na fedha za kujiendesha. Sina tatizo nayaunga mkono, naomba turidhie. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamatiameridhika na mapendekezo haya. Kwa hivyo nitawahoji sasa, kwa sababu hakuna haja ya kutoa hoja, hoja ilikuwa ni ya Mwenyekiti na Kamati yake. Nitawahoji kuhusu hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiwa ni taarifa yote aliyotuletea pamoja na mapendekezo na maazimio yote yaliyotolewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa pamoja na Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo imeliwezesha Bunge siku ya leo kuweza kujadili kwa pamoja lakini pia kuazimia kwenye mambo mbalimbali. Tunashukuru Waziri wa Nishati lakini pia Waziri wa Madini wamezungumza hapa utayari wao wa kuchukua mapendekezo na maazimio yote yaliyotolewa na Kamati. Wakati ule walikuwa wanazungumzia Kamati, sasa haya ni maamuzi ya Bunge ni maazimio ya Bunge. Kwa hiyo, tuwatakie kila la kheri kwenye utekelezajii wa hayo maamuzi ya Bunge na tunaamini kwamba mkiyatekeleza hayo mtaondoa zile changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuzionesha katika michango yao.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo hapa ambalo nalazimika kulizungumzia linatokana na mchango alioutoa Mheshimiwa Ally Keissy. Moja, ilikuwa ni kuhusu sehemu ya

taarifa ambayo niliagiza iondolewe kuhusu Rwanda na Congo.

Vilevile katika mchango wake pia alizungumza kuhusu Mheshimiwa Rais wa Marekani aliyepita alipokuja hapa nchini na kutembelea Ubongo na akahusisha na maneno ambayo yanaweza yakatuweka katika hali ambayo siyo nzuri. Kwa hiyo, naagiza upande wa Taarifa Rasmi za Bunge ziondoe pia eneo linalohusu kuja kwa Mheshimiwa Rais wa Marekani na kwenda kutembelea mitambo ya umeme Ubungo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho Alhamisi, tarehe 7 Februari, 2019 Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 2.06 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 7 Februari, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*